JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA ZA TAASISI ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2016

SERIKALI KUU

© March, 2017

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 16 Barabara ya Samora Machel, S.L.P. 9080, 11101 Dar es Salaam.
Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na.FA.27/249/01/2015/2016 31 Machi 2017

Mh. Dkt. John Pombe Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 9120, Ikulu,
1 Barabara ya Baraka Obama, 11400 DAR ES SALAAM.

YAH: KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI JUU YA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2016

Kulingana na Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, kwa heshima kubwa, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya Ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2015/16 kwa ajili ya hatua zaidi.

Wako mwaminifu;



Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

ORODHA YA MAJEDWALI iv
ORODHA YA VIELELEZO viii
MAMLAKA YA OFISI x
VIFUPISHO xi
DIBAJI xii
MUHTASARI xvi
SURA YA KWANZA 1
TAARIFA ZA AWALI 1
SURA YA PILI 10
HATI ZA UKAGUZI 10
SURA YA TATU 29
UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA 29
SURA YA NNE 40
UANDAAJI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI 40
SURA YA TANO 60
UKAGUZI WA DENI LA TAIFA, PENSIHENI, MALALAKA YA MAPATO NA HESABU JUMUIFU ZA TAIFA 60
SURA YA SITA 124
TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA 125
SURA YA SABA 131
SURA YA NANE 150
WAKALA ZA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE 150
SURA YA TISA 215
USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA 215
SURA YA KUMI 234
SURA YA KUMI NA MOJA 255
USIMAMIZI WA MALI NA MADENI 255
SURA YA KUMI NA MBILI 270

KAGUZI MAALUM NA UKAGUZI WA VYUAMA VYA SIASA 270
SURA YA KUMI NA TATU 291
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..... 291
VIAMBATISHO 302

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Mchanganuo wa Taasisi zilizokaguliwa na zisizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 6
Jedwali 2: Aina ya hati za Ukaguzi/Maoni ya Ukaguzi 10
Jedwali 3: Vigezo vya Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine 12
Jedwali 4: Taasisi na Msingi wa Hati zenye Shaka. 14
Jedwali 5: Vigezo/Sababu ya hati isiyoridhisha kwa Chama cha ACT Wazalendo na Mfuko wa Rais wa udham 22
Jedwali 6: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Kipindi cha Miaka Mitano 28
Jedwali 7: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa CAG juu ya ripoti ya kila Mkaguliwa 31
Jedwali 8: Mchanganuo wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2013/14 na 2014/15 32
Jedwali 10: Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu za Serikali kwa miaka ya nyuma 34
Jedwali 11: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguliwa 38
Jedwali 12: Mwenendo wa uchambuzi wa bajeti kwa miaka mitatu (Kiasi katika shilingi bilioni) 47
Jedwali 13: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida dhidi ya Makisio(Kiasi katika shilingi bilioni) 50
Jedwali 14: Fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo kwa miaka mine mfululizo. (Kiasi katika shilingi milioni) 52
Jedwali 15: Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotolewa na matumizi yake(Kiasi katika shilingi bilioni) 54
Jedwali 16: Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa miaka mitatu (Kiasi katika shilingi milioni) 55
Jedwali 17: Viashiria vya deni kwa miaka ishirini ijayo 67
Jedwali 18: Ulinganisho wa gharama za kukopa 2015/16 72
Jedwali 19: Mafaili ya wastaafu yaliyokaguliwa 2015/2016 79
Jedwali 20: Mafao ya hitimisho la kazi yaliyozidishwa 80

Jedwali 21: Idadi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa mwaka 2001/02 – 2014/15 83
Jedwali 22: Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo kwa ujumla 84
Jedwali 23: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2015/16 (Shilingi kwa mamillion) 85
Jedwali 24: Ufanisi kwa ujumla katika makusanyo ya mapato Tanzania (shilingi kwa milioni) 87
Jedwali 25: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania 94
Jedwali 26: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2012-2016 (shilingi kwa mamilioni) 100
Jedwali 27: Orodha ya bidhaa zilizokaa muda mrefu katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha 104
Jedwali 28: Kiasi cha kodi ya Ongezeko la thamani kitokanacho na maziwa yaliyoingizwa nchini kulipiwa kodi kwa vituo 106
Jedwali 29: Bidhaa zilizoruhusiwa kutoka zikiwa na kodi..... 108
Jedwali 30: Tozo za Maendeleo ya Reli isiyokusanywa kwa vituo . 110
Jedwali 31: Makadirio ya kodi ambayo haijakusanywa..... 111
Jedwali 32: Makadirio ya kodi ambayo haijakusanywa katika mikoa ya kodi 12 ya Kitengo cha ukusanyaji wa mapato ya ndani..... 113
Jedwali 33: Makosa ya Usahihi wa Jumla ya Fedha 117
Jedwali 34: Taasisi zenye mapungufu ya kiutawala 129
Jedwali 35: Malipo Ya Mishahara kwa Watumishi Ambao Hawapo Kwenye Utumishi wa Umma 131
Jedwali 36: Makato ya mishahara kwa watumishi ambao hawakuwa kwenye utumishi wa Umma 133
Jedwali 37: mishahara isiyolipwa ambayo haijarejeshwa Hazina. 135
Jedwali 38: Makato ya Mishahara yaliyocheleweshwa..... 136
Jedwali 39: Faini kwa kuchelewesha makato ya kisheria 137
Jedwali 40: Kuchelewa kulipa stahili za watumishi kwa muda mrefu 138
Jedwali 41: Kodi ya Mapato kutolipwa kutoka kwenye posho za kukaimu 139
Jedwali 42: Watumishi ambao hawajarejesha mikopo 140
Jedwali 43: Watumishi wanaokaimu zaidi ya miezi sita 141

Jedwali 44: Watumishi ambao wanapokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria 142
Jedwali 45: Taasisi ambazo hazikufanya tathmini na kupima watumishi 143
Jedwali 46: Upungufu wa wawatumishi 145
Jedwali 47: Kumbukumbu za watumishi zenye dosari..... 146
Jedwali 48: Orodha ya ofisi za balozi zenye watumishi waliofanya kazi ubalozini zaidi ya muda ulioidhinishwa. 148
Jedwali 49: : Mikataba iliyokwisha muda wake 149
Jedwali 50: Malipo yasiyoambatana na risiti za kielektroniki 156
Jedwali 51: Wakala zenye malipo yasiyo na viamboatisho 158
Jedwali 52: Wakala zenye masurufu yasiyorejeshwa..... 159
Jedwali 53: Riba kutokana na kucheleweshwa malipo 167
Jedwali 54: Madai ya Wakandarasi na Wazabuni Washauri yasiyolipwa 169
Jedwali 55: Mapato yasiyorjeshwa RITA..... 173
Jedwali 56: Mali zisizofaa kwa matumizi na mali zinazotumika taratibu..... 179
Jedwali 57: Orodha ya mikopo iliyotolewa isiyorejeshwa 193
Jedwali 58: Taasisi zenye madai yasiyokusanywa..... 195
Jedwali 59: Madeni yasiyolipwa 197
Jedwali 60: Dosari kwenye matumizi ya fedha 199
Jedwali 61: Madai yasiyorejeshwa 201
Jedwali 62: Mikopo iliyotolewa kinyume na malengo yaliyokusudiwa 203
Jedwali 63: Madeni yasiyokusanywa 204
Jedwali 64: Mapato yasiyokusanywa 206
Jedwali 65: Fedha zilizokusanywa ambazo hazikuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu..... 207
Jedwali 66: Upungufu wa watumishi..... 209
Jedwali 67: Manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa na huduma bila ya kuwapo kwa makubaliano ya mkataba 219
Jedwali 68: Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa..... 221
Jedwali 69: Mapungufu yaliyobainika katika mpango wa Manunuzi wa mwaka..... 223

Jedwali 70: Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa Ukaguzi..... 226
Jedwali 71: Vifaa na huduma zilizolipiwa hazikupokelewa..... 227
Jedwali 72: Tathimini ya Viashiria vya Rushwa..... 230
Jedwali 73: Mapungufu yaliyobainika katika taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki mali za Serikali 231
Jedwali 74: Taasisi zilizolipa zaidi ya malipo ya stahiki 237
Jedwali 75: Taasisi zenye malipo yasiyo na hati za malipo..... 239
Jedwali 76: Orodha ya Taasisi zilizolipa katika vifungu vya bajeti visivyostahili..... 245
Jedwali 77: Taasisi zilizofanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa 247
Jedwali 78 Taasisi zenye masurufu ya muda mrefu 249
Jedwali 79: Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi..... 251
Jedwali 80: Taasisi ambazo hazikuwakata watoa huduma kodi ya zuio 252
Jedwali 81: Ulinganisho wa Taasisi na kiasi cha Kodi ya Zuio isiyokatwa kwa miaka miwili (2):..... 253
Jedwali 82: Magari Mabovu Yasiyotumika ambayo Hayafanyiwi Matengenezo wala Hayauzwi..... 258
Jedwali 83: taasisi zenye bidhaa ambazo hazikuingizwa katika vitabu 260
Jedwali 84: kiambatisho Taasisi ambazo zina mapato yasiyokusanywa 261
Jedwali 85: Mali za Kudumu ambazo Hazina Alama za Utambulisho 264
Jedwali 86: Madeni tarajiwa 266
Jedwali 87: Hosipitali zinazodai 268
Jedwali 88: Madeni ambayo hayana nyaraka 269

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1: Chati ya mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa mwaka 2013/14 na 2014/15 33
Kielelezo 2: Hali halisi ya mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali na utekelezaji wake katika Ripoti ya jumla 35
Kielelezo 3: Muhtasari wa utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma juu ya Ripoti ya Jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali..... 36
Kielelezo 4: Mchanganuo wa utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwenye Ripoti kuu ya mwaka 37
Kielelezo 5: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa 39
Kielelezo 6: Mwenendo wa makisio ya mapato ya Serikali na ukusanyaji wake kwa miaka minne mfululizo 45
Kielelezo 7: Mwenendo wa Makisio..... 48
Kielelezo 8: Mwenendo wa mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara/Idara Sekretariati za Mikoa na Balozi(Kiasi katika shilingi milioni) 56
Kielelezo 9: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano 61
Kielelezo 10: Vyanzo vya deni la Nje hadi tarehe 30 Juni 2016..... 62
Kielelezo 11: Deni la nje kwa ulinganifu wa masharti nafuu na isiyo ya nafuu 65
Kielelezo 12: Mchanganuo wa deni la nje mwaka 2011/12 na 2015/16 68
Kielelezo 13: Asilimia ya Makusanyo halisi Kwa Idara kwa mwaka 2015/16 86
Kielelezo 14: Mlinganisho kati ya makisio ya ruzuku kutoka serikalini na vyanzo vya ndani vya mapato (kiasi katika shilingi trilioni) 151
Kielelezo 15: Mlinganisho makusanyo halisi ya ruzuku serikalini na mapato ya ndani(Kiasi katika shilingi trilioni) 154
Kielelezo 16: Mwenendo wa miaka minne (4) wa malipo yasiyokuwa na manufaa 234

Kielelezo 17: Mwenendo wa miaka sita (6) wa malipo zaidi ya Stahiki 238
Kielelezo 18: Kielelezo kifuatacho kinaonesha mwenendo wa malipo ambayo Hati zake za Malipo zilikosekana na Taasisi zake: 240
Kielelezo 19: Chati ya ulinganifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka minne (4) iliyopita : 241
Kielelezo 20: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu ... 242
Kielelezo 21: Mwenendo wa Kukosekana kwa EFD Stakabadhi kwa miaka minne (4)..... 244
Kielelezo 22: Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili..... 246
Kielelezo 23: Chati inayoonesha Mwenendo wa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyooidhinishwa 248
Kielelezo 24: Mwenendo wa Masurufu yasiyorejeshwa 250
Kielelezo 25: Malimbikizo ya madeni 268
.

MAMLAKA YA OFISI

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,
Ofisi Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vimeainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) kama ilivyofafanuliwa zaidi na vifungu vya 45 na 48 vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Dira ya Ofisi

Kuwa kituo cha ubora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma.

Lengo La Ofisi

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji ili kupata thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Misingi ya Maadili

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Zingatio kwa Wadau	Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamanduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo, weledi na ari ya kazi.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo kutoka ndani na nje ya taasisi.
Matumizi bora ya rasilimali	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake

© Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, baada ya taarifa hii kuwalishwa Bungeni, taarifa itakuwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hautakuwa na kikomo

VIFUPISHO

ACGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
ADEM	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu
AFRM	Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika
AGITF	Mfuko wa Pembejeo za Kilimo
AO	Afisa Masuuli
APP	Mpango wa Manunuzi wa Mwaka
ASA	Wakala wa Mbegu za Kilimo
BOQ	Mchanganuo wa Gharama za Ujenzi
BoT	Benki Kuu ya Tanzania
CAG	Mdibiti na Mkaguzi Mkuu
CDF	Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi
CG	Serikali Kuu
CTA	Kibali cha Kazi cha Muda Mfupi
DART	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam
DDCA	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa
EFD	Mashine za Kielekroniki
ETD	Hati za Dharura za Kusafiria
FETA	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo
FRF	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
GCLA	Wakala wa Maabara za Serikali
GN	Tangazo la Serikali
GoT	Serikali ya Tanzania
GPSA	Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi
GST	Wakala wa Utafiti wa Miamba
HESLB	Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu
HQ	Makao Makuu
IFMS	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha
IJA	Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA)
IPSAS	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma

DIBAJI

Ninafurahi kwamba, kwa mara nyingine tena nimeweza kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuwasilisha kwa Mh. Rais ripoti ya jumla ya ukaguzi ya kila mwaka kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2016 mwishoni mwa Machi 2017 kama inavyotakiwa na Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005). Katiba inatupa mamlaka sisi kama wakaguzi wa taifa.

Ripoti hii ina matokeo muhimu ya ukaguzi wa fedha, ukaguzi wa sheria mbalimbali kama zinafuatwa kikamilifu, tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani na masuala ya utawala wa Serikali Kuu ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Hesabu Jumuifu za Taifa. Pia inajumuisha matokeo ya ukaguzi wa mafaili ya pensheni kabla ya malipo, ukaguzi maalum chini ya Serikali Kuu na ukaguzi wa vyama vya siasa.

Serikali Kuu inajumuisha Wizara, Idara za Serikali zilizopo ndani ya Wizara, Wakala wa Serikali, Mifuko, Balozi, Sekretarieti za Mikoa, Bodi za Mabonde ya Maji na taasisi nyinginezo.

Hata hivyo, Wakala wawili wa Utendaji wawili wa Serikali, ambao ingawa wapo chini ya Serikali Kuu, wamekuwa wakikaguliwa na taarifa zake za ukaguzi kutolewa kwenye taarifa ya jumla ya Mashirika ya Umma.

Masuala yaliyotajwa katika ripoti hii ni yale yaliyobainika katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016 na yale ambayo yalibainika miaka ya nyuma lakini hayakutolewa taarifa zake kwa kipindi hicho. Pia, inatoa taarifa juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa

miaka ya nyuma na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC).

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) ambavyo ni viwango muhimu kwa ajili ya ukaguzi wa Taasisi za Umma viliyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC).

Kazi yangu ni kutoa uhakika usio na shaka kwa bunge na kwa umma kuwa Serikali inafanya kazi zake kwa kufuata viwango vya fedha vilivyopitishwa.

Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

SHUKRANI

Mafanikio ya kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi yalitokana na juhudi za pamoja za watu mbalimbali na makundi tofauti ambao walikuwa tayari kujitolea muda wao, maarifa, utaalamu na rasilimali fedha kuweza kufanikisha zoezi hili. Hasa, napenda kutambua michango kutoka kwa wafuatao:

Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania inapenda kutoa shukrani za kipekee kwa Mh. Rais: Kwanza, kwa imani kubwa aliyonayo kwa Ofisi yangu na kwa juhudi zake ambazo zilituwezesha kupata kiasi cha Shilingi bilioni 9 ilipofika mwishoni mwa mwezi Oktoba 2016. Bila kupata fedha hizi kazi ya ukaguzi iliyotegemewa kufanyika ingeathirika kwa kiasi kikubwa.

Wabunge wa Bunge la Tanzania
Shukrani zangu za dhati pia nazielekeza kwa Waheshimiwa wWabunge wa bunge la Jamhuri ya Muungano na Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuingia kwenye mdahalo uliozaa matunda na kwa kujitoa kwao kuhakikisha kwamba taarifa za ukaguzi zinabakia kuwa na manufaa na kwamba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inabakia kuwa na uhuru wake bila kuingiliwa kiutendaji.

Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu Tanzania (NAOT)
Ninawiwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa kujitoa kwao katika kuifanya kazi hii ya ukaguzi kwa moyo. Licha ya kuwapo kwa vipingamizi vingi, hasa rasilimali fedha tulivyokumbana navyo, watumishi wangu walifanya kazi yao kwa weledi bila kuathiri ubora wa kazi ya ukaguzi. Walifanya kazi bila kuchoka wakati mwingine hata baada ya muda wa kazi bila motisha yeyote ya kifedha wakiongozwa na dhamira yao njema ili kuhakikisha kazi ya ukaguzi inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

Menejimenti ya Taasisi Zilizokaguliwa

Ufanisi katika kazi ya ukaguzi hutokana na ukaribu na mawasiliano ya mara kwa mara kati ya timu ya ukaguzi na menejimenti ya taasisi inayokaguliwa. Katika kipindi chote cha ukaguzi, kumekuwepo na ushirikiano wakati wote, hasa wakati wa mahojiano, kuomba nyaraka na wakati wa kuhitaji ufafanuzi wa jambo kutoka kwa manejimenti. Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa menejimenti ya taasisi zote tulizozikagua kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia kipindi chote cha ukaguzi.

Wizara ya Fedha na Mipango

Napenda kutoa shukrani zangu za kipekee kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kwa ushirikiano wao wa dhati na kutupa taarifa za msingi tulizozihitaji wakati wa maandalizi ya taarifa hii. Napenda pia kumshukuru mpigachapa kwa kuwezesha taarifa hii kuchapishwa na kutoka kwa wakati.

Wafadhili wa na Wadau wengine

Mwisho kabisa napenda niwashukuru wafadhili wetu, hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia SIDA, Benki ya Dunia kupitia PFRMP na Sekretariati ya Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika – Nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI – E Secretariat), ambao, kwa sehemu kubwa walichangia kuleta mabadiliko kwenye ofisi yangu. Pia napenda kutambua mchango uliofanywa na vyombo vya habari katika kufanya ripoti zangu kuwafikia watumiaji wengi na wadau ambao kwa sehemu moja au nyingine wamechangia mafanikio ya ofisi yangu.

1. Utangulizi

Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wangu wa taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha uliomalizika Juni 30, 2016. Mawanda ya ukaguzi katika Serikali Kuu ni pamoja na Wizara na Idara za Serikali 62, Wakala 37, Mifuko maalum 18, taasisi nyingine 42, Vyama vya Siasa 19, Sekretariati za Mikoa 26, Balozi za Tanzania 34, Bodi za mabonde ya Maji 13. Pia, inajumuisha ukaguzi wa mamlaka ya kodi ya mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa, ukaguzi wa awali wa mafaili ya mafao ya wastaafu na kaguzi maalum.

2. Mwenendo wa jumla wa hati za Ukaguzi

Ukaguzi wa taarifa za fedha kwa mwaka uliomalizika Juni 30, 2016 inaonyesha kwamba kati ya taarifa za fedha 222 zilizokaguliwa ni 190 au (86%) zilipata hati inayoridhisha 24 au (11%) zilipata hati yenye shaka, 3 au (1%) zilipata hati isiyoridhisha, wakati 5 au (2%) zilipata hati mbaya.Jedwali Na.1 hapa chini linaonyesha muhtasari wa mwelekeo wa hati za ukaguzi katika serikali kuu kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016.

Jedwali Na.1 Mwenedo wa hati za ukaguzi

Mwaka	Hati zinaziridhisha		Hati yenye shaka		Hati isiyoridhisha		Hati mbaya		
	Idadi	%	Idadi	%	idadi	%	Idadi	%	Jumla ya wakaguliwa
2015-16	190	86	24	11	3	1	5	2	222
2014-15	181	91	17	9	1	1	0	0	199
2013-14	166	94	9	5	1	1	0	0	176
2012-13	85	73	30	26	1	1	1	1	117
2011-12	103	95	5	5	0	0	0	0	108

Kati ya taasisi zilizopata hati mbaya, ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mawanda ya ukaguzi yalikwazwa kwa mambo yafuatayo:

a) Hati za malipo sita (6) zilizolipwa kwa mzabuni mmoja na viambatisho vyake kiasi cha Sh. 91,261,040,310 ikiwa sawa na asilimia 31 ya matumizi yote ya fungu hili havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ingawa nilifuatilia hadi ngazi za juu, hivyo sikuhakiki uhalali wa matumizi.

b) Nilibaini kuwa fedha kiasi cha Sh. 5,444,127,508 zilizopelekwa Jeshi la Kujenga Taifa hazikuwa na mchanganuo wa matumizi

c) Kukosekana kwa usawa wa mali za kudumu PPE katika taarifa za fedha, kielekezi Na. 92 na taarifa ya mtirirko wa fedha, hivyo kushindwa kujua usahihi wa taarifa hizi.

d) Kazi iliyokuwa inaendelea ya thamani ya shilingi 8,086,336,381 ambayo ilijumlishwa kama sehemu ya mali za kudumu katika mwaka wa fedha, haikuwa na nyaraka/hati zozote za kuweza kuonesha kazi halisi iliyofanyika.

Zaidi ya hayo taarifa za hesabu za taasisi 10 za miaka ya nyuma zilikaguliwa katika kipindi hiki. Kati ya hizo, taasisi mbili(2) zilipata hati inayoridhisha, mbili(2) zilipata hati zenye shaka, taasisi moja(1) ilipata hati isiyoridhisha, na taasisi nne (4) zilipata hati mbaya. Maelezo yametolewa katika sura ya pili ya ripoti hii.

3. Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita

Nimefanya ufuatiliaji katika utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita juu ya ripoti moja moja na ripoti ya jumla ili kutathmini jinsi Taasisi zilivyotekeleza kikamilifu masuala yaliyopendekezwa katika kaguzi zangu zilizopita. Katika kufuatilia, nilizingatia kama menejimenti za Taasisi

zilichukua hatua katika kushughulikia mapungufu yaliyoripotiwa katika kuleta faida tarajiwa.

Kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, jumla ya mapendekezo ya ukaguzi 3898 yalitolewa. Kati ya hayo, 1449 (37%) yalitekelezwa kikamilifu, 1351 (35%) yapo kwenye hatua ya utekelezaji, 842 (22%) hayajatekelezwa na 256 (7%) yalipitwa na wakati. Kwa ujumla, utekelezaji ni wa wastani.

Kwenye ripoti ya jumla ya mwaka wa fedha 2014/2015, kulikuwa na mapendekezo 102 ambayo hayakutekelezwa yanayohitaji Serikali kuyafanyia kazi. Nimepokea majibu ya Serikali ambapo mapendekezo 19 (18.6%) yametekelezwa, 53 (52.0%) ziko kwenye hatua ya utekelezaji, 20 (19.6%) hayajatekelezwa na 10 (9.8) yamepitwa na wakati.

Utekelezaji wa Maelekezo ya kamati ya bunge ya hesabu za Serikali Kuu

Katika ripoti moja moja Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilitoa maelekezo 290 ambayo yalihitaji utekelezaji wa serikali kutoka kwa maofisa Masuuli husika. Kati ya maelekezo hayo; 102 (35%) yametekelezwa kikamilifu, 87 (30%) yapo katika hatua ya utekelezaji, 85 (29%) hayakutekelezwa na 16 (6%) yalipitwa na wakati. Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imekuwa mahususi katika kuhakikisha Taasisi zinazohusika zinachukua hatua za pamoja.

Maelezo ya kina ya utekelezaji wa mapendekezo yameonyesha katika sura ya tatu ya ripoti hii.

4. Uandaaji na Utekelezaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016 ilibainika kuwa serikali ilitenga shilingi bilioni 5,921.1 kati ya bajeti ya shilingi bilioni 22,495.5 kwa shughuli za maendeleo kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Hii ni pungufu ya 8.13%

ikilinganishwa na shilingi bilioni 6,445.11 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014 / 15.

Kutoka kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa za Serikali Kuu (Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa), nilibainisha makadirio ya maendeleo ya shilingi bilioni 4,968.86; lakini kiasi halisi kilichotolewa ni shilingi bilioni 3,768.86 kikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 1,200.26 (24.16%). Wakati huo huo, kiasi cha shilingi bilioni 38.88 (1.03%) ya fedha iliyotolewa hakikutumika.

Kadhalika, Serikali ilitenga shilingi bilioni 16,574 zitumike katika matumizi ya kawaida kukiwa na ongezeko la shilingi 3,166.18 bilioni (23.61%) ikilinganishwa na shilingi bilioni 13,408.22 zilizotengwa mwaka 2014/15. Taarifa za fedha zilizokaguliwa za Serikali Kuu, (Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa) zilibainisha kupitishwa kwa makadirio ya shilingi bilioni 12,904.75 lakini kiasi halisi kilichotolewa ni shilingi bilioni 12,065.22 ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 839.54 (6.51% ya makadirio yaliyopitishwa), wakati shilingi bilioni 19.28 hazikutumika sawa na 0.16% ya fedha iliyotolewa.

Kiasi chote kilichotolewa shilingi bilioni 5,731.07 (28.63% ya shilingi bilioni 20,020.95) iliyotolewa katika robo ya mwisho, wakati shilingi bilioni 2,629.40 (13.13% ya shilingi bilioni 20,020.95) kilitolewa mwezi Juni 2016 ikionyesha ucheleweshaji wa kutolewa kwa fedha kutokana na kutokuwa na usawa kati ya makusanyo halisi ya mapato na matarajio ya matumizi ya serikali.

Kumekuwa na ucheleweshaji katika utoaji wa fedha kutoka Hazina na kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii imesababisha kuchelewa kwa utekelezaji au kutotekeleza kabisa kwa miradi iliyopangwa. Kushindwa kutoa fedha kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti ,hasa fedha za maendeleo kuna athari kwenye kuongezeka kwa gharama za utekelezaji kutokana na kuongezeka kwa gharama na riba ambazo zinatokana na kutokulipa wazabuni kwa wakati na kusababisha kuongezeka kwa malimbikizo ya matumizi,

vile vile kuwa na kiasi kikubwa cha bakaa mwisho wa mwaka. Taarifa zimeelezwa kwa kina katika sura ya nne.

5. Hesabu za Taifa

(a) Deni la Taifa

Kufikia tarehe 30 Juni, 2016 deni la Taifa lilikuwa shilingi bilioni 41,039.39 ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 11,193.39 na deni la nje bilioni 29,846.00 ikiwa ni ongezeko la bilioni 7,499.80 sawa na asilimia 22 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 33,539.59 lililoripotiwa 30 Juni 2015.

Katika ukaguzi wangu nilibaini masuala ya msingi yafuatyo kuhusu deni la taifa na usimamizi wake; ongezeko la mikopo isiyo ya masharti nafuu kutoka asilimia 11 mwaka 2011/12 mpaka asilimia 31 ya deni la nje kufikia tarehe 30 Juni, 2016 ikiambatana na kuongeza gharama za kuhudumia deni la taifa, kushushwa kwa kiwango cha deni la taifa kwa kiasi cha shilingi bilioni 3,217 ikiwa ni madeni ya mifuko ya pensheni na dhamana zilizokiukwa masharti na kuisha muda wake, kukopa zaidi kutoka vyanzo vya ndani kwa asilimia 42, mapungufu katika usimamizi wa fedha za Serikali, sheria na kanuni za usimamizi wa deni la taifa kupitwa na wakati, kutapanywa kwa shughuli za ofisi ya mbele, kati na ya nyuma kunakoongeza changamoto katika kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa sahihi zinazohusu deni la taifa.

(b) Mamlaka ya Mapato Tanzania

Matumizi mabaya ya msamaha wa kodi Shilingi bilioni 3.46 ambao ulitolewa kwa walengwa wawili katika sekta ya usafirishaji walioagiza jumla ya magari 238 hata hivyo magari hayo yalisajiliwa na kutumika na watu tofauti na walengwa wa msamaha huo. Walengwa waliopewa misamaha hiyo wote walikana hali inayoonyesha kuwa bado kuna uhitaji wa kuboresha udhibiti na ufuatiliaji wa masuala ya msamaha wa kodi.

Tathmini ya udhibiti wa misamaha ya mafuta yanayoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya migodi ambapo nimebaini lita za mafuta 4,248,802 yaliyosafirishwa kutoka Dar es Salaam kati ya mwezi Oktoba 2014 na Disemba 2015 kwa ajili ya matumizi katika migodi ya Buzwagi, Bulyankulu na Geita, hatukuweza kupata nyaraka za uthibitisho wa kufikishwa kwa mafuta hayo katika vituo hali inayoashiria mafuta hayo yaliyosamehewa kodi kutumika tofauti na yalivyokusudiwa.

Pia nibaini lita 20,791,072 za mafuta yenye msamaha wa kodi wa Shilingi bilioni 10.17 kwa ajili ya Mgodi wa Buzwagi kwa miezi 18 (kuanzia Julai 2014 hadi Disemba 2015) yalisafirishwa kwa Kampuni ya M/S Aggreko mkandarasi mdogo ambaye sio mnufaika wa msamaha huo kwa mujibu wa sheria.

Mapungufu katika Usambazaji wa Mashine za kielektroniki (EFD): Ukaguzi wangu wa kipindi cha mwezi Julai, 2015 hadi Novemba, 2016 ulibaini upungufu wa mashine za EFD kwa asilimia 84 ambapo kati ya walipa kodi 9,743 waliosajiliwa kukusanya kodi ya ongezeko la dhamani (VAT) 8,165 hawakuwa na mashine za EFD. Kadhalika, kati ya walipa kodi 49,009 wanaostahili kutumia mashine hizo wasiosajili kukusanya kodi ya ongezeko la dhamani (VAT) 39,882 hawakua na mashine hizo sawa na asilimia 81.

Mapungufu katika usimamizi wa ukusanyaji wa kodi zilizofanyiwa tathmini shilingi bilioni 610.382. Kiasi hiki kinatotokana na tathmini ya kodi katika idara ya walipakodi wakubwa na mapato ya ndani kiasi cha shilingi bilioni 588.833, kutokusanywa kwa tozo za Maendeleo ya Reli shilingi bilioni 9.27 kwenye bidhaa na mafuta ikiwemo riba ya ucheleweshaji malipo ya shilingi bilioni 3.311, kutokusanywa kwa ushuru wa forodha kiasi cha shilingi bilioni 9.319 kutokana na bidhaa 9,942,810 ambazo hazikuepo kwenye maghala ya forodha na kutokusanywa

kwa kodi ya ongezeko la dhamani kwenye maziwa yaliyosindikwa shilingi bilioni 2.96 ambayo yaliingizwa nchini.

6. Mapungufu ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Menegimenti ina wajibu wa kuanzisha na kusimamia mifumo ya udhibiti. Wakaguzi katika mfumo wa udhibiti wa ndani wana wajibu wa kufanya tathmini na kutoa mapendekezo kwa ajili ya kuboreshwa kwa mifumo ya udhibiti. Tathmini yangu ililenga katika kuangalia ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi, kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, TEHAMA na Udhibiti na taratibu za usimamizi wa vihatarishi. Nilibaini yafuatayoutendaji usioridhisha kwenye kamati za ukaguzi na vitengo ukaguzi wa ndani kwenye taasisi 34 zilizokaguliwa; kukosekana kwa ufanisi juu ya udhibiti wa TEHAMA kwenye taasisi 31 zilizokaguliwa. Taasisi tatu zilikuwa na bodi duni (shirika moja halina bodi ya ushauri ya wizara, na moja bodi imemaliza muda wake). vile vile, taasisi 19 hazina mpango mkakati wa TEHEMA wakati majanga yakitokea. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya sita

7. Usimamizi wa raslimali watu na taarifa za Mishahara

Mabadiliko makubwa yamefanywa kutokana na ripoti yangu ya mwaka jana kuhusu usimamizi wa rasilimali watu hata hivyo, kuna maeneo yaliyoonekana yanayohitaji maboresho:

(a) Mishahara ya kiasi cha shilingi 1,400,554,592 ililipwa na taasisi za Serikali kumi na tisa, kwa watu 260 wasio wafanyakazi. Vile vile, taasisi saba zilifanya makato ya shilingi 50,525,057.96 kutoka kwa watu 28 wasio wafanyakazi. Ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka **uliopita, kuna ongezeko la shilingi 1,007,903,556 sawa na asilimia 257.**

(b) **Ukaguzi wangu katika sampuli ya taasisi nane ikiwa ni pamoja na Wizara mbili na Sekretarieti za Mikoa sita ulibaini mishahara ambayo haikulipwa kiasi cha**

shilingi 1,027,334,712.04 zikiwa zimewekwa kwenye akaunti ya amana bila kurejeshwa Hazina.

(c) **Ukaguzi wangu wa mishahara ulibainisha kuwa taasisi tano zilifanya makato ya mishahara ya kisheria kiasi cha shilingi 167,486,144.25 kutoka kwa watumishi wa umma, lakini taasisi zilichelewesha kuzipeleka kwenye mifuko ya jamii inayohusika. Ucheleweshaji umetofautiana kutoka mwezi mmoja hadi 138. Taasisi mbili zilitozwa adhabu ya malipo kiasi cha shilingi 17,050,249.95 ambazo ni upotevu wa fedha za umma.**

(d) **Ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali watu katika sampuli ya Taasisi 7 za Serikali Kuu umebaini kuwa kuna madai ya wafanyakazi kiasi cha shilingi 8,204,093,899.44 ambayo hayajalipwa kwa kipindi cha hadi miaka kumi.**

(e) **Ukaguzi uliofanyika katika sampuli ya taasisi tatu (3) ulibainisha kuwa posho za kukaimu kiasi cha shilingi 37,839,010 kwa wafanyakazi saba zililipwa bila kukata kodi ya mapato (PAYE) kinyume na Kifungu Na. 7 (2) (a) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2008) inayohitaji kodi ya mapato kutoka miongoni mwa vyanzo vingine, posho ya kukaimu ikatwe kodi na kupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.**

(f) **Kama sehemu ya ukaguzi wangu juu ya usimamizi wa rasilimali watu, nilibaini kuwa Maafisa Masuuli katika taasisi nane hawakuwa wakizingatia mahitaji ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa kushindwa kutoa taarifa kwa Bodi ya Mikopo juu ya wanufaika 659 waliopo ndani ya mamlaka yao kama vile kupanga kwa ajili ya makato ya kila mwezi na kuwasilisha bodi ya mkopo. Matokeo yake, jumla ya kiasi cha shilingi 913,391,857.82 kilichotolewa kama mkopo kwa wafanyakazi kilikuwa bado kufanyiwa makato.**

(g) **Nilibainisha kuwa wafanyakazi 49 kutoka taasisi kumi na nne wamekuwa wanakaimu katika nyadhifa mbalimbali zaidi ya miezi sita bila kuteua watu wa kushika nafasi hizo kinyume na matakwa ya kanuni za kudumu za watumishi wa umma.**

(h) **Katika sampuli ya taasisi thelathini na nane (38) zilizokaguliwa, nilibainisha nafasi za watumisha 11,892 zikiwa wazi dhidi ya mahitaji ya watumishi 24,568. Uhaba huu ni sawa na 48% ya kiwango cha idadi ya watumishi wanaohitajika. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya saba**

8. Wakala wa Serikali, Mifuko, na taasisi nyingine za Serikali.

A. Mapungufu Mtambuka ya Wakala za Serikali

i. Mapungufu katika Matumizi ya Wakala

Katika kupitia matumizi ya Wakala za Serikali kwa mwaka 2015/2016, nilibaini kwamba Wakala 11 zilifanya malipo ya shilingi 2,976,493,244.60 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD) kinyume na Kanuni. 24 ya Kanuni za EFD za 2012.

Nilibaini Wakala wa Serikali 9 kwa mwaka 2015/2016, sawa na asilimia 25 kati Wakala za Serikali 35 zilizokaguliwa zimeonekana na malipo ambayo hayana nyaraka ya kiasi cha shilingi 508,619,273 kinyume na Kanuni ya 86 (1) na 95 (4) ya Kanuni ya Fedha za Umma 2001 ambayo inahitaji kila malipo kuwa na nyaraka. Hivyo, kuathiri wigo wa ukaguzi. Na kwa sababu hiyo, usahihi wa matumizi ya shilingi 508,619,273 haukuweza kuthibitika.

ii. Ukaguzi Madeni ya Wakala

Kipindi cha mwaka 2015/2016 nilibaini Wakala za Serikali 28 zikiwa na limbikizo la madeni ya kiasi cha shilingi 1,875,266,954,590.27 kukiwa na ongezeko la shilingi 289,804,290,285.27 (18%) ikilinganishwa na deni la 2014/2015 la kiasi cha shilingi 1.585.462.664.305. Zaidi ya

hayo, nilibaini kuwa Tanzania National Road Agency (TANROAD) ina asilimia 95 ya jumla ya madeni yote.

Mwaka 2015/2016 ukaguzi wangu ulibaini SUMA- Idara ya ulinzi wana limbikizo la kodi kiasi cha shilingi 2,679,429,505 ambayo imelimbikizwa tangu 2011 mpaka 2016. Pia 2015/2016 nimebaini Taasisi za Serikali 15 zikiwa na limbikizo la madeni kiasi cha shilingi 14,933,537,786.54. Kati ya madeni hayo, jumla ya shilingi 10,614,191,293.06 (71%) hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12, wakati shilingi 4,319,346,493.48 (29%) hayajalipwa katika kipindi kisichozidi miezi 12.

Uhakiki wa Matumizi ya Magari ya Wakala

Uhakiki wa magari ulibainisha magari 92 ambayo ni mabovu na hayajatumika katika Wakala za Serikali sita; TMA magari 4 (4%), TBA gari 1 (1%), TFSA magari 26 (28%), NIDA magari 52 (57%), TANROADS magari 7 (8%) na ADEM magari 2 (2%). Ambapo, Maafisa Masuuli bado hawajafanya utaratibu wa kuyaondoa kwa mujibu wa Kanuni 254 (1) ya Fedha za Umma 2001.

B. Mapungufu ya Taasisi Mojamoja

i. Ukaguzi ALAT

Matumizi mabaya ya fedha za uwekezaji ALAT shilingi 367,929,276.06

Ukaguzi wa Shirikisho la Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT) umebaini kuwa ALAT ilipokea michango ya shilingi 525,717,522 kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) kwa ajili ya mfuko wa uwekezaji. Hata hivyo, mfuko wa uwekezaji uliokusudiwa haukuanzishwa na fedha zilitumika katika shughuli nyingine, menejimenti ya ALAT ilishindwa kutoa maelezo ya matumizi ya fedha hizo. Aina hii ya uwekezaji ilionekana kuwa matumizi mabaya ya fedha

za umma au matumizi batili; hadi sasa hakuna faida iliyopatikana.

ii) Ukaguzi Mfuko wa Rais wa Kujitegemea

Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji ulipewa mkopo wa kiasi cha shilingi 514,000,000 chini ya Mpango wa Taifa wa Uwezeshaji Kiuchumi (NEEP) mwaka 2007/2008. Nilibaini kuwa, fedha hizo hazikutumika tena kama ilivyokusudiwa tangu 2009/2010; badala yake fedha zilitumika kuwezesha shughuli za utawala kinyume na madhumuni ya awali. Imebainika kwamba marejesho ya fedha hizo hayajafanywa kama ilivyokubaliwa.

iii) Ukaguzi TANZANSINO

Wakati wa Ukaguzi wa 2015/16 tumebaini kuwa shilingi 773,000,875.99 zililipwa na SUMA JKT Makao makuu ikiwa ni sehemu ya malipo ya shilingi 1,292,003,500 kwa ajili ya kununua hisa za Holley, katika Uwekezaji usio na tija wa utengenezaji wa madawa, na mambo yanayohusiana na madawa. SUMA JKT iliingia makubalianao ya ubia wa pamoja na Kiwanda cha Holley, na baadaye, kununua kiwanda kutoka kwa Shanxi Provincial Technical Renovation and equipment Corporation. Ubia huo uliitwa TANZANSINO ambapo mwaka 2007 umiliki wa hisa ulikuwa 55% kwa Holley na 45% kwa SUMA. Kwa bahati mbaya, Biashara katika TANZANSINO ilihitimishwa kwa hiari na wanaubia mwaka 2014.

Nimebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa ubia huo wa TANZANSINO mwaka 2007 mpaka muda wa kuitimisha biashara 2014 hakuna mapato yoyote yaliyopokelewa kulingana na umiliki wa hisa uliokubaliwa.Hivyo haikuwa busara kwa SUMA kununua Uwekezaji usio kuwa na tija.

SUMA JKT ilichukua umiliki mzima katika TANZANSINO bila kuangalia mahitaji ya lazima kama vile Uchambuzi yakinifu, utaalamu wa kiufundi, wafanyakazi, Mchanganuo wa marejeo ya gharama/faida, na uzoefu waliojifunza kutoka kwa mbia aliyejiondoa.

iv) Shirika la Mzinga

Shirika la Mzinga lilishindwa kutoa taarifa ya manunuzi na nyaraka za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa boti ya usalama baharini kwa mkopo wa Euro 32,588,376 (Sh. 79,352,695,560). Kutokana na kukosekana kwa taarifa za manunuzi sikuweza kuthibitisha mchakato wa ununuzi pamoja na mapato ya mkopo katika akaunti ya escrow.

v) Ukaguzi wa TANROADS

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016, ukaguzi wa mikatabauilibainisha kuwa TANROADS ina limbikizo la riba lililofikia kiasi cha shilingi 7,874,921,250.36 na USD 714,066.08 kutokana na kuchelewasha malipo kwa wakandarasi ya kiasi cha shilingi 36,766,426,168.68 na USD 6,534,720.75

Mwaka 2015/2016 TANROADS haikulipa madai ya makandarasi na washauri kiasi cha shilingi 20,270,965,854.88. Kushindwa kulipa madai katika mwaka husika huathiri vibaya mipango ya miaka unayofuata ambayo madeni hayo yatalipwa.

vi) Ukaguzi TBA

Nilibaini manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanywa na TBA kwa kiasi cha shilingi 178,718,071.17 kutoka kwa chanzo kimoja kinyume na utaratibu. Pia, Wakala wa Majengo Tanzania, walinunuliwa vifaa vya ujenzi kiasi cha shilingi 74,139,416 kutoka kwa wauzaji ambao

hawakuwa wamekidhi viwango katika mazingira ambayo hayakuelezwa.

Nilibaini kuwa TBA ilipokea shilingi 500,000,000 kutoka kwa Katibu Mkuu - Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (Idara ya Ujenzi) kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara jijini Dar es Salaam. Baadaye Tanzania Building Agency (TBA) walihamisha shilingi 500,000,000 kwenda kwa Meneja wa TBA Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 5 eneo la Bunju ambapo sio lengo lililokusudiwa. Hata hivyo, hakuna nyaraka zilitolewa kwa wakaguzi ili kuthibitisha kiasi kilichopolewa na taarifa ya matumizi husika kama vile mchakato wa ununuzi.

vii) Ukaguzi RITA

Tathmini niliyofanya juu ya ubia kati ya RITA na NSSF ilibaini kuwa ubia uliokusudiwa haujaanza kutekelezwa na ulipaji mkopo haujaanza wakati riba kwa mkopo inazidi kuongezeka.

viii) Ukaguzi GPSA

Uhakiki wa akaunti ya amana kwa ajili ya ununuzi wa pamoja chini ya Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini (GPSA) nilibaini kuwa akaunti ya manunuzi ya pamoja taarifa zake haziandaliwi ipasavyo.Jumla ya fedha zilizoripotiwa kama amana za taasisi mbali mbali kwenye vitabu vya GPSA ni kiasi cha shilingi 12,161,412,069.06 wakati kiasi cha fedha kilichopo benki ni shilingi 24,351,093,634.89; kuwa na tofauti ya shilingi 12,189,681,566 bila kuwa na usuluhisho wa tofauti hiyo.

Ilibainika kuwa Taasisi zinalipia bidhaa GPSA ambazo hazipo stoo na kusababisha kusubiri bidhaa kwa kipindi cha kati ya siku 24 hadi miezi 3. Mbali na hivyo, uhesabuji mali/bidhaa uliofanywa GPSA makao makuu na

ofisi zake za kikanda ulibaini hifadhi ya bidhaa ambazo zinanunuliwa polepole sana, na ambazo hazifai kwa matumizi za kiasi cha shilingi. 498,240,662. Ukaguzi wangu ulibaini zaidi kuwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya vitabu vya kumbukumbu 3138 (asilimia 40) na kalenda 1263 (asilimia 42) zilibaki bila kununuliwa katika ofisi mbalimbali za kikanda, hivyo, kuchukuliwa kama vitu ambayo vimepitwa na wakati.

ix) Ukaguzi wa REA

Ukaguzi wa mapato ambayo hayajakusanywa kwa mwaka 2015/2016 katika taarifa za Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ulibaini kuwa REA ilifanya malipo yasiyo sahihi ya USD 91,168.48 kwa HIFAB badala ya dola 9,218.48; hivyo, kuwa na malipo zaidi ya USD 81,950

Ilibainika kuwa REA ilishindwa kukusanya kiasi cha shilingi 7,433,600,000 kutoka TANESCO kama malipo ya adhabu yatokanayo na mkusanyiko wa mauzo ya umeme (LUKU) kila mwezi ambayo yalitakiwa kulipwa tangu Mei 2011 licha ya jitihada kadhaa kufanywa na uongozi. Wizara ya Nishati na Madini aliingilia kati suala hilo na hakuna mafanikio.

x) Mapungufu Mfuko wa Mirathi

Pia, nilibaini fedha za mirathi ya kiasi cha shilingi 169,000,000 zilitumika kwa matumizi yasiyohusiana na madhumuni ya mfuko wa mirathi.

xi) Ukaguzi wa SUMA

SUMA - Idara ya Zana za Kilimo iliazima kiasi cha shilingi TZS 5,355,153,000 kwa idara mbalimbali ndani ya SUMA. Kati ya fedha hizo, ni kiasi cha shilingi 534,785,000 zilirudishwa na kuacha kiasi cha shilingi 4,820,368,000. Hakuna maelezo ya kuridhisha yaliyotolewa kwa nini kiasi hicho hakijarudishwa kutoka kwa walengwa.

Mwaka fedha 2015/2016 Shirika la uzalishaji mali la Magereza lilitoa mkopo wa shilingi 280,136,218 kwa Kamishna Mkuu wa Magereza kufadhili shughuli mbalimbali. Fedha hizo zilitolewa katika kipindi tofauti kati ya 07/08/2015 na 20/06/2016. Nilibaini kuwa hadi Januari, 2017 fedha hizo zilikuwa bado hazijarudishwa. Taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba kulikuwa hakuna sera au mamlaka aliyopewa kukopa kutoka kwenye mfuko, na hakuna maelezo yaliyotolewa na menegimenti ni kwa nini bakaa ya shilingi 280,136,218 haijarejeshwa.

xii) Ukaguzi Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi

Ukaguzi wa taarifa za fedha za Mfuko wa Mikopo kwa watumishi ulibaini kuwa shilingi. 1,098,566,332.69 ziliripotiwa kama mikopo ambayo haijarejeshwa. Ukaguzi zaidi ulibaini kuwa fedha hizo zililipwa kwa Fungu 23 na kutumika kwa shuhuli ambazo hazihusiani na malengo ya Mfuko.

xiii) Ukaguzi wa Taasisi Nyingine

Wakati wa ukaguzi wa Wakala na Serikali na Taasisi nyingene nilibaini mapungufu juu ya matumizi ya fedha; hivyo, sikuweza kuhakikisha usahihi na utaratibu wa matumizi haya. Mapungufu niliyoyabaini ni pamoja na: Malipo kutokuwa viambatisho (Sh. 206,521,652), malipo yaliyolipwa bila kuwepo risiti EFDs (Sh. 1,481,679,250), malipo bila ya kukata kodi ya zuio iliyofikia (Sh. 69,443,677) malipo bila kukata kodi ya zuio yaliyofikia (Sh. 36,589,303), matumizi nje ya bajeti iliyopitishwa (Sh. 107,307,565.14), masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu (Sh. 10,575,687.30) pamoja na malipo yaliyofanyika kwenye vifungu tofauti (Sh. 304,116,358.50).

Ukaguzi wa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF)

Taarifa za fedha za Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) zimeonyesha kuwa mfuko ulitoa mikopo ya shilingi 3,342,970,002 (mkopo pamoja na riba) kwa wateja

mbalimbali katika wilaya za mkoa wa Dodoma. Ilibainika kuwa kiasi cha shilingi 1,997,763,380 (60%) ndicho kilichorejeshwa na kuacha kiasi cha shilingi 1,345,206,622 (40%) ambacho hakijarejeshwa licha ya muda wa marejesho kupita.

xiv) Udhaifu katika usimamizi wa Bodi za Mabonde ya Maji

Nimebaini uhaba wa wafanyakazi 457 kwenye Bodi sita za mabonde ya maji katika idara tofauti. Hii ni asilimia 56 ya idadi ya wafanyakazi wanaotakiwa. Aidha, uchambuzi wa taarifa za mishahara zilizotolewa na bonde la maji Rukwa umebaini kuwa kuna maafisa wawili walikuwa wanapata mshahara uliofikia shilingi 20,916,000 wakati wafanyakazi walikuwa hawapo tena kazini. Wakati wa ukaguzi nimebaini udhaifu juu ya matumizi ya fedha; kwa hiyo, sikuweza kuhakikisha usahihi na utaratibu uliotumika kufanya matumizi haya. Hii ni pamoja na: Malipo kutokuwa na viambatisho (Sh. 53,862,324), malipo bila kuwa na risiti za EFD (Sh. 283,408,496), kutokukata kodi ya zuio (Sh. 45,057,351.09) na matumizi yasiyo sahihi (Sh. 12,290,200).

9. Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba

Katika mwaka huu, kwa mara nyingine tena nilibainisha matukio kadhaa ya kutokufuata sheria za manunuzi ya umma katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Mapungufu hayo ni:

a) Ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi 23,980,253,902 bila nukuu za bei angalau tatu kutoka kwa wazabuni.

b) Kuwepo kwa udhaifu katika usimamizi wa mikataba / mradi katika sampuli nane (8) za mikataba / miradi yenye thamani ya shilingi milioni 63,254 milioni na dola milioni 1,000 katika Wizara, Idara nane (8).

c) Wizara / Sekrtarieti za mikoa kumi na nne (14) ziliingia mikataba na makandarasi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya ujenzi.

d) Nilibaini ucheleweshaji katika kukamilika kwa miradi uliogharimu shilingi 23,328,603,706.

e) Wizara, Idara na Wakala za Serikali zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa kiasi cha shilingi 2,485,411,529 bila kuwa na kibali cha bodi ya zabuni.

f) Taasisi kumi (10) zilizokaguliwa zilifanya manunuzi ya ujenzi, bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi 11,253,346,373 & USD 29,606,100 bila ya kuwa na mikataba / makubaliano na wazabuni / makandarasi. Hii ni kinyume na Kanuni ya 10 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013, kumi na nne (14).

g) Wizara, Idara na Wakala za Serikali zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi 7,395,231,560 kutoka kwa wauzaji ambao hawakupitishwa na GPSA, TEMESA na MSD.

h) Katika tathmini yangu ya taratibu za manunuzi katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi nilibaini kuwa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi 980,345,532 ambazo zilikuwa hazimo katika mpango wa manunuzi zilinunuliwa kinyume na taratibu.

i) Taasisi tisa (9) zilinunua bidhaa kwa kiasi cha shilingi 2,315,756,038 bila kukaguliwa na kukubalika kinyume na Kanuni 244 (1) ya PPR 2013 inayozitaka Taasisi zikinunua bidhaa au huduma kukaguliwa na kupimwa ili kuthibitisha iwapo ina viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba.

j) Wizara ya Maji na Umwagiliaji (Fungu 49) iliingia mkataba wenye thamani ya shilingi 491,047, 500 na M / S Bi International Company kwa ajili ya usambazaji wa

mtambo wa Kusafisha maji Gidahababeig-Hanang bila mkataba kupitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kadhalika, Msajili wa Vyama vya Siasa alifanya Ununuzi wa Consultancy Services juu ya utoaji wa Usalama wa Anga, Usalama na Stadi za maisha kwa shilingi 668,000,000.

k) Taasisi nane (8) zilifanya malipo ya shilingi 3,452,112,838 kwa ajili ya bidhaa, kazi na huduma ambazo hazijapokelewa; hivyo, thamani ya fedha haikuweza kuthibitika. Bila kupata huduma iliyolipiwa, fedha iliyotumika inachukuliwa kama imepotea.

l) Nilipitia ripoti ya PPRA na uchambuzi ulionyesha kuwa wastani katika kufuata viwango kwa asilimia 71 ulikuwa na ongezeko la asilimia mbili juu ya wastani wa mwaka jana. Hata hivyo, kiwango kilikuwa chini ya asilimia 78 ambayo ilikuwa lengo lililowekwa na PPRA kwa mwaka wa fedha 2015/16. Wastani wa kufuata viwango kwa Wizara imeongezeka kutoka 69% mpaka 75% ikilinganishwa na matokeo ya mwaka jana. Matokeo ya kina yameonyeshwa katika sura ya tisa katika ripoti hii

10. Mapungufu Yaliyoonekana Katika Matumizi

Kutokana na udhaifu wa nyaraka na udhibiti wa ndani, matumizi yasiyokuwa na nyaraka za vithibitisho yameendelea kuwa tatizo, hasa katika mwaka huu. Baadhi ya Taasisi zilishindwa kuonyesha nyaraka za matumizi ya jumla shilingi 120,408,642,077.

Kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu na nyaraka, usahihi wa matumizi haukuweza kuthibitika. Eneo hili linajumuisha: hati za malipo ambazo hazikuletwa kwa ukaguzi shilingi 91,347,958,833 (75.7%), kutokuwa na nyaraka kamilifu za matumizi shilingi 12,504,745,476 (10.39%), kukosa risiti za kielekitroniki shilingi 7,790,299,407 (6.47%), fedha ambazo hazikutolewa maelezo ya matumizi shilingi 6,575,397,008 (5.46%),

malipo yasiyo na faida 1,445,045,913 (1.20) , madai yaliyokataliwa NHIF shilingi 569,994,807 (0.47%), malipo yasiyo na stakabadhi za kukiri mapokezi shilingi 97,719,677 (0.08%). Pamoja na malipo yaliyolipwa zaidi shilingi 77,480,956 (0.06%). Aidha, kulikuwa na mambo yanayohusiana na masuala ya bajeti, fedha zilizochepushwa na kutumika shilingi 3,830,032,676 kwa shughuli ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyopitishwa shilingi 3,830,036,676, matumizi ya jumla ya shilingi 4,563,915,835 kwenye vifungu vingine bila idhini, matumizi ya kiasi cha shilingi 4,563,915,835 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali ambazo hazikuwa kwenye bajeti, masurufu ambayo hayajarejeshwa kiasi cha shilingi 397,575,730 na mambo ya kutozingatia mahitaji ya kisheria katika Wizara sita (6) ya kuwasilisha kodi ya zuio Mamlaka ya Mapato (TRA) kinyume na kifungu. 83 (1) (b) cha Kodi ya Mapato, 2004 (iliyorekebishwa 2008). Maelezo ya kina yameonyeshwa katika sura ya kumi

11. Usimamizi na Mali na Madeni

Mapungufu katika usimamizi wa mali za kudumu

Ukaguzi wangu ulibani kuwa hakukuwa na uboreshaji katika usimamizi wa Mali za Kudumu katika Wizara na Taasisi za Umma kutokana na udhaifu kadhaa ulibainishwa ikiwa ni pamoja na Regista ya Mali za Kudumu ambayo haijaboreshwa kwenye Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa 69; ucheleweshaji katika kuthaminisha mali za kudumu katika idadi kubwa ya Wizara Idara na Sekretarieti za Mikoa, hivyo, kuwa na mali sisizo na thamani ya ukweli; ukosefu wa Sera ya Mali za Kudumu ambayo itaendana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi usio wa taslim; mfumo wa Mali za Kudumu kwenye epicor haufanyi kazi; ardhi na majengo kutokutenganishwa katika taasisi 69 zilizokaguliwa; magari mabovu 1270 ambayo hayajatengenezwa wala kuuzwa; kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa ardhi za serikali na majengo katika taasisi 11, na vifaa vya stoo ambavyo havikuthibitishwa shilingi12,818,718,047. Udhaifu mwingine ni Mali za Kudumu sizizo na alama za

utambulisho, kama nilivyobainisha katika ripoti yangu ya awali, Serikali haikuchukua hatua za kutosha na kwa wakati kukarabati majengo ya ofisi na makazi katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi. Baadhi ya majengo ni chakavu na yako katika hali mbaya, hazijafanyiwa matengenezo au ukarabati kwa muda mrefu. Pia, serikali inamiliki viwanja katika balozi 10 ambazo havijaendelezwa. Kati ya Balozi 34 , kumi na mbili (12) zilizokaguliwa zilikuwa na majengo 37 chakavu ambayo yanahitaji ukarabati na matengenezo makubwa.

Maelezo ya kina yametolewa katika sura ya kumi na moja ya ripoti hii.

Mapungufu katika usimamizi wa Madeni

Nilibainisha ongezeko kubwa la madeni katika Taasisi 92 la shilingi trilioni 1.979. Hili ni ongezeko la shilingi trilioni 0.536 (37%) ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.443 katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015. Deni lililoripotiwa ni pamoja na kiasi cha shilingi bilioni 19.192 ambazo ni hati za madai za matibabu kwa wagonjwa ambao wamekuwa wakutibiwa katika hospitali za rufaa nchini India. Kama jumla ya shilingi trilioni 1.979 zingelipwa katika mwaka wa fedha uliokaguliwa na matumizi kuripotiwa 2015/2016, baadhi ya Taasisi zingekuwa na matumizi ya ziada dhidi ya matumizi ya kawaida.

Nilibainisha kesi za kisheria zikiwa na jumla ya shilingi bilioni 850.740 kwenye Taasisi 15 zilizokaguliwa zinazosubiri uamuzi wa mahakama dhidi ya makampuni mbalimbali na watu binafsi. Baadhi ya kesi zimekaa zaidi ya miaka 10, na hakuna taarifa kutoka mahakamani juu ya tarehe ya kusikilizwa. Maelezo ya kina yameonyeshwa kwenye Sura ya kumi na moja ya ripoti hii.

12. Kaguzi Maalum Na Ukaguzi Wa Vyama Vya Siasa

Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Nilibaini uandaaji duni wa vitabu vya msingi vya fedha kama vile mizania ya majaribio, vitabu vya fedha taslimu, vitabu vya kila akaunti na vitabu vikuu ambavyo hutoa taarifa za kuaminika wakati wa uandaaji wa Taarifa za fedha. Hivyo, taarifa nyingi za fedha hazikuwa na nyaraka. Jambo hili linapunguza taratibu za hatua za ukaguzi, usahihi, uwazi na kuaminika kwa taarifa.

i. Ni dhahiri kwamba kuna mapungufu na utunzaji duni wa nyaraka za fedha katika Vyama vingi vya Siasa. Taarifa nyingi za fedha zilikuwa na misingi na miundo ya uandaaji wa Hesabu inayotofautiana. Miundo na muda wa kuandaa Hesabu vinatofautiana na havioneshi taarifa muhimu kuhusu misingi ya uandaaji wa wa taarifa za fedha. Pia, kukosekana kwa sera za fedha na maelezo ya ziada ya taarifa za fedha kulizuia mawanda ya ukaguzi

ii. Vyama vinne (4) vyenye usajili wa kudumu kati ya kumi na tisa (19) vilivyokaguliwa havikuwasilisha taarifa za fedha za kila mwaka kama inavyotakiwa na kifungu cha 14(1)(i) cha Sheria Na.5 ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992 (Iliyorejewa 2015). Vyama hivyo ni National Reconstruction Party (NRA), United People's Democratic Party (UPDP)), Party for People's Redemption (CHAUMMA) na Union for Multiparty Democracy (UMD).

iii. Kuhusu usimamizi wa rasilimli watu na mishahara, nimebaini kuwa mbali na Makatibu Wakuu wanajitolea, waajiriwa wengi wa Vyama vya Siasa hawana mikataba yenye nguvu za kisheria zinazoeleza majukumu, uwajibikaji na malipo.

iv. Udhibiti wa ndani unaohusiana na usululisho wa salio la vitabu vya fedha taslimu na taarifa za benki haukutekelezwa kwa ufasaha. Taarifa za fedha zilizoandaliwa na Vyama vya Siasa zilikuwa

zinapotosha. Licha ya hayo, Vyama vitatu havikuwa na akaunti za benki.

Kaguzi Maalum

Kaguzi Maalum zilizofanyika mwaka huu wa fedha ni mbili (2) ambazo ni:

i. Ukaguzi maalumu wa Mamlaka ya Vitabulisho vya Taifa

Ukaguzi umejiridhisha kwamba uongozi wafanyakazi na watoa huduma na wazabuni wameshiriki kwa namna moja au nyingine katika ubadhirifu na udanganyifu kwenye matumizi ya fedha katika mradi wa kuboredha Vitambulisho vya Taifa. Mradi huu unajumuisha mikataba ya manunuzi ya vifaa vya kuboresha Vitambulisho vya taifa, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kama vile ipad, programu na Vifaa vya kompyuta, upatikanaji wa vibarua, bima za magari na gharama za kusafirisha na kufunga vifaa vya kusajili raia ambapo, shilingi bilioni 4.5 zilikuwa na udanganyifu

Zaidi ya hayo, kutokana na hali ya usajili na kutoa vitambulisho vya taifa kuwa mpya, hali hiyo ilisababishwa na maandalizi hafifu kwa uongozi wa Mamlaka juu ya kuamua jinsi mfumo ambao ungeweza kutumika vizuri kulingana na uwezo wa Mamlaka.

Hali hiyo ilisababisha mabadiliko ya maelekezo yaliyoigharimu Serikali kupitia manunuzi yasiyo na tija na wakati huo huo wadanganyifu kutumia mianya iliyopo kujinufaisha wenyewe kinyume na taratibu.

ii. Ukaguzi Maalum wa Fedha za Gavi Alliance Kwa Ajili ya Chanjo ya Surua Rubella

Kutokana na ukaguzi maalum, udhaifu mkubwa ulionekana katika mfumo wa udhibiti wa ndani. Udanganyifu na viashiria vya rushwa katika maeneo ya manunuzi, masurufu, matumizi ya fedha na uendeshaji wa ruzuku

kwa jumla. Ilibainika wakati wa ukaguzi maalum kwamba memoranda ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na GAVI Alliance ilikiukwa kwa sababu msaada huo kwa ajili ya chanjo haukuwekwa kwenye Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF). Pia, haukufuata taratibu za Serikali za kuhamisha fedha kupitia hazina ndogo na baadaye kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA). Mapungufu mengine ni pamoja na: fedha ambazo hatukuweza kufahamu matumizi yake kiasi cha shilingi 2,153,289,221; Kiasi cha shilingi 1,077,167,188 zilizotumwa Serikali za Mitaa hazikuthibitishwa kupokelewa; ununuzi wa mafuta kwa ulaghai kiasi cha shilingi 248,034,893. Mafuta haya hayakuthibitika matumizi yake katika leja ya stoo shilingi 372,398,769; malipo ya shilingi 1,192,493,345 yaliyofanywa kwa halmashauri 54 na hospitali za mikoa 11 kwa ajili ya shughuli mbalimbali hayakuwa na nyaraka za kuthibisha uhalali wake. Kiasi cha shilingi 497,182,500 kilitumika kwa ajili ya mafunzo ya Surua Rubella bila kuwa na nyaraka za kuthibitisha hilo, matumizi ya shilingi 316,292,995 kwa ajili ya chakula yalikuwa na nyaraka za kughushi, timu ya ukaguzi haikuweza kuthibitisha ukarabati na matengenezo ya magari kiasi cha shilingi 137,743,754. Maelezo zaidi yanapatikana katika sura ya kumi na mbili

13. Mapendekezo ya jumla

Mapendekezo mengi yako katika hatua za utekelezaji au hayajatekelezwa kabisa na kusababisha kujirudia kwa hoja za ukaguzi. Hali hii inaashiria kwamba mapendekezo yangu na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali hayapewi umuhimu unaostahili na Maafisa Masuuli husika. Kwa hiyo Mlipaji Mkuu wa Serikali anashauriwa kuendelea kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli kuchukua hatua za muhimu kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani amabayo imekuwa chanzo kikuu kinachochangia kuchelewa kutekeleza mapendekezo yangu na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali.

Pia, Maafisa masuuli wanashauriwa kuandaa mpango kazi wa kutoa mwongozo juu ya utekelezaji wa mapendekezo

ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali. Mpango kazi huo huonesha muda, nani na namna mapendekezo yatatekelezwa

Nashauri Serikali kutumia vyanzo mbadala vya mapato ya ndani na kuendelea kuziba mianya ya kukwepa kodi. Serikali kupitia Mamlaka zake za kinidhamu wachukue hatua juu ya waajiriwa wasio na maadili pamoja na kuboresha udhibiti wa ndani juu ya mifumo ya kulipia kodi ambao ungerahisisha Miamala wakati wa kulipa kodi kwa hiari.

Pia, kuhakikisha ufanisi wa kutumia mifumo na vifaa vya kielektroniki katika kukusanya mapato ili kuongeza tija na kupunguza hasara ya mapato.

Udhibiti wa ziada na uhamasishaji juu ya kutumia vifaa vya kielektroniki unapaswa kuanza, kwani wachache wanatumia na wengine hawataki kutumiavifaa vya kielektroniki kwa sababu ya matatizo ya mtandao

Maafisa Masuuli wana jukumu la kuandaa mifumo makini ya udhibiti wa ndani ili kusimamia uendeshaji na kuchukua hatua za kurekebisha matatizo. Huu ni mchakato endelevu unaolenga kuimarisha udhibiti wa ndani kwa lengo la kuboresha utoaji wa Huduma kwa umma.

Deni la Taifa

Kwa kuzingatia hayo ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali; (i) Kupunguza kukopa mikopo yenye,

(ii) kuharakisha utoaji dhamana isiyo ya fedha kwa mifuko ya pensheni ili kuwezesha madeni yake kuingia katika kasma ya deni la taifa,

(iii) kufuata Mpango wa Ukopaji wa Ndani inapokopa ndani ya nchi,

(iv) kuimarisha taratibu na usimamizi wa fedha ili kuepuka gharama za riba zisizo za lazima kutokana na overdraft, (v) Kuhakikisha Sera ya usimamizi wa Deni la Taifa inakuwepo na kutekelezwa,

(vi) Kuharakisha marekebisho ya sheria ya Mikopo, Dhamana, na Misaada ya mwaka 1974 (ilivyorekebishwa 2004) na kanuni zake za 2003 ili kukabiliana na changamoto za sasa za usimamizi wa deni la Taifa, na

(vii) kuanzisha ofisi moja inayoshugulika na usimamizi wa deni la taifa hivyo kuzileta pamoja shughuli hizo.

Mamlaka ya mapato Tanzania

Naishauri Serikali (a) kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 15.26 kutokana na matumizi mabaya ya misamaha ya kodi kinyume na sheria kama ilivyoainishwa hapo juu. (b) Kuimarisha usimamizi wa matumizi ya misamaha ya kodi inayotolewa kwa mujibu wa sheria ili kuepusha upotevu wa mapato kwa Serikali.

Nashauri Serikali iendelee kuhimiza matumizi ya EFD Mashine hasa kwa kuhakikisha wahusika wananunua au kupewa na kutumia mashine hizo kama kifungu cha 36 cha sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2015 na kanuni za EFD zinavyoamuru.

Nashauri Serikali kuimarisha mifumo yake na kuchukua hatua stahiki katika ukusanyaji wa kodi zilizofanyiwa tathmini hususani kwa wadaiwa sugu ikiwemo kutoza faini na kuweka riba katika ucheleweshaji wa malipo.

Wakala, Mifuko, Taasisi nyingine na Bodi za Maji

Imebainika kuwa mapungufu mengi yanafanana na hoja za ukaguzi za miaka ya nyuma hali inayoashiria kuwa mapendekezo yetu hayapewi umuhimu unaostaili na Maafisa Masuuli, Maofisa Wakuu na uongozi mzima. Usimamizi wa Wakala, Mifuko, Taasisi nyingine pamoja na

Bodi za Maji wahakikishe wana utunzaji sahihi wa nyaraka na uzingatiaji wa sheria.

Nimebaini kuwa baadhi ya Taasisi zilichepusha fedha na kuzitumia kwenye shughuli nyingine zisizohusiana na Wakala, Mifuko, Taasisi nyingine au Bodi za Maji kiasi kwamba fedha hizo zilikosa uwajibikaji. Kwa sababu hiyo Maafisa Masuuli wa Shirikisho za Serikali za Mitaa(ALAT), Mfuko wa Rais wa Udhamini, Wakala wa Majengo Tanzania, SUMA-Zana za Kilimo, Shirika la Uzalishaji mali la Magereza, Mfuko wa Mikopo Hazina wanapaswa kuwajibika kwa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Nawasihi Maafisa Masuuli kusimamia mara kwa mara viatarishi vya fedha kwenye madeni kwa kutenga bajeti toshelezi. Menjimenti za Wakala, Mifuko, Taasisi nyingine, na Bodi za Maji kwa kushirikiana na Wizara husika kutoa fedha kwa wakati kulipia madeni yaliyoiva.

Nashauri Wakala wa Serikali kufanya ufuatiliaji wa Wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hawazingatii matakwa ya sheria ya kutumia mashine za kutoa risisi za kielektoniki (EFD) na kuanza mara moja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wakwepaji

Mapungufu katika Manunuzi

Nashauri tena uongozi wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretariati za Mikoa zilizokaguliwa kuhakikisha unatii kikamilifu matakwa ya sheria ya manunuzi, hasa katika eneo la uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa mwaka wa Manunuzi, manunuzi yaliyoidhinishwa na Bodi ya Zabuni, ukaguzi na upokeaji wa bidhaa/Huduma na kufanya manunuzi kutoka kwa Wazabuni walioidhinishwa.

Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa wahakikishe vitengo vya manunuzi na Bodi za Zabuni zinaundwa vizuri na kutimiza wajibu wao kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake.

Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, itenge fedha za kutosha kulipia miradi ambayo haijakamilika ambayo ucheleweshaji wake ulitokana na uhaba wa fedha.

Serikali itekeleze miradi mikubwa kwa awamu ili kuepusha ongezeko la gharama kutokana na riba na adhabu zilizosababishwa na ucheleweshaji wa kulipa hati za wakandarasi.

Serikali iiongezee uwezo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutoa rasilimali watu na fedha ili kuiwezesha kupitia vizuri manunuzi yote na mikataba kabla haijasainiwa. Ofisi itawajibika kuhakikisha mikataba ilalinda maslahi ya umma na ofisa yoyote atakayehusika kupitia mikataba atawajibishwa kwa mikataba yote isiyo na maslai kwa umma.

Serikali, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, itoe semina mbalimbali kwa lengo la kuziongezea uwezo Idara za Usimamizi wa Manunuzi juu ya umuhimu wa kuzingatia Sheria za manunuzi na kanuni zake.

Ni muhimu pia kuwa na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Manunuzi wenye ufanisi katika uendeshaji. Mfumo huu unamilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma.Mamlaka ya manunuzi ya Umma ihakikishe kuna utumiji fariki wa mfumo ili Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa ziweze kutumia mfumo kirahisi ili kuboresha taratibu za manunuzi

Mapungufu katika Usimamizi wa Matumizi

Nasisitiza uwepo wa uwezeshwaji imara wa fedha katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali. Msisitizo wangu bado upo kwenye mapungufu ya mfumo wa udhibiti wa ndani mambo ya bajeti na mifumo ya uandaaji wa nyaraka. Nawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha malipo yote yanaidhinishwa na mamlaka stahiki nna vidhibitisho vya nyaraka viendane na kanuni ya 86 na 95(4) ya kanuni za fedha za umma za mwaka 2001. Mifumo ya ndani kama vile ukaguzi wa awali unapaswa kuimarishwa. Nyaraka

zote zikiwemo hati za malipo zenye vidhibitisho ambazo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zitafutwe na kuwasilishwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Usimamizi wa Mali na Madeni

Kama nilivyopendekeza kwenye ripoti zangu za nyuma juu ya kasi ndogo ya utekelezaji ratiba kuelekea kutambua Mali, Mitambo na Vifaa na kuandaa Hesabu kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma Usio fuata msingi taslimu kwa mantiki ya kufanya tathimini, kuboresha rejista ya mali, kuandaa sera za uhasibu. Naendelea kupendekeza Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kuboresha na kutekeleza mbinu za usimamizi kuhakikisha Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za mikoa yote wanatekeleza maelekezo yaliyotolewa.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali afanye kazi kwa ukaribu na Wadau wengine ili kuongeza utekelezaji wa mpango kazi kwa ajili ya uzingatiaji mzuri wa IPSAS 17 na kufanya marekebisho muhimu kwenye taarifa za fedha kwa kutenganisha Ardhi na Majengo katika makundi tofauti

Zaidi ya hayo, Naishauri Serikali kuhakikisha Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa kupata hati za umiliki ili kulinda mali za Serikali. Licha ya hiyo, Naishauri pia Serikali kuchukua hatua za kuuza magari mabovu sana kulingana na sheria na kanuni ili kuokoa thamani ya Uchakavu inayoweza kupatikana kutokana na mauzo. Hatua kali zinapaswa kuwepo ili kupunguza madeni na madai ya muda mrefu kwa kuweka sera kali za mikopo/madai na kuongeza taratibu za kufuatilia ili kuhakikisha kiasi kinalipwa ndani ya muda mfupi kwa kadri itakavyowezekana.

Kuhusu nyumba na viwanja vilivyoko nje ya nchi, napendekeza kuundwa kwa kikosi kazi kati ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Mambo ya nje kushughulikia mambo yote ya majukumu ya

uendelezaji wa majengo na viwanja na kuwekwa chini ya kitengo cha usimamizi wa ardhi na majengo nje ya nchi.

Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Kuhusiana na ufanano wa uandaaji wa Hesabu, nasihi Wizara ya Fedha na Mipango (Mhasibu Mkuu) kwa kushirikiana na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi kutunga sheria itakayosimamia namna rasilimali watu, utunzaji wa vitabu vya fedha za Vyama vya Siasa na kuanzisha kanuni za kutambua mapato yao, matumizi, madeni na vyanzo vya fedha

Namsihi Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa na programu ya kujenga uwezo utakaowezesha Vyama vya Siasa kuzingatia matakwa ya Sheria Na.5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2009 (Iliyorejewa 2015) pamoja na kanuni zake.

Ukaguzi maalumu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

Kama ilivyobainika kutokana na hali ya usajili na utoaji wa vitambulisho vya taifa kuwa mpya kulitokana na maandalizi duni ya Uongozi wa Mamlaka katika kuamua namna mifumo ingefanya kazi vizuri na kupelekea kuwepo kwa mabadiliko makubwa juu ya maelekezo yaliyoigharimu Serikali kupitia manunuzi yasiyo na tija na wakati huohuo kwa wadanganyifu kutumia mianya iliyopo kujinufaisha kinyume na taratibu.

Mamlaka za upelelezi zichunguze viashiria vya udanganyifu vilivyotambuliwa kama ilivyoelezwa kwenye ukaguzi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika.

Hatua stahiki zichukulie dhidi ya maofisa wa umma walioshindwa kusimamia na kuongoza zoezi la kusajili vitambulisho vya Taifa kwa Raia wa Tanzania.

Mfumo wa udhibiti wa ndani uimarishwe ili kuhakikisha kuwa malipo ya huduma yanafanyika tu pale huduma inapokuwa imetolewa. Pia, hatua za kinidhamu na za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika waliotajwa kufanya

marejesho ya matumizi kwa kutumia nyaraka za wazabuni za kughushi na kiasi cha fedha kilicholipwa kwa huduma isiyotolewa kirejeshwe na wahusika waliotajwa.

.

SURA YA KWANZA

TAARIFA ZA AWALI

1.0 Utangulizi

Taarifa hii inaelezea ukaguzi wa Serikali Kuu uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2015/16 ikitoa uhakika usiotiliwa shaka kwa watumiaji wake jinsi Serikali ilivyowajibika katika kutumia rasilimali zake.

1.0 Misingi Ya Kisheria Kwa Ajili Ya Maandalizi,Uwasilishaji Na Ukaguzi Wa Taarifa Za Fedha

1.0.1 Maandalizi Na Uwasilishaji wa Taarifa Za Fedha

Kifungu Na.25(2) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004) na Kanuni ya 71 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inamtaka Afisa Masuuli kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha husika.

1.0.2 Misingi ya Maandalizi ya Taarifa za Fedha

Fungu Na.7 la Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004) inamtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kutoa miongozo itakayotoa misingi ya kihasibu na mifumo itakayotumika wakati wa kuandaa taarifa za fedha. Kifungu 25(4) la Sheria hiyo hiyo linahitaji taarifa zote za fedha zinazowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ziwe zimeandaliwa kwa kuzingatia misingi ya kihasibu inayokubalika na kwa kuzingatia maelekezo yaliyoidhinishwa na Katibu Mkuu na kutolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali yakielekeza misingi ya uandaaji wa taarifa za fedha na kutambua kama kuna ukiukwaji mkubwa kutoka kwenye maelekezo hayo na sababu zilizopelekea ukiukwaji huo..Serikali Kuu iliamua kutumia

Viwango vya Kimataifa vya misingi isiyo ya Taslimu katika uandaaji wa taarifa zake za fedha toka mwaka 2012 na kuandaa taarifa zake za kwanza fedha kwa kutumia viwango hivyo mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Hata hivyo kwa kuwa viwango hivyo vinatoa mwanya kwa mtumiaji wa mara ya kwanza kuweza kuitumia kwa ukamilifu, Serikali Kuu imeamua kutumia mwanya huo ambapo itaanza kutumika kwa ukamilifu wake ifikapo mwaka wa fedha 2016/2017.

Hata hivyo, Serikali inakabiliwa na changamoto kwenye kutengeneza Sera za Kihasibu sambamba na mahitaji ya Viwango vya Kimataifa visivyo vya Misingi ya Taslimu ikitilia maanani sheria mbalimbali na kanuni zinazoonekana kutofautiana na viwango hivyo vya Kimataifa.

Pia, ili kuhakikisha kuwa maandalizi ya Hesabu Jumuifu za Serikali yanafikiwa, Wizara ya Fedha ilitoa nyaraka mbalimbali, ambapo miongoni mwazo ni pamoja na maelekezo kwa mashirika ya umma ambayo mwaka wake wa fedha ulikuwa tofauti na mwaka wa fedha wa Serikali kubadilisha ili ufanane na mwaka wa fedha wa Serikali (Kuanzia Julai 1 hadi Juni 30) na kwa Serikali za Mitaa kubadilisha jinsi walivyokuwa wanatengeneza taarifa ya mtiririko wa fedha Taslimu (*Cash flow statements*) kutoka njia isiyokuwa ya moja kwa moja (*indirect method*) kwenda njia ya moja kwa moja (*direct method*).

1.0.3 Maendeleo ya Kihasibu

Matamko ya Kihasibu na matakwa ya Viwango vya Kimataifa katika sekta ya Umma visivyo na Msingi wa Taslimu

Kama sehemu ya Bodi ya Kimataifa inayojihusisha na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma lengo la kuimarisha menejimenti ya fedha za umma na maarifa kupitia

kuongezeka kwa matumizi ya Viwango vya Kimataifa visivyo vya Msingi wa Taslimu ambavyo kwa Serikali Kuu vitatumika kwa ukamilifu wake ifikapo mwaka 2017[1]. Ni muhimu kwa Serikali kuendelea kufuatilia matokeo ya matamko mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na Bodi inayosimamia Viwango vya Kimataifa visivyo vya Msingi wa Taslimu (*International Public Sector Accounting Standard Board's*) katika maeneo yafuatayo:-

i. Kuandaa mwongozo kwa ajili vyombo vya fedha (Financial Instruments) katika Sekta ya Umma zile ambazo hazijawekwa kwenye viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya msingi wa Taslimu 28[2],29[3] na 30[4].

ii. utambua mazingira ambayo baadhi ya matumizi na madeni yanayotokana na maslahi ya kijamii yanaakisiwa katika taarifa za fedha. (*Social Benefits)*

iii. Jinsi ya kujumuisha hesabu za sekta ya umma na viwango vipya kwa ajili ya kupima na kuainisha.

iv. Mahitaji ya kihasibu kuhusiana na mali za kudumu za urithi (*Heritage assets)*.

v. Kurudiwa kwa Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika sekta ya Umma visivyo na msingi ya Taslimu namba 25 (IPSAS 25) ili iweze kuendana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu namba 19 (IAS 19)[5].

Kufuatia kuandikwa kwa Viwango vipya vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma visivyo vya msingi ya Taslimu

[1] Kumalizika kwa kipindi cha mpito
[2] Jinsi ya kuwasilisha 'vyombo vya fedha kwenye taarifa za fedha
[3] Jinsi ya kupima na kutambua vyombo vya fedha kwenye taarifa za fedha

[4] Maslahi ya Wafanyakazi/watumishi
[5] Maslahi ya Wafanyakazi/watumishi

na bodi inayosimamia viwango hivyo Januari 2015 vikiwamo Na.34,35,36,37 na 38[6] ambavyo vimeanza kutumika rasmi baada ya Januari 2017, Serikali inatakiwa kuweka maandalizi yote muhimu ya jinsi ya kuvitumia baada ya kupitishwa.

1.0.4 Ukaguzi wa Taarifa za Fedha

Mamlaka ya Kisheria na msingi wa ukaguzi

Mamlaka ya kisheria ya kukagua taarifa za fedha za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na haki ya kupitia nyaraka zote za Serikali bila kuwapo kwa pingamizi na uhuru wa Ofisi ya Ukaguzi yametajwa katika ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ikafanyiwa marekebisho mwaka 2005) na Kifungu Na.5 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupeleka kwa Rais kila taarifa kufuatana na kifungu kidogo cha 2 cha ibara hii. Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inaelezea zaidi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais Taarifa ya Jumla ya Ukaguzi ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka ambayo itapelekwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitia kwa Waziri mweye dhamana (Waziri wa Fedha na Mipango).

Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya ukaguzi ni kuweza kutoa maoni huru ya ukaguzi kwamba taarifa za fedha kwa ujumla wake hazikuwa na makosa makubwa ambayo yanatokana na udanganyifu au kulikuwa na makosa wakati wa maandalizi na iwapo

[6] Taarifa za fedha za kila taasisi, Taarifa Jumuifu za fedha, uwekezaji katika washirika na ubia, taratibu za ubia na kutoa taarifa ya maslahi katika vyombo vingine kwa mtiririko huo.

ziliandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya uhasibu visivyo vya Misingi ya Taslimu pia iwapo Sheria nyingine pamoja na Kanuni zake zinazohitaji kutumika wakati wa kuandaa hesabu zimefuatwa.

Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi huu unajumuisha taarifa za fedha[7] za Serikali Kuu na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Taratibu zilizotumika ni pamoja na kupanga ukaguzi ili kutambua na kutathimini viashiria hatarishi iwapo vinatokana na udanganyifu au makosa kwa kuzingatia uelewa wa taasisi inayokaguliwa na mazingira yake pamoja na tathmini ya udhibiti wa ndani. Kupata vielelezo stahiki na ushahidi wa ukaguzi ulio sahihi na unaojitosheleza juu ya usahihi au kukosekana kwa taarifa muhimu katika kutathimini viashiria hatarishi. Kutoa maoni huru ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha kwa kuzingatia hitimisho la ushahidi wa ukaguzi uliopatikana

Inajumuisha pia kufanyia tathmini kama sera za kihasibu zilizopo zinafaa kwa matumizi pamoja na uhalisia wa makadirio yanayotumiwa na menejimenti wakati wa kuandaa taarifa za fedha na muonekano wa jumla wa taarifa za fedha. Hivyo basi, kwenye kila taasisi, ukaguzi wa taarifa za fedha ulifanyika kwa kutumia sampuli, na hoja za ukaguzi zilizopatikana zinatokana na sampuli hiyo iliyofanyiwa kazi ikiwa ni nyaraka za ukaguzi pamoja na taarifa nyingine mbalimbali nilizopitia.

[7] Taarifa ya mizania; Taarifa ya utendaji wa kifedha; Taarifa kuhusu mabadiliko ya mali; taarifa ya Mtiririko wa fedha Taslimu; Taarifa ya uwiano wa bajeti na kiasi halisi na maelezo mengine yaliyotumika wakati wa kuaandaa taarifa za fedha ikihusisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu na maelezo mengine

Hata hivyo kutokana na kupunguzwa kwa bajeti katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilikumbana na changamoto nyingi kutokana na kiasi cha bajeti kilichopunguzwa kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yangu ya Kikatiba. Kutokana na hili, ofisi yangu haikuweza kufanya kazi zote ambazo zilipangwa kufanyika kwa mwaka 2016/17 kama zilivyo katika mpango kazi. Mbali na hayo ofisi yangu imepata mgawo wa fedha kwa kuchelewa. Jambo hili lilikwamisha pia utekelezaji wa kazi za ukaguzi. Hali hii ilinizuia kufanya kazi zangu kama zilivyo katika jedwali hapa chini:-

Jedwali 1: Mchanganuo wa Taasisi zilizokaguliwa na zisizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2015/16

Mgawanyo wa Taasisi inayotoa taarifa	Jumla ya Taasisi zilizotakiwa kukaguliwa	Jumla ya Taasisi zilizokaguliwa	Sababu ya kutokaguliwa
Wizara/ Fungu	62	62	Zimekaguliwa zote
Wakala wa Serikali	37	33	Wakala wawili walikaguliwa na kutolewa taarifa zake kupitia Taarifa ya Jumla ya Mashirika ya Umma[8]. Wakala mmoja (1) (Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa) hakukaguliwa kutokana na ukosefu wa fedha. Wakala mmoja hakuleta hesabu zake kwa ajili ya ukaguzi[9]
Taasisi Nyinginezo	41	35	Taasisi nyingine nne hazikukaguliwa kutokana na ukosefu wa fedha[10] Taasisi nyingine moja (ALAT) haikuleta taarifa zake kwa ajili ya ukaguzi Taasisi moja mwaka wake wa fedha uliishia Disemba[11]

[8] Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Chakula na Dawa
[9] Mamlaka ya kuendeleza mji wa Kigamboni
[10] Taasisi ya Menejimenti ya Misitu (Olomomyi), Taasisi ya Menejiment ya Viwanda na Misitu (Moshi), Shule ya Sekondari Jitegemee na Taasisi ya utunzaji wa nyuki

Mgawanyo wa Taasisi inayotoa taarifa	Jumla ya Taasisi zilizotakiwa kukaguliwa	Jumla ya Taasisi zilizokaguliwa	Sababu ya kutokaguliwa
Balozi	34	34	Zimekaguliwa zote
Mifuko	19	17	Mfuko mmoja[12] ukaguzi bado unaendelea kutokana na kuchelewa kwa mapokezi ya fedha na Mifuko miwili[13] haikukaguliwa kabisa
Sekretarieti za Mikoa	26	25	Sekretarieti moja mkoa wa Songwe ilianza Juni 2016 kwa hiyo haikuwa sehemu ya ukaguzi huu
Bodi za Mabonde ya Maji	9	9	Zimekaguliwa zote
Mamlaka za Maji safi na maji taka za Taifa	4	4	Zimekaguliwa zote
Hesabu Jumuifu za Taifa	1	1	Zimekaguliwa zote
Vyama vya Siasa	19	14	Vyama vinne[14] vya siasa havikuleta taarifa zake kwa ajili ya ukaguzi. Chama kimoja (CHADEMA) hakikukaguliwa kutokana na ukosefu wa fedha
Mamlaka ya Mapato Tanzania	4	4	Zimekaguliwa zote
Jumla ndogo	**256**	**238**	
Mengineyo			
Kaguzi maalumu	16	1	Ukosefu wa fedha
Jumla KUU	**272**	**239**	

[11] Muungano wa Jumuiya ya Madola
[12] Mfuko wa Bodi ya barabara
[13] Mfuko wa kuzalisha na kukuza mbegu na Mfuko wa kukuza elimu na huduma za afya
[14] NCCR Mageuzi, NRA, UPDP & CHAUMA

Hali hii pia ilipelekea kuchelewa kufanyika kwa baadhi ya kazi nyingine kwa wakati uliopangwa wakati kazi nyingine hazikufanyika kabisa kama zinavyoonekana katika ***kiambatisho 1.1***

Kupunguza bajeti bila kutilia maanani mahitaji ya fedha ya ofisi yangu imenifanya nikakosa uwezo wa kufanya kazi zangu kama nilivyopanga na kutofikia malengo niliyokuwa nimejiwekea. Nashauri Serikali kutoa rasilimali fedha kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kulingana na mahitaji kama yalivyoidhinishwa katika bajeti na fedha zitolewe kwa wakati

Viwango vya Ukaguzi vilivyotumika

Kifungu cha 18 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa kutimiza majukumu yake kuamua viwango vya ukaguzi atakavyotumia. Wakati wa kuchagua viwango hivyo ataongozwa na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi au viwango vingine kama itakavyoonekana sawa.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika (AFROSAI), na Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika – Nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E). Ushirikiano na Taasisi nyingine kuu za Ukaguzi (SAI)

imewezesha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kuwa na eneo kubwa la kujifunza na kubadilishana uzoefu na utaalamu wa ukaguzi katika sekta ya umma.

Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI) hutoa viwango vya ukaguzi vinavyoendana na Sekta ya Umma ikiwa na maana ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Asasi Kuu ya Ukaguzi. Kama mwanachama wa Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatakiwa kutumia viwango hivyo.

Hivyo basi, ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Asasi Kuu za Ukaguzi. Matakwa ya viwango hivi ni pamoja na kuhakikisha kuwa nazingatia mahitaji ya maadili kupanga na kufanya ukaguzi ili kuweza kutoa maoni yangu ya ukaguzi pasi na shaka kuwa taarifa za fedha hazikuwa na makosa ya udanganyifu au ya kawaida na zilitengenezwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vinavyokubalika katika kuandaa taarifa za fedha..

HATI ZA UKAGUZI

2.1 Utangulizi

Kama ilivyoelezwa kwenye Sura zilizotangulia, Kaguzi zetu zinafanyika kwa muujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma (ISSAIs). ISSAI 1200 inawataka Wakaguzi kutoa maoni huru kama Taarifa za Fedha zimeandaliwa kulingana na viwango inayokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

Hii inafanikiwa kwa kubuni ukaguzi katika namna ambayo itawezesha Wakaguzi kupata uhakika kama Taarifa za Fedha kwa ujumla ni huru kutokana na kukosewa au udanganyifu.

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma 1700 na 1705, Mkaguzi anaweza kutoa aina tofauti za Maoni/hati kutegemena na mambo ya yaliyobainika wakati wa Ukaguzi. Kwa hiyo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilifanya tathimini ya chanzo, ukubwa na kuenea kwa makosa katika taarifa ili kuweza kutoa maoni/hati sahihi.

Hivyo, aina ya hati za Ukaguzi na matokeo yake yamezingatiwa ili kuweza kutoa hati za ukaguzi sahihi kama inavyoelezwa hapa chini.

;

Jedwali 2: Aina ya hati za Ukaguzi/Maoni ya Ukaguzi

Hati ya Ukaguzi	Vigezo
Hati inayoridhisha	**Taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuhusisha masuala yote muhimu, kulingana na mifumo ya uandaaji wa taarifa za fedha iliyokubalika kimataifa, [*ISSAI 1700.16]***
Hati yenye shaka	**Hati hii hutolewa;** • **Baada ya mkaguzi kukusanya ushahidi sahihi na wa kutosha na kuhitimisha**

Hati ya Ukaguzi	Vigezo
	taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa lakini siyo muhimu, makosa hayo yakichukuliwa moja moja au kwa ujumla wake kwenye taarifa za fedha, au • **Pale ambapo mkaguzi hakupata nyaraka za kutosha ili niweze kutoa hati ya Ukaguzi, na nimejidhihirisha kuwa madhara yanayoweza kutokea kwenye taarifa za fedha kutokana na makosa ambayo sijaweza kuyagundua kutokana na ukosefu wa nyaraka hizo ni makubwa, lakini sio ya muhimu. [ISSAI 1705.7]**
Hati isiyoridhisha	**Hati hii inatolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, taarifa zilizoandaliwa na kukaguliwa zina makosa makubwa na ya muhimu, likiangaliwa kosa moja moja au kwa ujumla wake *[ISSAI 1705.8]***
Hati Mbaya	**Hati mbaya hutolewa pale ambapo nimeshindwa kupata nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi ili kuweza kutoa hati sahihi na nimejidhihirisha kuwa, madhara yanayoweza kutokea kutokana na mapungufu ambayo sijaweza kuyagundua yanawea yakawa makubwa na ya muhimu sana. Katika hali hii mkaguzi anakataa kutoa hati ya ukaguzi. *[ISSAI 1705.9]***

Mbali na maoni hayo, wakaguzi wanapoona kuwa jambo fulani linapaswa kuwekwa wazi kwenye taarifa za fedha, na kwamba ni la muhimu kwa watumiaji kuelewa taarifa ya fedha wanaweza kufanya hivyo kwa kutumia aya yenye masuala ya msisitizo au aya ya masuala mengine.

Jedwali 3: Vigezo vya Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine

Aya	Vigezo
Masuala ya msisitizo	Aya hujumuishwa wakati mambo yanayoathiri taarifa za fedha yamewasilishwa au kuoneshwa kwenye taarifa za fedha na kwamba ni ya muhimu kwa watumiaji kuelewa taarifa ya fedha *[ISSAI 1706.6]*
Masuala mengine	Endapo kuna mambo zaidi ya yale yaliyowasilishwa au kuoneshwa kwenye taarifa za fedha, lakini kwa mtazamo wa Mkaguzi, anaona ni muhimu kwa watumiaji kuweza kuelewa Majukumu ya ukaguzi au ripoti ya ukaguzi *[ISSAI 1706.8].*

2.2 Matokeo ya Ukaguzi/Hati za Ukaguzi zilizotolewa

2.2.1 Taasisi zilizopata Hati inayoridhisha

Kati ya Taasisi za Serikali Kuu 222 zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2015/16; Taasisi 190 (86%) zilipata Hati inayoridhisha yaani taarifa zilizoandaliwa zinatoa picha halisi ya shughuli zilizofanywa na wakaguliwa. Hii inaonesha kuongezeka kwa asilimia 5% ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba kwa muujibu wa mahitaji ya ISSAI 1700. P3, ukaguzi wetu ulihusisha zaidi ya taarifa za fedha na kujumuisha tathmini ya uzingatiaji wa Sheria na ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani

Hivyo, Taasisi zilizopata Hati zinazoridhisha siyo kwamba Mifumo ya Ndani pamoja uzingatiaji wa Sheria ulikuwa unaridhisha. Mapungufu yaliyobainika katika mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja na uzingatiaji wa sheria yameripotiwa katika Taarifa kwa Menejimenti za Taasisi

husika pamoja na sura mbalimbali za ripoti hii ambazo hazikuathiri moja kwa moja taarifa za fedha za taasisi husika.

2.2.2 Hati zinazoridhisha na aya ya masuala ya msisitizo/aya ya masuala mengine.

Vile vile, nilibaini kuwa kati ya Taasisi zilizopata hati zinazoridhisha hapo juu, Taasisi 22 zilikuwa na aya zenye Masuala ya msisitizo na Taasisi 10 zilikuwa na aya zenye masuala mengine.

Taasisi zenye hati zinazoridhisha, Masuala ya msisitizo/na masuala mengine zimeorodheshwa kwenye **Kiambatisho Na.2-1**

Katika Mwaka huu wa Ukaguzi,hati zinazoridhisha zilitolewa pia kwa Taasisi[15] ambazo taarifa za fedha ni za mwaka 2014/2015 kwa kuwa hazikuingizwa kwenye ripoti ya mwaka uliopita.

2.2.3 Taasisi zilizopata Hati zenye Mashaka

Jumla ya Taasisi 24 (11%) katika mwaka wa fedha 2015/2016 zilipata hati zenye mashaka baada ya Wakaguzi kukusanya ushahidi wa kutosha kuhitimisha kuwa Taarifa za fedha[16] zilizoandaliwa zina makosa makubwa.

Taasisi zenye hati zenye mashaka, masuala ya msisitizo/na masuala mengine zimeorodheshwa kwenye **Kiambatisho Na 2.2.**

Vile vile, Taarifa za fedha za ALAT kwa mwaka Juni, 2012, Juni 2013 and Juni, 2014 zilipokelewa na kukaguliwa katika mwaka huu wa ukaguzi.Taarifa ya mwaka 2014 imepata hati

[15] Bodi ya Mfuko wa Barabara na Shirikisho la Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

[16] Malipo na Mapato makubwa yasiyokuwa na nyaraka za kutosha, kutozingatiwa kwa kiasi kikubwa katika kufuata Sheria, Matumizi na Mapato yasiyoidhinishwa, kutozingatia sheria ya manunuzi, Mali za kudumu na vifaa vya bohari visivyohesabiwa, kushindwa kuandaa orodha ya Mali za kudumu, Matumizi makubwa yaliyolipwa na Serikali bila ya Serikali kupata thamani ya fedha.

yenye mashaka . Pia Taarifa za Fedha za Chama cha TLP kwa mwaka 2014/2015 zilikaguliwa na kupata hati yenye Mashaka. Sababu za msingi zilizofanya Taasisi kupata hati zenye mashaka zimeorodheshwa kwenye Jedwali hapa chini:

Jedwali 4: Taasisi na Msingi wa Hati zenye Shaka.

ALAT [JUNI 2014]
Katika Taarifa ya fedha ya ALAT ya Mwaka Juni, 2014 bakaa ya fedha Taslimu (Cash and Cash Equivalent) ilikuwa ni Sh. 945, 245,359. Hata hivyo mapitio ya bakaa ya daftari la Mapato na Matumizi (Cash book), taarifa za usuluhishi wa kibenki ilibainika kuwa bakaa ilikuwa Sh. 852, 212,958.32 hivyo Bakaa ya fedha Taslimu ilikuwa na tofauti iliyozidi Sh. 93,032,400.68. Kufika tarehe 30/6/2014 Taarifa ya fedha ya ALAT ilikuwa na Wadai wenye thamani ya Sh.600, 411,332. Hata hivyo, mapitio ya taarifa za wadai ilibaini ni Sh. 135,064,846. Hivyo, kusababisha tofauti ya Sh. 465, 346,486 isiyokuwa na vielelezo. Mali za kudumu katika Taarifa za Fedha za ALAT zilikuwa na thamani ya Sh. 314,377,690, Hata hivyo, Daftari la Mali za Kudumu zilikuwa na thamani Sh.25,816,141 kupelekea tofauti ya Sh.288,561,549. Katika bakaa ya fedha Taslimu (Cash and Cash Equivalent) kwenye Taarifa za fedha, kiasi cha Sh.11,300,990 kilishindwa kuthibitishwa wakati wa uhakiki. Fedha Taslimu kiasi cha Sh.101,382,674 kilikusanywa bila ya kupelekwa benki kinyume na Kifungu cha 12(1) cha Sera ya Fedha za ALAT. Hati za Malipo zenye thamani ya Sh.166,067,654 hazikuwa na nyaraka za kutosha. Pia hati za Malipo zenye thamani ya Sh. 229,598,692.67 hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi.

Vile vile Malipo yenye thamani ya Sh.7,657,278 hayakustahili kwa wafanyakazi na hayakuwa na taarifa ya kazi iliyofanyika.

Tanzania Labour Party (TLP) [JUNI 2015]

Katika Taarifa ya fedha, nyumba na majengo yenye thamani ya Sh. 80,000,000 viliwekwa pamoja, badala ya kutenganishwa kama Viwango vya Kimataifa ya uandaaji wa hesabu za umma (aya 74 ya IPAS 17) vinavyoagiza.

TLP hawakutunza vitabu vya uhasibu kama leja za matumizi, daftari la mapato na matumizi na daftari la mali za chama kinyume cha Kifungu cha 14(1)(b) cha Sheria ya vyama vya Siasa.

Kukosekana kwa kumbukumbu hizi kunasababisha uandaaji wa Taarifa za Fedha kukosa vyanzo vya uhakika. Hivyo kufanya ukaguzi wa Taarifa kukosa mtiririko, usahihi, uwazi na taarifa za uhakika.

Ruzuku iliyopokelewa kwenye akaunti ya benki haikuingizwa kwenye vitabu vya fedha.

TLP haikufanya usuluhishi wa kibenki, hivyo kushindwa kuthibitisha bakaa ya fedha kwenye Taarifa ya Fedha.

Chama cha Mapinduzi (CCM)

Chama cha Mapinduzi kiliripoti Mali za Kudumu kwenye Taarifa za Fedha zenye thamani ya Sh. 36,869,775,776. Hata hivyo, hakikuwa na Daftari la Mali za Kudumu. Hivyo kushindwa kuthibitisha ukamilifu wa taarifa za Mali za kudumu. Chama hakikufanya tathimini ya Mali za kudumu(Revaluation). Hivyo, Mali za kudumu kwenye Taarifa za Fedha zenye thamani ya Sh. 36,869,775,776 hazikuwa sahihi.

Chama hakikutenganisha thamani ya Ardhi na thamani ya

Majengo kama viwango vya Kimataifa vya kihasibu vinavyotaka (aya 58 of IAS 16). Hivyo thamani ya Majengo ya kiasi cha Sh.9,809,498,407 yalijumuishwa na thamani ya ardhi ambayo inapanda thamani wakati majengo yanashuka thamani.

Hatukuweza kupata Taarifa za Fedha kuhusu Uwekezaji wa Chama kwenye makampuni mbalimbali; Hivyo, kushindwa kujiridhisha na uwekezaji wenye thamani ya Sh 10,879,571,868 uliyowasilishwa kwenye Taarifa za Fedha.

Katika Taarifa ya Matumizi, nilibaini kiasi cha Sh.32,863,793,631 kilipelekwa kwenye taasisi zilizo chini ya Chama, lakini Taarifa za Matumizi katika Taasisi hizi hazikuweza kupatikana ili kuweza kujiridhisha na matumizi haya.

Matumizi yenye thamani ya Sh. 82,400,000 yalikuwa na nyaraka pungufu, hivyo kushindwa kuthibitisha uhalali wake.

Madai yenye thamani ya Sh. 137,582,752 kutoka CCM Kinondoni hayakuingizwa kwenye Taarifa za fedha, hivyo kusababisha upungufu wa Sh. 137,582,752 kwenye taarifa za fedha.

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa kila Mkaguliwa 2015/16

2.2.4 Taasisi zilizopata hati zisizoridhisha.

Nilitoa hati zisizoridhisha kwa Taasisi[17] 3(1%) kati ya Taasisi 222 zilizokaguliwa.Hii ni baada ya kujidhihirisha kuwa, taarifa zilizoandaliwa na kukaguliwa zina makosa makubwa na ya muhimu[18]. Taasisi zenye hati zisizoridhisha, zimeorodheshwa kwenye jedwali hapa chini:

[17] Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa na Baraza la watoaji wa Tiba Asili na Tiba Mbadala

[18] Vigezo vya utoaji hati ni kama vilivyoelezwa hapo juu lakini umuhimu wake ulizingatiwa

Jina la taasisi na msingi wa hati Zisizoridhisha.
1. Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa
Noti ya 52 ya taarifa za fedha ilionesha mali zilizonunuliwa kwa matumizi ya mwaka husika ambazo hazikutumika (Inventories) zenye thamani ya shilingi 170,354,720. Hata hivyo, bakaa iliyooneshwa katika ripoti ya mali zilizohesabiwa mwishoni mwa mwaka zilionesha kiasi cha shilingi 115,228,295. Hivyo, kuleta tofauti ya kiasi cha shilingi 55,126,425 zaidi ya kiasi halisi kilichokuwepo. Noti ya 90 ya taarifa ya mizania kwa mwaka 2015/16 inaonesha Fedha za Walipakodi (taxpayers funds) kiasi cha shilingi 5,412,721,084; wakati bakaa katika taarifa ya kubadilika kwa mali za kudumu (Statement of changes in net assets) inaonesha kiasi cha shilingi 8,759,427,155; hivyo, kupelekea kuwapo kwa tofauti ya shilingi 3,346,706,071 ambayo haina maelezo. Pia, katika noti hiyo hiyo kuna marekebisho katika fedha za walipa kodi ya kiasi cha shilingi 2,285,952,663 kwa mwaka wa fedha 2015/16 na shilingi 1,956,756,118.25 kwa mwaka 2014/15. Hata hivyo, hakukuwa na jedwali la kusaidia kuelekeza marekebisho hayo. Pia, kulikuwa na marekebisho ya mali za kudumu ya shilingi 200,000,000 yaliyofanyika katika miaka yote 2015/16 na 2014/15 bila kuwepo uthibitisho wa marekebisho hayo. Noti ya 59 ya taarifa za fedha inaonesha vifaa vya kompyuta kama sehemu ya mali za kudumu za ofisi vikiwa na thamani ya shilingi 85,753,632. Hata hivyo, vifaa hivyo vilioneshwa kwenye jedwali la mabadiliko ya mali za kudumu vikiwa na thamani ya shilingi 98,774,932. Hivyo, kupelekea kuwepo kwa tofauti ya shilingi 13,021,300. Kwenye noti hiyo hiyo, kuna magari yameoneshwa yakiwa na thamani ya shilingi 2,802,018,604 wakati kwenye jedwali la mabadiliko ya mali za kudumu yameoneshwa yakiwa na thamani ya shilingi 2,982,018,604 ikapelekea tofauti ya shilingi 180,000,000. Tofauti hizi hazikweza kupata maelezo. Noti 41 ya taarifa za fedha inaonesha kiasi cha fedha za maendeleo kilichotolewa kwa mwaka 2015/16 kilikua shilingi 9,678,829,199. Hata hivyo fedha hizo zimeoneshwa kiasi cha shilingi 13,093,347,094

Jina la taasisi na msingi wa hati Zisizoridhisha.
katika Taarifa ya fedha ya fungu na kusababisha tofauti ya shilingi 3,414,517,895 ambazo hatukupata maelezo yake. Noti 41 pia imeonesha fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa shilingi 91,187,696,056 wakati Taarifa ya Fedha ya Fungu inaonesha kiasi cha shilingi 87,982,332,271 na kusababisha tofauti ya shilingi 3,205,363,784 ambayo hatukupata maelezo yake. Taarifa ya mtiririko wa fedha taslimu (Cash Flow Statements) kwa mwaka wa fedha 2015/16 inaonesha manunuzi ya mali za kudumu za kiasi cha shilingi 3,821,300. Hata hivyo, jedwali la mali za kudumu limeonesha ongezeko la shilingi 333,017,844 katika mwaka wa fedha, hivyo kusababisha tofauti ya shilingi 329,196,545 ambazo hatukupata maelezo yake. Taarifa za fedha za mwaka 2015/16 zinaonesha kiasi cha shilingi 2,721,079,388 zilipokelewa kama fedha za maendeleo. Kati ya hizo shilingi 2,202,821,466 zilikuwa ni kwa ajili ya huduma za afya (VVU/UKIMWI) kutoka kwa PEPFAR (Henry M. Jackson Foundation) kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hata hivyo, fedha hizi hazikuonyeshwa kwenye taarifa za fedha.
2. Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala
Ukaguzi wa taarifa za fedha za baraza kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016 ulionesha kuwa leja kuu (general ledger) ilikuwa na salio ambalo halikuwekwa kwenye taarifa za fedha, hivyo kaikukaguliwa. Hivyo, kiasi cha shilingi 300,545,522 hakikuhakikiwa.
3.Hesabu Jumuifu za Taifa
Kiasi kinachoonesha Ongezeko la mali katika Taarifa za Mtiririko wa Fedha Kwa mujibu wa aya ya 25 (a) ya Muongozo Na.2 wa uaandaaji wa Taarifa za Mtiririko wa Fedha (IPSAS 2), malipo ya fedha yanayohusisha manunuzi ya mali za kudumu zilizoingizwa katika taarifa ya mizania ya mali na madeni yataoneshwa kama fedha zilizotumika kwa ajili ya uwekezaji katika taarifa za mtiririko wa

Jina la taasisi na msingi wa hati Zisizoridhisha.

Fedha. Katika taarifa za maelezo ya ziada zinazoambatanishwa na taarifa za Hesabu (Na. 46, 69, 70, 71), zilionesha ongezeko la mali za kudumu zenye thamani ya Sh. Bilioni 6,306.02 wakati huohuo, taarifa ya mtiririko wa fedha ulionesha kiasi tofauti cha Sh. Bilioni 3,428.5. Hakukuwa na maelezoya ziada yaliyotolewa kuhusu utofauti huu. Utofauti huu na kukosekana kwa maelezo unadhihirisha kuwa taarifa zilizoandaliwa hazikuwa sahihi.

Taarifa za urali zenye vitu ambavyo havijaondolewa Sh. bilioni 2,479.6

Kanuni ya 162 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005 inataka kiasi chochote kilichooneshwa katika taarifa za fedha iliyowekwa benki ilinganishwe na taarifa ya fedha inayoandaliwa ofisini kila ifikapo mwisho wa mwezi. Pia, kipengele cha 25 cha waraka wa uhasibu Na.3 wa mwaka wa fedha 2015/16 unaohusu uandaaji wa Hesabu za kufunga mwaka kinawataka maafisa masuuli na wahasibu wote kuhakikisha urari wa tarrifa hizo unafanyika kila siku. Waraka unawataka pia kuwasiliana mapema iwezekanavyo baina ya CPO, wizara na mkoa pale utofauti unapojitokeza.

Nilibaini taarifa za urari za akaunti za maendeleo, akaunti za matumizi ya kawaida na akaunti za akiba kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2016 zilizowasilishwa na Kitengo cha Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Hesabu za mwaka kilionesha mapungufu katika urari huo unaofikia kiasi cha Sh. Bilioni 2,479.65 ambacho hakilingani hadi siku ya ukaguzi tarehe 15 Machi, 2017. Mapungufu hayo ni kama vile hundi ambazo hazikuwasilishwa benki, mapato yaliyo katika taarifa za ndani ya ofisi hakikuonekana katika taarifa za benki, n.k.Nina mashaka na usahihi wa kiasi cha fedha kilichooneshwa katika hesabu jumuifu za Taifa.

Kukosekana kwa vigezo vya uthaminishaji wa madeni ya Pensheni za Serikali shilingi bilioni 393.5

Aya ya 59 ya IPSAS 25 inaeleza changamoto za kiuhasibu katika kuandaa taarifa ya madeni ya Pensheni kwa sababu unahusisha makadirio ambayo yanaweza kusababisha hasara au faida. Vilevile,

Jina la taasisi na msingi wa hati Zisizoridhisha.
ni makadirio yanayopima thamani ya madeni yatokanayo na malipo yatakayofanyika baadaye baada ya wafanyakazi kumaliza muda wao wa kazi. Ukaguzi wangu wa Hesabu Jumuifu za Taifa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 pamoja na Hesabu moja moja kwa taasisi zinazojumuisha Hesabu Jumuifu za Taifa ulibaini kuwa Serikali inaendeshwa na mafao yaliyokwishwa kupangwa kupitia mifuko ya Hifadhi. Serikali iliripoti kiasi cha Sh. Bilioni 393.5 katika hesabu zake kama madeni yatokanayo na pensheni. Hata hivyo makadirio ya madeni haya hayakufanyika kama inavyohitajika na IPSAS 25. Kukosekana kwa makadirio hayo kunanipa walakini wa Hesabu Jumuifu za Taifa. Kukosekana kwa makadirio hayo pia kunanifanya nishindwe kupima faida au hasara inayoweza kujitokeza. **Mali za kibaiolojia ambazo haziainishwa ipasavyo Sh. Bilioni 122.9** Aya ya 39 na 42 ya IPSAS 27 inazitaka Taasisi kutoa ufafanuzi wa mali za kibaiolojia unaotofautisha kati ya mali za matumizi na mali za matumizi ya muda zaidi ya mara moja au zaidi ya mwaka; na kati ya mali za kibiolojia zilizohifadhiwa kwa ajili ya kuuzwa na zilizohifadhiwa kwa ajili ya kugawanywa bila malipo. Taasisi zinashauriwa pia kutofautisha kati ya mali zilizo tayari na ambazo hazipo tayari kwa matumizi kwa kadri inavyowezekana. Ukaguzi wa Hesabu za Taasisi zinazojumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa ulibaini mali za kibaiolojia zenye thamani ya Sh. Bilioni 122.9 hata hivyo mali hizo hazikuainishwa kwa mujibu wa aya ya 39 ya IPSAS 27. Vigezo vya kuainisha mali za kibailojia havikuandaliwa hivyo kuleta walakini katika usahihi wa Hesabu zilizoandaliwa. **Matumizi ya Hesabu ambazo hazijakaguliwa katika kuandaa Hesabu Jumuifu za Taifa** Ukaguzi wa Hesabu Jumuifu za Taifa kupitia sampuli ya Hesabu

Jina la taasisi na msingi wa hati Zisizoridhisha.
zilizokaguliwa kwa Taasisi zilizojuimuishwa ulibaini utofauti mkubwa. Nilibaini kuwa zoezi la kuandaa Hesabu Jumuifu lilianza kabla ya ukaguzi wa Hesabu za Taasisi zinazojumuishwa kukamilika wakati ambapo hesabu hizo zinafanyiwa marekebisho ya mara kwa mara. Utofauti baina ya Taarifa zilizokaguliwa na Taarifa zilizotumika kuandaa hesabu jumuifu unaleta shaka kuweka imani juu ya usahihi wa Hesabu hizo.

Vile vile, nimetoa hati isiyoridhisha kwa chama cha ACT Wazalendo na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea kwa Taarifa za Fedha za Mwaka 2014/2015 kutokana na vigezo hapa chini.

Jedwali 5: Vigezo/Sababu ya hati isiyoridhisha kwa Chama cha ACT Wazalendo na Mfuko wa Rais wa udham

ACT Wazalendo [MWAKA: JUNI 2015]
Chama cha ACT Wazalendo hakikutunza vitabu vya fedha kama, Vitabu vya Stakabadhi, daftari la fedha, daftari la leja na Daftari la Mali za kudumu kwa ajili ya Taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(10)(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa. Hali hii ilipunguza mawanda ya ukaguzi. ACT Wazalendo ilikusanya mapato ya Sh.498,730,000 kama Michango ya Wanachama lakini ni kiasi cha Sh. 410,295,659 kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha; hivyo, kupelekea upungufu wa Sh.88,434,341 kwenye taarifa za fedha. Mapato yatokanayo na mauzo ya matangazo hayakuingizwa kwenye vitabu vya stakabadhi; lakini taarifa ya fedha ya Mwaka ilikuwa na kiasi cha Sh.2,191,341; hivyo, kusababisha Taarifa kuwa na Makosa. Pamoja na hayo taarifa za fedha zilionyesha kiasi cha Sh.840,000 kama mapato yatokanayo na ada ya uchaguzi lakini vitabu vya stakabadhi viliripoti kiasi cha 1,560,000; hivyo, kusababisha kuwapo kwa pungufu ya Sh.720,000 Mali zenye za thamani ya Sh.11,343,340 zilioneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha taslimu (Cash Flow), lakini hazikuoneshwa kwenye Mizania ya Hesabu (Statement of Financial Position) kwa mwaka unaoishia Juni,2015 ACT Wazalendo kilikuwa na masurufu yasiyorejeshwa yenye thamani ya Sh 210,243,000. Hata hivyo, hayakuoneshwa kwenye taarifa ya fedha ya tarehe 30/6/2015.
2. **Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)**
Mapato yanayotokana na tiba yapo katika mfumo wa taslimu kulingania na sera ya uhasibu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Sera hii inatofautiana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa

katika Sekta ya Umma visivyo vya Msingi wa Taslimu (IPSAS) ambavyo vinataka mapato yatambuliwe hata kabla ya kupokea fedha taslimu. Sikuweza kuhakiki riba iliyokuwa inadaiwa kwa wateja kama riba tegemewa (interest receivable) ambayo ingetakiwa kuonekana kwenye taarifa ya mizania.

Kunaongezeka kwa kiasi cha madeni ambayo hayataweza kulipwa (*Loan impairement*) kiasi cha shilingi 4,115,606,705 ambacho hakikuoneshwa kwenye vitabu. Kiasi cha mikopo ambayo haikutegemewa kulipwa (*provision for bad debts*) ilikuwa shilingi 2,575,527,698 ambacho kilibakia. Hivyo, kwa miaka mitano bila kubadilika. PTF hawakuwa na nyaraka na kumbukumbu za kuweza kuhalalisha kiasi wanachotegemea kukipokea kutoka kwa wadaiwa wao (*receivble*).

Noti ya 16 ya taarifa za fedha ilionesha bakaa la shilingi 230,924,096 kama mali za kudumu za Mfuko. Hata hivyo, thamani iliyooneshwa kama samani za ofisi ni shilingi 79,722,530 ambapo samani zenye thamani ya shilingi 27,849,755 ziko kwenye hali mbaya, magari na pikipiki vya thamani ya shilingi 3,071,668 pia yapo kwenye hali mbaya na hayatumiki; hivyo, hakuna faida yoyote inayoweza kupatikana kwa kuendelea kuyaweka kweye vitabu maana havitumiki/hayatumiki. Kwa mantiki hiyo, taarifa za fedha hazikuweza kuonesha hali halisi ya mali za kudumu za Mfuko. Hii ni kinyume na aya ya 82 ya IPSAS 17 ambayo inataka mali za kudumu ziwe zinafanyiwa tathmini pale thamani yake inaposhuka na kuonekana kuwa haitakuwa na manufaa kwa baadaye au haitaweza kuendelea kutoa huduma.

PTF haijawahi kutathmini mali zake za kudumu zenye thamani ya shilingi 230,924,096. Kwa mantiki hiyo, mali za kudumu zilizooneshwa katika taarifa za fedha haziwezi kuonesha uhalisia wa mali za Mfuko.

PTF iliripoti jumla ya kiasi cha shilingi 148,129,899 kama ardhi na majengo. Thamani ya ardhi na majengo ilikuwa imekosewa kwa sababu ilijumuisha uchakavu wa ardhi ambayo haikutakiwa kuoneshwa kwenye vitabu vya uhasibu. Kiasi cha fedha kilichokosewa hakikuweza kufahamika kwa sababu thamani ya ardhi na majengo haijatenganishwa.

Jumla ya kiasi cha shilingi 1,826,926,519 kiliripotiwa kama madeni ya wateja yasiyolipwa kwa kipindi cha kuishia Juni, 30, 2014/15 kama ilivyoelezewa katika noti ya 25 ya taarifa za fedha. Jedwali

linaloonesha mchanganuo wa madeni ya wateja yasiyolipwa halikuwasilishwa kwa ukaguzi. Ilibainika kutokuwapo na nyaraka za kutosha kuweza kuthibisha uhalali wa kiasi cha deni lililotajwa hapo juu.

Chanzo:Taarifa ya ACT Wazalendo ya mwaka Juni, 2015

2.2.5 *Taasisi zilizopata Hati mbaya*

Nimetoa Hati Mbaya kwa Taasisi tano(5)(2%) kati ya Taasisi 222 zilizokaguliwa mwaka huu. Hati hii hutolewa pale ambapo nimeshindwa kupata nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi na mapungufu ambayo sijaweza kuyagundua yanaweza yakawa makubwa na ya muhimu sana. Taasisi zenye hati mbaya, zimeorodheshwa kwenye Jedwali hapa chini.

1. Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
Hati za Malipo zenye thamani ya shilingi 91,261,040,310 hazikutolewa kwa ukaguzi Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016 tulibaini malipo kiasi cha shilingi 91,261,040,310 sawa na asilimia 31 ya matumizi yote yalifanyika lakini hati za malipo zenye nyaraka za kuonesha uhalali wa malipo hayo hazikutolewa kwa ukaguzi; hivyo, sikuweza kubaini uhalali wa malipo hayo. **Fedha zilizohamishwa bila utaratibu (Unaccounted funds transfer of TZS) shilingi 5,444,127,508** Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 39) waliomba kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kiasi cha shilingi 1,000,000,000. Hata hivyo, Wizara ilihamisha kiasi cha shilingi 5,444,127,508 kutoka akaunti ya maendeleo kwenda Jeshi la Kujenga Taifa badala ya kiasi kilichokuwa kimeombwa. Hatukuweza kupata nyaraka zinazohusiana na kiasi cha fedha kilichohamishwa, hivyo, hatukuweza kuthibitisha uhalali wa muamala huo. **Kutofanana kwa jinsi ya kuripoti mali za kudumu katika taarifa za fedha**

Mapitio ya taarifa za fedha za mwaka 2015/16 yalibaini kutokuwapo kwa utaratibu maalumu wa kuripoti mali za kudumu mpya zinazonunuliwa. Katika taarifa za fedha, mali za kudumu zilizonunuliwa zilikuwa za shilingi 67,835,751,744 ikilinganishwa na bakaa la mwaka jana wakati noti ya 92 inaonesha ongezeko la shilingi 17,538,650,199. Pia kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha taslimu ongezeko la mali za kudumu limeoneshwa kuwa ni shilingi 73,052,714,340; wakati taarifa ya mabadiliko ya mali za kudumu ilionesha shilingi 75,111,756,436.

Tofauti hizi hazikuweza kufanyiwa kazi na menejimenti na hatukupewa nyaraka zozote zilizotuwezesha kusema kiasi kipi kati ya hivyo hapo juu ndicho sahihi kuoneshwa kwenye taarifa za fedha.

Pia, kazi iliyokuwa inaendelea yenye thamani ya shilingi 8,086,336,381 ambayo ilijumlishwa kama sehemu ya mali za kudumu katika mwaka wa fedha, haikuwa na nyaraka zozote za kuweza kuonesha kazi halisi iliyofanyika.

2. Chama cha AFP [Mwaka wa Fedha: JUNI 2016]

Katika ukaguzi wa huu tulibaini kuwa AFP hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Kutotunza vitabu vya uhasibu ipasavyo kulizuia mawanda ya ukaguzi.

AFP hawatumii mfumo wa taarifa za fedha kama unavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA). Tangazo namba 3 la mwaka 2009; na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo, hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa zao za fedha.

Malipo ya kiasi cha shilingi 21,588,150 yalilipwa kwa watu tofauti ambao walishiriki katika kazi za chama. Hata hivyo, hatukupata hati ya malipo iliyotumika kufanya malipo hayo na viambatisho vyake kinyume na Kanuni ya 86 (1), 95 (4) na 116 ya Kanuni za

Fedha za Umma yam waka 2001. Hivyo ukaguzi hakuweza kubaini uhalali wa malipo hayo.

Kiasi cha shilingi 21,693,850 kilipokelewa kama michango ya hiari ya wanachama kutoka katika ofisi za mikoani, Ofisi ya Zanzibar na Makao makuu Dar es Salaam ila hazikukatiwa stakabadhi za kukiri mapokezi wala kuingizwa kwenye vitabu vya fedha (cash book).

3. Chama Cha Kijamii (CCK) [FY: JUNE 2016]

Katika ukaguzi wa huu tulibaini kuwa CCK hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Matokeo yake ni kuwa, mapato na matumizi ya shilingi 3,200,000 hayakuwemo kwenye vitabu vya fedha. Kutotunza vitabu vya uhasibu ipasavyo kulizuia mawanda ya ukaguzi.

CCK hawatumii mfumo wa taarifa za fedha kama unavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA). Tangazo namba 3 la mwaka 2009; na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo, hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa zao za fedha.

4. Chama cha (NLD) [Mwaka wa Fedha: JUNI 2016]

Katika ukaguzi wa huu tulibaini kuwa NLD hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015. Kutotunza vitabu vya uhasibu ipasavyo kulizuia mawanda ya ukaguzi.

NLD hawatumii mfumo wa taarifa za fedha kama unavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA).Tangazo namba 3 la mwaka 2009 na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa zao za fedha.

Ilibainika kuwa NLD hawana akaunti ya benki kama inavyotakiwa na Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka

1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Matokeo yake fedha zilizopokelewa kutokana na michango ya hiari ya wanachama haikuwekwa kwenye akaunti ya benki. Vile vile, vitabu vya fedha (Cash book) havikuwa vimetunzwa vizuri hivyo ukaguzi kashindwa kuelewa miamala iliyofanyika katika mwaka husika.
5. Sauti ya Umma [FY: JUNE 2016]
Katika ukaguzi wa huu tulibaini kuwa SAU hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015. Kutotunza vitabu vya uhasibu ipasavyo kulizuia mawanda ya ukaguzi. SAU hawatumii mfumo wa taarifa za fedha kama unavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA). Tangazo namba 3 la mwaka 2009 na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa zao za fedha.

Katika mwaka huu wa Ukaguzi, pia nimetoa Hati Mbaya kwa vyama vinne(4) vya siasa[19] kwa Taarifa za Fedha za miaka iliyopita. Taarifa Zaidi zimeorodheshwa kwenye Kiambatisho Na 2.3

2.2.6 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Kipindi cha Miaka Mitano

Taasisi za Serikali Kuu zilizokaguliwa zimekuwa zikiongezeka kila mwaka kutoka 108 (2011/2012) hadi 222 (2015/2016). Hivyo mwendendo wa Hati za Ukaguzi umekuwa ukibadilika kwendana na taasisi kama jedwali hapa chini linavyoonesha katika Jedwali hapo chini:

[19] DP, ADC, ADA, TADEA & DM

Jedwali 6: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Kipindi cha Miaka Mitano

		Hati Inayoridhisha		Hati yenye Shaka		Hati Isiyoridhisha		Hati Mbaya		Jumla
Kundi	**Mwaka**	**Na**	**%**	**No**	**%**	**No**	**%**	**No.**	**%**	
Mafungu	**2015-16**	**76**	**86**	**9**	**11**	**1**	**1**	**1**	**1**	**87**
	2014-15	75	87	11	13	0	0	0	0	86
	2013-14	79	91	7	8	1	1	0	0	87
	2012-13	56	66	28	33	0	0	1	1	85
	2011-12	73	96	3	4	0	0	0	0	76
Balozi	**2015-16**	**33**	**97**	**1**	**3**	**0**	**0**	**0**	**1**	**34**
	2014-15	34	100	0	0	0	0	0	0	34
	2013-14	34	100	0	0	0	0	0	0	34
	2012-13	29	91	2	6	1	3	0	0	32
	2011-12	30	94	2	6	0	0	0	0	32
Taasisi Nyingine	**2015-16**	**50**	**74**	**12**	**18**	**2**	**3**	**4**	**1**	**68**
	2014-15	45	92	3	6	1	2	0	100	49
	2013-14	21		2	9	0	0	0	0	23
	2012-13	0	0	0	0	0	0	0	0	0
	2011-12	0	0	0	0	0	0	0	0	0
	2015-16	**31**	**94**	**2**	**6**	**0**	**0**	**0**	**1**	**33**
Wakala	2014-15	27	90	3	10	0	0	0	0	30
	2013-14	32	100	0	0	0	0	0	0	32
	2012-13	0	0	0	0	0	0	0	0	0
	2011-12	0	0	0	0	0	0	0	0	0

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya tathmini juu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguliwa, na kwa kila ripoti ya ujumla.Pia kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC). Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 40 cha sheria ya Ukaguzi wa Umma Na 11 ya mwaka 2008 (iliyorekebishwa mwaka 2013) kinachomtakaCAG kujumuisha hali ya utekelezaji wa mpango wa utekelezaji uliooandaliwa na Maafisa Masuuli na majibu jumuifu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) katika Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka.

Ufuatiliaji wa masuala ya miaka iliotangulia hutoa uhakika kwa raia wa nchi hii na wadau wengine juu ya jinsi Wizara, Idara na Wakala wa Serikali walivyoonesha umuhimu wa kujibu mapendekezo yangu na mapendekezo na maelekezo ya PAC ambayo huleta usahihi wa mapato, matumizi na mali za Serikali, pamoja na uadilifu na kujitosheleza kwa mifumo na taratibu za kutekeleza majukumu yao .Lengo ni kuleta utaratibu unaokubalika, ufanisi, ufasaha wa maendeleo ya kiuchumi wa mipango ya malengo ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kwa ajili ya matumizi bora ya rasilimali zilizopo

Hali ya mapitio ya kila pendekezo imeelezwa katika namna ifuatayo:

- **Yaliyotekelezwa:**
- Pendekezo limetekelezwa kikamilifu na Mkaguliwa: aidha ,kama ilivyoelezwa kwenye ripoti au katika namna ambayo jambo limetatuliwa.
- **Yaliyo katika utekelezaji:**

- Mkaguliwa ana mipango mahususi ya kuanza nayo au ameishaanza kutekeleza na amedhamiria kutekeleza pendekezo kikamilifu.
- **Yaliyotekelezwa kiasi:**
- Mkaguliwa ametekeleza sehemu ya pendekezo, lakini hafanyi jitihada za kutekeleza pendekezo kikamilifu.
- **Yasiyotekelezwa:**
- Mkaguliwa hajatekeleza pendekezo na inaonesha hatafanya hivyo.

3.1 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa

Lengo la kufanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa mapendekezo ni kutambua hoja za ukaguzi kwenye ripoti zinazohitaji umakini wa haraka kwa Uongozi na hoja nyingine ambazo ufuatiliaji wake unachukuliwa kuwa wa lazima kwa muda huu na kutoa taarifa kwa Mkaguliwa juu ya mapitio ya utekelezaji wa hizo hoja.

Kujibu mapendekezo ya ukaguzi ni muhimu ili kupata faida kamili ya kazi ya ukaguzi.

Ufuatiliaji wangu umebaini kwamba kati ya mapendekezo 3898 ya ukaguzi, 1449 (37%) yalitekelezwa, 1351 (35%) yalikuwa katika utekelezaji, 842 (21%) hayakutekelezwa na, 256 (7%) yalitegemea matukio mengine. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini na Kiambatisho Na 3.1 hadi 3.3

Jedwali 7: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa CAG juu ya ripoti ya kila Mkaguliwa

Hali Halisi ya Mapendekezo	Mafungu na Balozi anEmbassies	Wakala	Taasisi nyingine	Jumla	Asilimia
Yaliyotekelezwa	883	326	240	1449	37
Taliyo katika utekelezaji	866	220	265	1351	35
Yasiyotekelezwa	570	58	214	842	21
Yanayotegemea matukio mengine	183	9	64	256	7
Jumla	**2502**	**613**	**783**	**3898**	**100**

Chanzo: *Barua ya Mapungufu kwa kila Mkaguliwa kwa mwaka 2015/16*

Kwa ujumla, jedwali la hapo juu linabainisha kuwa mapendekezo mengi yemetekelezwa kwa 37% na 35% mengine yametekelezwa sehemu ya pendekezo, lakini hafanyi jitihada za kutekeleza pendekezo kikamilifu, Hata hivyo, bado nasisitiza juu ya utekelezaji wa 21% ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kabisa kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali.

3.2 Mwenendo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa kwa miaka miwili mfululizo

Jedwali la hapo chini linaonesha mwenendo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguliwa kutoka mwaka 2013/14 na 2016/15 kama yalivyowasilishwa na jedwali na Kielelezo hapo chini;

Jedwali 8: Mchanganuo wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2013/14 na 2014/15

Status	Mafungu na Balozi		Wakala		Taasisi nyingine		Jumla		Asilimia	
	2013/14	2014/15	2013/14	2014/15	2013/14	2014/15	2013/14	2014/15	2013/14	2014/15
Yaliyotekelezwa	803	883	132	326	93	240	1028	1449	39%	37%
Taliyo katika utekelezaji	666	866	168	220	57	265	891	1351	33%	35%
Yasiyotekelezwa	444	570	65	58	28	214	537	842	20%	21%
Yanayotegemea matukio mengine	188	183	11	9	5	64	204	256	8%	7%
Jumla	**2101**	**2502**	**376**	**613**	**183**	**783**	**2660**	**3898**	**100%**	**100%**

Chanzo: Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kila Mkaguliwa kwa mwaka wa fedha *2014/15 and 2015/16*

Jedwali hapo juu linawakilishwa katika kielelezo Na 3.1 hapo chini

Kielelezo 1: Chati ya mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa mwaka 2013/14 na 2014/15



Source: Taarifa ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kila Mkaguliwa 2014/15 na 2015/16

UFUNGUO
A-Yaliyotekelezwa; B-Yaliyo katika Utekelezaji; C-Ambayo hayajatekelezwa na D-Yanayotegemea matukio mengine

3.3 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwenye Ripoti ya Jumla

Majibu ya Serikali kwa ripoti ya jumla ya mwaka 2014/15 yaliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu za Serikalti na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa barua yenye Kumb.Na CHA.114 / 474/01 ya Julai 21, 2016. Nashukuru juhudi zinazofanywa na Maafisa Masuuli na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kushughulikia mapendekezo yangu.

Katika ripoti yangu ya jumla ya mwaka uliopita, kulikuwa na mapendekezo 102 yasiyoshughulikiwa ambayo yanajumuisha

mapendekezo mpaka mwaka unaoishia 30 Juni, 2015 mapendekezo hayo yalihitaji kujibiwa na Serikali.

Nilipokea majibu ya mapendekezo yangu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo 19 sawa na 18.6% ya mapendekezo yalitekelezwa, 53 sawa na 52.0% yanaendelea kutekelezwa, 20 sawa na 19.6% hayakutekelezwa na 10 sawa na 9.8% yaalikuwa yanategemea kwa tukio mengine. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo yametolewa katika Jedwali hapo chini na **Kiambatisho 3.5**.

Jedwali 9: Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu za Serikali kwa miaka ya nyuma

Hali ya Utekelezaji	Idadi ya Mapendekezo	Asilimia
Yaliyotekelezwa	19	18.6
Yaliyo katika utekelezaji	53	52.0
Ambayo hayajatekelezwa	20	19.6
Yanayotegemea matukio mengine	10	9.8
Total	**102**	**100**

Jedwali la hapo juu linaweza kuwasilisha kwa kielelezo Na. 3.2 hapo chini

Kielelezo 2: Hali halisi ya mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali na utekelezaji wake katika Ripoti ya jumla



Kwa ujumla, kutoka kwenye **jedwali Na.3.3** na **kielelezo Na. 3.2** hapo juu inlaonesha kuwa mapendekezo mengi (52.0%) bado yako katika hauta ya utekelezaji. Juhudi zaidi zinahitajika ili kuhakikisha mapendekezo yanatekelezwa kwa ukamilifu. Bado nasisitiza juu ya utekelezaji wa 19.6% ya mapendekezo ambayo bado hayajafanyiwa kazi ili kuzifanya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali wawajibike juu ya matumizi ya rasilimali za umma.

3.4 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwenye ripoti ya jumla

Ufuatiliaji wa mapendekezo na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa masuala ya miaka ya nyuma ni muhimu ili kuhakikisha kuwa uendeshaji unafanyika kwa kufuata utaratibu, maadili, kuzingatia hali ya uchumi, ufanisi na tija, kuhakikisha majukumu ya uwajibikaji yanatimia, kuhakikisha sheria na kanuni husika zinafuatwa na kuhakikisha rasilimali zinalindwa dhidi ya upotevu, matumizi mabaya na uharibifu.

Ni furaha yangu kubwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa msaada ninaopata kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali na Bunge kwa ujumla kwa mapitio ya ripoti yangu ninapokuwa natekeleza wajibu na majukumu yangu ya kikatiba na kisheria kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hii imewezekana kwa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa kutoa maelekezo muhimu kwa serikali juu ya mapendekezo ninayotoa hivyo, kufanya majukumu yangu kisheria kuwa na umuhimu zaidi. Ni muhimu sana kwa mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali yaKachukuliwa kwa uzito na kutekelezwa vizuri.

Katika ripoti ya nyuma, kulikuwa na mapendekezo 15 yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ambayo yalihitaji umakini wa serikali kwa ajili ya utekelezaji. Maelezo ya hali ya utekelezaji yametolewa chini ya jedwali hapa chini na **kiambatisho Na 3.6**

Kielelezo 3: Muhtasari wa utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma juu ya Ripoti ya Jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Hali ya Utekeleza \ Miaka	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	Jumla	Asilimia
Yaliyotekelezwa	-	1	-	-	1	7
Yaliyo katika utekelezaji	4	2	-	4	10	67
Ambayo hayajatekelezwa	-	-	-	2	2	13
Yanayotegemea matukio mengine	1	-	-	1	2	13
Jumla	**5**	**3**	**-**	**7**	**15**	**100**

Source: Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali juu ya maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali

Kutokana na jedwali la hapo juu hali ya utekelezaji inaweza kuoneshwa kwa **kielelezo Na 3.3**

Kielelezo 4: Mchanganuo wa utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwenye Ripoti kuu ya mwaka



Chanzo: Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali juu ya maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali

Kutoka kwenye **jedwali Na.3.5** na **kielelezo Na. 3.3** inaweza kuhitimishwa kuwa mapendekezo mengi ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali yako katika hatua ya utekelezaji. Hii inaashiria kwamba nguvu za ziada zinahitajika ili kuhakikisha kuwa mapendekezo yaliyo katika hatua ya utekelezaji (67%) yanatekelezwa. Vilevile, 13% ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa yanapaswa kutekelezwa ili maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali yawe na umuhimu.

3.5 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Nyuma ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali juu ya Taarifa ya kila Mkaguliwa

Nimefanya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa. Mapendekezo 102 (35%) yaliyotolewa yametekelezwa, 87 (30%) yako katika utekelezaji, 85 (29%) hayajatekelezwa na 16(6%) yanategemea matukio mengine. Hali ya utekelezaji

wa mapendekezo umetolewa katika jedwali hapo chini na maelezo ya utekelezaji katika **Kiambatisho 3.4**

Jedwali 10: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguliwa

Hali Halisi \ Mkaguliwa	Mafungu & Balozi	Wakala	Taasisi	Jumla	Asilimia
Yaliyotekelezwa	91	7	4	102	35
Yaliyo katika utekelezaji	75	10	2	87	30
Ambayo hayajatekelezwa	85	0	0	85	29
Yanayotegemea matukio mengine	16	0	0	16	6
Total	**267**	**17**	**6**	**290**	**100**

Chanzo: Barua za mapungufu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa 2015/16

Kutoka kwenye jedwali la hapo juu, hali ya utekelezaji unaweza kuoneshwa kwa kielelezo hapo chini;

Kielelezo 5: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa



Nawasihi sana Maafisa Masuuli husika kutekeleza kikamilifu maelekezo yote ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ambayo yako katika utekelezaji (30%) na yale ambayo hayajatekelezwa (29%) ili kupata faida kamili ya maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali. Angalia **Kiambatisho 3.4**;

SURA YA NNE

UANDAAJI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI

4.1 UTANGULIZI

Sura hii inatoa taswira ya Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge ikiwa ni makisio ya mapato na matumizi, fedha halisi zilizokusanywa na kutolewa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ikilinganishwa na makisio na mwenendo wa mapato na matumizi katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2016.

4.2 Mapitio ya Bajeti

Misingi inayotumika kuandaa taarifa za fedha za Serikali ni Viwango vya Kimataifa Visivyo vya Misingi ya Fedha Taslimu (IPSAS Accrual Basis of Accounting) ni tofauti na misingi inayotumika kuandaa Bajeti ya Serikali. Tofauti kati ya taarifa za fedha na bajeti huweza kutokea kwa sababu ya tofauti za misingi inayotumika kuziandaa.

Serikali ya Tanzania huandaa bajeti zake kwa misingi ya fedha taslimu na mwaka wa fedha huanzia Julai 1 hadi June 30 ya kila mwaka. Mwaka 2012 Serikali Kuu ilifanya maamuzi ya kuanza kutumia Viwango vya Kimataifa Visivyo vya Misingi ya Taslimu ambavyo vinategemea kufikia ukikamilifu wake mwaka 2017/18.

Bajeti ya Serikali imekua ikiongezeka mwaka hadi mwaka huku vyanzo vya fedha kutekeleza bajeti hiyo vikibakia vile vile vikiwa na tofauti ndogo msisitizo ukiwekwa zaidi kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuongeza udhibiti kwenye matumizi ya fedha.

Katika mwaka wa Fedha 2015/16 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 22,495.5 ikionesha ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 2,642.20 sawa na asilimia 13.13 ikilinganishwa na kiasi cha makisio ya shilingi bilioni 19,853.30 kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2014/15. Mapato ya Serikali kutoka katika vyanzo vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ni kama vinavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Vyanzo	Kiasi cha fedha katika shilingi bilioni	Asilimia
Kodi	12,362.96	54.96%
Yasiyo ya Kodi	1,634.50	7.27%
Mikopo ya Ndani	6,175.50	27.45%
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	2,322.50	10.32%
Jumla	**22,495.50**	

a utekelezaji wa Bajeti

Kutokana na jedwali hapo juu ninahitimisha kwamba mapato yatokanayo na kodi yanachangia sehemu kubwa ya mapato kwa asilimia 50 ya makisio ikifuatiwa na mikopo ya ndani kwa asilimia 27 na Fedha za Misaada ya Wahisani na mikopo ya nje kwa asilimia 10.

Katika makisio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/16 jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 22,495.5 kiliidhinishwa kikijumuisha kiasi cha shilingi bilioni 16,574.4 ambazo zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni ongezeko la asilimia 23.61 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 13,408.22 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15. Kiasi cha shilingi bilioni 5,921.1 zilitengwa kwa shughuli za Maendeleo ikionesha kupungua kwa asilimia 8.13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6,445.11 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/15. Hii inaonesha kwamba makisio ya matumizi ya kawaida yameongezeka wakati matumizi ya shughuli za maendeleo yameshuka.

4.3 Mwenendo wa jumla wa Ukusanyaji wa Mapato

Mapato halisi yaliyokusanywa kutoka katika vyanzo vilivyoainishwa yalifikia shilingi bilioni 21,108.86 (sawa na asilimia 93.84 ya makadirio ya shilingi bilioni 22,495.5) ikionyesha kushindwa kufikia lengo kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,386.64 (sawa na asilimia 6.16 ya makisio).

Kati ya shilingi bilioni 21,108.86 zilizokusanywa, shilingi bilioni 20,020.75 zilizotolewa kwa ajili ya Mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo, matumizi ya shughuli za Maendeleo na matumizi ya Mfuko Mkuu. Matumizi ya kawaida na uendeshaji wa shughuli za Serikali yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 15,970.12 sawa na asilimia 79.77 wakati fedha za shughuli za maendeleo zilifikia kiasi cha shilingi bilioni 4,050.83 sawa na asilimia 20.23. Hali hii inaonyesha kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali yalipelekwa kwenye matumizi ya kawaida ya Serikali kuliko katika shughuli za maendeleo.

Fedha halisi zilizotolewa zikilinganishwa na makisio, inaonyesha fedha za Mishahara ya watumishi zilitolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 72.71 wakati kiasi cha shilingi bilioni 107.39 zilitolewa zaidi kwenye shughuli za Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi cha shilingi bilioni 784.38 na shilingi bilioni 1,870.27 hazikutolewa kwa matumizi mengineyo na shughuli za maendeleo kwa mtiririko huo. Taarifa hizi ni kama zinavyoonekana katika jedwali hapa chini.



	Mishahara ya Watumishi	Matumizi Mengineyo	Fedha za Maendeleo	Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali
Makisio katika shilingi bilioni	6,466.50	3,711.30	5,921.10	6,396.60
Fedha zilizotolewa katika shilingi bilioni	6,539.2	2,926.9	4,050.8	6,504.0

***Chanzo**: Taarifa ya Utoaji fedha ya Hazina na Bajeti ya Wananchi*

Mwenendo wa Ukusanyaji Mapato

Mapato Yatokanayo na Kodi

Kumekuwa na ongezeko katika kodi zilizokusanywa katika mwaka wa ukaguzi ambapo mapato kutokana na kodi yalifikia shilingi bilioni 12,463.53 na kuvuka lengo kwa kiasi cha shilingi bilioni 100.57 (sawa na asilimia 0.81). Wakati ikilinganishwa na mapato halisi kutokana na kodi ilivyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2014/15 kumekuwa na ongezeko la shilingi bilioni 1,690.31 (sawa na asilimia 15.69). Haya ni matokeo chanya katika ukusanyaji wa mapato.

Mapato yasiyotokana na Kodi

Katika mwaka huu wa fedha, Mapato yasiyotokana na Kodi yalifika jumla ya shilingi bilioni 1,613.99 sawa na asilimia 98.74 ya makisio ya shilingi bilioni 1,634.56 na kushindwa kufikia lengo kwa kaisi cha shilingi bilioni 20.57 sawa na asilimia 1.3. Kumekuwa na ongezeko katika mapato yasiyotokana na kodi katika mwaka wa ukaguzi kwa asilimia

113.05 ikilinganishwa na zile zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2014/15. Kuongezeka kwa mapato yasiyotokana na kodi yamechangiwa na ukweli kwamba fedha za gawio za Mashirika ya Umma zimeweka kama sehemu ya mapato yasiyotokana na kodi ambayo katika mwaka wa ukaguzi yalivuka lengo kwa asilimia 73.[20]

Mapato yatokanayo na Mikopo ya Ndani

Mapato yanayotokana na Kukopa Ndani ambayo ni kwa ajili ya kugharamia bajeti na amana za Serikali zilizoiva (Rollovers) yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 5,304.94 sawa na asilimia 85.90 dhidi ya makisio ya shilingi bilioni 6,175.45. Kumekuwa na ongezeko katika kiasi cha mikopo ya ndani kwa asilimia 33.33 ikilinganishwa na kile ilikuwa alikopa katika mwaka wa fedha 2014/15.

Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani na Misaada ya Washirika wa Maendeleo.

Mapato yaliyotokana na Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani yenye masharti nafuu na Misaada ya Washirika wa Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2015/16 yalifika kiasi cha shilingi bilioni 1,726.40 sawa na asilimia 74.33 dhidi ya makisio yaliyoidhinishwa ya kiasi cha shilingi bilioni 2,322.53, hivyo kiasi cha shilingi bilioni 596.13 sawa na asilimia 25.67 hazikupokelewa. Katika mwaka huu kumekuwepo na upungufu wa misaada ya kibajeti kwa asilimia 54 na hatukupokea fedha zozote kutoka katika Akaunti ya Changamoto za Milenia (Millennium Challenge Account-MCA (T)). Hii ilipelekea kushuka kwa mapato tuliyotegemea kutokana na Misaada yenye masharti nafuu na kibajeti kwa asilimia 52 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,601.95 zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2014/15. Hii ina maana kwamba shughuli za maendeleo zilizopangwa kutekelezwa kwa kutumia fedha MCA (T) na zile za misaada ya kibajeti hazikuweza kufanyika katika mwaka husika na iliathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

[20] Makisio ya fedha za gawio na michango ya wakala wa Serikali yalikua kiasi cha shilingi bilioni 142.53 na makusanyo halisi yalifika kiasi cha shilingi bilioni 246.53 hivyo kuvuka lengo kwa kiasi cha shilingi bilioni 104 sawa na asilimia 73

Kielelezo 6: Mwenendo wa makisio ya mapato ya Serikali na ukusanyaji wake kwa miaka minne mfululizo



	2012/2013	2013/2014	2014/2015	2015/2016
Kodi	8,432	10,320	11,262	12,363
Yasiyotokana na Kodi	717	763	1,028	1,635
Mikopo ya Ndani	1,632	2,948	2,955	6,175
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	4,411	3,855	4,262	2,323



	2012/2013	2013/2014	2014/2015	2015/2016
Kodi	8,052	9,289	9,919	12,464
Yasiyotokana na Kodi	481	641	917	1,614
Mikopo ya Ndani	2,493	3,289	3,979	5,305
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	3,992	3,085	3,602	1,726

2015/2016			
Aina ya Mapato	**Makisio katika shilingi bilioni**	**Halisi katika shilingi bilioni**	**Tofauti Zaidi/(Pungufu)**
Kodi	12,362.96	12,463.53	100.57
Yasiyotokana na Kodi	1,634.56	1,613.99	(20.57)
Mikopo ya Ndani	6,175.45	5,304.94	(870.51)
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	2,322.53	1,726.40	(596.13)
JUMLA	**22,495.50**	**21,108.86**	**(1,386.64)**
2014/2015			
Aina ya Mapato	**Makisio katika shilingi bilioni**	**Halisi katika shilingi bilioni**	**Tofauti Zaidi/(Pungufu)**
Kodi	11,318.20	10,773.22	(544.98)
Yasiyotokana na Kodi	1,318.30	757.57	(560.73)
Mikopo ya Ndani	2,955.20	3,978.95	1,023.75
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	4,261.60	3,601.95	(659.65)
JUMLA	**19,853.30**	**19,111.68**	**(741.62)**
2013/2014			
Aina ya Mapato	**Makisio katika shilingi bilioni**	**Halisi katika shilingi bilioni**	**Tofauti Zaidi/(Pungufu)**
Kodi	10,412.95	9,289.00	(1,123.95)
Yasiyotokana na Kodi	763.43	640.95	(122.48)
Mikopo ya Ndani	1,699.87	3,289.41	1,589.54
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	5,011.60	3,084.93	(1,926.67)
JUMLA	**17,887.85**	**16,304.29**	**(1,583.56)**
2012/2013			
Aina ya Mapato	**Makisio katika shilingi bilioni**	**Halisi katika shilingi bilioni**	**Tofauti Zaidi/(Pungufu)**
Kodi	8,432.29	8,052.29	(380.01)
Yasiyotokana na Kodi	716.84	481.15	(235.69)
Mikopo ya Ndani	1,632.00	2,492.71	860.71
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	4,410.81	3,992.17	(418.64)
JUMLA	**15,191.94**	**15,018.32**	**(173.62)**

Vyanzo: *Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti, Taarifa ya fedha ya Mamlaka ya Mapato iliyokaguliwa na taarifa ya Wizara ya Fedha*

Uchambuzi wa makadirio ya mapato kugharamia matumizi

Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha yamekuwa yakiongezeka mwaka kwa mwaka huku kukiwa na ongezeko kidogo katika ukusanyaji maduhuli kuweza kugharamia bajeti. Kuendelea kutegemea mikopo ya ndani na Nje kugharimia bajeti inaleta changamoto kwani mikopo huwa na riba ambayo itaanza kuukausha uchumi wakati wa kulipa madeni.

Sehemu ya bajeti ambayo ilifadhiliwa na mapato ya ndani ya nchi kutokana na kodi na yasiyotokana na kodi yalikuwa kiasi cha shilingi bilioni 14,007.52 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 22,495.5 ikionesha kwamba bila kutumia mikopo ya ndani, na nje na misaada, Serikali ingeweza kugharamia asilimia 62.58 tu ya bajeti yake.

Mwenendo wa miaka mitatu mfululizo wa mapato na matumizi ni kama unavyoonekana kwa muhtasari katika jedwalii hapa chini.

Jedwali 11: Mwenendo wa uchambuzi wa bajeti kwa miaka mitatu (Kiasi katika shilingi bilioni)

	Makisio kiasi katika shilingi bilioni			D	E	% of D	% of E
Aina ya Mapato	2015/2016	2014/2015 (B)	2013/2014 (C)	Tofauti(A - B)	Tofauti (A - C)		
Kodi	12,362.96	11,318.20	10,412.95	1,044.76	1,950.01	9.23	18.73
Yasiyotokana na Kodi	1,634.56	1,318.30	763.43	316.26	871.13	23.99	114.11
Mikopo ya Ndani	6,175.45	2,955.20	1,699.87	3,220.25	4,475.58	108.97	263.29
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	2,322.53	4,261.60	5,011.60	(1,939.07)	(2,689.07)	-45.50	-53.66
JUMLA	**22,495.50**	**19,853.30**	**17,887.85**	**2,642.20**	**4,607.65**		
Aina ya Mapato							
	Makisio kiasi katika shilingi bilioni			D	E	% of D	% of E
	2015/2016	2014/2015 (B)	2013/2014 (C)	Tofauti(A - B)	Tofauti (A - C)		
Kodi	12,463.53	10,773.22	9,289.00	1,690.31	3,174.53	15.69	34.18
Yasiyotokana na Kodi	1,613.99	757.57	618.80	856.42	995.19	113.05	160.83
Mikopo ya Ndani	5,304.94	3,978.95	3,289.41	1,325.99	2,015.53	33.33	61.27
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	1,726.40	3,601.95	3,084.93	(1,875.55)	(1,358.53)	-52.07	-44.04
JUMLA	**21,108.86**	**19,111.68**	**16,282.14**	**1,997.18**	**4,826.72**		

Vyanzo: *Taarifa ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Deni la Taifa na Hazina*

Kielelezo 7: Mwenendo wa Makisio



	Kodi	Yasiyotokana na Kodi	Mikopo ya Ndani	Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani
2015/2016 (A)	12,362.96	1,634.56	6,175.45	2,322.53
2014/2015 (B)	11,318.20	1,318.30	2,955.20	4,261.60
2013/2014 (C)	10,412.95	763.43	1,699.87	5,011.60



	Kodi	Yasiyotokana na Kodi	Mikopo ya Ndani	Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani
2015/2016 (A)	12,463.53	1,613.99	5,304.94	1,726.40
2014/2015 (B)	10,773.22	757.57	3,978.95	3,601.95
2013/2014 (C)	9,289.00	618.80	3,289.41	3,084.93

Serikali inapaswa kuandaa bajeti yenye uhalisia kwa maana kwamba, mapato ya ndani yawe na uwezo kugharamia bajeti

kwa sehemu kubwa na kupunguza utegemezi kwenye mikopo hasa deni la ndani.

Deni la ndani limekua likiongezeka kila mwaka na wakopeshaji kwa sehemu kubwa ni benki za biashara ambazo kwa upande mwingine ina athari juu ya kiwango cha mikopo inayotolewa kwa watu binafsi na gharama za maisha.

4.4 Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Makisio ya matumizi ya kawaida katika mwaka husika wa ukaguzi kwa Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa yalikua kiasi cha shilingi bilioni 12,904.75 yakionesha ongezeko la shilingi bilioni 1,258.56 sawa na asilimia 10.81 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2014/15 ya shilingi bilioni 11,646.20

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa yalibainisha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 12,065.22.zilitolewa kama matumizi ya kawaida ikiwa ni ongezeko la asilmia 93.49 ya makisio yaliyoidhinishwa hivyo kiasi cha shilingi bilioni 839.54 sawa na asilimia 6.51.hazikutolewa kama zilivyoidhinishwa.

Pia kuna ongezeko la fedha zilizotolewa kiasi cha shilingi bilioni 875.10 sawa na asilimia 7.82 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2014/15. Fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/15 zilikua kiasi cha shilingi bilioni 11,1190.11.

Jedwali 12: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida dhidi ya Makisio(Kiasi katika shilingi bilioni)

Mwaka wa Fedha	Makisio	Fedha zilizotolewa	Fedha zisizotolewa
2015/16 (A)	12,904.75	12,065.22	839.54
2014/15 (B)	11,646.20	11,190.11	456.08
2013/14 (C)	9,959.81	9,559.56	400.26
2012/13 (D)	8,599.99	8,284.42	315.57
2011/12 (E)	9,214.89	8,687.23	527.66
Tofauti kati ya (A-B)	1,258.56	875.10	
Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua	10.81	7.82	

***Chanzo**: Hesabu za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Fedha zinazotolewa kwa kuchelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinakwamisha utendaji wa shughuli za Serikali Jedwali hapo juu linaonesha makisio yaliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida kwa kipindi cha miaka minne. Mchanganuo zaidi kuonesha makisio na mapato halisi kwa kila Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa zinapatikana katika **Kiambatisho 4.1**

4.5 Uwiano wa fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa na matumizi halisi

Kuna ongezeko la matumizi halisi la shilingi bilioni 889.51.sawa na asilimia 11.57.katika mwaka wa fedha 2015/16 ikilinganishwa na matumizi halisi yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2014/15.

Matumizi halisi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2015/16 yalifikia shilingi bilioni 12,045.94.dhidi ya fedha zilizotolewa kiasi cha shilingi bilioni 12,065.22 huku kiasi cha shilingi bilioni 19.28 sawa na asilimia 0.16 ya fedha zilizotolewa kutotumika.

Nilibaini pia wizara mbili ambazo zilitumia fedha zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha husika. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 68) walipangiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 43.20 kwa matumizi ya kawaida, walipewa kiasi cha shilingi bilioni 35 kutoka Hazina na walitumia kiasi cha shilingi bilioni 44.72

hivyo kutumia zaidi ya bajeti yao kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 sawa na asilimia 3.57. Hili pia lilionekana katika Wizara ya Afya (Fungu 52) ambao walikua wametengewa kiasi cha shilingi bilioni 331.16, wakatumia kiasi cha shilingi 332.26 ikiwa ni zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na bunge kwa shilingi bilioni 1.1 sawa na asilimia 0.33.

Kutumia fedha zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge inaonesha kuwa kuna kazi ambazo zimefanywa bila kuwepo kwenye mpango. Matokeo yake ni kuongeza gharama za Serikali kwa kuanzisha madeni ambayo yamekua yakiongezeka mwaka hadi mwaka na yamekua mzigo mkubwa kwa Serikali.

Jedwali hapo chini linaonesha fedha zilizotolewa na matumizi halisi. Mchanganuo zaidi unaoonesha mapato halisi na matumizi kwa kila Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho 4.2**

Mwaka wa Fedha	Fedha zilizotolewa	Fedha zilizotumika	Fedha zisizotumika
2015/16 (A)	12,065.22	12,045.94	19.28
2014/15 (B)	11,190.11	11,156.43	33.68
2013/14 (C)	9,559.56	9,551.29	8.27
2012/13 (D)	8,284.42	8,249.28	35.14
2011/12 (E)	8,687.23	8,685.28	1.96
Tofauti kati ya (A-B)	2,505.66	889.51	
Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua	26.21	7.97	

Chanzo: *Hesabu za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Uwepo wa bakaa mwishoni mwa mwaka wa fedha inaonesha kwamba baadhi ya kazi zilizokua zimepangwa kufanyika hazikufanyika kama zilivyopangwa ama kutokana na fedha kutolewa kwa kuchelewa au Ofisi husika kutokua na uwezo wa kutimiza majukumu yake.

Fedha kiasi cha shilingi bilioni 5,731.07 sawa na asilimia 28.63 ya fedha zote zilizotolewa kiasi cha bilioni 20,020.95 zilitolewa katika robo ya mwisho wa mwaka na kati ya hizo kiasi cha shilingi bilioni 2,629.40 sawa na asilimia 13.13

zilitolewa mwezi Juni 2016 ikionesha kuna uchelewaji katika utoaji wa fedha toka hazina.

4.6 Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo zikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Makisio yaliyoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika mwaka husika wa ukaguzi kwa Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa yalikua kiasi cha shilingi bilioni 4,968.86 ikipelekea ongezeko la shilingi bilioni 579.84 sawa na asilimia 13.21 ikilinganishwa na makisio ya kiasi cha shilingi bilioni 4,389.02 zilizotengwa kwa mwaka 2014/15.

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa yalibainisha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 3,768.59 zilitolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 75.84 ya makisio yaliyoidhinishwa na kupelekea kiasi cha shilingi bilioni 1,200.26 sawa na asilimia 24.16 ya fedha zilizoidhiniishwa hazikutolewa.

Hata hivyo kumekuwepo na ongezeko la fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo kwa kiasi cha shilingi bilioni 814.40 sawa na asilimia 27.57 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2014/15. Rejea Jedwali hapa chini. Maelezo zaidi ya makisio na fedha halisi zilizotolewa kwa kila Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa yanapatikana kwenye **Kiambatisho 4.3**.

Jedwali 13: Fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo kwa miaka mine mfululizo. (Kiasi katika shilingi milioni)

Mwaka wa Fedha	Makisio	Fedha zilizotolewa	Fedha zisizotolewa
2015/16 (A)	4,968.86	3,768.59	1,200.26
2014/15 (B)	4,389.02	2,954.20	1,434.83
2013/14 (C)	5,035.94	3,147.04	1,888.91
2012/13 (D)	4,225.47	3,247.53	977.95
2011/12 (E)	4,311.01	3,384.43	926.58
Tofauti kati ya (A-B)	579.84	814.40	
Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua	13.21	27.57	

Chanzo: *Taarifa za Fedha za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Fedha za maendeleo ambazo hazikutolewa zina athari kwenye shughuli zilizokuwa zimepangwa kama kuongezeka kwa gharama ya utekelezaji wa miradi iliyokuwa imetengewa fedha hizo na inaweza ikapelekea kuongezeka kwa gharama ya utekelezaji wa miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa na ambazo madai yake kwa kazi zilizokwishafanyika yameshaidhinishwa kwa maana ya kuongezeka kwa riba na kupelekea mzigo mkubwa kwa Serikali katika siku zijazo.

4.7 Uwiano wa fedha za matumizi ya maendeleo zilizotolewa na matumizi halisi

Fedha zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika mwaka wa fedha 2015/16 zilifikia kiasi cha shilingi bilioni 3,768.59 ikiwa ni ongezeko la asilimia 25.88 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka 2014/15. Matumizi halisi yalifika kiasi cha shilingi bilioni 3,729.72, bakaa ilikua kiasi cha shilingi bilioni 38.88 sawa na asilimia 1.03 ya fedha zilizotolewa.

Kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya fedha za maendeleo zilizotolewa kwa mwaka 2015/16 kwa kiasi cha shilingi bilioni 813.54 sawa na asilimia 25.87 ikilinganishwa na matumizi ya kiasi cha shilingi bilioni 2,916.18 kwa mwaka wa fedha 2014/15.

Jedwali chini linaonesha mchanganuo wa fedha zilizotolewa ikilinganishwa na matumizi yake. Maelezo zaidi ya fedha zilizotolewa kwa kila Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho 4.4**

Jedwali 14: Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotolewa na matumizi yake(Kiasi katika shilingi bilioni)

Mwaka wa Fedha	Fedha zilizotolewa	Fedha zilizotumika	Fedha zisizotumika
2015/16 (A)	3,768.59	3,729.72	38.88
2014/15 (B)	2,954.20	2,916.18	38.02
2013/14 (C)	3,147.04	3,145.08	1.95
2012/13 (D)	3,247.53	3,203.10	44.43
2011/12 (E)	3,384.43	3,376.30	8.14
Tofauti kati ya (A-B)	814.40	813.54	
Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua	25.88	25.87	

Chanzo: *Hesabu za Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa zilizokaguliwa*

4.8 Mapato yasiyotokana na Kodi na bajeti iliyoidhinishwa

Bajeti iliyoidhinishwa ya mapato yasiyotokana na kodi iliyoidhinishwa kwa Wizara, Sekretariati za Mikoa na Balozi kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilikua kiasi cha shilingi milioni 691,587, shilingi milioni 26. na shilingi miliioni 18,058 kwa mtiririko huo. Makusanyo halisi yalikua kiasi cha shilingi milioni 727,119, shilingi milioni 47.34 na shilingi milioni 22,023 kwa Wizara/Idara, Sekretariati za Mikoa na Balozi kwa mtiririko huo.

Wizara na Idara za Serikali ziliweza kuvuka lengo kwa kiasi cha shilingi milioni 35,532 sawa na asilimia 5.14, Balozi zilivuka lengo kwa kiasi cha shilingi milioni 3,966 sawa na asilimia 32.8 wakati Sekretarieti za Mikoa walivuka lengo kwa kiasi cha shilingi milioni 21 sawa na asilimia 82 ya makisio.

Bajeti ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Wizara/Idara Sekretariati za Mikoa na Balozi kwa mwaka wa fedha 2014/15 yalikua shilingi milioni 701,558, shilingi milioni 40 na shilingi milioni 15,510 kwa mtiririko huo. Makusanyo halisi yalifikia kiasi cha shilingi milioni 597,607, shilingi miliioni 89 na shilingi milioni 19,029 kwa Wizara/Idara Sekretariati za Mikoa na Balozi mtiririko huo.

Bajeti ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Wizara/Idara Sekretariati za Mikoa na Balozi kwa mwaka wa fedha 2013/14 yalikua shilingi milioni 639,631, shilingi milioni 49 na shilingi milioni 17,152 kwa mtiririko huo. Makusanyo halisi yalifikia

kiasi cha shilingi milioni 532,221, shilingi miliioni 14 na shilingi milioni 21,069 kwa Wizara/Idara Sekretariati za Mikoa na Balozi mtiririko huo.

Jedwali 15: Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa miaka mitatu (Kiasi katika shilingi milioni)

Mwaka wa Fedha	Taasisi	Makisio	Halisi zilizokusanywa	Makusanyo (Pungufu)/Zaidi ya Bajeti	% ya Halisi vs Makisio	% ya Makisio vs Zisizokusanywa
2015/16	Wizara/Idara	691,587	727,119	35,532	105.14	5.1
	Sekretarieti za Mikoa	26	47	21	182.00	82.0
	Balozi	19,368	22,023	2,655	113.71	13.7
2014/15	Wizara/Idara	701,558	597,607	(103,951)	85.18	(14.8)
	Sekretarieti za Mikoa	40	89	49	224.68	124.7
	Balozi	15,510	19,029	3,519	122.69	22.7
2013/14	Wizara/Idara	639,631	532,221	(107,410)	83.21	(16.8)
	Sekretarieti za Mikoa	49	14	(35)	28.57	(71.4)
	Balozi	17,152	21,069	3,917	122.84	22.8

Chanzo: *Hesabu za Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa zilizokaguliwa*

Kielelezo 8: Mwenendo wa mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara/Idara Sekretariati za Mikoa na Balozi(Kiasi katika shilingi milioni)



	2013/14	2014/15	2015/16
Makisio	639,631	701,558	691,587
Makusanyo Halisi	532,221	597,607	727,119

Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara na Idara za Serikali unaonesha mapato yaliyokadiriwa na makusanyo halisi yamekua yakiongezeka kwa miaka mitatu mfululizo. Licha ya kuwepo kwa ongezeko katika makusanyo baadhi ya Wizara na Idara za Serikali zimekua haziweki makisio ya mapato yasiyotokana na kodi ingawa wamekua wakikusanya. Hii inaonesha kuwa kumekuwapo na upungufu wa makisio ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Wizara na Idara za Serikali.



	2013/14	2014/15	2015/16
Makisio	49	40	26
Makusanyo Halisi	14	89	47

Kumekuwepo na kupanda na kushuka kwa makisio na makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Sekretariati za Mikoa. Baada ya kupitia taarifa za fedha za Sekretariati za Mikoa nimebaini kuwa wengi walikusanya ingawa walikua hawana makisio. Ninashauri Sekretariati za Mikoa kuweka makisio ya mapato yasiyotokana na kodi na kuongeza bidii katika kufikia malengo watakayokuwa wamejiwekea.



	2013/14	2014/15	2015/16
Makisio	17,152	15,510	19,368
Makusanyo Halisi	21,069	19,029	22,023

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi za Wizara/Idara, Sekretariati za Mikoa na Balozi zilizokaguliwa*

Mwenendo wa mapato yasiyotokana na kodi kwa balozi ingawa yanaonesha matokeo chanya baadhi ya balozi zimekua zikiweka makisio yasiyo halisi kwani wamekua wakikusanya zaidi sana ya walivyokadiria wakati baadhi ya balozi wamekuwa wakishindwa kufikia malengo ya makusanyo yao. Kati ya taarifa za balozi 33 nilizopitia, balozi 21 wamekusanya zaidi ya makisio yao wakati balozi 12 hawakuweza kufikia malengo waliyokuwa wamejiwekea.

4.9 Fedha za Ushuru wa Maendeleo ya Utalii ambazo hazikuletwa kiasi cha Shilingi bilioni 6.36

Kanuni ya 4(2) ya Kanuni ya Tozo za Maendeleo ya Utalii, 2013 inamtaka Mkurugenzi wa Utalii kupeleka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) orodha ya wote waliosajiliwa kuhusika na maswala ya malazi ya watalii na ambao wanapaswa kulipa tozo ya kulala/kitanda,(bed levy) Fedha zote zitumwe kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika mwaka wa fedha husika na baadaye kuwekwa katika akaunti ya Tozo za Maendeleo ya Utalii kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 9 (1).

Katika mwaka wa ukaguzi, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanywa kiasi cha shilingi bilioni 6.36 kama ilivyokuwa katika taarifa ya makusanyo ya kila mwezi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi mwezi Juni 30, 2016 fedha hizo zilizokua zimekusanywa hazikuwa zimehamishiwa kwenye akaunti ya Tozo za Maendeleo ya Utalii kama inavyotakiwa na Kanuni husika.

Kushindwa kuwasilisha makusanyo kama inavyotakiwa na kanuni husika inazuia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Utalii ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa bidhaa za utalii, kukuza masoko ya utalii, kujenga uwezo kwa watumishi wa sekta ya utalii, utafiti wa utalii na shughuli nyingine yoyote kwa ajili ya maendeleo na kuboresha sekta ya utalii kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 10 (a-e) cha Kanuni ya Tozo za Maendeleo ya Utalii, Kanuni, 2013.

.

UKAGUZI WA DENI LA TAIFA, PENSIHENI, MALALAKA YA MAPATO NA HESABU JUMUIFU ZA TAIFA

5.1 Ukaguzi na Usimamizi wa Deni la Taifa

5.1.1 Utangulizi

Deni la Taifa linahusu majukumu ambayo Serikali Kuu na Taasisi nyingine wanayo. Deni la Taifa linasimamiwa na Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebisha 2004) na Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali, 1974. Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali.

5.1.2 Mseto wa Deni la Taifa

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2016 lilikuwa shilingi bilioni 41,039.39 ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 11,193.39 na deni la nje bilioni 29,846.00 ikiwa ni ongezeko la bilioni 7,499.80 sawa na asilimia 22 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 33,539.59 lililoripotiwa 30 Juni 2015.

Deni la taifa limekuwa likiendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwepo kwa nakisi ya mapato ya serikali na matumizi, ubadilishwaji wa hati za ukwasi kugharamia bajeti ya serikali, na pia ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo na hasara katika kubadilisha fedha za kigeni ikisababishwa na kushuka kwa kasi kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na fedha nyingine za kigeni ambazo ni imara. Kielezo hapo chini kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa miaka mitano iliyopita;

Kielelezo 9: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano



	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Deni la Ndani	4,076	5,775	7,145	7,990	11,193
Deni la Nje	12,430	15,634	19,343	25,550	29,846
Jumla ya Deni	16,506	21,409	26,488	33,540	41,039

Chanzo: Hesabu za fedha za Fungu 22 - Deni la Taifa

5.1.3 Mseto wa Deni la Ndani

Mseto wa deni la ndani unajumuisha dhamana zinazouzwa sokoni, na zisizouzwa zenye ukomo tofauti kama vile dhamana za muda mrefu na hati fungani. Hadi kufikia 30 Juni 2016, Deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 11,193.39 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 7,989.77 zilizofikiwa mwishoni mwa Juni, 2015. Deni la ndani limeongezeka kwa shilingi bilioni 3,203.62 sawa na asilimia 40 ya deni la ndani lililorekodiwa mwaka jana.

Mikopo ya ndani katika mwaka ilifikia shilingi bilioni 6,698.99 ambapo sehemu yake shilingi bilioni 3,180.96 ilikuwa kwa ajili ya kukopea kipindi kingine na shilingi bilioni 1,802.25 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

5.1.4 Mseto wa Deni la Nje

Deni la nje linahusisha mikopo kutoka, Taasisi za Kimataifa na Washirika wa Maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni 2016 Deni

la nje lilikuwa shilingi bilioni 29,846.00 sawa na asilimia 73 ya deni la Taifa. Deni hili liliongezeka kwa shilingi bilioni 4,296.18 sawa na asilimia 17 ya deni la nje la shilingi bilioni 25,549.8 lililoripotiwa mwaka 2014/15. Mlinganisho wa Madeni ya nje kwa aina tofauti ya vyanzo ni kama ilivyo katika kielelezo hapa chini;

Kielelezo 10: Vyanzo vya deni la Nje hadi tarehe 30 Juni 2016



Ukaguzi wangu umebaini kwamba, ongezeko la deni la nje limechangiwa na ukopaji kutoka Mashirika ya Kimataifa kama vile Shirika la Maendeleo la Kimaitaifa (IDA) ambapo tumepokea jumla ya shilingi bilioni 927.7 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo na kijamii ikiwa ni pamoja na Mradi wa Kwanza wa Kuboresha Mazingira ya Kibiashara ili Kutengeneza Ajira (shilingi bilioni 169.5), Mradi wa Kuboresha Afya ya Msingi (shilingi bilioni 109.3), Miradi ya Usafiri (shilingi bilioni 75.9), na Programu ya Kuboresha Miji na Serikali za Mitaa (shilingi bilioni 52.6).

Vilevile, Serikali ilipokea fedha kutoka nchi wahisani (Ufaransa, Saudi Arabia na Japan) shilingi bilioni 108.1, Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara (ENCB) katika mfumo wa Mpangilio wa Mkopo wa nje kiasi cha shilingi bilioni

665.6. Mikopo kutoka ENCB ambayo hutolewa za Benki ya Korea, China na India zilielekezwa kwenye miradi muhimu kama vile Mitambo na Bomba la Gesi Asilia (Shilingi bilioni 201.4), Mpango wa Kuokoa Nishati na Nyumba Rafiki za Mazingira Tanzania (shilingi bilioni 196.5), Mradi wa Usambazaji Maji Dar Es Salaam na Chalinze (shilingi bilioni 54.6), Mradi wa Gesi Asilia wa Mnazi Bay na Songosongo (shilingi bilioni 59.9), na Awamu ya Tatu ya Mradi wa Taifa wa TEHAMA (shilingi bilioni 40.6).

Pia, Serikali ilipokea fedha kutoka Benki za biashara kiasi cha shilingi bilioni 349.5 ikiwemo shilingi bilioni 198.9 kutoka Benki ya Ushirikiano ya Kimataifa ya Japan kwa ajili ya Mradi wa Umeme Kinyerezi II-Megawati 240, na shilingi bilioni 127.6 kutoka Benki ya Hong Kong Shanghai kwa ajili Ujenzi wa Jengo Na. III la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Benki ya ING N.V. Corp. Serv. Amsterdam ilitoa shilingi bilioni 19.8 kwa ajili ya Ukarabati na Uboreshaji Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. **Kiambatisho 5.1** kinaonyesha mchanganuo wa miradi iliyowezeshwa na mikopo mipya iliyotolewa kwa Serikali kwa mwaka 2015/16.

5.1.5 Uwasilishaji pungufu na usio sahihi wa madeni na gharama za kuhudumia madeni

Kushushwa Kiwango cha Deni la Taifa kwa Kiasi cha Shilingi Bilioni 3,217

Mapitio ya machanganuo wa deni la taifa ilifahamika kwamba kiwango cha deni la taifa kilifikia shilingi bilioni 41,039.39 kufikia tarehe 30 Juni, 2016. Kiwango hiki hakijumuishi madeni ya shilingi bilioni 3,217 ikiwa ni madeni ya mifuko ya pensheni yaliyohakikiwa kiasi cha shilingi bilioni 2,991.4 (**Kiambatisho 5.2**) na dhamana zilizokiukwa masharti kiasi cha shilingi bilioni 225.6 **Kiambatisho 5.1** chini ya Idara ya Msajili wa Hazina.

Kwa upande mwingine, Serikali ilikuwa na madeni mengine ya mifuko ya pensheni ya kiasi cha shilingi bilioni 934 ambayo yalikuwa katika hatua za uhakiki. Kwa mtizamo wangu, madeni haya yanastahili kuwekwa wazi katika utaratibu na namna inavyotajwa kwenye aya ya 36 na 100 ya IPSAS 19. Pia, madeni haya yalipaswa kujumuishwa katika mnyumbuliko wa deni la taifa kwani Serikali ilishapokea huduma iliyotokana na mikopo hiyo. Kwa hiyo kuondolewa kwa madeni ya mifuko ya pensheni yaliyohakikiwa kiasi cha shilingi bilioni 2,991.4 na dhamana zilizokiukwa masharti kiasi cha shilingi bilioni 225.6 kwa mtizamo wangu imeshusha kiwango cha deni la taifa kufikia tarehe 30 Juni 2016 kwa kiasi cha shilingi bilioni 3,217.

Katika uchambuzi wangu wa hesabu za deni la taifa za mwaka 2015/16 na 2014/15 pamoja na Mpango wa Uuzaji Hati Fungani wa mwaka 2015/16 ulibaini kuwapo taarifa za madeni tarajiwa zisizoendana na ambazo hazikuwa na vielelezo vya kutosha.

Kwa kuzingatia hayo ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali; (i) kuharakisha utoaji dhamana isiyo ya fedha kwa mifuko ya pensheni ili kuwezesha madeni yake kuingia katika kasma ya deni la taifa, (ii) kuweka utaratibu madhubuti wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa waliokiuka masharti ya dhamana na kuweka masharti magumu ya utaratibu wa utoaji dhamana hapo mbeleni, na (iii) kuhakikisha madeni na madeni tarajiwa yanakuwa na vielelezo vya kutosha kabla ya kuwasilishwa katika vitabu.

Kuongezeka kwa Mikopo Isiyo ya Masharti Nafuu na Deni la Ndani Kunakopelekea Kuongezeka Gharama za Kuhudumia Deni.

Deni la taifa limekuwa likikua tangu mwaka 2007/08 wakati nchi ilipopata msamaha wa madeni. Uchambuzi wangu mseto wa deni umebaini kuwa deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 149 kwa miaka mitano iliyopita bila kuhusisha madeni yaliyoachwa nje ya mseto na asilimia 168 ikijumuishwa na madeni ya shilingi bilioni 3,127 yaliyo nje ya mseto.

Kama nilivyoeleza hapo awali, deni la taifa limekuwa likiendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwepo kwa nakisi ya mapato ya serikali na matumizi, ubadilishwaji wa hati za ukwasi kugharamia bajeti ya serikali, na pia ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo na hasara katika kubadilisha fedha za kigeni ikisababishwa na kushuka kwa kasi kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na fedha nyingine za kigeni ambazo ni imara. Kwa mfano, hasara katika kubadilisha fedha za kigeni iliyoripotiwa kwa mwaka 2015/16 ni kiasi cha shilingi bilioni 1,914.88 sawa ni asilimia 21 ya mikopo mipya ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,943 (42%) kwa mwaka 2014/15 na shilingi 663.6 (13%) kwa mwaka 2013/14. Kielelezo hapo chini kinaonyesha mjumuiko wa deni la nje yenye masharti nafuu na isiyo ya masharti nafuu kwa kipindi cha miaka mitano, 2011/12 mpaka 2015/16.

Kielelezo 11: Deni la nje kwa ulinganifu wa masharti nafuu na isiyo ya nafuu



	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Isiyo ya masharti nafuu	1,395	3,376	4,746	7,835	9,155
Yenye masharti nafuu	11,035	12,258	14,597	17,715	20,691

***Chanzo**: Hesabu za Fungu Na. 22 – Deni la Taifa*

Mwenendo wa deni la taifa unaonyesha kuwa bado kiwango kikubwa ni madeni ya masharti nafuu; shilingi bilioni 20,691 sawa na asilimia 69 ya deni la nje. Deni hilo limeendelea kubaki katika asilimia 69 kama kama ilivyokuwa mwaka 2014/15. Hata hivyo, mikopo isiyo ya masharti nafuu imeongezeka kutoka shilingi bilioni 7,835 mwaka 2014/15

mpaka shilingi bilioni 9,155 mwishoni mwaka 2015/16 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.

Mikopo nafuu ilikuwa asilimia 89 ya deni la nje mnamo tarehe 30 Juni, 2012 ikilinganishwa na asilimia 69 mwishoni mwa mwaka 2015/16. Hii ni kusema kuwa, mikopo isiyo ya masharti nafuu ilikuwa asilimia 31 ya deni la nje mnamo tarehe 30 Juni, 2016 ikilinganishwa na asilimia 11 miaka mitano iliyopita.

Inatarajiwa kuwa ongezeko la madeni ya nje yenye Masharti ya Kibiashara (ENCB) katika mseto wa deni la taifa utaongeza gharama za kuhudumia deni kadiri mikopo inavyoiva. Hii ni kutokana na vipindi vifupi vinavyotolewa katika kulipa deni ambapo mara nyingi huwa ni miaka mitatu, riba kubwa na muda mfupi wa deni kuiva mengi yakiwa ni miaka kumi.

Kupungua kwa mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa mashirika ya kimataifa na nchi wahisani na kuendelea kwa nakisi ya bajeti inalazimu Serikali kukopa mikopo isiyo ya nafuu ili fedha za kugharamia Bajeti ya Maendeleo. Ongezeko la mikopo isiyo ya masharti nafuu na mikopo ya ndani imesababisha gharama ya kukopa kuwa juu, hivyo natoa wito kwa watunga sera kuchukua tahadhari.

Ingawa uchambuzi wa uhimilivu wa deni kwa mwaka 2016 umeonyesha kuwa deni ni himilivu, uwiano wa gharama za kuhudumia deni na mapato ya ndani ulikaribia kuvuka kigezo cha asilimia 24 (Muongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti wa mwaka 2016/17, Januari 2016). Hii inaendana na matokea ya uchambuzi wa uhimilivu wa deni uliofanyika mwaka 2015 na 2016 ambayo ilionyesha kuwa uwiano wa gharama ya kuhudumia deni na mapato ya nchi unakuwa kwa kasi. Inatazamiwa kuwa kiwango cha uwiano huo kitaendelea kuwa kisichovutia kwa miaka 20 ijayo kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini :

Jedwali 16: Viashiria vya deni kwa miaka ishirini ijayo

External Public debt	Threshold	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2025	2035
PV of debt to GDP	50	20.9	19.9	23.5	22.9	21	20.2	20.9	18.4
PV of debt to Exports	200	104.4	97.7	99.2	96.9	95.7	99.3	98	89.5
PV of debt to Revenue	300	157.2	145.3	141.8	133.7	122.8	119.3	116	102.3
Debt service to exports	25	8.7	7.8	7.9	8.6	9.3	6.9	3.3	3
Debt service to revenue	22	13	11.5	11.4	11.9	11.9	8.3	4	3.5
Total Public debt									
PV of public debt to GDP	**74**	36.8	34.2	41	40.9	38.8	37.6	39.3	37.6
PV of public debt to revenue		277.4	249.9	247	238.9	227.2	222.2	219.5	209.4
Debt service to revenue ratio		23	30.8	27.9	32.9	47.5	28.2	27.5	31.1

Chanzo: Taarifa ya Uhimilivu wa Deni la Taifa, 2016

Kwa kuangalia gharama za kuhudumia deni la taifa, ni mtizamo kwamba ikilinganishwa na mapato ya ndani, gharama hizo ziko juu sana. Mapitio ya gharama za kuhudumia deni la taifa ikiwa inajumuisha marejesho ya mkopo, riba na malipo mengine yanayohusu deni yalibaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 3,858.37 ililipwa katika mwaka 2015/16.

Gharama za kulipa madeni zikichanganywa na gharama nyingine kama vile mishahara ya wafanyakazi ni gharama ambazo zinaiacha Serikali na kiasi kidogo cha fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii. Ni vyema kufahamu kuwa uchambuzi wa gharama hizi haujumuishi gharama ambazo zingetumika kugharamia madeni ya Serikali Kuu kiasi cha shilingi bilioni 3,127 ambayo hayakujumuishwa katika mseto wa deni la taifa. Kwa kuzingatia hayo, gharama za kuhudumia deni zimeshushwa.

Kwa mtizamo wangu, kutokana na rasilimali kuelekezwa katika kulipa madeni, ni kiashiria kuwa Serikali itaendelea kutegemea mikopo ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti na miradi ya maendeleo. Matokeo ya utegemezi huu ni kukua kwa madeni ya ndani na nje ambayo sio ya masharti nafuu kama vyanzo vya mapato ya ndani havitaimarishwa. Kwa

sababu hiyo, mikopo isiyo ya masharti nafuu na mikopo ya kibiashara itaendelea kuongeza gharama za kuhudumia deni (Tanzania Economic Update Report, May 2016).

Ingawa mikopo isiyo na masharti nafuu ni gharama na kwamba madeni ya ndani hayana hatari kubwa na hayaathiriki na kushuka kwa thamani ya shilingi, bado ni vyema kuwa na uwiano unaofaa kati ya vyanzo hivi viwili. Lengo la kufanya hivyo ni kuzuia msongamano wa sekta binafsi katika fedha chache zitakazokuwa zimebaki katika taasisi za fedha. Kielelezo hapo chini kinaonyesha mchanganuo wa deni la nje katika vipindi vya mwaka 2011/12 na 2015/16.

Kielelezo 12: Mchanganuo wa deni la nje mwaka 2011/12 na 2015/16



Chanzo: *Uchambuzi wa Hesabu za Deni la Taifa*

Kielelezo hapo juu kinaonyesha kuongezeka kwa kiwango cha mikopo ya kibiashara kutoka asilimia 9 mwaka 2011/12 hadi asilimia 15 mwaka 2015/16. Nayo mikopo kutoka Export import banks iliongezeka kutoka asilimia 3 hadi 16 katika kipindi hicho hicho. Kiujumla deni la nje limeongezeka kutoka shilingi bilioni 12,430.07 mwaka 2011/12 mpaka shilingi bilioni 29,846 bilioni mwishoni mwa mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia 140. Ndani ya ongezeko hilo mikopo ya masharti nafuu kutoka mashirika

ya kimataifa na nchi wahisani imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka.

Ni wazi kwamba, mashirika ya kimataifa yalichangia asilimia 66 ya deni la nje mpaka kufikia 30 Juni, 2012 ikilinganishwa na asilimia 56 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2015/16. Uwiano wa madeni ya nje kutoka nchi wahisani ulishuka kutoka asilimia 22 hadi asilimia 13 katika kipindi hicho. Katika mazingira haya, Serikali imelazimika kukopa katika vyanzo mbadala ambavyo ni mikopo isiyo ya masharti nafuu ili kupata fedha za kugharamia Bajeti ya Maendeleo.

Mapendekezo kwa Serikali;

(i) Iongeze juhudi za kukusanya mapato, ambapo itasaidia kuongeza uwezo wa kuhudumia madeni

(ii) Kupunguza kukopa mikopo yenye riba za juu sana na wakati huo huo kuweka mikakati ya kufikia viwango vya juu vya ukuaji uchumi

(iii) Kulipa sehemu ya deni la ndani kwa kununua sehemu ya hati fungani badala ya kusogeza mbele kila wakati

5.1.6 Kukopa Kutoka Benki Kuu ya Tanzania Kinyume na Sheria ya Benki Kuu ya 2006; Shilingi Bilioni 155

Katika mapitio ya mseto wa deni la ndani wa tarehe 30 Juni, 2016 nilibaini kwamba jumla ya deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 11.19 ndani yake ikiwemo kiasi cha shilingi 1.44 trilioni sawa na asilimia 13 (2015: shilingi trilioni 1.45) za hati fungani zinazoshikiliwa na Benki Kuu kwa masharti ya muda mrefu (zaidi ya mwaka) kinyume na Vifungu Na. 34(1)(b) na 35(1) vya Sheria ya Benki, 2006 ambavyo vinataja kuwa madeni ya namna hiyo yanapaswa kuiva sio zaidi ya miezi 12 tangu kuanza kwake.

Zaidi, nilibaini kwamba katika Mpango wa Uuzaji Hati Fungani za Serikali kwa mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kupunguza kiwango cha madeni inayodaiwa na Benki Kuu kwa shilingi bilioni 155. Hii ilikuwa ni hatua kuelekea kumaliza madeni ya namna hiyo na Benki Kuu ifikapo 2020/21 katika kuzingatia Ibara ya 5(2) ya Makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Masuala ya Kifedha (EAMU Protocol). Katika mapitio yangu ya utekelezaji wa Mpango wa Uuzaji Hati Fungani nilibaini kuwa Serikali ilikopa shilingi bilioni 155 kutoka Benki Kuu katika utaratibu wa muda mrefu. Ukopaji huo ulienda kinyume na malengo Serikali iliyojiwekea katika Mpango wa Uuzaji Hati Fungani. Hii inamaanisha pia kwamba Serikali inaweza isifikie malengo ya kumaliza madeni ya Benki Kuu ya muda mrefu ifikapo 2020/21 ili kuzingatia Ibara ya 5(2) ya Makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Masuala ya Kifedha.

Natoa wito kwa Serikali kuandaa mpango unaotekelezeka kumaliza madeni ya muda mrefu inayodaiwa na Benki Kuu. Napendekeza pia kuwa, Serikali iache kukopa kutoka Benki Kuu katika masharti ya muda mrefu ili kuendena na matakwa ya Makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Masuala ya Kifedha.

5.1.7 Kukopa Ndani ya Nchi Kupita Kiwango Kilichowekwa Katika Mpango wa Ukopaji wa Ndani

Mapitio yangu ya Mpango wa Ukopaji wa Ndani kwa mwaka 2015/16 na mseto wa deni la ndani kwa mwaka huo huo ulibaini kwamba Serikali ilikopa zaidi ya ilichopanga kwa asilimia 42.

Kulingana na mpango tajwa hapo juu mikopo ya ndani ya nchi ilitegemewa kutumika kwa kuhuisha hati fungani (shilingi bilioni 2,600), kugharamia bajeti (shilingi bilioni 1,464) na malipo ya malimbikizo (shilingi bilioni 660).

Ilibainika pia kwamba, Serikali ilipanga kusitisha kugharamia bajeti kwa kutumia hati fungani za muda mfupi. Hata hivyo, katika mapitio yangu ya mseto wa deni la ndani nilibaini kuwa hati fungani za muda mfupi za shilingi bilioni 4,476 zilitumika kugharamia bajeti kinyume na matakwa ya Mpango wa Ukopaji wa Ndani. Nina mashaka kwamba, Serikali kukopa bila kufuata mipango inayojiwekea inaweza kupelekea deni kufikia viwango ambavyo sio himilivu hapo mbeleni.

Napendekeza yafuatayo kwa Serikali, (i) kufuata Mpango wa Ukopaji wa Ndani inapokopa ndani ya nchi, (ii) kuboresha mseto wa deni lake la ndani ili kuakisi matumizi sahihi ya fedha zilizopatikana kutokana na mikopo ya ndani.

5.1.8 Kukopa Bila Ushindani Kutoka Benki za Biashara bila kupitishwa na Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Madeni (NDMC).

Katika mapitio yangu ya mseto wa deni la ndani, taarifa ya deni la taifa na mkataba Na. NMB/CBD/MOF/AUG/2015 dated 11th September 2015 wa mkopo kati ya Serikali na Benki ya NMB nilibaini kuwa Serikali ilikopa shilingi bilioni 118.34. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2016 kiasi cha shilingi bilioni 100 kilishatolewa na kuwekwa katika Akaunti ya Mapato ya Serikali Na. 39:901. Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 18.34 kilijumuishwa katika mkataba kwa ajili ya kufidia dhamana zilizokiukwa masharti zilizotokana na utaratibu wa Serikali kudhamini mikopo uliokuwa ukiratibiwa na Benki Kuu. Mapitio ya mkataba tajwa hapo juu yalibaini mapungufu yafuatayo;

5.1.8.1 Kukopa Bila Ushindanina kusababisha gharama zaidi shilingi milioni 535

Mkopo huu ulitolewa kwa mazungumzo ya moja kwa moja kati ya serikali na Benki ya NMB bila kuwakaribisha wakopeshaji wengine kitu ambacho kingeiwezesha Serikali

kulinganisha gharama na masharti ya mkopo. Matokeo yake riba sawa na hati fungani ya siku 182 na ada ya shilingi milioni 75. Jumla ya kiwango cha riba kwa hiyo ilikuwa 13.68% + 1% = 14.68% kwa mwaka.. Serikali ililipa gharama (riba + ada ya maandalizi) shilingi bilioni 6.706 ikiwa ni ziada ya shilingi milioni 535 kama ingekuwa ni asilimia 13.68 kwa mwaka na hakuna ada ya maandalizi kama mkopo ungepatikana kwa njia ya siku 182 za hati fungani. Hazina Jedwali 2 hapa chini linaelezea;

Jedwali 17: Ulinganisho wa gharama za kukopa 2015/16

Fungu kwa Awamu	Kiasi Shilingi bilioni			
	Kiasi cha mkopo	Riba Iliyolipwa	Riba ya ushindani	Riba iliyozidishwa
Disemba 31, 2015	33.3	3.07	2.86	0.21
Machi 31, 2016	33.3	2.44	2.27	0.17
Juni 30, 2016	33.3	1.22	1.14	0.08
Gharama za Mkopo		0.075		0.075
Jumla	**100**	**6.706**	**6.27**	**0.535**

Chanzo: *Hesabu zilizokaguliwa na uchambuzi wa kikaguzi*

Ukaguzi ulibaini pia, Serikali ilikopa mkopo wa kibiashara kutoka Benki njia ambayo haikuwa katika mpango wa mwaka 2015/2016 ambao ulitaka Serikali kuongeza madeni yake ya ndani kwa kutoa hati fungani.

5.1.8.2 Kukopa Kabla ya Mapitio na Idhini ya Kamati yaTaifa ya Usimamizi wa Madeni (NDMC)

Tathmini yangu ya taratibu zinazofuatwa kabla ya mikataba ya mkopo ilibainisha kuwa kuna wakati ambapo mikataba ya mikopo iliingiwa bila kufuata hatua zote muhimu kama ilivyoainishwa na Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya mwaka 1974 (kama ilivyorekebishwa 2004). Mfano Waziri wa Fedha alisaini mkataba upya (Working Capital Facility) kati ya NMB na Serikali wenye thamani ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya bajeti ya 2015/16 utakaosainiwa tena baada ya miezi 12 bila mapitio na

maamuzi ya awali ya Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Madeni (NDMC) ambayo ni kinyume na kifungu 16 na 17 cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 na Kanuni zake, 2003 ambayo inahitaji NDMC kujadili na kumshauri Waziri kuhusu masuala yote ya usimamizi wa madeni ya umma. Aidha, kama kukopa kutoka benki za biashara ilikuwa kinyume na mpango wa uuzaji wa hati fungani wa mwaka 2015/16 ambao ulitaka Serikali kukopa ndani kwa kutoa hati fungani.

Ingawa ninatambua kuwa Kamati ilipendekeza kusainiwa kwa mkataba wa thamani ya shilingi bilioni 100 kati ya NMB na Serikali kwa mwaka 2014/15 kusaidia bajeti ambao ulisainiwa kwa ziada ya miezi 12 lakini tathmini yangu ilibainisha kuwa mkataba wa mkopo wa mwaka 2015/16 ulikuwa na masharti ambayo hayakuwa sambamba na mkataba wa mwaka 2014/15 na hivyo haiwezi kuchukuliwa kama ni kusaini, mkataba wa awali upya kitaalam.

Kutofuata mchakato wa kupata mkopo, kwa maoni yangu, ulisababisha mapungufu yaliyoonekana awali kutokuwa na ushindani kabla ya kukopa na ushiriki duni wa NDMC ambayo ilisababisha kusaini mikataba ya mkopo yenye gharama kubwa za huduma ya kulipa deni suala ambalo ni mzigo kwa serikali. Hivyo suala la mikopo ya Serikali itaendelea kuleta walakini kama taratibu zilizofanyika awali hazitafanyiwa marekebisho kuongeza ufanisi.

Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa (a) Taratibu zote za kukopa zinapitiwa upya na vyombo vyote muhimu ikiwa ni pamoja na TDMC na NDMC kabla ya kusaini mikataba ya mikopo (b) Taratibu za kiushindani kabla ya kukopa zinatumika ili kuzingatia kifungu cha 7 cha Sheria ya Mikopo , Misaada na Dhamana ya mwaka 1974 (Ilivyorekebishwa 2004) na (c) Waziri wa Fedha kupata ushauri / mapendekezo kutoka kwa Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Madeni(NDMC) kabla ya kusaini mikataba yoyote ya mkopo ili kuhakikisha mikopo imefata taratibu ,

sheria na masharti ni mazuri , na (d) Kuzingatia mpango wa utoaji wa hati fungani katika kuingia mikopo ya ndani na nje.

5.1.9 Mapungufu katika Usimamizi wa Fedha za Serikali

Tathmini yangu ya Benki Kuu na mapitio ya hesabu za kasma hali ya kifedha vile vile mapitio ya taarifa zinazohusu akaunti ya overdraft kati ya Benki Kuu na Kitengo cha usimamizi wa Deni la Taifa (Fungu 22) ulibainisha kuwa Serikali ilikuwa na nakisi ya shilingi bilioni 1,188.09 kwa mwaka 2015/16 [2013/14: shilingi bilioni 608.86] ongezeko la asilimia 196 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.Matokeo yake, riba ya shilingi bilioni 162.57 ililipwa kutokana na overdraft kwa mwaka 2015/16 [2013/14: shilingi bilioni 72.55]. Ingawa overdraft (O / D) haikuzidi mipaka inayokubalika lakini kupanda kwa nakisi na gharama za riba ni vizuri kuangaliwa kwa umakini na Serikali.

Uchambuzi wangu zaidi ulibainisha kuendelea kupanda kwa overdraft na kuchangia katika Deni la Taifa na kusababisha kuwepo kwa nakisi ya bajeti hivyo kufanya serikali kuendelea kutumia vyanzo mbalimbali vilivyopo kuendesha bajeti ya nchi.Pamoja na kwamba, Serikali imechukua hatua katika fedha na ukwasi kwa kuhakikisha Taasisi zote za umma na Wizara kuwa na akaunti ya benki kuu, ni maoni kwamba bajeti ya Serikali ilikuwa na maoteo yasiyo halisi kwa kiasi nakisi na kukua kwa deni la Taifa.

Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwa jumla ya malipo yenye thamani ya bilioni 441.15 yalikua katika hatua ya malipo (CPO) kufikia Juni 30, 2016 jambo ambalo linaonyesha kuiweka Serikali katika hatua mbaya ya ukomo wa Overdraft kama malipo yangekubalika na kupitishwa na BoT. Kwa kuzingatia overdraft ya shilingi trilioni 1.188 katika tarehe hiyo hiyo, na kama hati za CPO zingelipwa

overdraft ingefikia trilioni 1.629 ambayo ni asilimia 23 zaidi ya ukomo wa shilingi trilioni 1.324 iliyowekwa kwa ajili ya serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Hii pia inamaanisha kuwa Serikali ilitoa idhini ya matumizi zaidi ya kiasi ambacho inaweza kukusanya hadi kufikia Juni 2016 na kama malipo ya CPO yote yangefanyika ukomo wa overdraft ungepitiliza na nakisi ya bajeti ingekua katika hali mbaya zaidi.Kwa maoni yangu kitendo hiki kilifanyika ili ukwasi wa Serikali kuonekana unaridhisha mazoea ambayo ni vyema kutafutiwa ufumbuzi sahihi na kuachana nayo.

Nashauri Serikali (i) kuimarisha taratibu za fedha na usimamizi ili kuepuka gharama za riba zisizo za lazima kutokana na overdraft, (ii) Kuhakikisha bajeti ya Serikali inakuwa halisi kuliko ilivyo sasa ili nakisi ya bajeti iwe rahisi kupata ufadhili na madeni kupunguzwa (iii) kuimarisha hatua za uhamasishaji makusanyo ya mapato na nidhamu ya matumizi ya serikali ili kuepuka kupanua nakisi na (iv) kuimarisha dhamira ya udhibiti wa matumizi na Serikali kutoa idhini ya matumizi kulingana na fedha zilizopo ili CPO iweze kulipa madai yanapojitokeza.

5.1.10 Muundo na Usimamizi wa Deni la Taifa nchini Tanzania kupitwa na wakati

Shughuli za Deni la Taifa ni muhimu kuwa wazi kwa kusimamiwa na Sheria, Kanuni na taratibu, ambapo tathmini itakuwa ikifanyika ili kuendana na masharti ya sasa. Mkakati wa Taifa wa Madeni (NDS) wa mwaka 2002 na malengo katika kufikia madeni ya muda mrefu ambayo ni himilivu na endelevu baada ya kukamilika kwa Mpango wa nchi masikini zenye Madeni Makubwa (HIPC) mpango ambao ulihitimishwa Novemba 2001 na kusainiwa kwa makubaliano ya Paris Club VII January 2002.

Mkakati wa Taifa wa Madeni (NDS) wa mwaka 2002 uliandaliwa kwa mazingira ya sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada ya 1974 (Ilivyorekebishwa 2004). Hali ya uchumi na mazingira wakati wa kuanzishwa kwa Sheria na mkakati wa NDS yamebadilika mno kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea.

Mkakati wa Taifa wa Madeni (NDS) wa mwaka 2002 haujawahi kufanyiwa marekebisho na marekebisho makubwa ya Sheria ya kusimamia deni la taifa yalifanywa Novemba 2004. Kutokana na kupanuka kwa wigo wa Deni la Taifa katika suala la vipengele na mikopo mikubwa ambayo imefanyika, Sheria na miongozo inayosimamia deni la taifa haiko sambamba na maendeleo hayo na vyombo vinavyotumika vimepitwa na wakati, na kwa sababu hiyo kufanya usimamizi wa deni la taifa kuwa changamoto.

Ninafahamu pia Serikali ilianza kuandaa Mkakati wa Kati wa Madeni (MTDS) kwa kushirikiana na IMF na Benki ya Dunia. Serikali ilitoa rasimu ya kwanza ya MTDS Juni 2011. Katika majadiliano yetu na Hazina ilibainika kuwa MTDS inaandaliwa katika nafasi ya Mkakati wa Madeni wa Taifa lakini Serikali bado inafikiria kuwa na Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa pamoja MTDS kutolewa kila mwaka kuisaidia sera. Pamoja na kupongeza juhudi hizi, MTDS na Sera ya Umma ya Madeni hazijaelezwa katika sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 (Ilivyorekebishwa 2004).

Natoa wito kwa Serikali (a) Kupitia Mkakati wa Taifa wa Madeni (b) Kuhakikisha Sera ya usimamizi wa Deni la Taifa inazingatiwa (c) Kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana, na Misaada ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004) na kanuni zake za 2003 ili kukabiliana na changamoto za sasa za usimamizi wa deni la Taifa.

5.1.11 Mfumo wa Kitaasisi wa Kusimamia Deni la Taifa Usioridhisha

Ukaguzi wa mfumo wa kitaasisi wa kusimamia Deni la Taifa ulibainisha kuwa majukumu ya msingi ya Deni la Taifa na usimamizi wake katika Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Katika ukaguzi nilibaini kuwa idara mbalimbali na Taasisi zinazohusika na masuala ya Deni la Taifa chini ya Wizara ya Fedha kama vile idara ya Uchambuzi wa Sera (PAD), Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN), Idara ya Fedha za Nje (EFD), Msajili wa Hazina, Tume ya Mipango na Benki Kuu ya Tanzania.

Wakati wa mahojiano kuhusu usimamizi wa Deni la Taifa nilibaini kuwa mfumo uliopo sasa wa usimamizi wa Deni la Taifa kugawanywa kwa mfumo waofisi ya mbele, kati na shughuli za ofisi ya nyuma zinaongeza uzembe katika uendeshaji, uratibu duni, na kutokuwa na taarifa za kutosha katika vitengo na taarifa sahihi kupitia taasisi na kusababisha kuwa na rekodi zisizo sahihi na zisizojitosheleza kuhusiana na deni.

Hali hii inatoa msisitizo kwa haja ya Serikali kuanzisha ofisi moja itakayojishugulisha na Usimamizi wa Deni la Taifa ndani ya Hazina ili kuimarisha shughuli za usimamizi wa Deni la Taifa ikiwa ni mbadala wa mfumo wa sasa ambao haujawa na matokeo mazuri.

Hivyo napendekeza, Serikali kuanzisha ofisi moja inayoshugulikia na usimamizi na kuimarisha usimamizi wa shughuli za Deni la Taifa.

5.2 Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu

Sehemu hii ya ripoti inawasilisha mambo ya msingi yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wa awali wa malipo ya Mafao ya wastaafu (Pensheni na kiinua Mgongo) katika kipindi cha mwaka 2015/16.

Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi hufanyika kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (iliyorekebishwa mwaka 2005) na Kifungu cha 29 na 5(a) cha Sheria ya Ukaguzi No.11 ya mwaka 2008 ambayo inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujiridhisha na kuidhinisha malipo yafanyike kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na kuhakikisha kwamba, Ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Hivyo, ni muhimu kufanya ukaguzi wa awali kwenye malipo yote ya Serikali ambayo siyo rahisi kuyatabiri na kutengewa fedha.

5.2.1 Lengo la Kufanya Ukaguzi wa Awali

Lengo la ukaguzi huu ni kuhakikisha usahihi wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi na kuwezesha kutambua makosa mapema ili kuhakikisha wastaafu wanalipwa kile wanachostahili. Hii ni muhimu kwa kuwa kiasi chochote kitakacholipwa kimakosa ni vigumu kurejeshwa kutoka kwa wastaafu.

Kwa upande mwingine, madhumuni ya uhakiki wa mafao ni kuhakikisha kuwa sheria husika na kanuni za mafao ya hitimisho la kazi, sera, miundo ya utumishi wa umma na muundo wa mishahara vinazingatiwa.

5.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi wa awali wa mafao ya hitimisho la kazi huhusisha watumishi wa umma ambao mafao yao hulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Ukaguzi hauhusishi Watumishi wa umma ambao mafao yao yanashughulikiwa na PSPF, PPF na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii. Ukaguzi wa awali wa mafao ulifanyika kwa kuhusisha:-

- Watumishi wa umma, watoa huduma mchanganyiko, wanajeshi na viongozi wengine, walimu na maafisa wa usalama.
- Malipo ya kimkataba kwa viongozi wa kisiasa, wageni toka nje, wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi, na raia waliopewa ajira wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45.
- Kiinua mgongo kwa watumishi wasiokuwa na mafao na pia.
- Malipo kwa viongozi wa juu na askari polisi.

5.2.3 Ufafanuzi wa Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo

Sehemu hii ya ripoti inaeleza mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao kwa mwaka wa fedha 2015/16.

5.2.4 Utekelezaji wa Mwaka (Ufanisi wa Kiutendaji)

Katika kipindi cha mwaka 2015/16, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilifanya ukaguzi wa awali wa mafao ya hitimisho la kazi kwa watumishi wa umma. Ofisi ilianza ukaguzi ikiwa na majalada 158 yaliyotokana na ukaguzi wa kipindi cha mwaka 2014/15. Katika kipindi hiki majalada ya wastaafu 4,514 yaliletwa kwa ajili ya kukaguliwa. Majalada 4,241 yalikaguliwa na kuidhinishwa, majalada **273** yalirejeshwa kwa Maafisa Masuuli husika kwa ajili ya masahihisho na yalikuwa bado yakiendelea na ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha 30 Juni, 2016 kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali 18: Mafaili ya wastaafu yaliyokaguliwa 2015/2016

Maelezo	Majalada
Idadi ya Majalada 1Julai, 2014	158
Majalada yaliyopokelewa	4,356
Jumla ya majalada ya ukaguzi	4,514
Majalada yaliyokaguliwa	4,241
Majalada yaliyobakia 30Juni, 2016	**273**

5.2.5 Makosa Katika Ukokotoaji wa Mafao ya Hitimisho la Kazi

Ukaguzi wa majalada kabla ya malipo ya Mafao ya hitimisho la kazi uliofanyika, ulibaini udhaifu katika ukokotoaji wa mafao yaliyofanywa na waandaji wa mafao husika kwa kuzidisha au kupunguza kiasi cha mafao ya hitimisho la kazi.

Kati ya majalada 4,241 yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 majalada 479 (11%) yalibainika kukokotolewa kimakosa. Ambapo majalada 274 yamebainika kuwa yamezidishwa kwa kiasi cha shilingi 1,120,442,386.01 huku majalada 205 yakiwa yamepunjwa malipo ya shilingi 595,863,986.41 kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini. Hata hivyo, makosa yaliyoainishwa hapo juu yanatia shaka juu ya utoshelevu wa utaratibu wa uhakiki wa karatasi za mafao, uwezo wa waandaji na wahakiki katika ustadi na uzoefu wa masuala ya pensheni na sheria husika.

Jedwali 19: Mafao ya hitimisho la kazi yaliyozidishwa

S/N	Maelezo	Mafao yaliyozidishwa (a)		Mafao yaliyopunjwa (b)		Jumla Halisi (a-b)
		Idadi ya kesi	Kiasi (shilingi)	Idadi ya kesi	Kiasi (shilingi)	(shilingi)
1	Kipindi cha utumishi kisicho sahihi	116	418,630,544.54	98	188,839,328.34	229,791,216.20
2	Mishahara ya iliyokosewa	69	441,320,838.11	50	215,011,588.36	226,309,249.75
3	Makosa katika ukokotoaji	6	62,103,624.41	21	125,436,541.43	(63,332,917.02)
4	Makosa katika michango ya NSSF	50	86,491,630.33	35	64,792,692.28	21,698,938.05
5	Mikopo/madeni	33	111,895,748.62	1	1,783,836.00	110,111,912.62
	Jumla	**274**	**1,120,442,386.01**	**205**	**595,863,986.41**	**524,578,399.60**

Chanzo: Fomu za malipo ya mafao

Kutokana na maelezo hapo juu, serikali ingepata hasara ya shilingi 1,120,442,386.01 kutokana na kuzidishwa kwa mafao ambapo wastaafu wangeweza kupunjwa mafao yao kwa kiasi cha shilingi.595,863,986.41 na hii ingepelekea hasara halisi ya shilingi. 524,578,399.60 kwa Serikali.

Kiasi hicho kilichookolewa ni matokeo ya ufanisi wa ukaguzi wa awali wa mafao yanayolipwa moja kwa moja toka

kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Zaidi ya hayo inaonesha jinsi ambavyo kushindwa kwa mifumo ya ndani ya udhibiti na mapungufu ya Maafisa Masuuli yangeweza kuigharimu Serikali na wastaafu kama ukaguzi wa awali usingefanyika.

5.2.6 Ucheleweshwaji Michango ya Kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii-shilingi 284 Billioni

Uhakiki wangu umebaini kuwa, makato ya kisheria ya jumla ya shilingi bilioni 284 yanayolipwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yalicheleweshwa kwa kipindi kati ya siku 30 mpaka siku 90 baada ya malipo ya mishahara ya mwezi. Hii ni kinyume cha Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hii pia ilikuwa kwa kesi ya madeni ya Mfuko wa Mafao kwa Watumishi wa Umma kabla ya mwaka 1999 na malimbikizo ya miaka iliyopita kwa mifuko yote ya hifadhi ya jamii.

Matokeo yake, niligundua ucheleweshwaji mkubwa wa ulipaji wa mafao kwa wastaafu waliokuwa wakichangia kwenye mfuko wa pensheni kwa watumishi wa umma mwaka huu. Kitu hiki kilikuwepo kwa mifuko yote ya hifadhi ya jamii. Kuchelewa kuwasilisha michango kwenye mfuko wa pensheni kwa watumishi wa umma nchini huigharimu serikali rasilimali nyingi kutokana adhabu zinazotozwa. Adhabu zinatozwa kwa Serikali na ugumu wa maisha kwa wastaafu (wanufaika) ungekuwa umeepukwa kama Serikali ingelipa michango hiyo kwa wakati hasa kwa mfuko wa pensheni kwa watumishi wa umma.

5.2.7 Hitimisho

Uchanganuzi huu unadhihirisha umuhimu wa ukaguzi wa awali katika malipo ya mafao ya wastaafu yanayolipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Hii ni kwa sababu bila kufanyika, Serikali ingepoteza jumla ya shilingi 1,120,442,386, ambapo wastaafu wangeweza kupunjwa mafao yao kwa kiasi cha shilingi 595,863,986 ambayo ingepelekea hasara halisi ya shilingi 524,578,399.60 kwa Serikali.

Uokoaji wa fedha hizo ni mojawapo ya mchango wa ofisi yangu kwa ukaguzi wa awali wa mafao yanayolipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na kuonyesha umuhimu wa kuimarisha mifumo ya ndani katika Taasisi za Serikali. Hii ni kwa sababu kwani mapungufu ya Maafisa Masuuli yangeweza kuigharimu serikali na wastaafu endapo ukaguzi wa awali wa mafao usingefanyika.

5.2.8 Mapendekezo

Napendekeza majalada ya mafao yaandaliwe vizuri kabla ya kuwasilisha katika ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi wa awali ili kupata taarifa sahihi na maelezo yenye usahihi na kuzuia wastaafu kulipwa mafao zaidi au kidogo kutokana na taarifa zisizo sahihi. Ni muhimu waajiri waelewe umuhimu wa kuwasilisha majalada ya pensheni kwa wakati na yakiwa yamekamilika, yakiwa na taarifa zote sahihi ambazo zitakazowezesha kufanyika kwa malipo sahihi ya mafao ya wastaafu.

Vile vile, napenda kusisitiza mapendekezo yangu kwa serikali;

- Maafisa masuuli wahakikishe waandaji wa mafao wanafuata kanuni na sheria za mafao. Wanapaswa pia kuhakikisha majalada ya pensheni yanayowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa awali ni kamili, sahihi na yanawasilishwa kwa wakati ili kuepuka ucheleshwaji wa malipo ya mafao ya wastaafu.
- Serikali itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa waandaji wa mafao ya pensheni ili kuongeza uelewa wao kuhusu sheria za mafao na mambo mengine yanayohusu mafao.

5.3 Ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania

5.3.1 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia na kukusanya mapato ya kodi kwa niaba ya Serikali.

Mamlaka inatayarisha aina mbili za Taarifa za Fedha; Taarifa za Mapato na Taarifa ya Hesabu za Matumizi. Taarifa ya Hesabu za Matumizi inaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya misingi ya fedha taslimu (IPSAS Accrual basis of accounting) wakati zile za Mapato zinaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha taslimu.

5.3.2 Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita

Katika barua ya mapungufu ya mwaka uliopita 2014/15, mapendekezo arobaini na tisa (49) yalitolewa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2015 na mapendekezo sabini na moja (71) yalisalia yakisubiri kufanyiwa kazi toka mwaka wa fedha 2001/02 mpaka 2013/14. Nimepitia hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa jumla ya mapendekezo mia moja na ishirini (120). Kati ya hayo 51 (43%) yanahusiana na Kitengo cha Forodha na ushuru wa bidhaa, 38 (32%) yanahusiana na kitengo cha walipakodi wakubwa na 31 (25%) kitengo cha mapato ya ndani kama ilivyoainishwa hapo chini.

Jedwali 20: Idadi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa mwaka 2001/02 – 2014/15

Na.	Mwaka	Kitengo cha Forodha na Ushuru wa Bidhaa	Kitengo cha Walipakodi Wakubwa	Kitengo cha Mapato ya ndani	Jumla
1.	2001/2002	1	0	0	1
2.	2002/2003	0	0	0	0
3.	2003/2004	0	0	1	1
4.	2004/2005	2	0	0	2
5.	2005/2006	4	0	0	4
6.	2006/2007	3	0	0	3
7.	2007/2008	5	1	1	7
8.	2008/2009	1	2	2	5
9.	2009/2010	2	2	2	6

Na.	Mwaka	Kitengo cha Forodha na Ushuru wa Bidhaa	Kitengo cha Walipakodi Wakubwa	Kitengo cha Mapato ya ndani	Jumla
10.	2010/2011	1	4	1	6
11.	2011/2012	3	4	0	7
12.	2012/2013	2	6	3	11
13.	2013/2014	7	6	5	18
	Jumla Ndogo	**31**	**25**	**15**	**71**
14.	2014/2015	20	13	16	49
	Jumla Kuu	**51**	**38**	**31**	**120**

Kati ya mapendekezo 120, ishirini na moja (17%) yalitekelezwa, sitini na nane (57%) yalikuwa kwenye hatua za utekelezaji na thelathini na moja (26%) hayakutekelezwa kabisa. Muhtasari wa mwelekeo wa utekelezwaji wa mapendekezo kwa vitengo vyote vitatu umeonyeshwa katika Jedwali hapo chini.

Jedwali 21: Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo kwa ujumla

Mwelekeo wa Utekelezaji	Kipaumbele cha Juu	Kipaumbele cha Kati	Kipaumbele cha Chini	Jumla	
	Na.	Na.	Na.	Na.	%
Yaliyotekelezwa	15	6	-	21	17
Hatua ya utekelezaji	60	8	-	68	57
Hayajatekelezwa	26	5	-	31	26
Total	**101**	**19**	**-**	**120**	**100**

Jumla ya mapendekezo yaliyo kwenye hatua za utekelezaji na yale ambayo hayajatekelezwa ni tisini na tisa (83%). Mapitio zaidi ya utekelezaji wa mapendekezo yaligundua kuwa, kati ya jumla ya mapendekezo yaliyotolewa, thelathini na moja (31) sawa na asilimia 37 yanahitaji maamuzi ya mamlaka nje ya Mamlaka ya mapato Tanzania kama vile Bodi za rufaa ya kodi, Mahakama ya rufaa ya Tanzania na Bunge kwa madeni ya kodi yaliyopendekezwa na Hazina kwa ajili ya kufutwa. Maamuzi ya kesi hizo na

kufutwa kwa madeni yamesubiriwa kwa muda toka mwaka wa fedha 2001/2002. Mapendekezo hamsini na mbili (52) yaliyobaki, sawa na asilimia 63, yanashughulikiwa na menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kulingana na uhalisia wa mapendekezo husika, mwelekeo wa utekelezaji unaridhisha, ila menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania inatakiwa kuongeza jitihada katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyoko chini ya utekelezaji ili kukomboa mapato yaliyozuiwa kutokana na mapungufu yaliyoainishwa na kukuza upatikanaji wa mapato zaidi.

5.3.3 Mwelekeo wa Mapato Tanzania

Katika ukaguzi huu, Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 13,383 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya shilingi bilioni 13,366. Hii inaonyesha ukusanyaji zaidi wa shilingi bilioni 17 ambazo ni sawa na asilimia 0.13 ya jumla ya makisio au malengo. Jumla ya makusanyo mbali na shilingi 25,689,882,934 zinazojumuisha misamaha ya kodi iliyotolewa na serikali, mapato halisi ya mwaka wa fedha 2015/2016 ni shilingi 13,408,852,308,300. Jedwali hapo chini linaonesha jumla ya makisio na makusanyo ya mapato toka Tanzania bara na visiwani:

Jedwali 22: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2015/16 (Shilingi kwa mamillion)

Idara	Lengo - Tanzania bara na visiwani	Makusanyo halisi kwa Tanzania bara na visiwani	Makusanyo pugufu	Makusanyo pugufu kwa asilimia	Asilimia ya makusanyo kwa Idara
Mapato ya ndani	2,355.73	2,330.40	(25.33)	(1.08%)	17.38 %
Walipako di wakubwa	5,591.60	5,602.78	11.18	0.20%	41.78 %
Forodha na ushuru wa bidhaa	5,419.07	5,449.99	30.91	0.57%	40.64 %
Jumla	13,366.40	13,383.16	16.76	0.13%	NA

Vocha	32.41	25.69	(6.72)	(20.74%)	0.19%
Jumla Kuu	**13,398.82**	**13,408.85**	**10.0**	**0.07%**	**100.00%**

Chanzo: **Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu za mwaka *2015/16***

Kwa ujumla, makusanyo yote katika idara zote tatu yalifikia malengo kwa mwaka huu. Hata hivyo, Idara ya Walipa kodi wa ndani ndiyo iliyoshindwa kufikia lengo kwa asilimia 1.08. Kielelezo hapo chini kinaonesha kwamba, Idara ya walipa kodi wakubwa ilikusanya asilimia 41.86 ya makusanyo halisi ambayo ndiyo sehemu kubwa kuliko zote; ikifuatiwa na Idara ya Forodha yenye asilimia 40.72; na kodi za ndani asilimia 17.41 ambayo ndiyo ya mwisho kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ukitoa hati za malipo ya Hazina.

Kielelezo 13: Asilimia ya Makusanyo halisi Kwa Idara kwa mwaka 2015/16



Kutokana na kiambatisho hapo juu ni dhahiri kuwa mchango wa makusanyo kutokana na mapato ya ndani umekuwa nyuma ikilinganishwa na vitengo vingine.

5.3.4 Ufanisi wa Kodi na Mwelekeo wa Mapato

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kwa wastani, ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na 2015/16 ambapo makusanyo halisi yalikuwa juu ya makadirio kwa asilimia 4 na 0.13 mtawalia. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha, Mamlaka imefanikiwa kuongeza

ufanisi wa mapato (uwiano wa kodi dhidi ya pato la jumla la ndani (GDP)) mpaka kufikia asilimia 13.68 baada ya kupungua kwa asilimia 4.12 kwa mwaka 2014/15. Ijapokuwa naipongeza Serikali kwa juhudi iliyochukua ya kuweka mikakati madhubuti dhidi ya wakwepa kodi na makusanyo ya mapato, uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani bado uko chini kwa asilimia 6.62 ya lengo lililowekwa na Mamlaka ya Mapato kufikia mwaka 2018 ambayo ni asilimia 19.9. **Jedwali** hapo chini linaonyesha mwelekeo wa makusanyo na uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani kwa kipindi cha miaka mitano kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Jedwali 23: Ufanisi kwa ujumla katika makusanyo ya mapato Tanzania (shilingi kwa milioni)

Maelezo	Mwaka wa fedha				
	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Lengo	6,329,413	7,978,158	10,957,001	12,078,015	13,220,252
Makusanyo halisi	6,586,585	7,912,304	10,026,659	10,743,765	13,238,045
Tofauti ya lengo na makusanyo	257,172	(65,854)	(930,342)	(1,334,250)	17,793
Tofauti ya lengo na makusanyo kwa asilimia	4	-1	-8	-11	0.13
Uwiano wa kodi dhidi ya zao la jumla la ndani (Tax/GDP)					
Tanzania	15.80%	16.00%	16.90%	12.78%	13.68%
Uganda			13.30%	12.77%	13.30%[21]
Kenya			22.10%	16.34%	19.70%[22]
Rwanda			14.90%	14.20%	16.10%

Chanzo: Takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2015/2016

Mchanganuo linganifu wa ufanisi wa kodi kwa nchi za Afrika Mashariki unaonesha kwamba, Tanzania iko nafasi ya tatu

[21] http://www.ubos.org/onlinefiles/uploads/ubos/KEI/KEI%20103rd%20Issue%20Q3%202016.pdf

[22] Republic of Kenya, Budget Speech for the Fiscal Year 2016/2017, June 08, 2016.

nyuma ya Kenya na Rwanda, na mbele ya Uganda katika uwiano wa zao la kodi dhidi ya zao la ndani la jumla. Kwa kuzingatia mwelekeo linganifu wa Kenya na Rwanda, ninaonelea kwamba, ufanisi wa kodi wa Tanzania kwa pande zote mbili za zao halisi na zao lengwa, zinaacha fursa ya maboresho zaidi ya kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato.

5.3.5 Mambo yaliyochangia kufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji mapato

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Mamlaka ya mapato Tanzania haikuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa kodi, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2011/12 na 2015/16 na mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato umekuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa kwa wastani wa asilimia 3 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Hatahivyo, mambo yaliyochangia ongezeko la makusanyo ya mapato katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 yanajumuisha;

(a) Usimamizi thabiti wa Serikali kuhusiana na usimamizi wa misamaha ya kodi pamoja na utekelezaji wa Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014 ambayo imesaidia kuziba mianya iliyokuwa inatumiwa katika ukwepaji wa kodi kwa kutumia Sheria ya zamani ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 na hivyo kupunguza utolewaji wa misamaha ya kodi kwa asilimia 32 kutoka miaka iliyopita.

(b) Uanzishaji wa Sheria mpya ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 ambayo imerahisisha mifumo ya ukusanyaji kodi na kuongeza nidhamu ya kufuata sheria za kodi kwa kuweka taratibu thabiti zinazosimamia marejesho ya fedha kwa walipa kodi ambao hawakutakiwa kulipa kodi ambapo malipo ya kodi yatafanyika kwanza na marejesho yataombwa baadaye.

(c) Ongezeko la udhibiti na usimamizi wa mifumo ya ushuru wa bidhaa zilizotoka nje na bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi, mifumo ya ukaguzi wa bidhaa zilizohifadhiwa kwa ajili ya kulipiwa kodi, usimamizi wa Mamlaka ya

maeneo huru ya uzalishaji wa bidhaa kwa mauzo nje ya nchi na usimamizi wa bidhaa zilizohifadhiwa katika bandari za nchi kavu.

(d) Ongezeko la usimamizi na uhakiki wa mifumo ya mafuta yaliyonunuliwa kutoka nchi za nje na mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi za nje limechangia katika kuongeza makusanyo ya mapato.

(e) Maboresho ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato na usimamizi yanayofanywa na Mamlaka ya mapato kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali katika ukusanyaji wa madeni ya kodi kutoka kwa wadaiwa wa muda mrefu na utozaji wa tozo kubwa kwa makosa yanayotokana na ukwepaji wa kulipa kodi yamechangia pia ongezeko la makusanyo ya mapato.

(f) Maboresho katika usimamizi na ufumbuzi wa malalamiko ya mapingamizi ya kodi yamechangia katika kuongeza makusanyo ya mapato katika mwaka huu wa fedha. Fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kuongeza kasi ya utoaji wa maamuzi wa madai ya malalamiko na pingamizi za kodi kwa vyombo vinavyosimamia pingamizi za kodi kama vile bodi ya rufaa za kodi na mahakama ya rufaa za kodi.

Natambua juhudi zilizochukuliwa na Serikali kuhusiana na ongezeko la makusanyo ya mapato nchini katika mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na Mamlaka ili kuongeza tija katika ukusanyaji zaidi wa mapato:

a) Kaguzi za kodi na uchunguzi wa kodi haukufanyika kwa kina na baadhi ya maeneo ambayo yalifanyiwa kaguzi hizo hakukuwa na ufuatiliaji wa kina wa kodi iliyotakiwa kulipwa. Nimegundua kuwa Mamlaka imeshindwa kukusanya riba na tozo zinazotokana na madeni ya kodi yasiyolipwa kwa muda mrefu yaliyotokana na kaguzi za kodi na uchunguzi wa kodi. Kasoro hizi pamoja na mifumo isiyoridhisha ya mapingamizi ya kodi

yamechangia kwa kiasi kikubwa ukwepaji wa kodi ambao unachangia katika kupunguza juhudi za makusanyo ya mapato.

b) Usimamizi usioridhisha wa uwasilishaji wa taarifa za hesabu za walipa kodi kwa ajili ya kufanyiwa makadirio ya kodi za mwaka, taarifa za Kodi ya ongezeko la thamani na wafanyabiashara wanaotakiwa kutambuliwa kuwa wamesajiliwa kwa ajili ya Kodi ya ongezeko la thamani. Kadhalika, kutotilia mkazo matumizi ya mashine za kielektroniki za kodi kwa wafanyabiashara wanaotakiwa kutumia mashine hizo, upangaji wa bei za bidhaa baina ya makampuni yenye mahusiano, kuwapo kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara zisizo rasmi na vyanzo vya mapato ambavyo havijagundulika kumechangia katika kupunguza kasi ya makusanyo.

c) Usimamizi usioridhisha wa uhakiki wa mifumo ya mafuta yaliyonunuliwa kutoka nchi za nje na mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi za nje katika bandari umechangia katika kupunguza makusanyo ya mapato.

d) Mapungufu katika usimamizi wa tozo na riba zinazotokana na kodi ambazo hazijalipwa na walipa kodi kwa kipindi kirefu kama ilivyotakiwa na Sheria za kodi yamesababisha kutofuatwa kwa matakwa ya Sheria na Kanuni za kodi; hivyo, kusababisha kushindwa kukusanya mapato kama yalivyokadiriwa.

e) Ucheleweshaji katika kushughulikia mapingamizi ya kodi ikiwa ni pamoja na kutokukusanywa kwa amana za kodi zinazotokana na mapingamizi ya kodi kabla ya kushughulikia pingamizi hizo. Mkusanyiko wa pingamizi za kodi katika mahakama za kodi ingawaje kumekuwa na maboresho kidogo.

5.3.6 Mapendekezo

Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa mikakati ya usimamizi madhubuti wa kodi inaimarishwa na inapewa

kipaumbele kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 na Sheria ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014. Na kuepuka uwekaji wa vifungu vya Sheria za kodi zinazotoa mianya ya ukwepaji wa ulipaji kodi. Katika maboresho ya Sheria za kodi zijazo, usimamizi wa ufuatiliaji wa kodi unapewa kipaumbele kikubwa ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya kodi ili hatimaye iongeze ufanisi kwenye makusanyo hasa katika maeneo yafuatayo;

5.3.6.1 Usimamizi wa Misamaha na Marejesho ya kodi

(a) Serikali iendelee kupitia sera na kanuni za kodi ili kuondoa misamaha isiyo na tija kwa nchi. Hii inaweza kufanyika kwa Mamlaka ya mapato kuongeza ufanisi kwenye uchunguzi na usimamizi madhubuti wa mifumo ya ulipaji wa misamaha ya kodi, pia iongeze ufanisi kwenye ufuatiliaji na uchunguzi kwa walengwa wa misamaha ya kodi ili kujiridhisha kama ilitumika ilivyokusudiwa.

(b) Serikali iendelee kusisitiza uwazi kwenye misamaha ya kodi kupitia machapisho ya misamaha ya kodi na ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuuu wa Hesabu za Serikali.

(c) Serikali iimarishe usimamizi wa marejesho ya kodi na kuongeza mifumo thabiti ya ukaguzi wa nyaraka za kudai marejesho ili kuondokana na madai batili kutoka kwa mtandao wa walipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT network). Pia isisitize utoaji na matumizi ya mashine za kielekitroni (EFD) kwa wafanyabishara wanaostahili.

5.3.6.2 Kaguzi na pelelezi za walipakodi

(a) Serikali iimarishe ukaguzi na kuweka mikakati madhubuti ili kupunguza ukwepaji wa kodi.

(b) Serikali isamehe sehemu ya riba na faini kwa walipa kodi walio radhi kulipa madeni yao na kuweka mbadala wa kuyalipa kwa vipindi ili kuwawekea mazingira mazuri ya kuwa waaminifu na kuendelea kulipa kodi zijazo kwa wakati.

5.3.6.3 Usimamizi madhubuti wa bidhaa na mafuta yanayoingizwa nchini

(a) Serikali iimarishe upekuzi na ukaguzi wa bidhaa zinazoingia kwa matumizi nchini na zinazokwenda nchi nyingine kupitia nchini na kuhakikisha kuwa hazitumiki nchini kinyemela bila kulipa kodi stahiki; na endapo zimeuzwa katika soko la ndani, mamlaka ikusanye kodi stahiki kwa mujibu wa sheria.

(b) Serikali iendelee kusisitiza matumizi ya "off-bond meters" na kuweka au kujenga Tenki la akiba la mafuta (National Reserve Tank (RT)) kwa kila bandari ya kuingilia ili kuhakikisha kuwa taarifa za mafuta yanayoingizwa nchini zinaandikwa sawasawa na usimamizi wa utoaji mafuta unaimarishwa sambamba na ulipaji wa kodi zinazotakiwa. Matumizi ya "flow meters" na tenki la akiba (Reserve tank) yatasaidia Mamlaka kuwa na taarifa sahihi ya mafuta yaliyoingia na yanayotoka; na hatimaye kuimarisha makusanyo kwenye mafuta yanayoagizwa.

5.3.7 Masuala maalum yaliyoonekana katika ukaguzi wa mwaka 2015/16

Sehemu hii inatoa taarifa juu ya maeneo makuu matatu ambayo yanahitaji usimamizi na uangalifu wa karibu wa menejimenti ya Mamlaka ya Mapato ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Maeneo hayo muhimu ni: Usimamizi wa pingamizi za Kodi, Usimamizi wa Misamaha ya Kodi na Usimamizi wa Makusanyo ya Kodi.

5.3.7.1 Usimamizi wa Pingamizi za Kodi: Kesi za muda mrefu katika bodi za rufaa za kodi shilingi bilioni 7,274

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina masuala yaliyo katika bodi za rufaa za kodi na Mahakama ya rufaa kwa muda mrefu yenye jumla ya shilingi bilioni 7,274. Ambapo, kiasi cha shilingi bilioni 214 kimekwama katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, shilingi bilioni 206 kimekwama katika Baraza la Rufaa za Kodi, na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 6,854 kinasubiri maamuzi katika bodi ya rufaa za kodi. Taarifa hii inaonekana kwenye Jedwali hapo chini:

Jedwali 24: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania

Na.	Mwaka	Bodi ya rufaa za kodi (Tax Appeals Board)		Baraza la rufaa za kodi (Tax Appeals Tribunal)		Mahakama ya rufaa Tanzania (Court of Appeals)		Jumla	
		USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")
1	2008			3,197.00	6,262.00			3,197.00	6,262.00
2	20			-	-	-	-	-	-
3	2010	-	526.00	-	-	-	-	-	526.00
4	2011	-	1,884.00	-	-	-	32,280.00	-	34,164.00
5	2012	-	295.00	279.00	3,154.00	-	16,736.00	279.00	20,185.00
6	2013	-	28,321.00	4,505.00	17,970.00	-	50,114.00	4,505.00	96,405.00
7	20	193.00	77,292.00	-	6,066.00	-	9,384.00	193.00	92,742.00

Na.	Mwaka	Bodi ya rufaa za kodi (Tax Appeals Board)		Baraza la rufaa za kodi (Tax Appeals Tribunal)		Mahakama ya rufaa Tanzania (Court of Appeals)		Jumla	
		USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")
	14								
8	2015	55,997.00	297,279.00	4,706.00	42,930.00	-	7,672.00	60,703.00	347,881.00
Sub-Total		**56,190.00**	**405,597.00**	**12,687.00**	**76,382.00**	**-**	**116,186.00**	**68,877.00**	**598,165.00**
9	2016	-	6,286,258.00	17,991.00	62,809.00	41,250.00	8,396.00	59,241.00	6,357,463.00
Total		**56,190.00**	**6,691,855.00**	**30,678**	**139,191.00**	**41,250.00**	**124,582.00**	**128,118.00**	**6,955,628.00**
Kiwango cha kubadilisha fedha kilichotumika SH.2170/USD									
		Jumla ya mapato yaliyokwama katika kesi (Sh. Milioni)						**278,016.00**	**6,955,628.00**
	A	Jumla ya mapato yaliyokwama katika kesi (Sh. Milioni)							**7,233,644.00**
	B	Bajeti ya mwaka 2015/16 (Sh. Mioni)							**22,495,492.00**
	C	Sehemu ya mapato ya kodi kwa asilimia ya bajeti (A/B*100)							**32%**
	D	Pato la jumla la ndani kwa mwaka 2015/16 (Sh. millions)							**96,769,156.00**

Na.	Mwaka	Bodi ya rufaa za kodi (Tax Appeals Board)		Baraza la rufaa za kodi (Tax Appeals Tribunal)		Mahakama ya rufaa Tanzania (Court of Appeals)		Jumla	
		USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")	USD ("000")	SH ("000'000")
E	Sehemu ya mapato ya kodi kwa asilimia ya zao la ndani (GDP) (A/D*100)								8%

Chanzo: Ripoti za mapato za Mamlaka ya Mapato Tanzania na daftari la kesi, 2015/16.

Ikilinganishwa na taarifa yangu ya mwaka wa fedha uliopita, mapato yaliyokwama katika rufaa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 6,850 hadi shilingi bilioni 7,274 kwa mwaka 2015/16 ambayo ni ongezeko la shilingi bilioni 423 sawa na asilimia 6. Uchanganuzi wangu unaonyesha mapato yaliyokwama katika rufaa ni asilimia thelathini na mbili (32%) ya bajeti ya mwaka 2015/2016 na asilimia nane (8) ya zao la jumla la ndani (GDP) kwa mwaka 2014/2015. Hivyo, thamani ya kodi inayobishaniwa katika bodi ya rufaa ya kodi na mahakama ya rufaa za kodi iko juu. Na serikali inaingia gharama katika kuendesha kesi hizi kwa muda mrefu. Pia, huingia hasara kwenye mapato pale mrufani atakapofilisika kabla ya kesi kuamuliwa.

5.3.7.2 Mapungufu na mifumo isiyoridhisha dhidi ya mapingamizi ya kodi

Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya pingamizi 140 za kodi kutoka kwa walipa kodi zenye thamani ya shilingi 858,236,909,894 ziliwasilishwa katika Mamlaka ya Mapato zikipinga kiasi cha kodi kilichokokotolewa na kufanyiwa tathmini na Kamishna wa kodi. Kuwapo kwa pingamizi nyingi za kodi ambazo hazishughulikiwi kwa wakati na kutolewa maamuzi kunatokana na upungufu wa wataalamu na rasilimali watu katika Mamlaka ya Mapato wa kushughulikia mapingamizi ya kodi ikilinganishwa na idadi ya mapingamizi yaliyoletwa na walipa kodi.

Kadhalika, ukaguzi wa pingamizi za kodi zilizowasilishwa na walipa kodi kwa mwaka wa fedha wa ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka ya Mapato ilishindwa kukusanya shilingi 13,744,500,270 ambazo ni fedha za amana zinazotokana na malipo yaliyotakiwa kulipwa ikiwa ni chochote kitakachokuwa kikubwa kati ya moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichofanyiwa tathmini na kutakiwa kulipwa na walipa kodi au kiasi cha kodi ambacho hakipo katika pingamizi, kinyume na Kifungu Na. 51 (5) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015.
Kutokukusanywa kwa fedha hizi kunachangia kwa kiasi kikubwa walipa kodi kutumia mwanya huu kukwepa kulipa

kodi. Hii inatokana na kutokuwepo kwa ufanisi katika kushughulikia mifumo ya pingamizi za kodi, hivyo, kusababisha mapato ya serikali kutokukusanywa kwa wakati. Hii inasababisha kutokufikiwa kwa makadirio ya makusanyo ya mapato ya Serikali, hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Vile vile, Ukaguzi wangu wa nyaraka mbalimbali za mapingamizi ya kodi katika mikoa saba (7) umegundua kuwa maombi ya mapingamizi ya kodi yenye thamani ya shilingi 15,083,331,726 yalikataliwa na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kutokana na kutokuwepo kwa sababu za msingi zinazoelezea mapingamizi hayo kinyume na Kifungu Na. 51 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015. Mapitio zaidi ya ripoti za mapingamizi ya kodi za kila mwezi yameonesha kuwa mapingamizi ya kodi yenye thamani ya shilingi 1,378,200,249 yalitolewa maamuzi na fedha hii ilitakiwa kukusanywa lakini haikukusanywa na Mameneja wa kodi wa mikoa husika na hivyo kufanya jumla ya shilingi 16,461,531,975 kutokukusanywa.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuongeza jitihada za kushughulikia kesi za mapingamizi ya kodi yaliyoletwa na walipa kodi kwa wakati ili kutoa maamuzi sahihi juu ya kodi sahihi inayopaswa kulipwa kwa wakati. Hili linawezekana kwa kuongeza idadi ya watumishi wenye utaalamu na ujuzi pamoja na kuwaongezea mafunzo ya kimbinu watumishi wote walio katika kitengo cha Huduma za Kiufundi ili kuboresha hatua za kutoa tathmini ya kodi inayopaswa kulipwa kwa wakati; hivyo, kupunguza idadi kubwa ya kesi za pingamizi za kodi ambazo zinachelewa kushughulikiwa.

(b) Kuangalia mahitaji ya kisheria ya kukusanywa kwa amana ya kodi inayotokana na ama moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichofanyiwa tathmini na kutakiwa kulipwa na walipa kodi au kiasi cha kodi ambacho hakipo katika pingamizi chochote kitakachokuwa kikubwa kabla mlipakodi hajaleta pingamizi la kulipa kodi kwa ajili ya kusikilizwa.

(c) Kuhakikisha ukusanyaji wa kodi zote ambazo pingamizi zake zilizowasilishwa zilikataliwa na ambazo maamuzi ya pingamizi yametolewa.

5.3.7.3 Ufuatiliaji na usimamizi usioridhisha wa Misamaha ya Kodi

Serikali, kwa kupitia Mamlaka ya Mapato, ilitoa misamaha ya kodi kwa ajili ya shughuli maalum zilizoainishwa katika sheria za kodi mbalimbali kama vile uwekezaji katika bidhaa za mtaji kwa kipindi maalum ili kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi. Vilevile na kukuza sera maalum za kiuchumi kama vile kuhamasisha uwekezaji katika sekta maalum, kuendeleza uhusiano na mataifa mengine kwa kutoa misamaha kwa shughuli za kidiplomasia na kwa sababu za kibinadamu.

Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2015/16 zinaonesha misamaha ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 1,100 ikiwa ni punguzo la shilingi bilioni 527 (asilimia 32) ikilinganishwa na misamaha ya kodi iliyotolewa mwaka 2014/15 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,627 (**Kiambatisho 5.4**). Ingawa kiasi cha misamaha ya kodi iliyotolewa katika mwaka huu wa fedha kimepungua, kiasi kilichotolewa bado ni kikubwa kwani ni asilimia 1.14 ya pato la ndani (GDP) kwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na malengo ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi kuwa chini ya asilimia moja (1) ya pato la ndani (GDP). Jitihada za kupunguza misamaha ya kodi zitasaidia Mamlaka ya Mapato kuongeza uwezo wake wa kukusanya kodi, hivyo kufikia malengo yaliyowekwa. Mwenendo wa misamaha ya kodi iliyotolewa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini;

Jedwali 25: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2012-2016 (shilingi kwa mamilioni)

Mwaka	Pato la Taifa kwa mwaka	Jumla ya misamaha ya kodi	Asilimia ya misamaha ikilinganishwa na pato la Taifa
2011/12	41,125,313	1,806,204	4.39
2012/13	48,385,100	1,515,607	3.13
2013/14	55,619,077	1,834,097	3.3
2014/15	84,279,922	1,627,012	1.93
2015/16	96,769,156	1,100,337	1.14

Kutokana na mchanganuo wa hapo juu, kiasi cha misamaha ya kodi cha asilimia ya pato la Taifa la jumla (GDP) kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kilikuwa asilimia 2.8 ya GDP. Kwa wastani, kiwango hicho bado kiko juu ikilinganishwa na lengo la asilimia moja ya pato la Taifa au asilimia tano ya makusanyo yote (Rejea bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2013/14). Misamaha iliyotolewa ilifikia kiwango cha chini cha asilimia 1.14 ya GDP katika mwaka wa fedha wa Ukaguzi kutokana na matumizi ya Sheria mpya ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 na Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali, nimebaini mapungufu yafuatayo yanayotokana na udhibiti na usimamizi wa misamaha ya kodi katika mwaka huu wa fedha.

5.3.7.3.1 Matumizi yasiyostahiki ya misamaha ya kodi kwa wanufaika wasiostahili Shs. bilioni 3.46

Mapitio yangu ya ripoti za kiuchunguzi wa kodi za tarehe 31 Mei, 2016 yalibaini manunuzi ya magari 238 kutoka nje ya nchi katika kipindi cha mwaka 2012 na 2014 kwa kutumia majina ya walipakodi wawili; ambapo, magari 175 yaliingizwa nchini kwa kutumia jina la M/s Lake Trans Ltd na magari mengine 63 yaliyobaki yaliingizwa nchini kwa kutumia jina la mlipakodi M/s State Oil (T) Ltd. Magari yote yalisajiliwa na kumilikiwa na walipakodi wasiostahiki

kunufaika kupewa misamaha ya kodi iliyotolewa. Jedwali hapo chini linaonyesha linaonyesha orodha ya magari yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi na kupewa misamaha ya kodi kwa wanufaika wasiostahiki.

Na.	Jina la Kampuni	Idadi	Kiasi cha Kodi inayodaiwa (Sh.)
1	A.Gure Transport Ltd	110	1,540,563,984.38
2	Al-Hushoom Investment	58	957,997,155.02
3	Lake Trans Ltd	5	70,496,098.40
4	E. Awadh & Co. Ltd	24	363,238,932.25
5	ATN Petroleum Co. Ltd	11	169,927,729.92
6	Simera Transport Ltd	6	71,137,753.92
7	FAA Truck (T) Ltd	18	192,809,247.31
8	Bafadhil Transports Ltd	6	88,837,365.51
	Total	238	3,455,008,266.71

Halikadhalika, nilibaini kuwa, wanunuzi wote wawili wa magari haya walikataa kuwa hawakununua magari haya. Hii inamaanisha kuwa uhalali wa misamaha ya kodi iliyotolewa ulikuwa ni na ubadhirifu kwa lengo la kuidanganya Serikali ili kukwepa kulipa mapato ya Serikali bila Serikali kufahamu; hivyo, suala hili linashughulikiwa na polisi kitengo cha uchunguzi. Swali la msingi ni kuwa iliwezekana vipi umiliki wa magari haya uliwezekana kusajiliwa kabla ya kulipa kodi iliyotolewa msamaha ya kiasi cha shilingi 3,455,008,267 au ni namna gani magari haya yaliyopewa misamaha ya kodi yalinunuliwa na wanufaika ambao hawakustahili kupewa misamaha ya kodi. Kwa namna yoyote ile, hii inathibitisha kuwa usimamizi wa mifumo ya utoaji wa misamaha ya kodi bado unahitaji kuboreshwa ili kupunguza matumizi mabaya ya misamaha ya kodi kwa wafanyabiashara wasiostahiki.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuendelea kupitia upya motisha za kodi zinazotolewa kwa lengo la kupunguza viwango vya misamaha ya

kodi hadi kufikia asilimia moja (1%) au chini ya zao la ndani (GDP) na kuongeza kiwango cha makusanyo ya mapato.

(b) Kuendelea kupitia sera za kiuchumi na kodi kwa lengo la kuondoa misamaha yote ya kodi isiyokuwa na tija. Hili linawezekana kwa kuboresha kaguzi na udhibiti wa motisha za kodi, kuimarisha usimamizi na uchunguzi dhidi ya matumizi ya motisha za kodi.

(c) Ichunguze na kukusanya kodi iliyotakiwa kulipwa yenye thamani ya shilingi 3,455,008,266.71 kutokana na magari yaliyonunuliwa nje ya nchi na kisha kuchukua hatua za kisheria kwa watuhumiwa wote waliohusika.

(d) Kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi inayotolewa kutokana na ununuzi wa magari kutoka nchi za nje kwa kuhakikisha kuwa magari hayo hayasajiliwi kwa kutumia majina ya watumiaji wengine zaidi ya watu waliyoyaagiza.

(e) Kuboresha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa misamaha ya kodi ya magari yanayonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa magari hayo hayasajiliwi kwa kutumia majina ya watu tofauti na waliyoyaagiza.

5.3.7.3.2 Tathmini ya mifumo ya udhibiti wa misamaha ya kodi za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji wa madini

Ulinganishi wa nyaraka za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za matumizi ya uchimbaji wa madini zinazohusiana na kampuni za uchimbaji wa madini za Buzwagi, Bulyanhulu na Geita pamoja na mapitio ya mifumo inayotunza taarifa za bidhaa za mafuta kupitia kitengo cha forodha makao makuu ulibaini jumla ya magari 49 na lita 4,248,802 za mafuta yalinunuliwa kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, sikuweza kujiridhisha kuwa mafuta hayo yalipokelewa na makampuni ya uchimbaji madini kwa

sababu hakukuwa na nyaraka zinazothibitisha mapokezi ya mafuta hayo. Magari husika yaliondoka Dar es Salaam katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2014 na Desemba, 2015. Nina mashaka kuwa lita 4,248,802 za mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi yanaweza kuwa yametumika kwa ajili ya matumizi mengine tofauti na shughuli za uchimbaji wa madini; hivyo, kuisababishia Serikali hasara ya ukosefu wa mapato.

Kadhalika, uchambuzi wangu wa nyaraka za matumizi ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi katika kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ya Buzwagi uligundua lita 20,791,072 za mafuta katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Julai, 2014 na Disemba, 2015 yalikuwa yamesafirishwa kwenda kwa mkandarasi M/S Aggreko Company Ltd ambaye hakustahili kupewa msamaha wa kodi. Jumla ya thamani ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi ilikuwa ni shilingi 10,174,647,166. Usafirishaji wa mafuta kwenda kwa makampuni ambayo hayastahiki kunufaika na misamaha ya kodi ni kinyume na matakwa ya Agizo Na. 480 la Serikali lilitolewa tarehe 25 Octoba, 2002 ambalo linataka kuachwa kutolewa kwa misamaha ya kodi za mafuta kwa makampuni ambayo hayastahiki kunufaika na misamaha hiyo.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na mafuta ambayo hayakupokelewa na makampuni ya uchimbaji wa madini na kukusanya ushuru wa forodha wenye jumla ya kiasi cha shilingi 1,599,031,214.

(b) Kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa kila mara wa walipa kodi wanaostahiki kupewa misamaha ya kodi ili kuhakikisha kuwa makampuni stahiki yanafuata taratibu na matakwa ya sheria na kanuni ili kuepuka hasara inayoweza kupatikana kutokana na utoaji wa misamaha ya kodi kwa wanufaika wasiostahili. Kuhakikisha makusanyo ya kodi ya mafuta ya shilingi 10,174,647,166 yaliyosafirishwa kwenda kwa mkandarasi asiyestahiki inakusanywa.

(c) Kufanya Ukaguzi na uchunguzi wa kila mara wa wanufaika wanaopewa misamaha ya kodi ili kuhakikisha kuwa makampuni yanatii sheria na kanuni; hivyo, kuepuka hasara inayoweza kutokea kutokana na matumizi tofauti ya misamaha.

5.3.7.4 Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizokaa katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na bidhaa zilizoruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum

Ukaguzi wa uhakiki uliofanyika katika ofisi za Ushuru wa forodha za mikoa na mipakani ulibaini kuwa, bidhaa 704 zilikuwa hazijalipiwa kodi kwa zaidi ya miaka kumi (10) zikisubiri taratibu na hatua za utoaji mizigo inayotakiwa kulipiwa ushuru wa forodha na hazikuwa katika hali nzuri. Kipindi hiki ni zaidi ya kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 42(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambacho kinahitaji bidhaa zote ambazo zimekaa katika maghala yaliyo chini ya uangalizi wa Idara ya Forodha (customs warehouses and customs bonded warehouses) kwa zaidi ya siku 60 ziuzwe kwa njia ya mnada wa wazi au kwa njia yoyote ambayo Kamishna ataona inafaa. Kuchelewa kuzinadi bidhaa hizi kunaweza kusababisha hasara ya kukosa mapato ya Serikali kutokana na uchakavu wa bidhaa hizi wakati wa mauzo.

Jedwali 26: Orodha ya bidhaa zilizokaa muda mrefu katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha

Na.	Mahali	Idadi
1	Bagamoyo, Misugusugu	62
2	Morogoro	12
3	Isaka	10
4	Kigoma	30
5	Rukwa	58
6	Kagera (Bukoba, Mtukula, Kabanga, Rusumo and Kyaka)	90
7	Mwanza	12
8	Sirari	198
9	Mbeya, Tunduma and	73

Na.	Mahali	Idadi
	Kasumulu	
10	Tanga, Horohoro, Pangani	70
11	Iringa, Makambako	62
12	Dodoma	9
13	Malindi	18
	Jumla	**704**

Mapitio yangu zaidi ya rejesta zinazohifadhi taarifa za bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje ya nchi na kuruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum katika mipaka ya Mtukula na Namanga ulibaini bidhaa zenye thamani ya shilingi 42,892,721,756 ambazo zilitakiwa kulipiwa ushuru wa forodha wenye thamani ya shilingi 2,461,287,015 hazikuweza kusafirishwa nje ya nchi kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12 na hakukuwa na vibali vilivyotolewa kisheria kuruhusu kuongezwa kwa muda wa bidhaa hizo kuendelea kukaa nchini. Hii ilibainika pia kwa magari 952 ambayo yaliruhusiwa kuingia ndani ya nchi na kupewa kibali cha kukaa kwa muda maalum kati ya mwaka 2015 hadi Juni, 2016. Hata hivyo hakukuwa na ushahidi unaothibitisha kuwa magari haya yaliondoka nje ya nchi baada ya kuisha kwa kipindi yaliyoruhusiwa kukaa nchini kinyume na Kifungu Na. 117(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

Kwa mtazamo wangu, kuwepo kwa bidhaa zilizokaa zaidi katika maghala ya kuhifadhia bidhaa zikisubiri kulipiwa ushuru wa forodha na magari yaliyokaa zaidi ya muda ulioruhusiwa kunaonyesha usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizokaa katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na bidhaa zilizoruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum kinyume na Kifungu Na. 117(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Mapungufu haya yanatoa mianya kwa wafanyabiasha wasio waaminifu, hivyo, Serikali kushindwa kukukusanya kodi stahiki.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuanzisha mifumo imara ya ufuatiliaji na utambuaji wa bidhaa zilizokaa zaidi katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na kuzinadi ili kuepuka hasara itakayotokana na uchakavu wa bidhaa hizo, hivyo, kuisababishia Serikali hasara ya kukosa mapato.

(b) Kuimarisha mifumo itakayoimarisha utoaji wa taarifa za bidhaa na magari yaliyoingia nchini na kupewa muda maalum ili kuweza kujua mahali yalipo na kuiunganisha mifumo hii katika mipaka yote ambayo magari haya yatatokea ili kuweza kuyafuatilia kwa ukaribu.

5.3.7.5 Kutokukusanya ushuru wa forodha kwenye maziwa yaliyoingizwa nchini wa shilingi 2,960,291,947

Upitiaji wa nyaraka mbalimbali za uingizwaji wa bidhaa nchini kupitia Mutukula, Bandari ya Mwanza Kusini na bandari ya Dar es Salaam ulibaini kuingizwa kwa maziwa yenye thamani ya shilingi 16,728,641,671 bila kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya shilingi 2,960,291,947 kinyume na jedwali namba mbili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la thamani ya mwaka 1997 (kwa maziwa yaliyoingizwa kabla ya Julai, 2015); na jedwali namba mbili la Kanuni za ushuru wa pamoja wa nje katika Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki ya mwaka 2012 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini;

Jedwali 27: Kiasi cha kodi ya Ongezeko la thamani kitokanacho na maziwa yaliyoingizwa nchini kulipiwa kodi kwa vituo

Na	Kituo	Thamani ya maziwa (SHS)	Kodi ya Ongezeko la thamani (SHS)
1	Mutukula	78,744,784	14,174,061
2	Mwanza South Port	311,538,159	56,076,869
3	Dar es Salaam Wharf	16,338,358,728	2,890,041,017
Jumla		**16,728,641,671**	**2,960,291,947**

Ninaishauri Serikali:
Nashauri serikali kuimarisha mifumo yake katika ukusanyaji wa kodi zitokanazo na uingizaji wa maziwa kuepuka upotevu wa mapato na pia kukusanya kiasi cha shilingi 2,960,291,947.

5.3.7.6 Mifumo isiyoridhisha ya Udhibiti wa mizigo katika bandari kavu

Ukaguzi wangu ulibaini nyaraka 769 za mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kupitia nchini kwenda nje ya nchi kupitia Tunduma na Kigoma yenye thamani ya kodi ya forodha ya shilingi 4,598,307,737. Aidha, sikuweza kupata ushahidi katika muundo wa rejista au mfumo kuthibitisha bidhaa hizo kutoka nje ya nchi kupitia mipaka hiyo. Kukosekana kwa ushahidi kunaashiria uwezekano wa bidhaa hizo kuuzwa na kutumika ndani ya nchi bila kulipiwa ushuru na kodi stahiki hivyo kuikosesha serikali mapato.

Ninaishauri Serikali:
Iimarishe mifumo ya bidhaa zinazopita ndani ya nchi kuelekea nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kuambatana na taratibu zilizowekwa kuepuka uuzwaji holela wa bidhaa zisizolipiwa ushuru, hivyo, kuisababishia serikali upotevu wa mapato.

5.3.7.7 Mifumo isiyoridhisha ya Udhibiti wa bidhaa katika maghala ya forodha na utoaji wa mizigo

Uchunguzi uliofanyika kwa bidhaa zilizoingizwa nchini katika ofisi za forodha tisa (9) mipakani, viwanja vya ndege, na bandari ulibaini miamala 327 yenye thamani ya shilingi 25,676,187,561 na kodi ya shilingi 5,139,493,119 zikiwa katika taratibu za utoaji kwa mujibu wa mfumo wa TANCIS kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali hapa chini wakati bidhaa husika zilikua zimeshatolewa. Kadhalika,

tuligundua bidhaa zilizokuwa katika mchakato wa kutolewa kwa muda mrefu zaidi ya miezi 12 toka tarehe ya TANSAD bila kukusanya kodi husika.

Jedwali 28: Bidhaa zilizoruhusiwa kutoka zikiwa na kodi

Na.	Mahali	Thamani ya Ushuru wa forodha (Shs)	Kodi iliyotakiwa kulipiwa (Shs)
1	Mutukula	5,491,843,279.02	1,241,438,609
2	Rusumo	37,769,581.77	7,146,514
3	Kabanga	1,039,509,352.66	240,766,549
3	Bukoba	2,125,934,483.87	373,730,151
4	Sirari	11,598,909,949.60	2,578,150,759
5	Uwanja wa Ndege Mwanza	1,071,097,801.61	247,269,899
6	Mwanza Bandari ya Kusini	3,853,203,735.20	355,767,936
7	Sumbawanga	120,091,678.10	38,735,252
8	Kasesya	54,796,992.77	47,734,428
9	Kigoma	283,030,705.95	8,753,022
	Jumla	**25,676,187,560.55**	**5,139,493,119**

Vilevile, ukaguzi wa taarifa zilizopo kutoka kwenye mfumo wa TANCIS kwa bidhaa zilizo hifadhiwa katika maghala ya forodha ulibaini makadirio ya kodi ya shilingi 9,319,598,661 inayotokana na bidhaa 9,943,906 zilizohifadhiwa katika maghala 10 ya ushuru wa forodha na hatukuweza kuziona bidhaa hizo katika maghala husika.

Ninaishauri Serikali:
limarisha na isimamie mifumo ya utekelezaji wa taratibu za utoaji mizigo katika ofisi za forodha, kufanya uchunguzi kwa bidhaa zilizotolewa kabla ya kukamilisha taratibu za forodha na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kukusanya kodi zote zinazotokana na bidhaa hizo.

5.3.7.8 Kodi ya thamani ya Shilingi bilioni 4.87 isiyo na ushahidi

Ukaguzi ulibaini kiasi cha lita 3,874,263 chenye kodi ya shilingi bilioni 2.45 kilichoingizwa nchini pasipo ushahidi wa taarifa za malipo ya kiasi cha kodi husika.

Katika nyakati tofauti, sikupatiwa nyaraka za ukusanyaji wa kodi kiasi cha Shilingi bilioni 2.42 kutoka kwenye lita 3,234,420 za mafuta yaliyoingizwa nchini na kampuni 24 za mafuta na kuchukuliwa na wamiliki kati ya tarehe 1 Januari hadi tarehe 30 Juni, 2016. Hii inaonesha mapungufu katika ukusanyaji wa kodi zitokanazo na uingizwaji wa mafuta.

Mapendekezo

Nashauri Serikali ifanye uchunguzi ili kubaini usahihi wa matumizi ya mafuta hayo na pale itakapoanika hayakutika ipasavyo, kodi husika zitozwe pamoja na riba. Pia Serikali iboreshe mifumo ya kusimamia uagizaji wa mafuta ili kuzuia matatizo haya kujitokeza katika siku zijazo

5.3.7.9 Ukusanyaji na usimamizi usioridhisha wa Tozo za Maendeleo ya Reli

Ukaguzi wangu wa miamala 1,005 ya vitu kutoka nje ya nchi vyenye thamani ya shilingi 19,505,289,410 katika ofisi za forodha Mtukula, Bukoba, Sirari na Mwanza ulibaini kuwa tozo za Maendeleo ya Reli ya kiasi cha shilingi 296,376,354 haikukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, upitiaji wa nyaraka mbalimbali za mafuta yaliyoingizwa kwa ajili ya matumizi hapa nchini kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulibaini kutokukusanywa kwa tozo za Maendeleo ya Reli ya kiasi cha Shilingi 5,664,388,491 inayotokana na lita 630,729,664 za mafuta zilizoingizwa na makampuni 27 ya usambazaji wa mafuta. Utaratibu huu ni kinyume na Waraka Na.10 wa tarehe 22/06/2015 unaoweka tozo ya asilimia 1.5 ya thamani ya bidhaa zote zinazoingizwa Tanzania Bara kwa matumizi kutoka nchi mbalimbali isipokua za Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vituo vya Mipakani, miamala iliyofanyika na orodha ya makampuni yaliyohusika ni kama inavyoonesha kwenye Jedwali hapo chini na **Kiambatisho 5.5**

Jedwali 29: Tozo za Maendeleo ya Reli isiyokusanywa kwa vituo

Na.	Kituo	Idadi ya miamala	Thamani ya Ushuru wa forodha (Shs)	Tozo ya Maendeleo ya Reli (Shs)
1	Sirari	19	10,251,972,266	153,779,584
2	Mutukula	929	7,910,631,178	118,659,468
3	Bukoba	43	1,260,810,169	18,912,153
4	Mwanza	14	81,875,797	5,025,149
Jumla		**1005**	**19,505,289,410**	**296,376,354**

Kadhalika, upitiaji wa makadirio na makusanyo ya kodi inayotokana na mafuta yaliyoingizwa nchini na mafuta yanayopita kwenda nje yaliyoidhinishwa kutumika nchini ulibaini ucheleweshaji wa malipo ya ushuru wa forodha; hivyo, kuvutia riba ya kiasi cha shilingi 3,311,171,293 ikiwa ni asilimia mbili (2) kwa mujibu wa kifungu Na.249 cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha kwa Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Hata hivyo, hapakuwa na ushahidi wa malipo hayo ya riba toka kwa makampuni 28 ya usambazaji wa mafuta yaliyochelewesha malipo hayo ya ushuru wa forodha.

Ninaishauri Serikali:

(a) Ikusanye Tozo za Maendeleo ya Reli kwa bidhaa zote zinazoingizwa nchini kwa matumizi kikamilifu kwa mujibu wa waraka na 10 wa tarehe 22/06/2015, ikiwemo kukusanya kiasi cha shilingi 5,960,764,845.

(b) Isimamie kikamilifu ukusanyaji wa riba ya asilimia mbili (2) kwa mwezi au sehemu ya mwezi kwa ucheleweshaji wa malipo ya ushuru wa forodha kwenye mafuta ikiwemo kukusanya kiasi cha shilingi 3,311,171,293.

Usimamizi usioridhisha wa makusanyo ya madeni ya kodi

Ukaguzi wangu wa usimamizi na makusanyo ya madeni ya kodi ulibaini kasoro zifuatazo :

5.3.7.10 Makadirio ya kodi ambayo haijakusanywa Sh. 588,833,422,160

Mapitio ya rejista inayohifadhi taarifa za uchunguzi wa kodi, rejista inayohifadhi taarifa za kodi ambazo hazijalipwa pamoja na nyaraka mbalimbali umeonesha kuwa kiasi cha kodi cha shilingi 588,833,422,160 hakikukusanywa kutoka kwa walipa kodi. Katika kiasi hicho, jumla ya shilingi 70,974,430,676 kinatokana na Idara ya Walipa kodi Wakubwa ambacho kinajumuisha riba ya kiasi cha shilingi 3,446,958,859.60. Kiasi cha shilingi 92,025,604,941 kinahusiana na Idara ya Uchunguzi wa Kodi. Na, kiasi cha shilingi 425,833,386,543.07 kinahusiana na Idara ya Mapato ya Ndani katika mikoa 10 ya kodi kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Kiasi hicho pia kinajumuisha pia riba inayotokana na kodi isiyolipwa na walipa kodi katika mikoa minne ya kiasi cha shilingi 31,002,818,053.75 na makusanyo ya kodi ambayo hayakuwa na viambatisho vinavyothibitisha makusanyo hayo ya shilingi 9,451,269,539.73 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapo chini:

Jedwali 30: Makadirio ya kodi ambayo haijakusanywa- Sh. 588,833,422,160

Mkoa wa kodi	Jumla ya Kodi (Shs)	Riba (Shs)	Makusanyo ya mapato yasiyo na viambatanishi (Shs)	Jumla Kuu ya Kodi (Shs)
Kilimanjaro	3,586.44	-	215.00	3,801.44
Temeke	41,870.97	-	507.00	42,377.97
Mbeya	1,810.02	-	-	1,810.02
Dodoma	8,777.40	-	-	8,777.40
Mtwara	1,307.60	-	-	1,307.60
Iringa	6,460.71	9,553.00	-	16,013.71
Morogoro	3,650.35	-	-	3,650.35
Shinyanga	955.97	-	-	955.97
Tanga	2,681.60	1,527.00	-	4,208.60
Ilala	314,278.24	12,385.00	5,360.00	332,023.24

Mkoa wa kodi	Jumla ya Kodi (Shs)	Riba (Shs)	Makusanyo ya mapato yasiyo na viambatanishi (Shs)	Jumla Kuu ya Kodi (Shs)
Mwanza	-	7,536.00		7,536.00
Kinondoni	-	-	3,367.00	3,367.00
Jumla-Ndogo	**385,379.30**	**31,001.00**	**9,449.00**	**425,829.30**
Idara ya Walipa Kodi Wakubwa	67,527	3,447	-	70,974
Idara ya Uchunguzi wa Kodi	-	-	-	92,025
Jumla Kuu				**588,828.30**

Kuwepo kwa madeni ya kodi ambayo hayajakusanywa kwa muda mrefu kunaleta swali kwa nini Mamlaka imeshindwa kukusanya kodi hizo. Kwa mtazamo wangu, mifumo na mikakati isiyoridhisha ya ukusanyaji wa madeni ya kodi hasa katika mikoa ya nje ya kodi umechangia katika kushindwa kukusanya madeni haya. Hii inamaanisha kuwa bado kuna nafasi ya kuongeza uboreshaji wa mifumo ya ukusanya wa madeni yanayotokana na kodi.

Makadirio pungufu ya kodi Sh. 7,534,260,240

Mapitio yangu katika baadhi ya majalada ya walipakodi na nyaraka nyingine zinazowahusu walipakodi kama vile marejesho ya kodi za mapato, taarifa za wanufaika wa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani, marejesho ya za kodi ya ongezeko la thamani na nyaraka mbalimbali kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka yalibaini kuwa kiasi cha kodi chenye thamani ya shilingi 7,534,260,240 kilifanyiwa makadirio pungufu. Katika kiasi hicho cha kodi, shilingi 1,309,978,057.42 kilitokana na uchunguzi wa taarifa za walipakodi 6 wa kodi ya ongezeko la thamani katika kitengo cha walipakodi wakubwa na shilingi 6,224,282,182.36 kilitokana na uchunguzi wa taarifa za

walipakodi katika mikoa ya kodi 12 katika kitengo cha mapato ya ndani kana jedwali hapo chini linavyoonyesha.

Jedwali 31: Makadirio ya kodi ambayo haijakusanywa katika mikoa ya kodi 12 ya Kitengo cha ukusanyaji wa mapato ya ndani

Na.	Mkoa wa kodi	Mapato pungufu (Shs)	Kodi pungufu isiyokusanywa (Shs)
1	Temeke	17,197,913,674.57	1,060,309,354.97
2	Arusha	113,438,363.58	49,940,320.52
3	Mbeya	79,740,447.00	23,922,134.10
4	Mwanza	600,382,327.00	180,114,698.10
5	Coast	402,882,555.00	106,647,366.50
6	Dodoma	3,868,160,968.00	1,145,864,521.80
7	Iringa	223,725,938.00	59,117,781.40
8	Morogoro	5,521,026,747.00	557,989,683.33
9	Shinyanga	54,067,171.00	6,414,571.05
10	Mara	1,754,355,620.00	105,271,416.00
11	Kinondoni	7,778,067,476.30	2,281,076,813.89
12	Ilala	3,118,085,701.00	647,613,520.70
	Jumla	**40,711,846,988.45**	**6,224,282,182.36**

Makadirio pungufu ya kodi yalisababishwa na makadirio pungufu ya mapato ya walipakodi katika marejesho yao ya kodi za mapato ya kila mwaka, marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani pamoja na mapitio hafifu ya taarifa za mapato ya walipakodi na taarifa za Mamlaka kuhusiana na makadirio ya mapato.

Kwa mtazamo wangu, kutokuwepo kwa ufanisi wa mifumo thabiti kunaweza kutoa mianya kwa watumishi wa Mamlaka wasio waaminifu kushirikiana kutoa makadirio yasiyostahiki ; hivyo, kuikosesha Serikali kupata mapato yake stahiki.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuimarisha uhakiki na udhibiti wa kaguzi na uchunguzi wa kodi ili kupunguza udanganyifu wa madai ya kodi zisizostahiki zinazotokana na mtandao wa walipakodi ya kodi ya ongezeko la thamani na kupunguza utoaji wa taarifa zisizostahiki za mapato kutoka kwa walipakodi.

(b) Kuboresha Ukaguzi na uchunguzi ili kupunguza madai yasiyostahiki ya walipa kodi wanaotokana na ukusanyaji wa kodi za ongezeko la thamani.

(c) Kufanya uchunguzi katika maeneo yote yaliyogundulika kuwa na upungufu wa kodi na kuhakikisha ukusanyaji wa kodi hizo pamoja na riba kama inavyotakiwa na Sheria za kodi.

5.3.7.11 Usimamizi wa utumiaji na utoaji wa mashine za kielektroniki

Upungufu wa mashine za kielektroniki kwa wafanyabiashara wanaostahili kutumia

Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 kinahitaji kila mtu anayeuza bidhaa, kutoa huduma au kupokea pesa kutokana na bidhaa au huduma aliyotoa kutoa risiti ya kielektroniki kwa kutumia mashine za kielektroniki. Ukaguzi wangu katika mwaka wa fedha 2015/2016 ulibaini kuwa wafanyabiashara waliosajiliwa kukusanya kodi ya Ongezeko la dhamani (VAT) wapatao 8,165 kati ya 9,743 sawa na asilimia 84 hawakuwa na mashine za kielektroniki kwa ajili ya kutoa risiti kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa kodi.

Aidha, ukaguzi wa walipa kodi wapatao 49,009 wanaotakiwa kutumia mashine hizo ingawa hawajasajiliwa na kodi ya ongezeko la thamani katika mikoa mitano (5) ulibaini kuwa walipa kodi 36,882 sawa na asilimia 81, hawana na hawatumii mashine za kielektroniki. Kutokutumia mashine za kielektroniki kunazuia usimamizi mzuri wa mapato kwa kurekodi miamala yote inayofanyika

hivyo, kutoa mianya ya ukwepaji wa kodi kwa wafanyabiashara kuficha kipato chao.

Ninaishauri Serikali:
Iendeleze uhamasishaji wa matumizi ya mashine za kielektroniki, hususani kwa wafanyabiasha wanaostahili kuzitumia kwa ajili ya kuimarisha utii wa sheria za kodi na kanuni za usimamizi wa mashine za kielektroniki.

5.4 UKAGUZI WA HESABU ZA TAIFA-HESABU JUMUIFU

5.4.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilirasimisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Hivyo Serikali iliiandaa hesabu jumuifu kwa mara ya kwanza mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2013 kwa kuzingatia matakwa ya IPSAS 6. Pamoja na nia ya dhati ya serikali katika kuboresha uwazi na uwajibikaji, ujumuishwaji wa taasisi za umma kwenye Taarifa za Hesabu za Majumuisho umeendelea kukumbwa na changamoto kadha wa kadha katika utekelezaji. Changamoto hizo ni pamoja na:

5.4.2 akosa ya Usahihi wa Jumla ya Fedha zilizoonyeshwa kwenye Vitabu vya Hesabu

Kanuni Na.25 (a) ya IPSAS 2 inahitaji kwamba fedha zinazotolewa tu ndio zitambuliwe kama mali kwenye mizania ya hesabu (Statement of Financial Position) na uainishaji katika kuwekeza shughuli kama vile malipo ya fedha kupata mali, vifaa na mali nyingine za muda mrefu. Malipo hayo ni pamoja na yale yanayohusiana na gharama za mtaji wa maendeleo na mali zilizojengwa za kujitegemea, mitambo, na vifaa.

Tathmini yangu ya notisi za Hesabu za Taifa kwa mwaka 2015/2016 kuhusiana na ujumlishaji wa fedha,upatikanaji wa mali za uwekezaji, Mali na Vifaa (PPE), mali zisizogusika (intangibles) na mali za kibayolojia ilionesha utofauti. Hii ni tofauti na hesabu mtiririko wa fedha (Cash flow) kutoka

kwenye shughuli za uwekezaji katika mtiririko wa fedha kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini

Jedwali 32: Makosa ya Usahihi wa Jumla ya Fedha

Bidhaa	Noti Na.	Jumla ya Kifedha kwenye Noti za Hesabu '000'	Jumla ya Kifedha kwenye mtiririko wa Hesabu '000'
Vifaa vya Uwekezaji	46	447,763,534	651,385,075
Mali na Vifaa	69	5,827,200,932	2,571,568,646
Mali zisizoshikika (Intangibles)	70	29,338,936	199,079,766
Mali za Kibayolojia	71	1,911,047	6,491,572

Ukaguzi zaidi na mahojiano kuhusu utofauti wa kifedha ulioonekana kwenye mali, mali zisizoshikika (intangibles) Uwekezaji, Mali za Kibayolojia na mali nyingine za muda mrefu kama zilivyoripotiwa katika taarifa hizi mbili,sikuweza kupata ushahidi wowote wa kuonesha sababu za utofauti. Hivyo, tofauti hizi zinaonesha kuwa Hesabu za Taifa zina makosa ya jumla za kifedha katika jumla za kifedha za mali.

Mapendekezo

Nashauri Serikali iwe na mfumo wa kuoanisha taarifa za Taasisi ili kuwa na uwezo wa moja kwa moja wa kutumia mfumo katika kuandaa hesabu jumuifu.

5.4.3 Kuandaa Hesabu za Majumuisho kwa Taasisi zinazofunga Hesabu kwa Tarehe Tofauti Bila Kufanya Marekebisho

Ukaguzi wa Hesabu za Majumuisho za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazoishia tarehe 30 Juni 2015 ulibaini kuwa taarifa za hesabu za Majumuisho zinazohusisha Taasisi za Umma haziwiani katika tarehe za kufunga hesabu. Hii ni kinyume na aya ya 46 ya IPSAS Na. 35 na Waraka wa Hazina Na.12 wa uliotolewa tarehe 9 Januari 2015 ambazo zinahitaji taarifa za fedha za Taasisi inayodhibiti na Taasisi zinazodhibitiwa kuwa na tarehe sawa ya utoaji taarifa. Pia, nilibaini kuwa hakuna marekebisho yaliyofanyika katika

hesabu ili kuoanisha tarehe. Hali hii inatia shaka kwenye uhalisia wa hesabu za majumuisho na inakinzana na aya ya 46 ya IPSAS Na. 35; kwamba, marekebisho yatafanywa ili kurekebisha matukio yanayotokea kati ya tarehe hiyo na tarehe ya taarifa za fedha na tarehe ya hesabu za Taasisi inayodhibiti. Katika hali yoyote, tofauti ya kuripoti kati ya Taasisi inayodhibiti na inayodhibitiwa isizidi miezi mitatu. Utaratibu huu unakiuka Waraka Na 3 wa 2015/16 katika kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2015/16 ambapo msisitizo wa Taasisi zinazofunga hesabu kwa vipindi tofauti kubadili ili kufuata utaratibu wa mwaka wa fedha unaoanzia tarehe 1 Julai hadi 30 Juni. Muhtasari wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini:

Na.	Jina la Taasisi	Mwaka wa Fedha wa Taasisi
1	TIB Development Bank	Dec-15
2	TIB Corporate Bank	Dec-15
3	Tanzania Postal Bank	Dec-15
4	Tanzania Women's Bank	Dec-15
5	Twiga Bancorp	Dec-15
6	Tanzania Telecommunications Company Ltd.	Dec-15
7	Kilimanjaro Airport Development Company Limited	Dec-15

Kuna haja ya serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ifuatilie kwa ukaribu jitihada zake ili kuhakikisha kwamba, taasisi za umma zinafunga hesabu katika vipindi sawa ili kupunguza muda unaotumika kufanya masahihisho ya hesabu zao. Kutokana na hali hii, naishauri serikali isimamie miongozo inayotolewa ili taasisi zote za umma zifunge hesabu zake sambamba na mwaka wa serikali. Pia, kupunguza changamoto zinazoweza kutokea wakati wa kusuluhisha vipindi tofauti vya hesabu na kuzingatia

Mapendekezo

Serikali ihakikishe kuwa Taasisi zake zinaandaa taarifa za ziada na marekebisho ya kifedha yanafanyika kwa usahihi ili kufuata mahitaji ya IPSAS 35, Waraka wa Hazina No 12 wa tarehe 9 Januari 2015 na Waraka wa Uhasibu Na 3 wa 2015/16.

5.4.4 Kukosekana kwa Tathmini ya Madai ya Pensheni kwa Serikali shilingi Bilioni 393.5

Tathmini ya Hesabu Jumuifu kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2016 ilibainisha kuwa shilingi bilioni 459.56 zilitengwa na Taasisi za Serikali kwa kwa ajili ya pensheni kwa wastaafu, likizo, kesi za kisheria na dhamana za kifedha. Uchunguzi zaidi uligundua kuwa asilimia 86 ya fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya mifuko ya pensheni kwa wastaafu.Nilibainisha kuwa Serikali ilionyesha katika Hesabu Jumuifu za shilingi bilioni 393.5 kwa ajili ya wastaafu, lakini hakuna tathmini ya madai iliyokuwa imefanyika ili kuainisha madeni halisi ya pensheni. Hii ni kinyume na aya 61 (a) ya IPSAS 25 ambayo inataka tathmini ifanyike ili kuwa na mpango wa pensheni ili kuwa na makadirio ya kuaminika kuonesha kiasi ambacho watumishi watanufaika kwa huduma ambayo wameitoa kwa kipindi cha nyuma na sasa.

Ninashawishika kusema kuwa bila Serikali kufanya tathmini ya madai ya Pensheni ili kujua jukumu lake kwa wastaafu, taarifa zinazotolewa kwenye hesabu Jumuifu zinaweza kuwa sio sahihi. Hivyo, bila kuwa na taarifa ya tathmini ni vigumu kujua mafao yaliyokadiriwa kama ni pungufu au sahihi.

Mapendekezo

Serikali inashauriwa kuzingatia IPSAS 25 kuonesha stahili za watumishi kwa kufanya tathmini ya madai ili kujua kiasi cha madeni kinachotokana na madeni ya wastaafu ya pensheni.

5.4.5 Kuandaa Hesabu za Majumuisho kwa Kutumia Mfumo Usiojiendesha

Wakati wa ukaguzi wa Hesabu Jumuifu nilibaini kuwepo kwa uandaaji wa hesabu bila kuwa na mfumo maalum unaojiendesha ingawa taasisi zote za Serikali kuu na Serikali za Mtaa, zinatumia mfumo wa EPICOR Kupitia mahojiano niliyofanya, nilibaini kuwa:

a) Balozi ambazo ziko chini ya Fungu 34 Wizara ya Mambo ya Nje na Mahusiano ya Kimataifa hazijaunganishwa kwenye mfumo wa EPICOR ;

b) Mifumo ya EPICOR ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa haijaunganishwa pamoja ingawa wote wanatumia EPICOR 9.05 ambayo kama ingetumika ipasavyo ingewezesha kuandaa taarifa za hesabu kwa ufasaha zaidi. Hii inamzuia Mhasibu Mkuu wa Serikali ya kupata taarifa moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa Serikali za Mitaa na kusaidia maandalizi ya Hesabu Jumuifu za Taarifa; na

c) baadhi ya Mafungu kutumia mfumo huru wa Epicor kutokana na hali ya shughuli zao, hivyo kuwa kikwazo katika kuandaa hesabu.

Aidha, katika ukaguzi wangu wa Hesabu Hesabu za Taifa, nilibainisha upungufu wa Madeni (sasa) kwa asilimia 21 ikilinganishwa na mwaka jana. Lakini uchunguzi wangu zaidi ulibainisha kuwa jumla ya madai katika Hesabu Jumuifu na za kutoka Taasisi mbalimbali ilitokana na mfumo wa EPICOR. Mahojiano na Menejimenti yalinibainishia kuwa hakuna malipo ambayo yanaweza kuruhusiwa bila kuwa na uhakika wa malipo. Hivyo, madeni ambayo hayajalipwa yalitakiwa yawe yameonekana kwenye mfumo kwa kutengewa fedha ndani ya bajeti iliyoidhinishwa. Hii inafanya malipo bila mfumo kuwa kama chaguo pekee kukwepa EPICOR. Kutokana na udhaifu huu, niliona Taasisi zikionyesha madeni makubwa kuliko bakaa ya fedha mwishoni mwa mwaka.Hii inaashiria kuwa madeni mengi yaliingizwa bila kutumia mfumo mwishoni mwa

mwaka kwa sababu yaliingizwa wakati taasisi hazina fedha kwenye mfumo.

Ni maoni yangu kuwa kuandaa hesabu Jumuifu bila kutumia mfumo kunasababisha makosa mengi ya kibinadamu ambayo mwisho yanasababisha taarifa za hesabu zisizo sahihi na hata marekebisho ya hesabu huchukua muda mrefu. Kukiuka utaratibu uliowekwa kwenye EPICOR kunasababisha madeni nje ya mfumo na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ingawa nakiri kuna changamoto ya kuandaa hesabu Jumuifu hasa kwa baadhi ya Mashirika ya Serikali ya Kibiashara (GBEs) hasa kwa wale wasiotumia Epicor na IPSAS Accrual, lakini naamini kwamba bado kuna nafasi kwa serikali kuunganisha mfumo wa serikali kuu na Serikali za Mitaa na hata mashirika ya umma. Kama mfumo utaunganishwa pamoja kwa kiasi kikubwa, utapunguza uwezekano wa makosa ya kibinadamu. Na utaimarisha ufuatiliaji na kufanya marekebisho kirahisi na kuwa taarifa sahihi na za kuaminika muda wote.

Naendelea kusisitiza mapendekezo yangu kwamba, serikali:

(a) Iunganishe mfumo wa moja kwa moja kuimarisha Wizara, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Serikali ya Kibiashara (GBEs);
(b) Iongeze kasi na jitihada za kuunganisha Balozi katika mfumo wa EPICOR ili kuimarisha udhibiti wa bajeti na usahihi wa taarifa zao za fedha;

(c) Ioanishe orodha ya halmashauri na Wizara, Idara na Taasisi ili kuwa na uwezo wa moja kwa moja kuandaa taarifa za fedha kutokana na mfumo wa EPICOR, na hivyo, kuunganisha taarifa za fedha za Taasisi za serikali kwa kutumia EPICOR; lakini mifumo ya uendeshaji imefanya Taasisi hizo zitenganishwe;

(d) Izalishe madeni kupitia mfumo wa EPICOR ili kudhibiti matumizi na kuhakikisha usahihi wa taarifa za fedha ambazo zinaandaliwa.

5.4.6 Mali za kibayolojia hazijabainishwa shilingi bilioni 122.9

Aya ya 39 ya IPSAS Na.27 inaeleza kwamba, “Taasisi itatoa maelezo ya mali za kibayolojia na kutofautisha kati ya mali za kutumiwa na mali za matumizi ya muda zaidi ya mara moja au zaidi ya mwaka; na kati ya mali za kibayolojia zilizohifadhiwa kwa ajili ya kuuzwa na zilizohifadhiwa kwa ajili ya kusambazwa bila malipo.

Pia, aya ya 42 inasema kwamba, “Katika kuonesha matakwa ya aya 39, Taasisi inatakiwa kutofautisha kati ya mali za kibayolojia zilizokomaa na ambazo hazijakomaa kama inavyotakiwa. Tofauti hizi hutoa taarifa ambazo zinaweza kuwa na manufaa katika kutathmini majira ya mtiririko wa fedha na uwezo wa huduma. Taasisi huweka wazi vigezo vya kuonesha tofauti”.

Katika mwaka wa ukaguzi, mali za kibayolojia ikiwa ni pamoja na ng’ombe wa maziwa, mizabibu, misitu, miti ya matunda na misitu ya mashamba vilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 84.0.

Pamoja na mapendekezo niliyotoa katika kaguzi zilizopita, katika ukaguzi wa mwaka huu, kutoka sampuli ambayo ilikuwa asilimia 93 ya mali za kibayolojia zilizo katika taarifa za kifedha nilibaini kuwa taarifa ya mali za kibayolojia hazikugawanywa kama inavyotakiwa na aya ya 39 ya IPSAS 27. Kwa upande mwingine, hesabu jumuishi katika noti 71 ilionyesha mali za kibayolojia kwa ujumla kiasi cha shilingi bilioni 122.9 kama mali za kibaiolojia zilizokomaa.

Kigezo cha kutambua mali hizo kama zilizokomaa hakikueleweka pamoja na kwamba, kwa mwaka huu, mali za kibayolojia kiasi cha shilingi bilioni 34.6 zimeongezeka kwa kuzaliwa na kununuliwa. Hii ni kinyume na waraka wa Kihasibu Na.3 wa mwaka 2015/16 juu ya namna taasisi zinapaswa kutoa taarifa ya mali za kibayolojia katika makundi kwa usahihi. Hivyo, kuna mashaka kama taarifa za mali za kibaiolojia zimeelezewa kwa usahihi.

Hivyo, nasisitizia mapendekezo yangu ya awali kuwa, Serikali itoe taarifa za mali za kibayolojia kwa kufuata IPSAS 27 na iingize taratibu za kutoa taarifa ya mali za kibaiolojia kwa taratibu za uhasibu na kutoa mwongozo kuongoza Taasisi namna ya kutaja mali za kibayolojia.

5.4.7 Mkanganyiko wa Taarifa za Mali "PPE" katika Regista ya Mali za Kudumu

Sehemu ya XII ya Waraka wa Kihasibu Na.3 wa mwaka 2015/16 uliotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali ilielekeza maafisa masuuli kuhakikisha kuwa Regista ya Mali inaakisi jumla ya thamani ya mali za kudumu ambazo zimo katika Taarifa ya Mizania.

Ili kufanikisha utaratibu wa kuandaa regista ya mali za Serikali, Mhasibu Mkuu wa Serikali aliunda kikosi kazi ambacho kilikusanya taarifa kutoka wizara, idara na taasisi zilizopo Dar es Salaam.

Mapitio yangu ya regista ya mali kutoka katika mfumo wa Epicor na ulinganisho wa taarifa kutoka mafungu 26 kati ya 55 ya Serikali Kuu, yalibaini kuwa, taarifa katika regista za mali hazijahuishwa. Hii ni kinyume na Waraka wa Kihasibu Na.3 wa mwaka 2015/16. Hivyo, taarifa zilizopo katika regista kuu ya mali iliyopo kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali haziendani na taarifa zilizopo katika regista za mafungu husika.

Ni mtizamo wangu kuwa, kuhuisha taarifa za mali kwa wakati kunawezesha taasisi kwa wakati wowote kuwa na kumbukumbu sahihi ya idadi na thamani ya mali zake; na pia, kuzuia matumizi ya mali yasiyofaa.

Ninaishauri Serikali: (i) Kuhakikisha kuwa taarifa katika regista za mali zinahuishwa kwa wakati na kutunzwa vyema ili kuwa na taarifa sahihi na zilizokamilika katika taarifa za kifedha, na (ii) Kuharakisha zoezi la kuunga akaunti ya madeni 'account payable' na mfumo wa kusimamia mali 'assets management module'.

5.4.8 Tofauti ya Taarifa Kati ya Hesabu Zilizokaguliwa Katika Taarifa Binafsi za Kifedha na Zile Zilizopo Katika Hesabu za Majumuisho

Mapitio yangu ya hesabu za majumuisho ili kupata uhakika wa usahihi wa taarifa zilizotumika katika uandaaji wake yalibaini kuwapo kwa tofauti kati ya taarifa za taasisi zinazomilikiwa na Serikali ambazo zimekaguliwa na taarifa ambazo zimetumika katika kuandaa hesabu za majumuisho.

Katika mahojiano na viongozi husika, ilifahamika kwamba tofauti hiyo inatokana na changamoto ya muda; ambapo, hesabu jumuishi zinaanza kuandaliwa kabla ya ukaguzi wa taasisi za Serikali kukamilika. Ilibainika kwamba hesabu jumuishi zinapowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kaguzi za baadhi ya taasisi za Serikali zinakuwa hazijakamilika. Hivyo, panapojitokeza marekebisho katika taarifa za kifedha za taasisi hizo ndipo tofauti hizo hujitokeza ikizingatiwa kwamba mfumo wa majumuisho sio wa kujiendesha wenyewe 'automated'. Mazingira haya yanaweka hatarini utegemezi wa taarifa zilizopo katika hesabu za majumuisho.

Hivyo ninaishauri Serikali: (i) Kufanya marekebisho ya taarifa zilizopo katika hesabu za majumuisho kwa kuingiza taarifa zilizokaguliwa; na (ii) Kufanya mfumo wa kutengeneza hesabu za majumuisho kuwa wa kujiendesha wenyewe 'automated'.

SURA YA SITA

TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA

6.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia udhaifu katika mifumo ya udhibiti na masuala ya utawala, udhaifu huo umeonyeshwa katika ripoti hii.

Udhibiti wa ndani ni mchakato kwa kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa Hii ikijumuisha: uwepo wa ufanisi, kuzingatia sheria, kanuni na sera katika kulinda mali na kuwa na taarifa sahihi za kihasibu. Wakaguzi wa ndani wana wajibu wa kupitia na kuthibitisha kama taasisi inazingatia sheria, kanuni na sera, taratibu zilizowekwa.

Afisa Masuuli, Bodi za wakurugenzi, menegimenti za taasisi na wafanyakazi wengine wana jukumu la udhibiti wa mfumo wa ndani.

Wakati wa kuandaa mpango wa ukaguzi na wakati wa ukaguzi, udhibiti wa ndani kwa ajili ya maandalizi na uwasilishaji wa taarifa za fedha ulizingatiwa ili kuwa na taratibu za ukaguzi ambazo ni sahihi, lakini si kwa lengo la kutoa maoni juu ya ufanisi wa udhibiti wa ndani.

Tathimini mahususi ilifanywa juu ya vyombo vya usimamizi na udhibiti ya mifumo ya ndani ikijumuisha utendaji wa Kamati za Ukaguzi, kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, TEHAMA, tathmini ya viashiria vya hatari, na kuzuia udanganyifu.

6.2 Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani katika Taasisi

Kulingana na Kanuni ya 28(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inamtaka kila Afsa Masuuli kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kutoa uhakika iwapo mifumo ya ndani ya Taasisi inafanya kazi ipasavyo.

Hata hivyo, tathmini ya ukaguzi iliyofanyika kuhusu ukaguzi wa ndani kwenye sampuli ya Wizara, Idara na Taasisi pamoja na sekretarieti za Mikoa nilibani Taasisi 33 zikijumuisha Wizara na Idara 14, Sekretarieti za Mikoa 17 na Taasisi zingine 2 zilionekana na mapungufu yakiwemo; kutokuwanzishwa kwa vitengo vya ndani, vitendea kazi

hafifu na mipango ya ukaguzi wa ndani kutoidhinishwa na Kamati ya Ukaguzi. Angalia

Inaonyesha kuwa idadi ya Taasisi zenye mapungufu zimeongezeka kutoka 32 hadi 34 mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana sawa na ongezeko la asilimia 5.

Orodha ya Taasisi zenye mapungufu kwenye kitengo cha Ukaguzi wa Ndani zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 6.1**

Kutokuwepo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani ambacho ni madhubuti hatari ya kuwepo udanganyifu, kutofuata sheria, taratibu, maelekezo na sera huongezeka. Mbali na hayo Taasisi zinakosa nafasi ya kupata mapendekezo kwa ajili ya kuimarisha sera na taratibu za utendaji.

Mapitio ya shuhuli za Taasisi na kitengo huru ni muhimu sana na napenda kushauri Maafisa Masuuli kuwa na vitengo vya Ukaguzi wa Ndani vyenye rasilimali za kutosha; na kutimiza wajibu wake ambapo ni pamoja na kuainisha mapungufu ya udhibiti wa ndani na kutoa mapendekezo ya marekebisho na ushauri utakaoleta tija.

6.3 Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi

Kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inataka kila Taasisi kuwa na kamati ya Ukaguzi. Wajumbe wa Kamati na majukumu yake vimeainishwa kwenye Kanuni ya 31 na 32 ya Sheria ya Fedha. Majukumu yake ni pamoja na lakini si hayo tu; kuwa na vikao vya kila robo mwaka, Kuidhinisha mpango wa ukaguzi wa ndani kila mwaka, kupitia taarifa za ukaguzi wa ndani na nje, kutoa ushauri kwa Afisa Masuuli juu ya hatua za kuchukuliwa juu ya mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti ya ukaguzi wa ndani au kwenye ripoti ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa ripoti ya kila mwaka juu ya kazi zake.

Hata hivyo, tathmini ya ukaguzi katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi katika Wizara, Idara, Sekretari za Mikoa nilibaini Taasisi 31 zikijumuisha Wizara na Idara 14 ,Sekretarieti za Mikoa 12 na Taasisi zingine 5 zilipatikana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na; Taasisi kutokuwa na Kamati ya Ukaguzi, kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa

mwaka wa ukaguzi wa ndani na kutokupitia taarifa za hesabu za Taasisi.

Inaonyesha kuwa idadi ya Taasisi zenye mapungufu katika Kamati za Ukaguzi hazikuongezeka wala kupungua ukilinganisha na mwaka uliopita.

Orodha ya Taasisi zenye mapungufu kwenye Kamati za Ukaguzi zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 6.2**

Napendekeza kwamba, Maafisa Masuhuli wahakikishe Kamati za Ukaguzi zinafanya kazi kulingana na sheria kama zilivyoanishwa kwenye sheria ya Fedha za Umma ili kuhakikisha malengo ya Taasisi husika yanafikiwa na kuhakikisha uwajibikaji, uwepo wa taarifa za fedha zakuaminika pamoja na kufuata sheria, taratibu na sera.

6.4 Mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi

Usimamizi wa vihatarishi ni utaratibu wa kufanya na kutekeleza maamuzi ambayo hupunguza madhara makubwa katika utendaji wa Taasisi. Utaratibu wa usimamizi wa vihatarishi inahusisha; kutambua na kuchambua vihatarishi vinavyoweza kuleta hasara, kuchuchunguza mbinu mbadala za kuthibiti vihatarishi, kuchagua mbinu sahihi zaidi ya usimamizi wa vihatarishi, kutekeleza mbinu iliyochaguliwa na ufuatiliaji wa matokeo.

Pia nilitathimini Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa katika utaratibu uliopo wa usimamizi wa vihatarishi kwa lengo la kupima maandalizi yao kwa matukio yasiyotarajiwa ambayo kama yatatokea yataathiri uendelevu wa utoaji wa huduma kwa umma na kubaini Taasisi 21 ikiwa ni pamoja na Wizara na Idara 9, Sekretarieti za Mikoa 12 ambazo zina mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kutokuwa na Rejista ya vihatarishi, kutokuwa na sera ya kudhibiti vihatarishi, kuwa na Rejista isiyoenda na wakati, kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na majanga.

Inaonyesha kuwa idadi ya Taasisi zenye mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi imeongezeka kutoka 11 hadi 21 ikilinganishwa na mwaka jana ikiwa ni ongezeko la asilimia 91.Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 6.3**

Ili kuhakikisha huduma bora kwa umma na kuwa na athari ndogo ya matukio yenye athari yasiyotarajiwa, Maafisa Masuuli wanashauriwa kuimarisha taratibu za usimamizi wa vihatarishi kwa kuhakikisha kwamba; kuwa na kumbukumbu za usimamizi wa vihatarishi kwa kuvitambua, kuvichunguza, mbinu mbadala ya usimamizi wa vihatarishi, kuchagua mbinu sahihi zaidi ya usimamizi wa vihatarishi, kutekeleza mbinu iliyochaguliwa na ufuatiliaji wa matokeo.

6.5 Kupitia Mifumi ya TEHAMA

Ikiwa ni sehemu ya ukaguzi, tathmini ilifanyika kwenye mifumo ya TEHAMA ili kujiridhisha kama Taasisi za Serikali zimeweka mfumo wa ndani wa TEHAMA unaodhihirisha usiri, wenye uwezo wa kutoa taarifa sahihi za kihasibu na nyinginezo ambazo zinatunzwa humo.

Matokeo ya ukaguzi yalionyesha kuwa Taasisi 19 zimekiuka taratibu za TEHAMA, ukiukwaji huo ni pamoja na;

Kutokuwa na Mpango wa kukabiliana na majanga ya TEHAMA, sera, kutokujaribu ufanisi wa mpango uliopo wa kukabiliana na majanga. Hii inapelekea kuwa vigumu katika kurejesha mfumo kwa wakati kama mfumo utapata hitilafu yeyote, hivyo kupata hasara ya taarifa ambazo zinaweza kusababisha mwendelezo wa shuhuli za taasisi kusitishwa.

Hakuna Kamati ya Uendeshaji ya TEHAMA ambayo ina wajibu wa kuboresha ubora wa taarifa, mfumo na teknolojia ya habari na mawasiliano. kamati inatakiwa kubuni mikakati ya TEHAMA katika Taasisi na mipango ya kuhakikisha gharama zinakuwa nafuu katika usimamizi wa mfumo na rasilimali kupitia taasisi za serikali

Inaonyesha kuwa idadi ya Taasisi zenye mapungufu katika TEHAMA imepungua kutoka 58 hadi 19 ikilinganishwa na mwaka jana ikiwa ni pungufu ya asilimia 67. Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 6.4**

Teknolojia ya Habari imekuwa muhimu katika shughuli za Serikali. Hata hivyo, pia ina madhara yake ambapo kuna haja ya Taasisi za Serikali kuhakikisha usiri, usalama, usahihi wa taarifa za uhasibu na taarifa nyingine.

Serikali inapaswa kuwa na muundo mzuri wa mipango ya kukabiliana na majanga na mikakati ya kuhakikisha kuwa vifaa vya kompyuta na programu vinatunzwa ili kuweza kukabiliana na majanga pale yanapotokea.

6.6 Masuala ya Kiutawala

Utawala bora ni mchanganyiko wa taratibu na miundo ya Taasisi inayotekelezwa na Bodi ya Wakurugenzi kuwajulisha, kuelekeza, kusimamia, na kufuatilia mali za Taasisi, mikakati na sera katika kufikia malengo ya taasisi. Kama sehemu ya ukaguzi wangu, nilitathmini uwepo na utendaji wa Bodi za Wakurugenzi katika Taasisi za Serikali.

Jedwali lifuatalo linaonyesha Taasisi na taratibu zilizokiukwa zilizobainishwa wakati wa ukaguzi;

Jedwali 33: Taasisi zenye mapungufu ya kiutawala

Na.	Jina la Taasisi	Taratibu iliyokiukwa
1	Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki	Kukosekana kwa Bodi ya Ushauri ya Wizara; Kwamba kwa kiasi kikubwa huathiri shughuli za taasisi kama vile idhini ya bajeti, sera na mchakato wa ukaguzi.
2	Mfuko wa Rais	Uwepo wa maelekezo ya Bodi

Na.	Jina la Taasisi	Taratibu iliyokiukwa
		ya Wadhamini ambayo hayatekelezwa .
3	Mfuko wa Uhifadhi wa wanyamapori	Bodi ya Mfuko ilimaliza muda wake mnamo 2014/02/06 tangu wakati huo mamlaka ya uteuzi bado haijateua wajumbe wengine wa Bodi, hii kwa kiasi kikubwa huathiri shughuli za Mfuko kama vile kuidhinisha bajeti, sera na mchakato wa ukaguzi.

Kazi ya Bodi ni kutoa ushauri kwa Wizara na Katibu Mkuu juu ya maendeleo na kutengeneza muundo wa mikakati na malengo ya Mfuko, Bodi hufanya mapitio ya mipango ya Afisa Mtendaji na bajeti inayohusika, na utendaji wa kila mwaka wa Mfuko.

Nina mtazamo kwamba, kutokana na kukosekana kwa Bodi ya Wadhamini maamuzi ya kisera hayakuweza kufanyika na kwa ujumla mwelekeo na mkakati wa shughuli za Mfuko hazikuweza kutathiminiwa.

Nashauri kwamba mamlaka husika ihakikishe uteuzi wa Bodi unafanyika ili kuongeza utawala na kusimamia kazi na majukumu ya Mfuko.

Wakati baadhi ya taasisi zimeonyesha maboresho hasa katika eneo la kuanzisha na kufuata sheria na kanuni kuhusiana na kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Bodi za Wakurugenzi, Kamati ya Ukaguzi na usimamizi wa vihatarishi. vile vile kuna kurudi nyuma katika masuala ya TEHAMA ili kuhakikisha usiri na uadilifu wa shughuli zao.

Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, hatua zaidi kutoka Serikalini zinahitajika ili kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Serikali zinaweka mifumo ya ndani madhubuti kwa ajili ya kutimiza kwa ufanisi majukumu yao ya kisheria.

USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

7.1 Utangulizi

Sura hii inahusu matokeo muhimu kutokana na ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali watu na mishahara kwa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na balozi kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Masuala muhimu ni kama ifuatavyo:

7.2 Malipo ya Mishahara kwa Wafanyakazi ambao Hawapo kwenye Utumishi wa Umma Shilingi 1,400,554,592

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa taaasisi 19 zililipa kiasi cha Shilingi 1,400,554,592 kama mishahara kwa watumishi 260 walioacha kazi, waliokufa, waliostaafu na waliofukuzwa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali** hapo chini. Mishahara hii ililipwa kwa kipindi kati ya mwezi mmoja hadi sabini na miwili. Hii ni kinyume na Kanuni ya 113 ya kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) inayosema Maafisa Masuuli watunze nyaraka za watumishi ili watumishi wanaolipwa wawe ni wale waliokuwepo na kufanya kazi.Hadi kufikia Januari 2017 kiasi cha Shilingi 158,350,788 kilikuwa kimesharejeshwa.

Jedwali 34: Malipo Ya Mishahara kwa Watumishi Ambao Hawapo Kwenye Utumishi wa Umma

Na.	Taasisi	Fungu	Idadi ya watumishi	Kiasi (Shilingi)	Kiasi kilichorejeshwa(Shilingi)
1	Bunge	42	2	2,536,000	0
2	Idara ya Zimamoto na Uokoaji	14	4	2,818,000	0
3	Jeshi la Polisi	28	139	757,316,000	14,034,700
4	Mahakama	40	27	182,913,133	35,031,519.66
5	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	46	8	62,541,948	0.00
6	Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi	48	1	22,623,980	10,058,338
7	Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto	52	8	18,508,632	0.00
8	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na	98	4	5,382,958	4,459,232

Na.	Taasisi	Fungu	Idadi ya watumishi	Kiasi (Shilingi)	Kiasi kilichorejeshwa(Shilingi)
	Mawasiliano				
9	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	49	26	63,324,829	47,040,101.40
10	Sekretarieti ya Mkoa - Kagera	87	8	12,196,493	6,784,200
11	Sekretarieti ya Mkoa - Shinyanga	83	1	43,932,185	22,250,000
12	Sekretarieti ya Mkoa - Geita	63	4	26,604,200	17,360,000.00
13	Sekretarieti ya Mkoa - Kigoma	74	12	150,573,228	0.00
14	Sekretarieti ya Mkoa - Rukwa	89	6	2,756,903	0.00
15	Sekretarieti ya Mkoa - Ruvuma	82	4	15,857,080	0.00
16	Sekretarieti ya Mkoa - Tanga	86	3	3,017,687	1,332,697
17	Msajili wa Vyama vya siasa	27	1	22,442,888.80	0
18	Sekretarieti ya Mkoa - Manyara	95	1	1,568,445	0
19	Sekretarieti ya Mkoa - Mtwara	80	1	3,640,000	0
Jumla			**260**	**1,400,554,592**	**158,350,788**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma ni hasara kwa fedha za Umma, hivyo juhudi za Serikali zinahitajika zaidi kushughulikia dosari hii.

Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita, kuna ongezeko kutoka taasisi kumi na sita hadi kumi na tisa (asilimia 19) na kutoka shilingi 392,651,036 hadi shilingi 1, 400,554,592 (asilimia 257). Hili ni tatizo la kimfumo kwenye taasisi za serikali.

Ninaendelea kushauri kwamba Maafisa Masuuli wahakikishe kuwa fedha zilizolipwa zinarejeshwa Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, wahakikishe uimarishaji wa udhibiti katika urekebishaji wa kumbukumbu za watumishi ili kuzuia upotevu wa fedha za Umma.

7.3 Makato ya Kisheria kwa Watumishi ambao Hawapo kwenye Utumishi wa Umma Shs 50,525,057.96

Katika ukaguzi wa mwaka huu wa fedha, taasisi saba zilifanya makato mbalimbali ya kisheria kiasi cha Shilingi 50,525,057.96 kwa muda hadi miezi minne kwa watumishi 28 ambao hawakuwa kwenye utumishi wa Umma. Makato hayo ya kisheria yalilipwa kwenye mifuko ya hifadi ya jamii kama vile Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mifuko ya Pensheni (PSPF, PPF, NSSF na LAPF). Mishahara itokanayo na makato hayo ililipwa kwa watumishi husika.

Jedwali 35: Makato ya mishahara kwa watumishi ambao hawakuwa kwenye utumishi wa Umma

No.	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi	Kiasi Shs
1	14	Idara ya Zimamoto na Uokozi	4	7,446,893.84
2	98	Wizara ya Kazi, Usafirishaji na Mawasiliano	4	1,918,708
3	87	Sekretarieti ya Mkoa Kagera	8	11,549,688.00
4	89	Sekretarieti ya Mkoa Rukwa	6	1,069,094.12
5	82	Sekretarieti ya Mkoa Ruvuma	4	9,277,920
6	52	Sekretarieti ya Mkoa Geita	1	18,177,000
7	95	Sekretarieti ya Mkoa Manyara	1	1,085,754
Jumla			**28**	**50,525,057.96**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016*

Katika ripoti yangu ya mwaka uliopita, taasisi tano zikiwemo fungu 89 na 82, ambazo zimeonekana katika ukaguzi huu zilikuwa na dosari hii. Ninaendelea kuwashauri Maafisa Masuuli wahakikishe kuwa fedha hizo zinarudishwa kutoka mamlaka husika na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, nashauri uimarishaji wa mifumo ya udhibiti ili kuzuia ongezeko la gharama ya mishahara.

7.4 Malipo ya Posho ya Kuhudumu nje ya Nchi Yasiyostahiki Shilingi 84,055,880.46

Ukaguzi wa rasilimali watu katika ubalozi wa Tanzania Brussels ulibaini kuwa kiasi cha Shilingi 52,768,512.96 (€ 22,789.25) kwa ajili ya posho ya kuhudumu nje ya chi (foreign service allowance) kwa mwezi Agosti hadi Novemba 2015 kwa mtumishi ambaye alipewa likizo bila malipo na baadaye akachaguliwa na chama cha siasa kwa ajili ya kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 2015. Hali kadhalika, kiasi cha Shilingi 31,287,367.50 (€ 12,930.00) kililipwa kwa ajili ya ada kwa watoto wa mtumishi huyo kwa kipindi ambacho hakuwa mtumishi wa Umma.

Ibara ya 72 (b) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza kuwa iwapo mtu yoyote mwenye madaraka katika utumishi wa serikali ataamua kugombea uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha siasa, mtu huyo atahesabiwa kuwa utumishi wake umekoma tangu tarehe yake ya kuwa mgombea wa uchaguzi au kugombea uongozi katika chama cha siasa. Malipo kwa ajili ya mtumishi ambaye utumishi wake umekoma kwa mujibu wa sheria ni hasara kwa fedha za Umma.

Nilishauri kuwa Afisa Masuuli mhusika ahakikishe kuwa kiasi hicho kilicholipwa kinarejeshwa. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhakikisha kwamba malipo yanayostahiki ndiyo yanayolipwa.

7.5 Mishahara Isiyolipwa Ambayo Haijarejeshwa Hazina Shilingi 1,027,334,712.04

Wizara ya Fedha na Mipango kupitia barua yenye kumbukumbu namba No. EB/AG/485/01/Vol. V/32 ya tarehe 03 June 2016 iliagiza Maafisa Masuuli wote kuwa mishahara yote ambayo haijalipwa irejeshwe Hazina kupitia akaunti maalumu iliyofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania.

Ukaguzi wa taasisi nane,zikiwemo wizara mbili na Sekretarieti za Mikoa sita ulibaini kuwa kiasi cha shilingi 1,027,334,712.04 ikiwa ni mishahara isiyolipwa haikurejeshwa Hazina kinyume na maelekezo hayo kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo

chini Hii inaashiria kuwa fedha hizo zinaweza kutumika kinyume na makusudio.

Jedwali 36: mishahara isiyolipwa ambayo haijarejeshwa Hazina.

Na	Fungu	Taasisi	Kiasi (Shs)
1	52	Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto	423,500,680
2	63	Sekretarieti ya Mkoa - Geita	7,924,200
3	87	Sekretarieti ya Mkoa - Kagera	29,168,116
4	46	Wizara ya Elimu, Mafunzo na Ufundi	451,753,872
5	85	Sekretarieti ya Mkoa - Tabora	43,589,538
6	79	Sekretarieti ya Mkoa - Morogoro	17,781,000
7	80	Sekretarieti ya Mkoa - Mtwara	16,534,000
8	76	Sekretarieti ya Mkoa - Lindi	37,083,305
Jumla			**1,027,334,712**

***Chanzo**: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016*

Aidha, nilibaini kuwa kati ya shilingi 423,500,680.7 ambazo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto (Vote 52) haikurejesha Hazina, Shilingi 157,350,136.47 zilitumika kwa ajili ya kuilipa Mamlaka ya Mapato Tanzania fedha ambazo wizara ilishindwa kukusanya na kupeleka kodi zuiliwa (*withholding tax*) kutoka kwa wazabuni mbalimbali. Wizara ilikiri kuwa fedha hizo zitarudishwa kutoka kwa wazabuni hao.

Nilishauri kwamba Maafisa Masuuli warejeshe Hazina fedha za mishahara ambayo haijalipwa. Pia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto ihakikishe fedha za mishahara zinatumika kwa ajili ya lengo lililokusudiwa na fedha hizo zirejeshwe Hazina.

7.6 Kuchelewa Kutuma Makato ya Kisheria ya Mishahara Shilingi 284,582,429,219

Vifungu 40 na 41 vya Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Umma, 1999 vinaelekeza kwamba kila mwajiri mwanachama wa mifuko ya hifadhi achangie mfuko kwa wanachama kwa kukata makato kutoka kwenye mshahara wa mwajiriwa kiasi cha asilimia tano na mwajiri kuchangia asilimia kumi na tano ya mshahara kwa kila mwezi.

Mifuko ya Hifadhi ya jamii na Bima ya Afya inawataka waajiri wote wakate na kuwasilisha makato kutoka kwa waajiriwa na michango ya waajiri kila mwezi. Ucheleweshaji wa makato ya Kisheria husababisha faini kutoka kwa Taasisi husika.

Ukaguzi wangu kwa serikali kuhusiana na matakwa ya kuwasilisha makato na michango ya waajiri kwenye mifuko ya hifadhi pamoja na Bima ya Afya ulibaini kuwa kiasi cha shilingi 284 bilioni kilicheleweshwa kuwasilishwa kwa muda wa siku 30 hadi 90 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho 7.1** Hali kadhalika, serikali, kupitia deni la taifa, ililipa faini ya kiasi cha shilingi 4,089,000 kwa kuchelewa kuwasilisha michango ya watumishi.

Katika ukaguzi wa taasisi za serikali, nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 167,486,144.25 ambacho ni makato ya kisheria ya mishahara kama inavyoonekana kwenye jedwali 7.5. kilikatwa kutoka kwenye mishahara ya watumishi wa umma kutoka taasisi tano kilicheleweshwa kuwasilishwa kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya kwa kipindi cha mwezi mmoja hadi 138.

Jedwali 37: Makato ya Mishahara yaliyocheleweshwa

Na.	Fungu	Taasisi	Mifuko	Kiasi (Shs)	Miezi iliyochelewe shwa
1	16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	PSPF	35,194,104.00	3 hadi 138
2	92	TACAIDS	PSPF	4,301,350	1
			PPF	349,680	
			NHIF	3,865,188	
			LAPF	1,006,400	
3	97	Wizara ya Mambo ya Nje Idara ya Afrika Mashariki	LAPF	428,100	3
			NSSF	726,800	
			PSPF	6,725,300	
			NHIF	4,510,080	
4	61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	PSPF	6,348,150.00	12
			LAPF	101,805,120.25	3
5	38	Jeshi la Wananchi wa	PSPF	2,225,872	1 hadi 71

Na.	Fungu	Taasisi	Mifuko	Kiasi (Shs)	Miezi iliyochelewesha
		Tanzania			
Jumla				**167,486,144.25**	

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Nilibaini kuwa taasisi mbili zilitozwa faini ya shilingi 17,050,249.95 kwa kucheleweshe makato hayo kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini. Malipo kama haya ni hasara kwa walipa kodi.

Jedwali 38: Faini kwa kucheleweshe makato ya kisheria

Na.	Fungu	Taasisi	Kiasi (Shs)
1	38	Jeshi la Wananchi wa Tanzania	11,181,362.25
2	49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	5,868,887.70
		Jumla	**17,050,249.95**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Niliwashauri Maafisa Masuuli kuwa makato ya kisheria yawe yanawasilishwa kwenye vyombo husika kwa wakati. Mifumo ya udhibiti iimarishwe ili kuzuia upotevu wa fedha za Umma.

7.7. Stahili za Watumishi Ambazo Hazijalipwa kwa Muda Mrefu Shilingi 8,204,093,899.44

Ukaguzi wa rasilimali watu katika taasisi saba nilibaini kuwa stahili mbalimbali za watumishi kiasi cha shilingi 8,204,093,899.44 hazikuwa zimelipwa kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi kumi kama inavyooneshwa katika jedwali 7.6. Kucheleweshe kulipa stahili za watumishi kunaweza kusababisha kukosa motisha, hivyo kusababisha ufanisi mdogo katika kutoa huduma bora kwa Umma.

Jedwali 39: Kuchelewa kulipa stahili za watumishi kwa muda mrefu

Na.	Fungu	Taasisi	Kiasi ambacho hakijalipwa(Shs)	Muda (miaka)
1	38	Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ)	1,826,556,675.00	4
2	28	Jeshi la Polisi	4,519,726,982	3
3	46	Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia	252,826,971	3
4	58	Wizara ya Nishati na Madini	274,101,694	8
5	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS)	79,318,937.44	3
6	89	Sekretarieti ya Mkoa - Rukwa	1,164,521,890	2
7	68	Wizara ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano.	87,040,750	1 hadi 10
		Jumla	**8,204,093,899.44**	

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Ninashauri Maafisa Masuuli, kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha na Mipango, wahakikishe kuwa stahili za watumishi zinalipwa kwa wakati.

7.8. Kodi ya Mapato Kutolipwa kutoka kwenye Posho za Kukaimu Shilingi 37,839,010

Kwa mujibu wa Kanuni D.18 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, kuteuliwa kukaimu hutokea pale ambapo mfanyakazi atapangwa kwa muda kutekeleza majukumu ya nafasi inayohitaji uteuzi.

Kifungu Na. 7 (2) (a) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa 2008) inahitaji mapato yote yanayotokana na ajira yakatwe kodi isipokuwa posho ya kujikimu, safari, ukarimu au posho zinginezo anazolipwa mtumishi ili kumwezesha kufanya kazi itakayomfanya apate kipato katika ajira yake au kutoa huduma.

Ukaguzi wangu katika taasisi tatu ulibaini kuwa kiasi cha posho ya kukaimu cha shilingi 37,839,010 kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 7.7 hapo chini kililipwa kwa watumishi saba bila kukatwa kodi ya mapato. Hivyo, wafanyakazi hao walilipwa sehemu ya kodi ya mapato badala ya kuipeleka Mamlaka ya Mapato Tanzania kama inavyotakiwa na kifungu Na. 7(2)(a) cha Sheria ya kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa 2008)

Jedwali 40: Kodi ya Mapato kutolipwa kutoka kwenye posho za kukaimu

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi	Kiasi (Shs)
1	14	Jeshi la Zimamoto na Uokozi	1	33,591,000
2	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS)	1	2,070,000
3	95	Sekretarieti ya mkoa Manyara	5	2,178,010
Jumla			**7**	**37,839,010**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Nashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha posho ya kukaimu inakatwa kodi ya mapato. Pia, Maafisa Masuuli wahakikishe kodi ambayo haikukatwa inalipwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kwa kutokukata na kulipa kodi ya posho ya kukaimu, Serikali inakosa mapato ambayo yangeweza kutumika kutoa huduma kwa Umma. Suala hili lilibainishwa katika ukaguzi uliopita; kwa hiyo, naendelea kuhimiza kuwa Maafisa Masuuli wahakikishe kuwa posho ya kukaimu inakatwa kodi ya mapato. Pia, Maafisa Masuuli wahakikishe kodi ambayo haikukatwa inalipwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

7.9. Ukiukwaji wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Kifungu 20 cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kama ilivyorekebishwa mwaka 2007 kinawataka waajiri wa wanufaikaji wa mikopo ya elimu ya juu kuwasilisha taarifa za wanufaikaji katika sehemu zao za kazi na kuhakikisha makato ya kila mwezi yanafanyika na kurejeshwa Bodi ya Mikopo.

Katika ukaguzi wangu wa rasilimali watu, nilibaini kuwa Maafisa Masuuli katika taasisi nane walikiuka sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kushindwa kuijulisha Bodi ya Mikopo taarifa za wanufaika 659 katika sehemu zao za kazi pamoja na kuanza utaratibu wa kuwakata kila mwezi ili kurejesha makato hayo Bodi ya Mikopo. Kwa matokeo hayo, kiasi cha Shilingi 913,391,857.82 kama mikopo

kwa wanufaika kilikuwa hakijaanza kurejeshwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali 7.8.

Kutokuijulisha Bodi ya Mikopo na kutokuanza kukata na kurejesha makato ya mikopo kunaweza kusababisha Bodi ya Mikopo kuwa na dhiki ya kifedha na kushindwa kuwahudumia wahitaji wengine.

Jedwali 41: Watumishi ambao hawajarejesha mikopo

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya wanufaika	Kiasi cha mkopo (Shs)
1	55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	22	110,804,759
2	16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu was Serikali	14	77,542,913
3	32	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	5	44,690,460
4	48	Wizara ya Ardhi,Nyumba na Makazi	62	-
5	41	Wizara ya Katiba na Sheria	7	55,754,844
6	74	Sekretarieti ya mkoa - Kigoma	390	-
7	85	Sekretarieti ya mkoa - Tabora	113	-
8	75	Sektretarieti ya mkoa - Kilimanjaro	46	624,598,881
		Jumla	659	913,391,857

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka uliopita, kuna ongezeko kutoka taasisi sita hadi nane ambazo zilikiuka sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Ninaendelea kushauri kuwa Maafisa Masuuli wazingatie sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuijulisha bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu taarifa za wanufaika katika sehemu zao za kazi pamoja na kuwasiliana

na waajiriwa kuhusu utaratibu wa kukata na kutuma makato ya kila mwezi kwenda Bodi ya Mikopo.

7.10. Watumishi Wanaokaimu Zaidi ya Miezi Sita

Kanuni ya 24(3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa pale inapowezekana, wafanyakazi wa umma wasikaimu kwenye nafasi kwa kipindi kinachozidi miezi sita. Mamlaka ya uteuzi ifanye mchakato wa uteuzi kwa nafasi iliyo wazi ndani ya kipindi cha miezi sita.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa watumishi 49 katika taasisi 14 wanakaimu nafasi mbalimbali zaidi ya miezi sita bila kuthibitishwa au nafasi hizo kujazwa kinyume na kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma. Watumishi hao wamekaimu kwa kipindi cha kuanzia miezi 7 hadi 84 kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini.

Jedwali 42: Watumishi wanaokaimu zaidi ya miezi sita

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi	Muda (miezi)
1	5	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	17	11 hadi 26
2	66	Tume ya Mipango	6	7 hadi 51
3	14	Jeshi la Zimamoto na Uokozi	1	48
4	24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika	4	15 hadi 18
5	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	3	24
7	87	Sekretarieti ya Mkoa - Kagera	3	7 hadi 84
8	81	Sekretarieti ya Mkoa - Mwanza	3	10 hadi 50
9	47	Sekretarieti ya Mkoa - Simiyu	4	
10	10	Tume ya Pamoja ya Fedha	1	39
11	70	Sekretarieti ya Mkoa - Arusha	1	36
12	91	Tume ya kupambana na madawa ya Kulevya	1	
13	74	Sekretarieti ya Mkoa - Lindi	2	10 hadi 35
14	79	Sekretarieti ya Mkoa - Morogoro	3	51 hadi 60
		Jumla	**49**	

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Nimewashauri Maafisa Masuuli washirikiane na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora kuhakikisha kuwa kanuni za kudumu za utumishi wa Umma zinazingatiwa kwa watumishi kutokukaimu nafasi kwa zaidi ya miezi sita.

7.11. Watumishi wa Umma Kupokea Mishahara Chini ya Kiwango Kinachokubalika Kisheria

Ukaguzi wa rasilimali watu na mishahara umebaini kuwa baadhi ya Taasisi zinafanya makato ya mishahara kwa watumishi kwa ajili ya kurejesha mikopo katika mwezi zaidi ya theluthi mbili ya mshahara wa mwezi kinyume na sheria ya kurejesha madeni ya mwaka 1970 - na waraka wenye Kumb. C / CE.45 / 271/01 / I / 87 wa Machi, 2009 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais –Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Ukaguzi katika sampuli ya taasisi sita ulibaini kuwa watumishi 49 walilipwa mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria. Watumishi wanapopata mishahara midogo hukosa ari ya kufanya kazi na kupelekea utendaji duni na kutoa huduma chini ya viwango.

Taasisi ambazo watumishi hupokea mshahara chini ya kiwango kinachokubalika ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali hapo chini.

Jedwali 43: Watumishi ambao wanapokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi
1	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	23
2	53	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	6
3	96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	2
4	72	Sekretarieti ya mkoa - Dodoma	2
5	76	Sekretarieti ya mkoa - Lindi	14
6	70	Sekretarieti ya mkoa - Arusha	2
		Jumla	**49**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Kama ilivyoonekana mwaka uliopita, taasisi nyingi hazizingatii matakwa ya sheria hii. Idadi ya watumishi ambao wanapokea mshahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria imepungua kutoka 875 hadi 35, lakini idadi ya taasisi imeongezeka kutoka 2 hadi sita mwaka huu.

Nasisitiza ushauri wangu kwamba Maafisa Masuuli waimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani katika kuthibitisha mikopo ya watumishi kwa kushirikiana na watoa mikopo ili kuhakikisha kuwa makato hayazidi theluthi mbili ya mshahara wa mwezi kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha sheria ya kurejesha madeni ya mwaka 1970 - na waraka wenye Kumb. C / CE.45 / 271/01

/ I / 87 wa Machi, 2009 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais –Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

7.12. Kutokufanya Tathimini na Kupima Utendaji wa Wafanyakazi

Kanuni ya D.62 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa taasisi zote ziwe na mfumo wa uwazi wa kutathimini utendaji kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni ya 22 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003.

Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 inasema kuwa kila taasisi iliyopo kwenye utumishi wa umma iwe na mfumo wa uwazi wa kutathmini utendaji wa wafanyakazi wake wote. Matakwa haya ni kwa mujibu wa kanuni ya D.62 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009.

Pia, Kanuni ya 22(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 inasema kuwa lengo la kutathmini utendaji ni kubainisha, kupima na kuweka kumbukumbu za uwezo na mapungufu ya kila mfanyakazi ili kuweza kuchukua hatua za kuboresha ufanisi katika utumishi wa umma kama lengo endelevu.

Ukaguzi wangu kuhusiana na muongozo wa kanuni za utumishi wa Umma wa kufanya tathmini na kupima utendaji wa watumishi wa Umma katika sampuli ya taasisi saba ulibaini kuwa watumishi 764 hawakufanyiwa tathmini na kupima utendaji wao kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapo chini.

Jedwali 44: Taasisi ambazo hazikufanya tathmini na kupima watumishi

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi
1	75	Sekretarieti ya mkoa – Kilimanjaro	19
2	86	Sekretarieti ya mkoa - Tanga	27
3	57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	9
4	2004	Ubalozi wa Tanzania Kinshasa	6

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi
5	71	Sekretarieti ya mkoa – Pwani	20
6	84	Sekretarieti ya mkoa – Singida	7
7	35	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka	676
		Jumla	**764**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Kushindwa kutathimini na kupima utendaji wa wafanyakazi husababisha uongozi kushindwa kutambua mapungufu ya kiutendaji ya wafanyakazi wake ili kutengeneza mikakati na namna bora ya kuyashungulikia. Mbali na hayo, ni vema kuwa na mfumo wa wazi wa kupima na kutathmini utendaji ambao utazingatia utendaji wa mtumishi katika kupanda vyeo, mafunzo na uhamisho.

Nawashauri Maafisa Masuuli wapime na kutathimini utendaji wa wafanyakazi kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009.

7.13. Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi wangu wa taasisi za serikali, nilibaini tatizo la upungufu wa watumishi wa Umma. Upungufu wa watumishi wa umma unaathiri kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kukosa mchango wa taaluma mbalimbali. Aidha, mgawanyo wa majukumu na uhamisho wa watumishi ambavyo ni muhimu katika mfumo wa ndani wa udhibiti hauwezi kufanyika kwa ufanisi.

Katika sampuli ya taasisi thelathini na nane, nilibaini kuwa nafasi 11,892 zilikuwa wazi ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi 24,568, kama inavyoonekana kwenye jedwali 7.12 hapo chini. Upungufu huu ni asilimia 48 ya mahitaji ya watumishi.

Upungufu wa watumishi huathiri utoaji wa huduma katika Taasisi za Serikali.

Serikali inapaswa kuongeza jitihada za kuboresha idadi ya watumishi.

Jedwali 45: Upungufu wa wawatumishi

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi inayotakiwa	Idadi iliyopo	Upungufu
1	55	Tume ya Haki za Bianadamu na Utawala Bora	171	159	12
2	91	Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevya	-	12	12
3	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	448	397	51
4	48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi	2,163	871	1,292
5	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	2,138	246	1,894
6	53	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	4,372	1475	2,897
7	72	Sekretarieti ya Mkoa - Dodoma	1,141	681	460
8	73	Sekretarieti ya Mkoa - Iringa	951	588	363
9	77	Sekretarieti ya Mkoa - Mara	820	510	310
10	81	Sekretarieti ya Mkoa - Mwanza	1,027	599	428
11	83	Sekretarieti ya Mkoa - Shinyanga	722	500	222
12	82	Sekretarieti ya Mkoa - Ruvuma	946	782	164
13	85	Sekretarieti ya Mkoa - Tabora	976	558	418
14	13	Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu	51	16	35
15	70	Sekretarieti ya Mkoa - Arusha	1,041	790	251
16	75	Sekretarieti ya Mkoa - Kilimanjaro	1,026	777	249
17	95	Sekretarieti ya Mkoa - Manyara	828	339	489
18	71	Sekretarieti ya Mkoa - Pwani	386	301	85
19	79	Sekretarieti ya Mkoa - Morogoro	1,111	858	253
20	76	Sekretarieti ya Mkoa - Lindi	1,061	404	657
21	80	Sekretarieti ya Mkoa - Mtwara	1,063	462	601
22	78	Sekretarieti ya Mkoa - Mbeya	857	572	285
23	88	Sekretarieti ya Mkoa - Dar es Salaam	192	161	31
24	2034	Ubalozi wa Tanzania Moroni	10	5	5
25	2027	Ubalozi wa Tanzania Abbu Dhabi	17	16	1
26	2014	Ubalozi wa Tanzania Beijing	9	6	3
27	2019	Ubalozi wa Tanzania Brussels	7	0	7
28	84	Sekretarieti ya Mkoa - Singida	940	562	378
29	2021	Ubalozi wa Tanzania Uganda	6	2	4
30	2004	Ubalozi wa Tanzania Kinshasa	8	6	2
31	2029	Ubalozi wa Tanzania Maskati	14	11	3
32	2013	Ubalozi wa Tanzania Paris	10	3	7
33	2024	Ubalozi wa Tanzania Riyadh	19	15	4
34	2020	Ubalozi wa Tanzania Geneva	14	8	6
35	2001	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa	7	2	5
36	2028	Ubalozi wa Tanzania Bujumbura	6	4	2
37	2015	Ubalozi wa Tanzania Rome	1	0	1
38	2023	Ubalozi wa Tanzania Nairobi	9	4	5
		Jumla	**24,568**	**12,702**	**11,892**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Nawashauri Maafisa Masuuli wakishirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhakikisha nafasi zote zilizo wazi zinajazwa au Serikali ipitie upya Miundo ya Utumishi ili iendane na mahitaji halisi.

7.14. Kumbukumbu za Mishahara Zenye Dosari

Kanuni ya 110 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001(iliyorekebishwa 2004), inawapa jukumu Maafisa Masuuli kuweka taarifa sahihi za watumishi katika sehemu zao, na kwamba, zinahakikiwa kila mara.

Katika ukaguzi wangu wa utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kwenye mfumo wa mishahara (Lawson) kwenye taasisi sita, nilibaini kuwa kulikuwa na dosari katika taarifa za watumishi kama vile tarehe za kuzaliwa kutokuwa sahihi, watumishi waliohamishwa bila kurekebisha kumbukumbu zao, watumishi waliostaafu lakini majina yao bado hayajafutwa kwenye mfumo wa mishahara ingawa mishahara kwa watumishi hao haikulipwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.

Jedwali 46: Kumbukumbu za watumishi zenye dosari

Na.	Fungu	Taasisi	Dosari
1	14	Jeshi la Zimamoto na Uokozi	Taarifa kwenye mfumo wa mishahara (Lawson) zinaonesha kuwa watumishi watano walizaliwa tarehe 02/01/1900, na kwamba, watastaafu mwaka 1960 wakati waliajiriwa kati ya mwaka 2007 hadi 2009.
2	46	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Taarifa kwenye mfumo wa mishahara (Lawson) zinaonesha kuwa watumishi wanne walizaliwa tarehe 02/01/1900. Watumishi wawili hawakuwa na namba ya utambulisho ya utumishi (check number)
3	95	Sekretarieti ya mkoa wa Manyara.	Taarifa za mishahara zinaonesha kuwa watumishi wanne walihamishwa kutoka Manyara (fungu 95) kwenda sehemu zingine lakini walikuwa kwenye taarifa za Manyara, hivyo, kusababisha

Na.	Fungu	Taasisi	Dosari
			gharama za mishahara kuonekana kuwa zaidi kwa Shilingi 34,365,000.
4	74	Sekretarieti ya mkoa wa Kigoma.	Watumishi wawili walihamishwa vituo vyao vya kazi bila kurekebisha taarifa zao za mishahara hivyo kiasi cha Shilingi 5,664,000 kikalipwa kwa watu hao.
5	72	Sekretarieti ya mkoa wa Dodoma.	Kumbukumbu za mishahara zilionesha kuwa kuna watumishi saba walistaafu utumishi wa Umma na hawapokei mishahara lakini taarifa za mishahara kutoka Hazina zilionesha kuwa watumishi hao wapo kwenye utumishi. Watumishi hao walistaafu mwisho wa mwaka wa Fedha 2015/2016.
6	63	Sekretarieti ya mkoa wa Geita.	Kumbukumbu za mishahara zilionesha kuwa Watumishi 15 ambao walikuwa sio wafanyakazi tena waliendelea kuwepo kwenye kumbukumbu za mishahara bila kufutwa, ijapokuwa hakuna mshahara uliolipwa kwa watumishi hao.

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Dosari kwenye kumbukumbu za watumishi zinaweza kusababisha kulipa watumishi ambao sio waajiriwa wa taasisi husika.

Ninashauri kuwa Maafisa Masuuli wahakikishe dosari zilizojitokeza kwenye kumbukumbu za misharaha zinarekebishwa na kuhakikiwa kila mara. Aidha, Maafisa Masuuli wakishirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wahakikishe kuwa watumishi wanapohamishwa, kumbukumbu zao za mishahara zihamishiwe kwenye vituo walivyohamishiwa bila kuchelewa.

7.15. Kufanya Kazi Ubalozini Zaidi ya Muda Ulioidhinishwa

Kifungu cha 31(1) na (2) cha Kanuni za Tanzania za kuhudumu nje ya nchi za mwaka 2013 ***(Tanzania Foreign services Regulations of 2013)*** kinasema afisa anaweza kupelekwa kituo chochote ambapo anahitajika kufanya kazi, vinginevyo iwe imeelezwa kwenye fomu ya kazi ila itakuwa ni kipindi cha miezi arobaini na nane. Pia, barua za uteuzi wa wafanyakazi huwapa muda wa miaka minne kufanya kazi ubalozini.

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa rasililmali watu na mishahara kwenye sampuli ya balozi mbili (2) ulibaini kuwa watumishi wawili (2) wamehudumu zaidi ya muda ulioidhinishwa. Watumishi hao walikaa zaidi ya muda ulioidhinishwa ikiwa ni kati ya miaka miwili na nusu hadi mitatu baada ya muda wao kwisha. Hii inatokana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutowarejesha kutoka ubalozini. Maelezo ya watumishi waliokaa ubalozini zaidi ya muda uliothibitishwa ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali Na.7.14 hapo chini.

Jedwali 47: Orodha ya ofisi za balozi zenye watumishi waliofanya kazi ubalozini zaidi ya muda ulioidhinishwa.

Na.	Fungu	Ubalozi	Idadi ya watumishi	Muda zaidi(miaka)
1	2020	Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa Geneva	1	3
2	2019	Ubalozi wa Tanzania - Brussels, Belgium	1	2.5
		Jumla	2	

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2015/2016

Ikilinganishwa na ukaguzi wangu uliopita, balozi zilizokuwa na dosari hii zimepungua kutoka tisa hadi mbili. Hii inaonesha jitihada zilizochukuliwa na serikali katika kurekebisha dosari hii.

Naendelea kumshauri Afisa Masuuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuzingatia kanuni Na. 31(1) na (2) ya Kanuni za Tanzania za kuhudumu nje ya nchi za mwaka 2013 *(Tanzania Foreign services Regulations of 2013)* katika kufanya uhamisho wa watumishi.

7.16. Mikataba Iliyoisha Muda Wake kwenye Balozi za Heshima

Ukaguzi wa nyaraka za balozi ulibaini kuwa mikataba ya balozi nne za heshima ilikwisha muda wake kwa kipindi cha

hadi miezi 17 bila kuhuishwa mikataba hiyo au kutoa mikataba mipya inayopaswa kutolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Pia, balozi mbili za heshima hazikuwa na mikataba. Jedwali hapo chini linaonesha balozi ambazo mikataba imekwisha muda wake na ambazo hazina mikataba.

Jedwali 48: : Mikataba iliyokwisha muda wake

Ubalozi	Tarehe ya kuanza mkataba	Tarehe ya kumalizika kwa mkataba	Muda uliopita bila mkataba (miezi)
Osaka, Japan	06/12/2010	5/12/2015	13
Melbourne West Australia	24/08/2010	23/8/2015	17
Perth Australia	06/12/2010	5/12/2015	13
Adelaide Australia	24/08/2010	23/8/2015	17
Christchurch New Zealand	Hakukuwa na Mkataba.		Haujulikani
Seoul South Korea	Ni mgonjwa kwa muda mrefu na ubalozi wa heshima alimpa mwanawe. Hakukuwa na mkataba.		Haujulikani

Chanzo: Majalada ya Ubalozi 2016

Nilibaini kuwa, tangu kuchaguliwa kwa balozi wa Tanzania Tokyo Japan mnamo May 2015, hati za utambulisho hazijatumwa kwa balozi ndogo sita za heshima ambapo mheshimiwa balozi anasimamia. Suala hili pia lilijitokeza Moscow ambapo tangu mwaka 2014 hati za utambulisho hazijapelekwa katika balozi za heshima kama vile Belarus, Georgia, Uzbekistan, Azerbaijan, Turkmenistan, Kyrgyzstan, Moldova, Armenia, Kazakhstan na Tajikistan ambazo ubalozi unasimamia.

Ukosefu wa mikataba kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Afrika Mashariki na Mabalozi wa Heshima unasababisha kukosekana kwa makubaliano ya kisheria katika kutekeleza majukumu yao. Kukosekana kwa hati za utambulisho kunasababisha Mheshimiwa Balozi kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Ninashauri Afisa Masuuli wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki ahakikishe kuwa mikataba iliyokwisha muda wake inahuishwa kwa wakati au kutoa

mikataba mipya katika balozi za heshima. Pia, hati za utambulisho zitumwe kwa balozi za Japani na Moscow.

WAKALA ZA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE

8.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali 32, Mifuko Maalumu ya Fedha 14 na Taasisi nyingine za Serikali 33, Mabonde 11 na vyama vya Siasa.

Sura hii inaonyesha masuala mahususi yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Bunge, Bodi ya Ushauri ya Wizara na usimamizi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli zao. Yafutayo ni matokeo muhimu ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Wakala za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016:

8.2 Masuala Mtambuka Yaliyojitokeza Kwenye Ukaguzi wa Wakala za Serikali

8.2.1 Utegemezi wa Ruzuku ya Serikali

Vyanzo vya fedha kwa ajili ya bajeti ya Wakala wa Serikali ni pamoja na vyanzo vya ndani na misaada ya serikali (kawaida na ya maendeleo). Hali halisi ya upatikanaji wa fedha kutoka katika kila moja ya vyanzo hivi una athari juu ya utendaji wa jumla wa bajeti ya Wakala.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya makisio ya mapato ya Wakala yalifikia kiasi cha shilingi 1,722,618,305,256. Hii ni pungufu ya shilingi 226,766,756,316.00 (12%) ikilinganishwa na makisio ya mwaka wa fedha 2014/2015 ya kiasi cha shilingi 1,949,385,061,572. Katika jumla ya makisio yote kiasi cha shilingi 1,375,812,131,311 (80%) kilitarajiwa kufadhiliwa na ruzuku kutoka serikalini; na kiasi cha shilingi 346,806,173,945.00 (20%) kutoka vyanzo vya ndani vya mapato. Kati ya ruzuku kutoka serikalini kiasi cha shilingi 598,777,973,841 (44%) kilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 777,034,157,470 (56%) kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kielelezo cha hapo chini kinaonesha mjumuiko wa vyanzo vya mapato:

Kielelezo 14: Mlinganisho kati ya makisio ya ruzuku kutoka serikalini na vyanzo vya ndani vya mapato (kiasi katika shilingi trilioni)



Kielelezo cha hapo juu kinaonesha uwezo wa wakala wa serikali kuendesha shughuli zake kwa kutegemea vyanzo vya ndani vya mapato. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ruzuku kutoka serikalini ya kugharamia bajeti ya wakala wa serikali ilikuwa shilingi 1.38(80%) trilioni pungufu ya shilingi 0.27(16%) trilioni ikilinganishwa na makisio ya mwaka wa fedha 2014/2015 ya shilingi 1.65 trilioni. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 makisio ya mapato ya ndani yalikuwa kiasi cha shilingi 0.35 trilioni ongezeko la shilingi 0.06 (21%) trilioni ikilinganishwa na makisio ya mwaka 2014/2015 ya shilingi 0.29 trilioni. Hii inaonesha kwamba uwezo wa wakala kuendesha shughuli zake kwa kutumia vyanzo vya ndani umeongezeka kwa asilimia 21 ikilinganishwa na mwaka 2014/2015

Makusanyo halisi yalikuwa shilingi 2,026,537,365,152 (118%) dhidi ya makisio halisi ya shilingi 1,722,618,305,256. Hivyo

kulikuwa na ogezeko la shilingi 303,919,059,896.09, sawa na asilimia 18 ya makisio yote. Hili ni ongezeko la shilingi 823,627,129,104 (68%) ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2014/2015 ya kiasi cha shilingi 1,202,910,236,048. **Angalia Jedwali hapo chini:**

Kiambatisho 8.1: Makisio yaliyopitishwa dhidi makusanyo halisi

Na.	Walaka wa serikali	Jumla ya makisio(shilingi)	Jumla ya makusanyo(shilingi)
1	Wakala wa serikali Mtandao	2,618,008,050	6,926,034,409
2	Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi	15,107,429,000	7,339,726,613
3	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania	97,830,849,000	106,176,052,309
4	Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa	3,208,557,000	2,434,659,053
5	Chuo cha Utumishi wa Umma	21,823,999,400	20,095,840,544
6	Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania	1,475,271,000	946,443,864
7	Wakala wa Mbegu za Kilimo	8,796,258,444	4,989,080,402
8	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	28,782,300,196	12,425,373,634
9	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo	4,237,326,000	2,356,702,057
10	Wakala wa Utafiti wa Miamba	8,281,670,000	4,675,118,719
11	Chuo cha Mafunzo ya Mifugo	5,456,226,000	3,918,943,416
12	Wakala wa Majengo Tanzania	63,183,205,780	48,470,519,695
13	Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi	51,248,709,421	47,021,537,597
14	Wakala wa Ndege za Serikali	17,442,707,180	16,206,472,993
15	Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa	20,042,284,513	19,569,296,061
16	Wakala wa Barabara Tanzania	726,903,520,000	1,254,457,847,000
17	Wakala wa Maabara za Mifugo	3,756,508,000	1,697,500,502
18	Wakala wa Vipimo	24,337,635,622	21,144,080,603

Na.	Walaka wa serikali	Jumla ya makisio(shilingi)	Jumla ya makusanyo(shilingi)
19	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	4,336,144,014	2,199,712,695
20	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu	5,585,296,040	2,320,295,882
21	Wakala wa Maabara za Serikali	14,682,809,000	12,979,455,434.49
22	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo	2,631,346,760	1,034,157,189
23	Wakala wa Usalama na Afya Kazini	17,008,818,828	19,993,576,559
24	Wakala wa Huduma za Ajira	1,483,594,489	973,781,380
25	Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania	11,178,436,000	9,240,091,000
26	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam	15,393,730,810	9,840,964,223
27	Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi	11,718,000,000	10,945,503,590
28	Wakala wa Umeme Vijijini	362,692,701,200	295,227,433,140
29	Chuo cha mafunzo ya takwimu Afrika Mashariki	3,057,994,762	2,780,023,347.60
30	Mamlaka ya viwanja vya ndege	161,807,193,202	75,058,946,727
31	Chuo cha Taifa cha Utalii	6,509,775,545	3,092,194,514
	Jumla	**1,722,618,305,256**	**2,026,537,365,152.09**

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, kati ya makusanyo yote, kiasi cha shilingi 1,679,022,960,959 (83%) ilikuwa ni ruzuku kutoka serikalini na shilingi 347,514,404,193.09 (17%) kutoka vyanzo vya ndani vya mapato. Kati ya ruzuku kutoka serikalini iliyopokelewa kiasi cha shilingi 565,955,113,766 (34%) kilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,113,067,847,193 (66%) kwa shughuli za maendeleo

Kielelezo cha hapo chini kinaonesha makusanyo halisi kutoka vyanzo vya ndani na ruzuku ya serikali

Kielelezo 15: Mlinganisho makusanyo halisi ya ruzuku serikalini na mapato ya ndani(Kiasi katika shilingi trilioni)



Kielelezo cha hapo juu kinaonesha makusanyo halisi kutoka ruzuku serikalini na mapato ya ndani. Kwa mwaka 2015/2016, makusanyo halisi kutoka ruzuku ya serikalini yalikuwa shilingi 1.68 trilioni, pungufu ya shilingi 0.79(89%) trilioni ukilinganisha na makusanyo halisi ya mwaka 2014/2015 ya kiasi cha shilingi 0.89 trilioni. Makusanyo ya ndani yalikuwa shilingi 0.35 trilioni; ongezeko la shilingi 0.03(9%) trilioni ukilinganisha na makusanyo halisi ya waka 2014/2015 ya shilingi 0.32 trilioni

8.2.2 Fedha iliyoidhinishwa na serikali kwa matumizi ya kawaida haikutolewa

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, nimebaini shilingi 565,955,113,766 ilitolewa kwa matumizi ya kawaida ikilinganishwa na makisio ya shilingi 598,777,973,841. Hivyo, kulikuwa na pungufu ya shilingi 32,822,860,075. Hii inadhihirisha kwamba shughuli za Wakala wa Serikali hazikufanyika kwa kiwango kinachotarajiwa kutokana na fedha kutolewa pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mchanganuo wa fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha halisi zilizotolewa umeoneshwa kwenye **Kiambatisho 8.1**

8.2.3 Fedha za maendeleo zilizotolewa zaidi ya bajeti

Katika mwaka wa ukaguzi shilingi 1,113,067,847,193 ilitolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi ya makisio yaliyoidhinishwa ya shilingi 777,034,157,470. Hivyo, kulikuwa na ongezeko la shilingi 336,033,689,723. Hii inaashiria kwamba makisio kwa fedha za maendeleo hayakuwa sahihi. Mchanganuo wa makisio ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na kiasi kilichotolewa kimeoneshwa kwenye **kiambatisho 8.1**

8.2.4 Makusanyo ya vyanzo vya ndani vya mapato

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini kwamba mapato ya vyanzo vya ndani kiasi cha shilingi 347,514,404,193 kilikusanywa na wakala wa serikali 29 dhidi ya makisio yaliyoidhinishwa ya shilingi 346,806,173,945. Kwa ujumla, kulikuwa na ongezeko la makusanyo ya shilingi 708,230,248 (0.2%) dhidi ya makisio yaliyoidhinisha. Licha ya kuwa na upungufu wa makusanyo, kulikuwa na wakala 8 ambazo zilikusanya zaidi ya makisio yaliyoidhinishwa ya shilingi 31,496,467,763 (15%) na wakala 21 ambazo zilikusanya pungufu ya makisio yaliyoidhinishwa kwa shilingi 32,204,698,011 (21%).

Napendekeza serikali iandae mkakati ambao utasaidia wakala wa serikali kutegemea vyanzo vya ndani vya mapato kuliko ruzuku kutoka serikalini.

8.2.5 Madeni yasiyolipwa shilingi 1,875,798,730,303.27

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, wakala 28 zilikuwa na madeni kiasi cha shilingi 1,875,266,954,590.27. Hili ni ongezeko la shilingi 289,804,290,285.27(18%) ikilinganishwa na madeni ya mwaka 2014/2015 ya kiasi cha shilingi 1,585,462,664,305. Hii inaonesha uwezo wa wakala katika kulipa madeni yake umepungua kwa (18%). Kati ya madeni yote, shilingi 1,827,688,484,688.38 (97%) yalikuwa ni madeni yaliyozidi miezi 12 wakati shilingi 47,578,469,901.89 (3%) ni

madeni yasiyolipwa kwa miezi 12. Kutokana na asilimia 97 ya madeni yote kutolipwa kwa zaidi ya mwaka, inapunguza sifa ya wakala kwa wazabuni. Pia, nimebaini kwamba wakala wa barabara ilikuwa na kiasi kikubwa cha madeni cha 95% ya madeni yote.

Napendekeza Maafisa Masuuli wa Wakala za Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kulipia madeni yaliyofikia muda wake.

Orodha ya wakala zenye madeni yasiyolipwa imeoneshwa kwenye kiambatisho **Kiambatisho 8.2**

8.2.6 Mapungufu yaliyoonekana kwenye matumizi

Malipo yasiyoambatana na risiti za Kielektoniki (EFD) shilingi 2,976,493,244.60

Wakati wa kupitia matumizi ya wakala kwa mwaka 2015/2016 nimebaini kwamba Wakala 11 zililipa kiasi cha shilingi 2,976,493,244.60 kwa Wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielektroniki (EFD). Hii ni kinyume na kanuni 24 ya EFD ya mwaka 2012. Kutokudai risiti za kielektroniki kunawahamasisha walipakodi kukwepa kodi, hivyo, kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.

Orodha ya wakala zilizofanya malipo bila kudai risiti za kielekitroniki zimeainishwa kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali 49: Malipo yasiyoambatana na risiti za kielektroniki

Na.	Wakala	Kiasi (shilingi)
1	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	585,682,265.00
2	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam	14,560,317
3	Wakala wa Vipimo	317,869,399
4	Bodi ya mikopo kwa Serikali za Mitaa	23,461,900
5	Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi	27,249,440
6	Wakala wa Barabara Tanzania	386,347,303.10
7	Wakala wa Utafiti wa Miamba	114,033,386.50
8	Wakala wa Majengo Tanzania	63,423,985
9	Mamlaka ya viwanja vya ndege	1,310,886,516
10	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya	40,719,732

Na.	Wakala	Kiasi (shilingi)
	Elimu	
11	Chuo cha Taifa cha Utalii	92,259,001
	Jumla	**2,976,493,244.60**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza wakala wadai risiti za kielektroniki wakati wa kufanya malipo kwa Wazabuni. Pia, wakala zinashauriwa kutokufanya miamala na Wazabuni wasiotumia mashine za kielektroniki.

Malipo bila kukata kodi ya zuio

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 nimebaini wakala nane zilifanya malipo kwa Wazabuni mbalimbali bila kukata kodi ya zuio kiasi ha shilingi 114,056,170.46. Pia malipo ya kiasi cha shilingi 991,182,807.00 yalifanywa na wakala tatu bila kukata kodi ya zuio. Hii ni kinyume na kifungu 83 cha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2006 inayotaka taasisi zinazofanya manunuzi kukata kodi ya zuio kiasi cha 2% kwa bidhaa na huduma zote zinazonunuliwa. Kushindwa kukata kodi ya zuio kunaashiria upotevu wa mapato ya Serikali. Orodha ya Wakala ambazo hazikukata kodi ya zuio imeainishwa kwenye jedwali hapo chini:

Na.	Wakala	Kiasi (Shilingi)
	Malipo bila kutata tozo ya zuio	
1	Wakala wa Vipimo	919,188,041.00
2	Wakala wa Majengo Tanzania	29,015,706.00
3	Wakala wa Utafiti wa Miamba	42,979,060.00
	Jumla	**991,182,807.00**
	Kodi ya zuio isiyokatwa	
1	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	15,589,444.00
2	Wakala wa Ndege za Serikali	8,190,167.60
3	Shirika la Mzinga	4,283,694.00
4	Chuo cha Utumishi wa Umma	28,600,000.00
5	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania	6,264,937.50
6	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo	5,400,000.00

Na.	Wakala	Kiasi (Shilingi)
7	Shirikisho la serikali za Mitaa Tanzania	37,340,384.00
8	Shirika la Mzinga	8,387,543.36
	Jumla	**114,056,170.46**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza wakala za serikali zizingatie kifungu Na. 83 cha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2006 kwa kukata kodi ya zuio ya 2% au 5% ya kiasi cha bidhaa au huduma zilizonunuliwa.

Malipo yasiyokuwa na viambatisho shilingi 508,619,273

Nimebaini kwamba, katika mwaka 2015/2016 Wakala tisa (25%) kati ya 32 zilizokaguliwa zilikuwa na malipo ya kiasi cha shilingi 508,619,273 ambayo hayakuwa na viambatisho. Hii ni kinyume na Kanuni 86(1) na 95(4) Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inayotaka malipo yote kuwa na viambatisho. Hivyo, halali malipo ya shilingi 508,619,273 haukuweza kuthibitika.

Orodha ya wakala zenye malipo yasiyo na viambatisho yameainishwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali 50: Wakala zenye malipo yasiyo na viamboatisho

Na.	Wakala	Kiasi(shilingi)
1	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	16,649,558.00
2	Wakala wa umeme Vijijini	67,582,025.79
3	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam	8,609,360.32
4	Wakala wa serikali Mtandao	5,253,574.00
5	Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania	5,645,538.00
6	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	305,520,308.83
7	Wakala wa Maabara za Serikali	8,784,282.00
8	Shirikisho la Serikali za Mitaa Tanzania	22,992,600.00
9	Wakala wa Umeme Vijijini	67,582,025.79
	Jumla	**508,619,273**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza maafisa masuuli wazingatie Kanuni 86(1); na 95(4) na kuhakikisha kwamba, malipo yote yanakuwa na viambatisho vya kutosha.

Masurufu yasiyorejeshwa shilingi 1,179,670,314

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, nimebaini wakala tano zenye masurufu yasiyorejeshwa kiasi cha shilingi 1,179,670,314. Hata hivyo, hadi tarehe 30/06/2016 masurufu hayo yalikuwa hayajarejeshwa kinyume na Kanuni 103(1) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(iliyorekebishwa 2004) ambayo inahitaji masurufu kurejeshwa ndani ya siku 14 baada ya kukamilika kwa shughuli husika. Orodha ya wakala zenye masurufu yasiyorejeshwa imeoneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali 51: Wakala zenye masurufu yasiyorejeshwa

Na.	Wakala	Kiasi (shilingi)
1	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	94,907,400.00
2	Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa	3,843,000.00
3	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam	2,910,000.00
4	Wakala wa usajili na leseni za biashara	189,700,716.00
5	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	436,657,119.00
6	Shirikisho la serikali za Mitaa Tanzania	69,507,764.80
7	Shirika la Mzinga	382,144,314.00
	Jumla	**1,179,670,314.00**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza kuwa wakala za Serikali zizingatie kanuni za Fedha Umma kwa kuhakikisha masurufu yanarejeshwa baada ya kazi husika kukamilika.

Uchepushaji wa fedha za mirathi shilingi 169,000,000

Kwa mujibu wa sheria 352 ya Usimamizi wa Fedha za Mirathi hakuna kifungu kinachompa madaraka na wajibu Kabidhi Wasii Mkuu kufanya malipo kinyume na matakwa ya Sheria.

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016, nimebini kwamba fedha za mirathi kiasi cha shilingi 169,000,000 uliolipwa kutoka kwenye akaunti ya mirathi ili kugharamia matumizi ambayo hayaendani na malengo ya fedha. Fedha hizo zilihifadhiwa kwa malengo ya kugawiwa kwa wanufaika wa marehemu. Uchepushaji wa fedha za mirathi unasababisha athari ya kifedha kwa walengwa kwa kushindwa kupata fedha zao pindi wanapozihitaji.

Napendekeza Wakala warejeshe kiasi chote cha fedha cha shilingi 169,000,000 kilichochepushwa kutoka akaunti ya mirathi ili kusaidia shughuli za mirathi kwa wakati. Pia, wakala ihakikishe kwamba fedha za mirathi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

8.2.7 Rejista ya mali za kudumu kutoandaliwa

Kanuni 265(2) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inataka tarehe na taarifa nyingine za mabadiliko ya mali zinatakiwa kuwekewa kumbukumbu kadiri yanavyotokea.

Wakati wa kupitia mifumo ya ndani, nimebaini kwamba rejista ya mali za kudumu kwa wakala mbili hazikufanyiwa mapitio na kwa Wakala moja haikuandaliwa kabisa. Hii ni kinyume na Kanuni 265(2) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

Na.	Wakala	Rejista ambayo haikufnyiwa mapitio	Rejista isiyoandaliwa
1	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	v	
2	Chuo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki	v	
3	Wakala wa Maabara za Mifugo		v

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza kuwa wakala zizingatie Kanuni 265(2) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 kwa kuhakikisha kwamba rejista ya mali za kudumu za wakala zinaenda na wakati ili kuhakikisha

kwamba kiasi cha mali za kudumu zinazooneshwa kwenye taarifa za fedha zinalingana na kiasi kilichooneshwa kwenye Rejista ya Mali za Kudumu.

8.2.8 Magari yaliyoegeshwa bila matengenezo kwa muda mrefu

Katika ukaguzi nimebaini magari 92 katika wakala sita yaliyoegeshwa: TMA 4(4%), TBA 1(1%), TFSA 26(28%), NIDA 52(57%), TANROADS 7(8%) and 2(2%) ADEM. Maafisa Masuuli hawajachukua taratibu za uuzaji kulingana na matakwa ya Kanuni 254(1) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001. Kutokuchukua hatua za haraka dhidi ya magari chakavu kunasababisha upotevu wa mali za serikali.

Napendekeza kuwa wakala husika ziuze magari yaliyoegeshwa bila matengenezo ili kuepuka hasara zaidi inayoweza kujitokeza.

Madeni yasiyokusanywa Shilingi 626,045,446,452

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 nimebaini wakala 29 zenye madeni yasiyokusanywa kiasi cha shilingi 626,045,446,452 pungufu ya shilingi 61,976,961,241.57 (9%) ikilinganishwa na madeni yasiyokusanywa ya shilingi 688,022,407,694 ya mwaka 2014/2015. Kati ya madeni yasiyokusanywa, shilingi 562,411,109,508.26 yalikuwa hayajakusanywa kwa zaidi ya miezi 12 na shilingi 63,634,336,944.17 kwa miezi 12. Aidha, nimebaini kwamba wakala wa barabara ilibeba 79%, ikifuatiwa na Wakala wa majengo 5% na Wakala wa Ndege za Serikali 3% ya mapato yote yasiyokusanywa yaliyooneshwa kwenye katika mwaka wa ukaguzi.

Orodha ya Wakala zenye madeni yasiyokusanywa imeoneshwa katika **Kiambatisho 8.3**

Kiasi kikubwa cha madeni yasiyokusanywa hupunguza shughuli za kiutendaji za wakala.

Napendekeza kuwa wakala zifuatilie kwa karibu Madeni yasiyokusanywa ili kuepuka ucheleweshaji wa Wakala kutekeleza malengo yake.

8.3 Masuala Maalum ya Ukaguzi juu ya Wakala, Taasisi nyingine, Fedha Maalum na Maji Mabonde

8.3.1 Ukaguzi wa Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART)

Mapungufu yaliyojitokeza katika mkataba wa utoaji wa huduma ya usalama katika vituo vya DART na Jangwani Shilingi 178,652,000

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini kwamba tarehe 05/05/2016 Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam iliingia mkataba wa miezi 12 na M/S China Tanzania Security Company Ltd wa utoaji huduma ya ulinzi kwenye vituo vya DART na Jangwani kwa jumla ya shilingi 178,652,000. Hata hivyo, mapitio ya taratibu za manunuzi imebaini mapungufu yafuatayo:

Matangazo na Zabuni zilizotolewa hazikuwasilishwa PPRA. Mkataba ulisainiwa baada ya tarehe ya kukamilisha mkataba kuisha kinyume na Kanuni 370(1) ya kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. Pia, nakala ya mkataba haikuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupitia na kuhakikiwa (Vetting) kinyume na Kanuni 59(1 na 2) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Kutokana na mazingira hayo ni vigumu kuthibitisha kwamba taratibu sahihi za manunuzi zilifuatwa katika utoaji wa huduma za usalama, na iwapo matumizi ya shilingi 178,652,000 yalikuwa matumizi sahihi ya fedha za umma.

Napendekeza kuwa menejimenti ya Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam ifuate sheria na Kanuni dhidi ya usimamizi wa mikataba; na kuweka mikakati ya jinsi ya kutatua mapungufu yanayojitokeza. Hivyo, wahakikishe

wanaimarisha mifumo ya ndani ili kuhakikisha mapungufu hayajitokezi kwa baadae.

Manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi shilingi 332,652,800

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2015/2016, nimebaini kwamba Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam ilinunua bidhaa na huduma za jumla ya shilingi 332,652,800 nje ya mpango wa manunuzi. Huduma ilikuwa kwa ajili ya kukodi sehemu ya ndani, nishati na mnara wa mawasiliano kwa kiasi cha shilingi 154,000,800.00 na kutoa huduma ya usalama katika vituo vya Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam na kituo kikuu cha Jangwani kwa kiasi cha shilingi 178,652,000.00. Hii ni kinyume na kanuni 69(3) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inayotaka Taasisi inayofanya manunuzi kufanya makisio sahihi ya mahitaji ya bidhaa na huduma na kazi.

Kushindwa kufuata Kanuni 69(3) ya Kanuni ya Manunuzi ya umma ya mwaka 2013, kunasababisha kufanya manunuzi yasiyo na ufanisi.

Napendekeza uongozi wa Wakala wa Usafiri wa Mwendokasi Dar es Salaam ufuate Kanuni 69 na 64 ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kwa kuhakikisha kwamba Manunuzi yote yanapangwa na kuidhinishwa ipasasvyo.

Matangazo katika Miundombinu ya DART Isiyo na Mikataba

Jumla ya mapato ya shilingi 90,498,542.57 yaliyooneshwa kwenye taarifa za fedha yaliyotokana na matangazo katika miundombinu ya DART hayakuwa na uthibitisho ikiwemo nyaraka za manunuzi ya zabuni. Hii ni kinyume na kanuni 55(1) ya kanuni ya manunuzi ya umma ya mwaka 2013, hivyo ilishindikana kuthibitisha usahihi wa taratibu za manunuzi.

Napendekeza kuwa wakala wa serikali wafuate taratibu za manunuzi na kuandaa mikataba kwa kila taasisi inayotumia miundombinu ya DART kufanya matangazo.

Ada ambayo DART Haikulipwa na Meneja wa Mfuko wa ISP Shilingi 287,600,000

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016 nimebaini shilingi 372,600,000 zilitakiwa kulipwa na meneja wa mfuko wa ISP kwenda DART kama ada ya ISP kati ya mwezi 16/05/2016 mpaka 30/06/2016; Mpaka kufikia Juni 2016, kiasi cha shilingi 85,000,000 zililipwa na kubaki kiasi cha shilingi 287,000,000 ambazo hazijalipwa na ISP kupitia meneja wa mfuko DART. Hii ni kinyume na jedwali E la mkataba ambao ulifanyiwa marekebisho kwenye nyongeza namba 1 ya mkataba kwenye makubliano kati ya DART na UDART ya tarehe 31/05/2016; ambapo, meneja wa mfuko alitakiwa kufanya malipo ya kila siku ya shilingi 8,100,000 kwa wakala kama ada ya upatikanaji wa huduma. Na ikiwa siyo siku ya kazi, malipo yafanyike siku ya kazi inayofuata.

Kutokulipa ada ya upatikanaji wa huduma kunaathiri ukwasi wa wakala, na hivyo, kucheleweshe utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Napendekeza kuwa wakala afuatilie na kuzingatia matakwa ya mikataba.

8.3.2 Ukaguzi wa wakala wa mbegu za kilimo

Gharama za mafunzo zisizo na viambatisho shilingi 88,689,406

Katika mwaka wa ukaguzi nimebaini kwamba Wakala wa mbegu za kilimo ulilipa shilingi 88,689,406 kwa wafanyakazi kuhudhuria mkutano wa wanasayansi ulioitishwa na waanzilishi wa EAAPP uliofanyika mjini Nairobi Kenya kuanzia tarehe 14 hadi Septemba 18, 2015. Uchunguzi zaidi ulionesha kwamba hakukuwa na nyaraka kama barua za mwaliko, fomu za masurufu, vibali vya ofisi, tiketi za ndege na vibali vya safari kutoka kwa washiriki ili kuthibitisha kwamba wafanyakazi walihudhuria mkutano husika. Kushindwa kuwasilisha nyaraka zinazotakiwa uhalali wa shilingi 88,689,406 hakuweza kuthibitishwa, hivyo, inaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha.

Napendekeza kuwa wakala aboreshe mfumo wake wa ndani kwa kuweka vema nyaraka na kuhakikisha zinapatikana wakati wa ukaguzi.

Mapungufu katika usimamizi wa mikopo

Katika ukaguzi wa wakala wa mbegu za kilimo nimebaini kwamba, wakala wa mbegu za kilimo alisambaza bidhaa kwa mkopo za shilingi 92,958,000 kwa mawakala wa mbegu ambao mikataba yao imeisha muda bila kuhuishwa. Ukaguzi wangu ulibaini zaidi kuwa Mwanza Agrovet ilikuwa na jumla deni kiasi cha shilingi 51,440,000; ambapo, walipaswa kulipa shilingi 5,000,000 kwa kila mwezi. Hata hivyo, wakala wa mbegu alishindwa kuzingatia makubaliano ya mkataba lakini Wakala wa mbegu za kilimo aliendelea kutoa mikopo kwa wakala na kusababisha mkopo kuongezeka kufikia shilingi 93,072,000 hadi kufikia 18/8/2014. Udhaifu katika usimamizi wa mikopo unasababisha kuongezeka kwa madeni yasiyolipika.

Napendekeza wakala kuanzisha utaratibu ambao utahakikisha taratibu za mikopo zinafuatwa ili kusaidia urejeshaji wa mikopo kwa wakati.

8.3.3 Ukaguzi wa shirika la Mzinga

Ununuzi wa boti haujathibitishwa shilingi 79,352,695,560(Euro 32,588,376)

Katika ukaguzi wa mikataba nimebaini kwamba, mnamo Juni, 2015 shirika la Mzinga liliingia mkataba na benki ya uwekezaji Tanzania wa mkopo wa Dola za kimarekani ambazo ni sawa na Euro 32,588,376 (shilingi 79,352,695,560 kulingana na kiwango cha kubadilishia fedha cha benki kuu ya Tanzania cha tarehe 30/6/2016) kwa ajili ya ununuzi wa boti. Katika mkataba huu shirika la kimaendeleo ya petroli Tanzania lilihusika kufungua akaunti ya escrow kuhudumia mkopo huo. Hata hivyo, menejimenti ilishindwa kutoa taarifa za kumbukumbu za manunuzi na zabuni. Kwa hiyo, sikuweza kuthibitisha mchakato wa ununuzi pamoja na mapato mkopo katika akaunti ya escrow.

Nashauri Afisa Masuuli kuwasilisha nyaraka za manunuzi ya boti zilizonunuliwa.

8.3.4 Ukaguzi wa Wakala wa Barabara Tanzania

Ucheleweshwaji wa malipo ya awali ya wakandarasi

Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2015/2016, nilibaini kuwa malipo ya awali ya kiasi cha shilingi 1,339,604,636.92 hayakulipwa na Wakala wa Barabara Tanzania kwa M/S China New Era International Engineering Corporation, 128 Huancheng Namlu Road Xián 710054, P.R China kwa ajili ya kuboresha barabara ya Tenende-Matema (34.6KM) kwa kiwango cha lami kupitia mkataba Na. TRD/HQ/1050/2014/2015 kwa shilingi 56,911,253,695. Hii ni kinyume na kifungu 24 cha masharti maalumu ya mkataba yanayotaka malipo ya awali kulipwa ndani ya siku 60 baada ya mkandarasi kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali. Aidha, nimebaini kwamba malipo ya awali kiasi cha shilingi 8,430,248,435.06 kwa ajili ya kuboresha barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (171 KM) kwa kiwango cha lami yalicheleweshwa kulipwa kwa M/S China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) kwa muda wa siku 241 kupitia mkataba Na. TRD/HQ/1004/2015/2016. Kulingana na kifungu 53.1 cha masharti maalumu ya mkataba Wakala wa Barabara Tanzania ilitakiwa kulipa 15% ya bei ya mkataba kama malipo ya awali kwa mkandarasi ndani ya siku 30 baada ya kuwasilisha dhamana. Badala yake, malipo yalifanyika tarehe 07 Januari, 2016. Kucheleweshwa kulipa malipo ya awali kutasababisha kuongezeka kwa gharama kutokana na muda zaidi na vifaa kutokutumika.

Napendekeza Wakala na Wizara ya Fedha na Mipango kulipa malipo ya wkandarasi kwa wakati ili shughuli za ujenzi ziweze kukamilika kwa muda uliopangwa.

Riba iliyotokana na kucheleweshwa kwa malipo shilingi 7,874,921,250.36 na Dola za Kimarekani 714,066.08

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, nimebaini kwamba Wakala wa Barabara Tanzania ilitozwa riba ya shilingi

7,874,921,250.36 na Dola za Kimarekani 714,066.08 kutokana na kucheleweshwa malipo ya kiasi cha shilingi 36,766,426,168.68 na USD 6,534,720.75. Hii ni kinyume na kifungu 45.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinachotaka mkandarasi kulipwa malipo yaliyoidhinishwa na meneja wa mradi ndani ya siku 28 baada ya hati ya madai ya malipo kutoka; na iwapo mwajiri atacheleweshe malipo, mkandarasi atatakiwa kulipwa riba ya kucheleweshwa malipo kwa kiwango cha kitakachokuwa kinatumika kwa wakati huo. Riba kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ni matumizi yasiyo na faida ambayo yangeweza kuepukika na Serikali. Riba kutokana na kucheleweshwa kwa malipo imeoneshwa kwenye jedwali Na. hapo chini:

Jedwali 52: Riba kutokana na kucheleweshwa malipo

Mkataba	Mkandarasi	Tarehe iliyoidhinishwa	Tarehe ya malipo	IPC Na.	Kiasi cha IPCs kilichobaki (shilingi)	Riba iliyolimbikizwa (shilingi)
Mkataba wa ukarabati wa barabara ya Tenende-Matema(kilomita 34.6) kwa kiwango cha lami	M/S China New Era International Engineering Corporation, 128 Huancheng Namlu Road Xián 710054, P.R China	19/10/2015	15/11/2015	1	3,874,797,535	0
		22/04/2016	18/05/2015	2	1,944,917,925	246,676,618
		29/07/2016	25/08/2016	3	3,342,419,859	347,808,371
		25/10/2016	22/11/2016	4	4,051,405,120	-141,807,421
Mkataba namba TRD/HQ/1007/2013/14 wa ukarabati wa barabara ya KIA-MERERANI kwa kiwango cha lami	M/S China Henan international Cooperation Group Co Ltd (CHICO)	24/11/2015	24/11/2015	1	1,459,884,871.15	243,062,663.21
			15/03/2016	2	1,827,546,919.63	141,642,542.39
			29/04/2016	3	1,882,671,286.42	110,849,578.62
			08/06/2016	4	2,385,232,947.83	103,168,948.82
			28/06/2016	5	1,020,371,543.37	36,073,525.47
			28/07/2016	6	1,475,497,330.57	36,213,037.04
			02/09/2016	7	1,739,851,446.96	19,627,589.95
			20/09/2016	8	1,973,697,386.12	7,871,924.96
			12/10/2016	9	2,207,005,632.82	0
		12/11/2016	12/11/2016	10	734,809,065.01	0
Ukarabati wa barabara ya Bagamoyo-Makofia-Msata(kilomita 64) kwa kiwango cha lami	M/s Estim Construction Company Ltd of BOX 19716 Dar es Salaam			22	3,854,022,564.37	0
				23	2,992,294,735.43	6,723,733,871.90
		JUMLA			**36,766,426,168.68**	**7,874,921,250.36**
		Tarehe iliyoidhinishwa	**Tarehe ya malipo**	**IPC Na**	**Kiasi cha IPCs kilichobaki (Dola za Kimarekani)**	**Riba iliyolimbikizwa(Dola za Kimarekani)**
				IPC 22	3,944,206.57	
				IPC 23	2,590,514.18	714,066.08
		JUMLA			**6,534,720.75**	**714,066.08**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza wakala kufuatilia fedha Wizara ya Fedha na Mipango ili kuweza kulipa wakandarasi kwa wakati ili kuepuka riba ambayo itaongeza gharama kwa Serikali.

Madai ya wakandarasi na mzabuni mshauri yasiyolipwa shilingi 22,539,391,406.30

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 nimebaini kwamba TANROAD haikulipa madeni ya Wakandarasi na Wazabuni Washauri kiasi cha shilingi 20,270,965,854.88. Kushindwa kulipa hati za madai kwa mwaka unaotakiwa huathiri utoaji wa fedha kwa mwaka unaofuata.

Aidha, nilibaini kuwa malipo kwa Mzabuni Mshauri kiasi cha shilingi 1,639,898,497.55 hayakulipwa kutokana na kucheleweshe kulipwa kwa hati za malipo za mpito (Interim Payment Certificates). Hii ilisababisha kuongezeka kwa muda wa Mkandarasi mshauri; pia, nyongeza namba 5 kwa Mkandarasi kama malipo yasiyo na tija ya kiasi cha shilingi 1,872,927,984.96 ili kuweza kukamilisha shughuli zake kama zilivyopangwa kwenye mkataba ulioingiwa tarehe 16/11/2016 ambao bado haujaidhinishwa. Zaidi ya hapo, ankara namba 19 mpaka 24 za mzabuni mshauri hazikulipwa. Hii imesababisha limbikizo la shilingi 628,527,053.87 kwa wazabuni washauri. Hii ni kinyume na Kifungu 54.3 cha masharti ya jumla ya mkataba kinachoeleza kwamba, tofauti yoyote kati ya malipo halisi na malipo yanayotakiwa kulipwa lakini hayakulipwa kwa muda yanatakiwa kutozwa riba sawa na kiwango cha riba kinachotozwa na Benki kuu ya Tanzania. Kuchelewa kulipa malipo ya wakandarasi na wazabuni washauri kunasababisha kuwa na matumizi yasiyo na tija kwa mfumo wa riba na adhabu kwa siku za mbeleni. Malipo ya wakandarasi na wazabuni washauri yasiyolipwa yameoneshwa katika katika jedwali hapa chini:

Jedwali 53: Madai ya Wakandarasi na Wazabuni Washauri yasiyolipwa

Madai ya mkandarasi yasiyolipwa					
Mkataba	**Mkandarasi**	**IPC Na.**	**Tarehe ya kuwasilisha**	**Tarehe ya malipo (shilingi)**	**Kiasi kilichopaswa kulipwa (shilingi)**
Ukarabati wa barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi-Lamadi(kilomita 171) kwa kiwango cha lami, Lot: Mwigumbi-Maswa - Sect.(kilomita 50.3) yenye thamani ya shilingi 61,461,656,234	M/S China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO)	1	23-Apr-16	18-Jun-16	2,775,608,310.64
		2	05-Jul-16	30-Aug-16	4,660,824,858.22
		3	11-Aug-16	06-Oct-16	2,503,845,079.07
		4	05-Sep-16	31-Oct-16	1,888,057,804.32
		5	02-Oct-16	27-Nov-16	2,667,331,658.91
		6	03-Nov-16	29-Dec-16	3,399,366,557.70
Ukarabati wa barabara Usagara-Kisesa(kilomita 16) kwa kiwango cha lami	M/s Nyanza Road Work Limited - Mwanza	12	03-Jan-15	31-Jan-15	561,499,103.07
		13	04-May-15	01-Jun-15	712,377,650.93
		14	12-Oct-16	09-Nov-16	1,102,054,832.02
Jumla ya madai ya wakandarasi					**20,270,965,854.88**
Madai ya wakandarasi washauri					
Mkataba	**Mkandarasi**				**kiasi (shilingi)**
Mkataba namba TRD/HQ/1007/2013/14 wa kukarabati barabara ya KIA-MERERANI (kilomita 26) kwa kiwango cha lami	Consultant Engineers M/s LEA associate South Asia JV, M/s LEA associate Canada in Association with M/s DOCH ltd				628,527,053.87
Ukarabati wa barabara ya Bagamoyo-Makofia-Msata(kilomita 64) kwa kingo cha lami	M/s H.P Gauff Ingenieure GmbH CO. JBG in association with Nimeta Consult (T) ltd				1,639,898,497.55
Jumla ya madai ya wakandarasi					**2,268,425,551.42**
Jumla ya madai ya wakandarasi na wakandarasi washauri					**22,539,391,406.30**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Napendekeza wakala kutafuta fedha kutoka Hazina na kuhakikisha Mkandarasi na Mzabuni mshauri analipwa pasipo kuchelewa.

Kodi ya ongezeko la thamani iliyoingizwa kwenye malipo ya mkandarasi kwa makosa shilingi 13,611,589

Wakala wa barabara ililipa shilingi 13,611,589 kwa M/s Mahenda Sogoni Construction Co. Ltd wa Mwanza kama kodi ya ongezeko la thamani (na shilingi 233,413.20 ililipwa kwa M/s Mgalula Investment Co. Ltd wa Shinyanga badala ya Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania). Kiasi kilicholipwa hakikurejeshwa na Mkandarasi wala haikukatwa kwenye Hati ya Malipo ya mpito namba 2. Kushindwa kurejesha kodi ya

ongezeko la thamani iliyolipwa kimakosa kwa mkandarasi inaashiria upotevu wa mapato ya Serikali.

Napendekeza Wakala wa barabara kuhakikisha kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa inarejeshwa kwa kamishna wa mamlaka ya mapato Tanzania.

8.3.5 Ukaguzi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

Ununuzi kupitia chanzo kimoja shilingi 178,718,071.17

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini kwamba Wakala mbili zilinunua bidhaa za shilingi 178,718,071.17 kupitia chanzo kimoja bila kufuata utaratibu. Manunuzi hayakuwa shindani, pia hayakufuata kanuni 76, 159 na 161 ya manunuzi ya umma ya mwaka 2013 inayotoa msharti ya manunuzi kupitia chanzo kimoja.

Kati ya manunuzi yote, jumla ya shilingi 81,559,471.17 (46%) yalinunuliwa na Wakala wa majengo na shilingi 97,158,600 (54%) yalinunuliwa na Wakala wa maabara za serikali

Jedwali 46: Bidhaa zilizonunuliwa kupitia chanzo kimoja

Wakala	Tarehe	PV Na.	Maelezo	Mlipwaji	Kiasi (shilingi)
Wakala wa majengo Tanzania	06/04/2016	Pv00001305	Gharama za manunuzi ya nyumba kwa ajili ya mkuu wa mkoa w Tanga na Simiyu. Hati namba 10074 ya kuagiza bidhaa, sofa seti	Royal Furnishers Ltd	24,759,118.64
	06/04/2016	PV00001304	Gharama za mununuzi ya thamani kwa ajili ya mkuu wa mkoa wa Tanga na Simiyu (vitanda na meza ya kulia chakula)	ORCA deco	32,303,050.84
	26/01/2016	PV 0000819	Gharama za kurudia usanifu wa jengo kwa ajili ya watumishi wa umma- Aina B iliyopo Bunju kwa dola za kimarekani 3000 kwa kiwango cha shilingi 2224 cha kubadilisha fedha za kigeni cha tarehe 16/12/2015	MSM MUHENDISLIK INSTAAT SAN. VE TIC LTD STI	5,671,200
	28/04/2016	PV 00001561	Gharama za ununuzi wa samani za nyumba ya mkuu wa mkoa wa Songwe	ORCA DECO	11,826,101.69
	02/10/2015	DISB 000014365	Gharama za kukodisha jenereta kwa siku 14	KAMENE ELECTRICAL SERVICE	7,000,000
Jumla					**81,559,471.17**
Wakala wa maabara za serikali	Energy dispersive X-Ray fluorescence machine				97,158,600
Jumla kuu					**178,718,071.17**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Ni maoni yangu kwamba kutokufuata taratibu za manunuzi kunapelekea ufujaji wa fedha za Serikali kutokana na manunuzi yasiyofuata taratibu.

8.3.6 Ukaguzi wa wakala wa usajili, ufilisi na udhamini (RITA)

Mapungufu katika usimamizi wa Mkataba wa ubia

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016, nimepitia mkataba wa ubia na makubaliano ya mkopo kati ya wakala wa usajili, ufilisi na udhamini (RITA) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), na kubaini kwamba, jumla ya shilingi 12,291,575,722 iliripotiwa katika taarifa za fedha kama riba

ya mkopo uliotolewa na NSSF kwa RITA kwa ajili ya ujenzi a mnara wa RITA. Kati ya fedha zote, jumla ya shilingi 7,608,859,091 zilikuwa ni limbikizi la riba tangu mwaka 2011 ambapo shilingi 4,682,716,631 zilikuwa ni riba ya asilimi 15 ya mwaka ya mkopo wa shilingi 27,213,704,328 kutoka NSSF kwenda RITA. Aidha, nimebaini kwamba riba imekuwa ikiongezeka siku hadi siku kutokana na rita kutokulipa mkopo.

Kulingana na makubaliano ya mkataba yaliyoingiwa 19/04/2011 kati ya RITA na NSSF, kiasi cha mkopo kilichokubalika ni shilingi 22,747,852,323.28. Hata hivyo, mapitio ya nyaraka za mkopo yanaonesha shilingi 27,213,704,328 zilihamishwa kutoka NSSF kwenda RITA kama mkopo ikiwa ni zaidi ya shilingi 4,465,852,005 ya kiasi cha mkopo uliokubaliwa bila ya makubaliano mapya ya mkopo au marekebisho ya makubaliano ya nyongeza ya kiasi cha fedha.

Aidha, kutokana na makubaliano ya ubia yaliyoingiwa tarehe 10/11/2010, moja kati ya majukumu ya pande zote yaliyoelezwa kwenye aya 1.2 ni kufungua kampuni ndani ya Tanzania ambayo itakuwa ya ubia ambapo fedha zote zitapitia huko. Mpaka sasa, kampuni hiyo haijaanzishwa na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zilipelekwa RITA moja kwa moja. Zaidi ya hayo, ilikubalika kuanzisha akaunti ya pamoja chini ya aya 4.6 ya makubaliano; ambapo, mapato yote yatakuwa yanawekwa kwenye akaunti hiyo. Hata hivyo yote hayakuweza kuzingatiwa na pande zote mbili.

Kuchelewa kulipa mkopo pamoja na riba kwa wakati kunapelekea kuongezeka kwa deni na pia inaongeza mzigo kwa wakala.

Napendekeza wakala wa usajili, ufilisi na udhamini (RITA) kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa mkopo ili kupunguza gharama zinazoongezeka siku hadi siku.

Mapato yasiyorejeshwa RITA shilingi 17,652,050

Katika kupitia mapato yliyokusanywa na ofisi ya Afisa tawala wa wilaya kwa niaba ya RITA, nimebaini kwamba shilingi 17,652,050 zilikusanywa na ofisa za Maafisa Tawala wa Wilaya sita, lakini hazikuhamishiwa kwenye akaunti ya makusanyo ya

RITA. Mapato hayo yalitumiwa na ofisi za Maafisa Tawala wa Wilaya kufidia matumizi ya ofisi kinyume na Kanuni 78(1) ya Fedha za Umma. Mchanganuo wa makusanyo kutoka mikoa hiyo imeoneshwa katika jewali hapo chini

Jedwali 54: Mapato yasiyorjeshwa RITA

Mkoa	Wilaya	Kiasi(Sh)
Tabora	Igunga	874,000
	Tabora	1,440,000
Tanga	Mkinga	11,712,875
	Korogwe	1,491,000
Kilimanjaro	Siha	800,675
	Hai	1,333,500
Jumla		**17,652,050**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Kutokupeleka mapato yaliyokusanywa kupitia ofisi za Afisa Tawala wa Wilaya kwa niaba ya RITA kunaashiria kuwapo kwa mifumo duni ya udhibiti wa mapato ambayo inapelekea ufujaji wa fedha zinazokusanywa na ofisi hizo.

Napendekeza mapato yasiyorejeshwa kiasi ha shilingi 17,652,050 kilichokusanywa na ofisi ya Afisa Tawala wa Wilaya kuejeshwa kwenye akaunti ya makusanyo ya Wakala.

8.3.7 Ukaguzi wa Wakala wa Majengo (TBA)

Ununuzi wa vifaa vya ujenzi/malighafi za ujenzi kwa Wazabuni wasioidhinishwa shilingi 74,139,416

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, wakala wa majengo Tanzania ilinunua vifaa vya ujenzi vya shilingi 74,139,416 kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa. Hii ni kinyume na Kanuni 131(5) ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inayoeleza taratibu za manunuzi kufanywa na Wazabuni walioidhinishwa. Vifaa vya ujenzi vilinunuliwa kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa katika utaratibu ambao haukuelezeka.

Kushindwa kununua vifaa vya ujenzi kwa Wazabuni walioidhinishwa kunaashiria kwamba ubora wa vifaa usingeweza kuthibitishwa.

Napendekekeza Wakala wa majengo kuzingatia masharti ya Sheria ya Manunuzi wa Umma ya kuhakikisha kwamba manunuzi ya umma yanafanywa kwa Wazabuni walioidhinishwa ili kuhakikisha thamani ya fedha na uwazi zinazingatiwa katika manunuzi.

Uchepushaji wa fedha shilingi 500,000,000

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2015/2016 nimebaini kwamba wakala wa majengo (TBA) ilipokea shilingi 500,000,000 kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (sekta ya ujenzi) kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya wizara Dar es salaam. Wakala wa ujenzi ilihamisha fedha hizo shilingi 500,000,000 kwenda kwa meneja wa mkoa wa Dar es salaam kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tano Bunju kinyume na malengo yaliyokusudiwa ya fedha hizo. Hata hivyo, hakukuwa na viambatisho vilivyowasilishwa wakati wa ukaguzi ili kuthibitisha mapokezi na matumizi ya fedha hizo pamoja na taratibu za manunuzi zilizohusika.

Kutokana na hayo, ni vigumu kuthibitisha uhalali na uhalisia wa matumizi ya shilingi 500,000,000 zilizotumika kwenye shughuli ambazo hazikuhusiana na ujenzi wa makao makuu ya jengo la wizara Dar es Salaam.

Ninashauri Wakala wa Majeno Tanzania(TBA) kuhakikisha kuwa fedha zinatumika ipasavyo na kwa mtumizi yasiyokusudiwa.

8.3.8 Ukaguzi wa mamlaka ya viwanja vya ndege

Utekelezaji hafifu wa ukarabati wa kiwanja cha ndege Mwanza

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016, nimebaini kwamba Mamlaka ya viwanja vya ndege iliingia mkataba na AE-027/2011-12/MWZ/W/44 with M/S Beijing Construction Engineering Group Company Ltd – Tawi la Tanzania wa ukarabati wa uwanja wa ndege wa Mwanza kwa kipindi cha miezi 24 kwa bei iliyorekebishwa ya jumla ya shilingi

105,943,140,184. Tarehe rasmi ya kuanza mkataba ilikuwa 01/10/2012. Hadi kufikia septemba 2014, ikiwa ni miezi 23 baada ya kuanza kwa mkataba lakini kazi bado ilikuwa inaendelea na mkandarasi alikuwa amelipwa shilingi 17,884,454,478 sawa na asilimia 17 ya jumla ya bei ya mkataba. Kufikia oktoba 2014 Consulting Engineer M/S UNETEC (United Engineering & Technical Consultants Limited) ilieleza kwamba mwendelezo wa kazi ulikuwa ni chini ya asilimia 30.

Kucheleweshaji kumalizika kwa kazi kutaathiri manufaa ya kiuchumi kama ilivyokusudiwa. Pia, gharama za uendeshaji zitaongezeka kwa mfumo wa adhabu ya kucheleweshaji malipo ya hati za madai na mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya mkataba.

Ninashauri Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwasiliana na Hazina kupata fedha za kutosha ili kumalizia mradi kwa wakati.

8.3.9 Ukaguzi wa wakala wa umeme vijijini(REA)

Mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini

Ukaguzi wa mradi wa umeme vijijini unaonesha kwamba jumla ya miradi 268 ilipangwa kutekelezwa ambapo miradi 185(69%) ilikamilika, na miradi 83(31%) utekelezaji wake ulikuwa unaendelea kulingana na matakwa ya mradi.

Nimepitia mikoa 19 ambayo mradi wa umeme vijijini ilikuwa inatekelezwa; ambapo, mikataba mbalimbali ilitolewa kwa wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Mapungufu mbalimbali yalibainika kama yalivyooneshwa kwenye Jedwali hapa Chini:

Mkoa/Wilaya	Mapungufu yaliyojitokeza

Mkoa/Wilaya	Mapungufu yaliyojitokeza
Arumeru Arusha	Wateja 308 kati ya 549(56%) waliunganishwa na gridi ya Taifa. Kulikuwa na kasoro za kiufundi katika vijiji vinne[23] vya Arumeru ambavyo vilikuwa havijarekebishwa. Marekebisho yanahusisha High Tension and Low Voltage lines; na nguzo zilizojengwa karibu na nyumba za watu na nyingine zilipita kwenye mashamba/viwanja. Hali hii ilisababisha malalamiko ya madai ya kutaka kufidiwa.
Longido mjini	Hakukuwa na ripoti ya pamoja ya kazi iliyokamilika na kuthibitishwa na Trust Agent kulingana na matakwa ya Ibara ya 5 ya mkataba.
Kilimanjaro	Mkandarasi alichelewesha kuanza mkataba kwa siku 30, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Wakala wa Umeme Vijijini kama vile tozo ya kuchelewa kukamilisha kazi kama ilivyoelezwa kwenye kifungu 26.2 cha makubalino ya mkataba inayotaka Mkandarasi kumlipa mwajiri wake tozo ya kuchelewa kukamilisha kazi ya kiasi kilichoelezwa kwenye masharti maalumu ya mkataba kwa kiwango cha asilimia ya bei ya mkataba.
Wilaya ya Hai Kilimanjaro	Kati ya vijiji vinne, viwili vilikuwa vimeingizwa kwenye mawanda/wigo ya kazi havikuwekewa umeme kutokana na migogoro ya ardhi inayodaiwa kuwa mali ya Mamlaka ya viwanja vya ndege iliyohifadhiwa kwa matumizi ya baadaye ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro

[23] Kimnyaki, Mlangarini, Ngaramtoni na Kisongo

Mkoa/Wilaya	Mapungufu yaliyojitokeza
Babati	Kijiji cha Bonga hakikuwekewa umeme kutokana na asili ya kijiografia; hivyo, nguzo hazitaweza kudumu kwa muda uliokusudiwa. Ombi la kutumia mnara wa chuma wa TANESCO uliopewa REA halijaidhinishwa. Hii imezuia vijiji kadhaa kupata mtandao wa umeme vijijini vikiwemo Endanachang, Gidas, Gidabagara, Rirodi, Boay, na Duru.
Kagera	Hali ya mradi haikuweza kuthibitishwa kutokana na kukosekana kwa hati ya mwisho ya awamu ya kwanza ya mradi.
Wilaya ya Maswa mkoa wa Shinyanga	Wigo wa kazi umeongezwa na mkandarasi bila kuidhinishwa na wakala wa umeme vijijini; ambapo, transfoma 21 badala ya 10 ziliwekwa kinyume na makubaliano ya mkataba.
Simiyu	Hakukuwa na ushahidi wa usimamizi wa kazi iliyofanywa na TANESCO kama vile Muhtasari wa vikao vya Usimamizi wa mradi.
Musoma	Katika kijiji cha Mwibagi ilibainika kwamba mkandarasi aliweka transfoma zenye 50 kVA badala 100 Kva; pia, transfoma yenye 50 kVA ufungaji wake haukukamilika.
Mwanza	Hakukuwa na uthibitisho wa ushahidi wa ukaguzi wa kazi iliyokamilika ili kubaini vikwazo vyovyote vinavyohitaji marekebisho kabla ya kukabidhi kazi na vifaa vilivyobaki. Hii ilitakiwa kufanywa na TANESCO
Geita	Kikao cha mwisho kilifanyika Septemba 2014, miaka miwili iliyopita ingawa mradi bado unaoendelea.

Mkoa/Wilaya	Mapungufu yaliyojitokeza
Morogoro	Utekelezaji mdogo wa mradi ulibainika Morogoro; ambapo, wateja 32 kati ya 205(15.6%) wa umeme wa njia tatu na wateja 1592 kati ya 5457(29%) wa umeme wa njia moja waliunganishiwa umeme; wakati mkandarasi alikuwa ameshalipwa 69.6% ya fedha zote.

Napendekeza Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Umeme Vijijini kuimarisha usimamizi na kuhakikisha kwamba, mapungufu yaliyobainika yanarekebishwa na mkandarasi kwa wakati. Kushirikiana na wadau walioshiriki katika mradi ili kuhakikisha kwamba changamoto zinafanyiwa kazi ili kukamilisha Mradi kwa wakati. Zaidi ya hayo, kukamilisha kazi zilizobaki kwa ufanisi na kwa wakati.

Ushuru wa umeme ambao haukukusanywa shilingi 7,433,600,000

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 147 lililochapishwa tarehe 22 Aprili 2011, TANESCO ilitakiwa kupeleka kwa Wakala wa Umeme vijijini 3% ya makusanyo yake ya uuzaji wa umeme (LUKU) kila mwezi. Pia, itahitajika kulipa adhabu ya 5% kulingana na kifungu 6(1) cha Sheria ya Umeme Vijijini (Sura 321).

Hata hivyo, ilibainika kwamba Wakala wa Umeme Vijijini ilishindwa kukusanya adhabu ya ushuru wa umeme kiasi cha shilingi 7,433,600,000 kutoka TANESCO kama makusanyo ya mauzo ya umeme (LUKU) kila mwezi ambayo ilipaswa kulipwa tangu Mei 2011 licha ya jitihada mbalimbali ziizofanywa na menejimenti. Wizara ya Nishati na Madini iliingilia suala hilo hadi 30/06/2016 bila mafanikio.

Mapato yasiyokusanywa kutoka TANESCO ni kinyume na matakwa ya kifungu 19(3) ya cha sheria ya wakala wa umeme vijijini ya mwaka 2005 na Tangazo la Serikali Na. 147 la serikali liliyotolewa tarehe 22/04/2011. Hii iinasababisha uhaba wa fedha kwa Wakala wa Umeme Vijijini, hivyo kushindwa kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Napendekeza Menejimenti kufuatilia na kushauriana na Mlipaji Mkuu wa Serikali-Hazina kwa ajili ya utatuzi wa suala hili. Pia, mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato ya Wakala wa Umeme Vijijini uimarishwe ili kuepuka jambo hili kujitokeza tena katika siku zijazo.

Malipo zaidi yasiyorejeshwa shilingi 97,935,493.04 (Dola za Kimarekani 44,725.53)

Tathmini yangu ya mwaka 2015/2016 ya wadaiwa wa Wakala wa Nishati Vijijini imebaini kwamba, Wakala wa Nishati Vijijini ililipa kimakosa kiasi cha dola 91,168.48 kwa HIFAB badala ya Dola 9,218.48. Hivyo, kusababisha malipo ya zaidi ya dola 81,950. Mapitio ya Juni 2016 yanaonesha kwamba dola 37,224.47 zilirejeshwa, hivyo, kubaki salio la Dola 44,725.53 (Shilingi 97,935,493.04) ambazo hazijarejeshwa.

Napendekeza kwamba menejimenti iimarishe mfumo wa ndani kwa kufuata Kanuni 81 ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(iliyorekebishwa mwaka 2004); Pia ifuatilie kwa HIFAB kurejesha kasi cha ziada kilicholipwa cha shilingi 97.93 milioni (dola 44,725).

8.3.10 Ukaguzi wa Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi

Mali zisizofaa kwa matumizi na mali zinazotumika taratibu Shilingi 498,240,662

Zoezi la kuhesabu mali lililofanyika makao makuu ya Ofisi za GPSA na mikoani lilibaini mali zinazotumika taratibu za kiasi cha shilingi 498,240,662 kama zilivyooneshwa kwenye Jedwali hapo chini, ambapo, uwezekano wa mali hizo kuuzika ni mdogo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutokuendana na mahitaji ya kiteknolojia ya sasa.

Jedwali 55: Mali zisizofaa kwa matumizi na mali zinazotumika taratibu

Na.	Mkoa	Kiasi (Sh)
1	Arusha	56,893,409
2	Dodoma	16,515,200
3	Mara	30,419,019

Na.	Mkoa	Kiasi (Sh)
4	Morogoro	17,645,040
5	Tanga	38,778,237
6	Shinyanga	43,309,405
7	Mwanza	23,706,355
8	Tabora	38,402,015
9	Mtwara	91,205,807
10	Lindi	70,174,269
11	Dar-Es-Salaam	46,918,226
12	Singida	24,273,680
	Jumla	**498,240,662**

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Kutokuziondoa mali zisizofaa kwenye orodha ya mali kunafanya mali hizo zichukue nafasi ambayo ingeweza kutumika kuweka mali zingine zenye thamani.

Napendekeza kuwa Afisa Masuuli wahakikishe kwamba mali zisizofaa na zilizoharibika zinaondolewa kwenye hesabu ya mali.

Hasara kutokana na kucheleweshwa kupokea mzigo shilingi 56,016,276

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 nimebaini kwamba Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi ilinunua shajara 7,920 na kalenda 3000 zenye thamani ya shilingi 129,903,840 na 10,800,000 kutoka kwa M. I. Printing and Stationery Supplies Limited na Ms Malindi Printing mtawalia. Shajara na kalenda zilikuwa kwa ajili ya kuuza kwa Taasisi mbalimbali za Serikali. Katika kupitia upokeaji na usambazaji wake, nilibaini kwamba shajara zilipokelewa tarehe 13/01/2016 kupitia Hati ya mapokezi namba 1742 ya tarehe 11/01/2016 na kalenda zilipokelea tarehe 11/04/2016. Mwisho wa mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya shajara 3138 (40%) na kalenda 1263 (42%) kutoka ofisi za Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi za mikoa mbalimbali zilikuwa hazijauzwa.

Napendekeza Wakala kuhakikisha bidhaa zinafika na kusambazwa kwa wakati ili kuepuka upotevu wa mali za umma kwa nyakati zijazo. Kutokana na hayo, mikataba inatakiwa iandaliwe kwa namna ambayo wauzaji watawajibika

kwa hasara yoyote itakayotokana na ucheleweshaji wa bidhaa.

Uendeshaji wa Akaunti ya pamoja ya manununzi ya magari usioridhisha

Kanuni 130(a) na (b) ya Fedha za Umma inahitaji kuwapo kwa akaunti ya amana ambayo itaonesha taarifa za kila amana na kiasi kilichobaki.

Ukaguzi wa akaunti ya pamoja inayomilikiwa na GPSA ulibaini kwamba akaunti ya pamoja haiendeshwi vizuri. Katika ukaguzi wangu nilibaini mapungufu yafuatayo:

i. Miamala ya Akaunti ya Amana haikufanyika kwa kupitia mfumo wa Epicor ambao ni mfumo wa kuandaa hesabu kwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Taasisi 31(24%) kati ya 131 zilitumia zaidi ya amana zao kwa kiasi cha shilingi 17,825,033,951.07.

ii. Jumla ya salio la akaunti ya amana inayomilikiwa na GPSA kwa Taasisi zote ilikuwa ni shilingi 12,161,412,069.06. Wakati kiasi cha fedha kilichopo benki kilikuwa ni shilingi 24,351,093,634.89, hivyo kusababisha salio lisilosuluhishwa kuwa shilingi 12,189,681,566.

iii. Mamlaka ya mapato Tanzania iliweka amana ya shilingi 4,392,690,682.24 tangu tarehe 18/03/2015. Hata hivyo, mpaka tarehe ya kuandaa hesabu fedha hizo zilikuwa hazijatumika. Hii inamaana kwamba hakuna mwongozo wa wazi wa muda ambao fedha zinatakiwa kukaa kwenye akaunti mpaka gari litakapoletwa; hivyo kupelekea fedha kukaa bila kutumika ambapo zingeweza kutumika kwa shughuli zingine.

iv. GPSA ilishindwa kutumia fursa ya UNDP ambayo ingewawezesha kuokoa baadhi ya gharama, badala yake katika mwaka wa ukaguzi GPSA ilifanya manunuzi ya kiasi cha dola za kimarekani 29,684,707,278.23 kwa Wauzaji wa ndani.

Kuna uwezekano mkubwa wa kutokuhudumia wateja kutokana na baadhi ya wateja kutumia fedha zaidi ya walizonazo kwenye akaunti.

Napendekeza kwa Afisa Masuuli: (a) kuhakikisha mfumo wa kihasibu wa Epicor unatumika; akaunti za amana na salio la benki zinasuluhishwa; (b) mahitaji ya wateja yanafanyiwa kazi kwa wakati ili kupata thamani ya fedha; (c) GPSA inatakiwa kutumia fursa ili kuokoa fedha za umma.

Kutokuwa na bidhaa kwa muda mrefu

Kwa mujibu wa sheria ya uanzishaji wa Wakala wa Ugavi na huduma za Manunuzi (GPSA) ya mwaka 2007, GPSA inawajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora na za kutosha za manunuzi kwa Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali katika njia endelevu na gharama nafuu.

Katika ukaguzi wa ofisi za GPSA mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma imekuwa katika uhaba wa bidhaa kwa muda wa siku 121 mpaka 209 (miezi saba). Ilibainika kwamba Taasisi za manunuzi zililipia bidhaa ambazo hazikuwepo na walisubiri kuzikusanya kutoka ofisi za GPSA kwa kipindi cha kuanzia siku 24 mpaka miezi mitatu. Jedwali hapo chini linaonesha haya:

Jedwali 50: Kipindi ambacho hakukuwa na bidhaa

Mahali	Idadi	Muda ambao hakukuwa na bidhaa (siku)
Iringa	6	113 mpaka 196
Njombe	3	68 mpaka 208
Ruvuma	5	82 mpaka 441

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa menjimenti 2015/2016

Kutokuwa na bidhaa kwa muda mrefu kitazifanya taasisi zinazofanya manunuzi kushindwa kutegemea Wakala wa Ugavi na huduma za Manunuzi katika kufanya manunuzi. Lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora na za kutosheleza za manunuzi kwa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali linaweza lisifikiwe

Napendekea menejimenti kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa wa kutosheleza na kwa wakati.

8.3.11 Ukaguzi wa Shirikisho la serikali za mitaa

Ubadhirifu wa mfuko wa uwekezaji shilingi 523,929,646.06

Mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika mkoani Singida tarehe 28 na 29 Agusti 2009 ulipitisha azimio kuhusu ujenzi wa uwekezaji katika jengo la Dodoma; ambapo sera ya uwekezaji ya mwaka 2009 iliwasilishwa kwa kuidhinishwa. Wanachama walielekezwa kuchangia jumla ya Shilingi 6,500,000,000 kwa kipindi cha miaka mitatu (2009/2010 mpaka 2011/2012) kwa ajili ya uwekezaji. Mpaka kufikia tarehe 29/01/2016, jumla ya shilingi 525,717,522 ilikusanywa kutoka kwa wanachama mbalimbali.

Ilibainika kwamba Shirikisho la Serikali za Mitaa lilitumia jumla ya shilingi 523,929,676.06 kati ya tarehe 16/06/2012 na 22/03/2013 bila mamlaka ya mkutano mkuu wa mwaka au Kamati Tendaji. Jumla ya shilingi 76,000,400 zilitumika kwa shughuli za kila siku. Shilingi 80,000,000 iliwekwa katika akaunti ya muda maalumu katika benki ya ABC kwa mwaka mmoja kuanzia 29/01/2016 kwa riba ya asilimia 12 kwa mwaka; shilingi 367,929,276.06 hazikuwa na viambatisho vya matumizi yake. Kiasi kilichobaki katika akaunti tarehe 11/03/2016 kilikuwa shilingi 1,787,845.94. Matumizi ya fedha kinyume na malengo yaliyokusudiwa yanaashiria kutokuwa na nidhamu ya kifedha; na inaweza kusababisha ufujaji wa fedha za umma.

Napendekeza menejimenti ya Shirikisho la Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba fedha za uwekezaji zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa; au vinginevyo, mkutano Mkuu wa mwaka au Kamati Tendaji inatakiwa kuidhinisha matumizi hayo. Aidha, menejimenti inahitajika kuhakikisha kwamba nyaraka za matumizi zinahifadhiwa na zinapatikana mara zinapohitajika. Mamlaka zinazohusika na uchunguzi zinatakiwa kufuatilia kuwapo kwa fedha za uwekezaji.

8.3.12 Ukaguzi wa Wakala za Mbegu za Miti Tanzania

Madeni yasiyokuwa na viambatisho vya kutosha shilingi 32,669, 387

Wakala wa Mbegu za Miti aliripoti madeni kiasi cha shilingi 181,612,860.32. Kiasi cha madeni kimejumuisha madai mbalimbali kwa ajili ya vifaa na huduma, madai ya wafanyakazi, huduma za chakula, kodi ya pango la ofisi, marekebisho na huduma nyingine. Katika kupitia madai na Ankara, nimebaini kwamba viambatisho vya madeni ya shilingi 32,669,387 vilikosekana.

Kutokana na kukosekana kwa nyaraka, sikuweza kuthibitisha madeni na matumizi yanayohusiana na madeni hayo; hivyo, kuna uwezekano madeni yakawa yameongezeka kwa kiasi cha shilingi 32,669,387.

Napendekeza Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania kutafuta na kuwasilisha viambatisho vya madeni, vinginevyo madeni hayo yatachukuliwa kama madeni batili.

8.3.13 Ukaguzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Vitambulisho vya Taifa havikutolewa

Katika mwaka wa ukaguzi wa mwaka 015/2016 nimebaini kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilikusanya taarifa za watu 3,614,168 kwa ajili ya kutengeneza vitambulisho. Kati ya taarifa zilizokusanywa, vitambulisho 2,655,086(73%) vilitengenezwa; kati ya vitambulisho 2,655,086 vilivyotengenezwa, vitambulisho 1,047,217 vyenye thamani ya shilingi 29,513,905,368 havikusambazwa kwa wahusika.

Napendekeza Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa kupitia na kuja na mikakati itakayohakikisha vitambulisho vyote vinavyotengenezwa vinagawiwa kwa wahusika kwa wakati.

8.3.14 Ukaguzi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara 2014/2015

Ushuru wa mafuta lita 451,203 hayakuthibitishwa kufika eneo la mgodi shilingi 127,695,589

Tangazo la Serikali Na. 190 na 191 la mwaka 2011 na jedwali la tatu la sheria ya kodi ya ongezeko la thamani ya mwaka 1997 limetoa msamaha wa malipo ya ushuru wa bidhaa, ushuru wa mafuta, na kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta yanayoingia kwa lengo la kutumika katika migodi kwa ajili ya uchimbaji wa madini. Katika ukaguzi, nilibaini jumla ya magari 49 yaliyobeba lita 451,203 yenye jumla ya ushuru wa shilingi 127,695,589 yaliyotumwa kutoka bandari ya Dar es Salaam kati ya Oktoba 2014 na Disemba, 2015 (kulingana na nyaraka zilizopo); lakini haikuweza kuthibitika kama mafuta hayo yalifika katika migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu.

Napendekeza menejimenti ya bodi ya barabara kufuatilia Mamlaka ya mapato Tanzania ili kujua iwapo mafuta hayo yalifika katika migodi na yalitumika kwa matumizi yaliyokusudiwa; vinginevyo, yaweze kuchajiwa ushuru wa shilingi 127,695,589.

Ushuru wa lita 4,916,085 za mafuta yaliyoingizwa na walengwa wasiostahili shilingi 1,292,930,355

Tathmini ya TANSADs (IM4) ya misamaha ya mafuta yanayopelekwa migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu kwa kipindi cha Julai 2014 mpaka Disemba 2014 imeonesha lita 4,916,085 za mafuta zenye ushuru wa mafuta wa kiasi cha shilingi 1,292,930,355 yalibainika kwenda kwa M/S Oryx Ltd badala ya Migodini. Hii ni kinyume na matakwa ya Tangazo la Serikali linalotoa msamaha wa ushuru wa mafuta na kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta yanayoingia kwa ajili ya kutumika kwenye migodi kwa ajili ya uchimbaji wa madini. Pia, msamaha uliotolewa kwa wanufaika unatakiwa kutumika kwa wanufaika tu na hauruhusiwi kuhamishiwa kwa mtu mwingine.

Napendekeza menejimenti ya Bodi ya Barabara kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuchunguza ili kuthibitisha iwapo mafuta hayo yalienda kutumika migodini kwa kusudi lililokusudiwa; vinginevyo, ushuru wa shilingi 1,292,930,355 uweze kutozwa.

Ushuru wa mafuta yaliyotumiwa na mkandarasi mdogo(subcontractor) shilingi 5,704,566,686

Sehemu ya 2(g) ya jedwali la Tangazo la Serikali namba 190 na 191 la mwaka 2011 inasema kwamba tofauti yoyote inyosababishwa na kutokupokea mafuta yaliyotoka katika makampuni ya masoko ya mafuta, ukaguzi, matumizi ya mafuta kwa mtu mwingine zaidi ya makampuni ya migodi au matumizi yoyote yasiyokusudiwa yanatakiwa kutozwa kodi itakayokatwa kutoka kwenye akaunti ya escrow.

Tathimini ya ripoti ya matumizi ya mafuta ya mgodi wa Buzwagi ilibaini kwamba lita 20,791,072 za mafuta zilitolewa kwa mkandarasi mdogo, M/S Aggreko Company Ltd kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia Julai 2014 mpaka Disemba 2015. Uchunguzi zaidi ulibaini kwamba hakukuwa na stakabadhi ya tozo ya mafuta ya shilingi 5,704,566,686 kinyume na matakwa ya Tangazo la Serikali.

Napendekeza menejimenti ya Bodi ya Barabara kushirikiana na menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhakikisha kwamba Sheria kuhusiana na mafuta yanayotumiwa na wakandarasi wadogo katika migodi zinafuatwa. Zaidi ya hayo, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhakikisha makusanyo ya ushuru wa mafuta kiasi cha shilingi 5,704,566,686 yanakusanywa kutoka kwa Wakandarasi wadogo wanaotumia mafuta.

Ushuru wa mafuta lita 1,052,121.15 kwenye salio la mafuta (closing stock) shilingi 329,313,919.95 hazikuoneshwa

Ukaguzi wa ripoti za mafuta katika migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi na Geita kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia tarehe 01/07/2014 mpaka 31/12/2015. Mapitio ya salio la tarehe 31/12/2015 yamebaini kiasi cha lita 1,052,121.15 za mafuta hazikuoneshwa. Salio ambalo halikuoneshwa limesababisha ushuru wa mafuta wa kiasi cha shilingi 329,313,919.95.

Napendekeza menejimenti ya Bodi ya Barabara kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhakikisha kunakuwa na

mikakati ya kutosha ya kukusanya ushuru wa mafuta kwenye salio la mafuta ambao haujaoneshwa.

Ushuru wa mafuta lita 3,302,058 yaliyosafirishwa kutoka bandari ya Dar es Salaam hayakupokelewa mpaka wa Sirari shilingi 904,289,504

Ulifanyika ukaguzi wa mafuta yaliyopakiwa bandari ya Dar es Salaam kwa kipindi cha kuanzia 01/07/2014 mpaka 31/12/2015 kupelekwa Mgodi wa North Mara kupitia mpaka wa Sirari uliofanyika katika kitengo cha uangalizi wa mafuta kilichopo chini ya ofisi za forodha makao makuu Dar es Salaam. Wakati wa kupitia nyaraka zinazohifadhiwa na TRA kwenye mpaka wa Sirari, nimebaini kwamba magari ya mafuta 107 yenye jumla ya lita 3,302,058 za mafuta hayakufika mpaka wa Sirari. Hii inasababisha tubaini ushuru wa mafuta kiasi cha shilingi 904,289,504 kisicholipwa.

Napendekeza Menejimenti ya Bodi ya Barabara kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuhakikisha kunakuwa na mikakati ya kutosha ya kufuatilia mafuta yanapotoka na yanapokwenda. Pia, kutoza ushuru wa mafuta kwa mafuta yote ambayo hayafiki kwenye migodi husika na kutumika katika matumizi yaliyokusudiwa.

Mapungufu yaliyojitokeza katika uondoshaji wa mafuta lita 3,500,000 ya migodini kwa kutumia maghala yanayohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi.

Kifungu 74-75 cha Kanuni ya Ushuru wa Forodha Afrika Mashariki ya mwaka 2010 inahitaji mlipa kodi kupata leseni na kutimiza masharti yote yaliyoainishwa katika kifungu 74(1-4) na 75(1-2) ili kuweza kuendesha ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi. Zaidi ya hayo, kifungu 76 kinahitaji mmiliki leseni wa ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi kutekeleza dhamana kwa bidhaa zinazohifadhiwa katika ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi.

Ukaguzi wa mafuta kwa ajili ya migodi kupitia mpaka wa Sirari ulibaini kwamba lita 3,500,000 za mafuta ya petroli

yaliyonunuliwa na kampuni ya mafuta ya Oryx na kuondoshwa kupitia TANSAD yenye kumbukumbu namba TZSR-14-1171746 ya tarehe 10/12/2014. Uondoshaji ulifanywa chini ya usimamizi wa ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi hata hivyo mapungufu yafuatayo yalibainika:

a) Hakukuwa na ushahidi kwamba M/S Oryx Oil Company Limited ilikuwa na leseni ya kuendesha ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi;

b) Mizigo iliyookolewa chini ya usimamizi wa ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi bila kutekeleza dhamana kinyume na kifungu 76 cha Kanuni ya ushuru wa forodha Afrika Mashariki ya mwaka 2010;

c) Hakukuwa na ushahidi kwamba lita 49,046 za mafuta ya petrol yenye jumla ya kodi na ushuru wa kiasi cha shilingi 32,213,412.80 pamoja na shilingi 12,899,098 ilihamishwa kwenda kampuni ya migodi (North Mara) na kampuni ya mafuta ya Oryx; na

d) Ilibainika kwamba Oryx ilijulikana kama muingizaji wa mafuta; na siyo North Mara ambaye alifuzu kupata msamaha wa kodi.

Napendekeza kwamba, menejimenti ya Bodi ya Barabara kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kupata ushahidi wa leseni ya uendeshaji wa ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi iliyotolea kwa kampuni ya mafuta ya Oryx. Kurejesha kodi na ushuru wa kiasi cha shilingi 32,213,412.80 kinachojumuisha ushuru wa mafuta wa kiasi cha shilingi 12,899,098 cha mafuta yaliyopelekwa kampuni ya migodi (mgodi wa North Mara). Zaidi ya hayo, uondoshaji wa mizigo iliyo chini ya ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi inafanywa na kampuni zenye leseni tu na dhamana inatolewa kabla ya mzigo haijaondoshwa kwa mwenye ghala kama inavyohitajika na sheria ya ushuru wa forodha Afrika Mashariki.

8.3.15 Ukaguzi wa Bodi ya mikopo kwa Serikali za Mitaa

Matumizi yasiyo ya lazima yaliyotumika katika kufanya marekebisho ya bodi shilingi 438,143,514

Katika mwaka wa ukaguzi nilibaini kwamba Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilitumia shilingi 438,143,514 kwa ajili ya marekebisho ya Bodi kwa kipindi cha 2011/2012 mpaka 205/2016 ambayo iliidhinishwa kwenye kikao cha menejimenti kilichofanyika tarehe 29/02/2012 Dodoma. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba jumla ya shilingi 438,143,514 zilikuwa zimeshatumika wakati wa mchakato wa marekebisho ya Bodi ambao uliahirishwa na menejimenti na kikosi kazi kipya kiliundwa ili kuweza kuja na mkakati mpya ambao utaboresha utendaji/ ufanisi wa Bodi. Kutokana na maelezo ya hapo juu, matumizi ya kiasi cha shilingi 438,143,514 hayakuweza kuthibitika hivyo kuchukuliwa kama matumizi yasiyo na tija.

Menejimenti inatakiwa kuhakikisha kwamba, inafanya uchambuzi wa faida na hasara ambao utakuwa msingi wa kuidhinisha au kutokuidhinisha marekebisho yoyote. Bodi itawajibika kwa hasara yoyote ambayo ingeweza kuepukika.

8.3.16 Ukaguzi wa Shirika la Uzalishaji Mali

Mkataba usiotekelezwa Shilingi 119,900,000,000

Ukaguzi wa mwaka huu wa fedha ulibaini kuwa SUMA JKT (kwa niaba ya Matrekta ya kilimo) iliingia mkataba tarehe 22/10/2015 na kampuni ya Ursus S.A kutoka Polandi kwa ajili ya ununuzi wa matrekta, vifaa maalumu vya matrekta, vipuri na huduma nyinginezo.

Manunuzi hayo yalifanyika kupitia mkopo kutoka Serikali ya Polandi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi cha dola za Kimarekani 55,000,000 bila kodi ya ongezeko

la thamani (sawa na shilingi 119,900,000,000 kwa bei ya kubadilisha USD/shilingi 2180).

Ukaguzi wa nyaraka mbalimbali ulibaini kuwa mkandarasi (Ursus S.A) hakukamilisha kazi yake kama alivyotakiwa. Hivyo, hadi Januari 2016 mkataba haukutekelezwa ili kukamilisha malengo yaliyokusudiwa.

Malengo yaliyokusudiwa hayakutekelezwa hivyo kurudisha nyuma malengo ya kuendeleza kilimo kwa kuweka mazingira ya kisasa. Kushindwa kutekeleza mkataba ni kiashiria kwamba upembuzi yakinifu haukufanyika.

Ninashauri SUMA JKT ifuatilie kwa Mkandarasi na kuhakikisha kuwa mkataba unatekelezwa bila kuchelewa zaidi.

Uwekezaji usio na tija katika TANZANSINO

Wakati wa Ukaguzi wa 2015/16, tumebaini kuwa shilingi 773,000,875.99 zililipwa na SUMA Makao makuu ikiwa ni sehemu ya malipo ya shilingi 1,292,003,500 kwa ajili ya kununua Hisa za Holley katika uwekezaji usio na tija wa utengenezaji wa madawa, pamoja na mambo yahayohusiana na madawa. SUMA JKT iliingia makubalianao ya ubia wa pamoja na Kiwanda cha Holley na baadaye kununua kiwanda kutoka kwa Shanxi Provincial Technical Renovation and Equipment Corporation. Ubia huo uliitwa TANZANSINO ambapo mwaka 2007 umiliki wa hisa ulikuwa 55% kwa Holley na 45% kwa SUMA.

Kwa bahati, mbaya Biashara katika TANZANSINO ilihitimishwa kwa hiari mwaka 2014.

Nimebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa ubia huo wa TANZANSINO mwaka 2007 mpaka muda wa kuhitimisha biashara mwaka 2014, hakuna mapato yoyote yaliyopokelewa kulingana na umiliki wa hisa uliokubaliwa. Hivyo haikuwa busara kwa Suma kununua uwekezaji mfu.

SUMA JKT ilichukua umiliki mzima katika TANZANSINO bila kuangalia mahitaji ya lazima kama vile uchambuzi yakinifu, utaalamu wa kiufundi, wafanyakazi, mchanganuo wa marejeo ya gharama/faida, na uzoefu waliojifunza kutoka kwa mbia aliyejiondoa.

Mali ambazo hazikuthibitishwa Shilingi 2,657,611,230

Shirika la Uzalishaji Mali (SUMA) -JKT kitengo cha Ujenzi lilikuwa na mali kiasi cha shilingi 2,657,611,230 ambazo kuwepo kwake hakukuthibitishwa kwa sababu uongozi ulishindwa kuhesabu mali kinyume na Kanuni 237(1) na (2) ya Kanuni za Fedha za 2001.

Kushindwa kuhesabu mali ni ishara kuwa uwepo, thamani na hali ya mali hizo havikuweza kuthibitika.

Nilishauri uongozi wa SUMA - JKT kuhakikisha Kanuni ya 237(1) na (2) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 inazingatiwa kwa kuhakikisha zoezi la kuhesabu mali linafanyika kila mwisho wa mwaka ili kuweza kuthibitisha thamani ya mali hizo kwenye taarifa za Fedha.

Malimbikizo ya deni la kodi shilingi 2,679,429,505

Ukaguzi wangu wa kampuni ya ulinzi ya SUMA katika kipindi cha mwaka wa Fedha ulioishia 30/06/2016 ulibaini malimbikizo ya deni la kodi kiasi cha shilingi 2,679,429,505 ambalo halijalipwa tangu 30/11/2011.

Nilibaini kuwa kati ya deni hili, kiasi cha shilingi 1,283,547,210 (48%) kilitokana na riba na tozo kwa kushindwa kulipa. Kiasi hiki kingeweza kuepukika kama Taasisi hii ingelipa kodi ndani ya muda. Mchanganuo wa deni hili ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini:

Na.	Maelezo	Kiasi (Shilingi)
1	Ushuru wa maendeleo ya	515,638,476

Na.	Maelezo	Kiasi (Shilingi)
	ujuzi	
2	Kodi ya kampuni	876,363,819
3	Ada kwa ajili ya magari	3,880,000
4	Riba na tozo kwa kutokulipa kodi	1,283,547,210
	Jumla	**2,679,429,505**

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka 2015/2016

Ni maoni yangu kwamba, kulimbikiza deni la kodi ni mzigo kwa Taasisi na pia hasara kwa Serikali. Napendekeza Taasisi kulipa kodi kwa wakati ili kuepuka riba ambayo ni hasara.

Mikopo isiyorejeshwa Shilingi 4,820,368,000

Ukaguzi wangu wa SUMA kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulibaini kuwa kitengo cha Matrekta ya Kilimo kilitoa mikopo kiasi cha shilingi 5,355,153,000 kwa vitengo mbalimbali vya SUMA. Kati ya kiasi hicho, shilingi 534,785,000 zilirejeshwa, bado shilingi 4,820,368,000 ambavyo hazijarejeshwa kwa muda wa miaka minne. Maelezo ya kuridhisha hayakutolewa kwa nini fedha hizo hazijarejeshwa. Orodha ya walipwaji ni kama ifuatavyo:

Jedwali 56: Orodha ya mikopo iliyotolewa isiyorejeshwa

Mkopaji	Mwaka	Dhumuni	Kiasi kilichokopwa(shilingi)	Kiasi kilicholipwa (shilingi)	Kiasi ambacho hakijalipwa (shilingi)
SUMA Makao Makuu	2013	Mchango kwenye mradi wa kokoto	1,600,000,000	0	1,600,000,000
	2015	Kugharama mbalimbali za makao makuu	572,036,000	0	572,036,000
		Kugharama mbalimbali za makao makuu	52,036,000	0	52,036,000
		Kugharama mbalimbali za makao makuu	35,000,000	0	35,000,000
		Kugharama mbalimbali za makao makuu	50,000,000	0	50,000,000
		Kugharamia maonesho ya sabasaba	19,988,000	0	19,988,000
		Kugharama mbalimbali za makao makuu	1,000,000	0	1,000,000
		Kugharama mbalimbali za makao makuu	2,000,000	0	2,000,000
		Kugharamia kuomba zabuni	30,000,000	25,710,000	4,290,000
	2016	Manunuzi ya ardhi	230,598,000	0	230,598,000
		Ununuzi wa samani	11,128,000	0	11,128,000
		Kulipia deni la TANESCO	200,000,000	0	200,000,000
Mkuu wa JKT	2014	Kugharamia gharama za usafiri	1,000,000,000	449,075,000	550,925,000
SUMA Makao Makuu	2015	Kugharamia kuomba zabuni	660,000,000	0	660,000,000
		Kugharamia kuomba zabuni	50,000,000	40,000,000	10,000,000
		Utengenezaji wa vifaa	4,000,000	0	4,000,000
SUMA Kanda ya Kaskazini	2014	Utengenezaji wa ofisi ya Waziri Mkuu	20,000,000	0	20,000,000
		Jengo	40,000,000	20,000,000	20,000,000
URSUS S.A	2015	Gharama za uondoshaji wa matrekta	22,682,000	0	22,682,000
		Gharama za kukuza biashara na matangazo na gharama za mkataba	54,470,000	0	54,470,000
SUMA JKT ANTI-ASFALT	2015	Fidia ya ardhi	71,015,000	0	71,015,000
		Gharama za mishahara	32,200,000	0	32,200,000
Chita	2012	Kugharamia uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa umwagiliaji	287,000,000	0	287,000,000
Misenyi	2012	Gharama za kutunza mifugo	280,000,000	0	280,000,000
Mlale	2012	Kugharamia mradi wa mbegu	30,000,000	0	30,000,000
		Jumla	5,355,153,000	534,785,000	4,820,368,000

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka 2015/2016

Pamoja na kushindwa kurejeshwa kwa mikopo hiyo, SUMA kitengo cha Matrekta ya Kilimo haijaweka mikakati ya namna bora ya kushughulikia dosari hii. Nashauri uongozi wa SUMA kitengo cha matrekta ya kilimo uhakikishe kuwa fedha hizo zinarejeshwa.

8.3.17 Ukaguzi wa Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania

Kukosekana kwa kumbukumbu za wafanyakazi

Wakala wa ukaguzi wa uchimbaji madini Tanzania iliajiri wafanyakazi 103 wa kufanya kazi ya mkataba wa muda mfupi kama Wakaguzi Wasaidizi wa Madini kwenye vituo vya ukaguzi vilivyopo sehemu mbalimbali nchini na kulipwa mshahara wa jumla ya shilingi 769,318,179. Wakati wa kupitia taratibu za kuajiri, nilibaini kwamba hakukuwa na miongozo rasmi ya kuajiri na miundo ya mishahara iliyoidhinishwa. Hata hivyo menejimenti ya wakala wa ukaguzi wa uchimbaji madini Tanzania haikufanya uchunguzi wowote kuthibitisha utendaji na uwepo wa wafanyakazi hao katika vituo vyao vya kazi.

Kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za wafanyakazi, baadhi ya wafanyakazi wa muda wanaweza wasiwepo katika vituo vya kazi; bila menejimenti kujua na hivyo, kusababisha upotevu wa fedha za umma. Hivyo, nimeshindwa kuthibitisha taratibu za ajira ya muda mfupi na gharama zilizoingiwa.

Napendekeza menejimenti kuimarisha udhibiti wa usimamizi rasilimali watu kwa kutumia miongozo ya kuajiri ya utumishi wa umma. Pia, kufanya ukaguzi wa wafanyakazi na kuweka kumbukumbu sahihi za wafanyakazi wote.

8.3.18 Matokeo ya ukaguzi wa taasisi nyingine za Serikali

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi katika Taasisi nyingine 30 za serikali kwa mwaka wa Fedha 2015/2016. Matokeo haya yanaashiria kuwapo kwa dosari mbalimbali katika kuzingatia sheria zilizopo. Dosari hizi zinaonesha kukosekana kwa jitahada thabiti za kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

Madai yasiyokusanywa Shilingi 77,382,529,105.54

Ukaguzi wangu wa mwaka 2015/2016 ulibaini kuwa taasisi 17 za Serikali zilikuwa na madai yasiyokusanywa kiasi cha shilingi 77,602,467,926. Kati ya madai, hayo kiasi cha shilingi 62,811,954,035.30 (81%) kilikuwa hakijakusanywa kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12; wakati kiasi cha shilingi 14,790,513,890.24 (19%) kilikuwa hakijakusanywa ndani ya miezi 12.

Kiasi hiki kikubwa cha madai yasiyokusanywa kinapunguza ukuaji na uwezo wa taasisi kujiendesha.

Orodha ya taasisi zenye madai yasiyokusanywa ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali la hapo chini:

Jedwali 57: Taasisi zenye madai yasiyokusanywa

Na.	Taasisi	Ndani ya miezi 12	Zaidi ya miezi 12
		Kiasi (shilingi)	Kiasi (shilingi)
1	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania(MKURABITA)	0	32,279,235
2	Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto	90,658,869.26	39,182,748.14
3	Shule ya Sheria Tanzania	43,732,680.98	98,655,733.46
4	Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori	24,788,000.00	17,470,000.00
5	Chuo cha Mafunzo serikali za Mitaa Hombolo	151,617,820.00	68,321,000.00
6	Kituo cha Teknolojia ya Uundaji wa Magari Tanzania	93,077,000	203,825,390
7	Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru	241,610,061	0
8	Taasisi ya Kuthibitisha Mbegu Tanzania	213,150,881.00	351,540,257.70
9	Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela	563,498,100	7,822,015,358
10	Shirika la Uzalishaji Magereza	5,261,803,409	4,139,123,517
11	Kampuni ya Utinzi ya SUMA	4,006,295,232	50,630,000
12	Taasisi ya utafiti wa Mifugo Tanzania	5,100,000	0
13	Shirika la Uzalishaji Mali pekee JKT 2014/2015	0	1,066,054,000
14	Bodi ya Usimamizi wa Taasisi zisizo za Serikali	2,200,000	279,480,000
15	Taasisi ya Maji	84,541,500	23,560,796
16	Taasisi ya Uhasibu Tanzania	1,983,190,337	0
17	SUMA Matrekta ya Kilimo	2,025,250,000	47,198,079,000
18	SUMA JKT-Idara ya Kilimo na Viwanda		1,421,737,000
	Jumla	**14,790,513,890.24**	**62,811,954,035.30**

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka 2015/2016

Ni maoni yangu kwamba kulimbikiza deni la kodi ni mzigo kwa taasisi; pia ni hasara kwa serikali. Napendekeza taasisi kulipa kodi kwa wakati ili kuepuka riba ambayo ni hasara.

Madeni yasiyokuwa na viambatisho Shilingi 189,904,160.65

Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori ya Pasiansi iliripoti madeni ya shilingi 189,904,160.65; hata hivyo, viambatisho vya kutosha kuthibitisha madeni hayo havikuwasilishwa vilipohitajika kwa ajili ya ukaguzi. Kukosekana kwa viambatisho vya kutosha kunaashiria kuwa madeni hayo hayapo. Halikadhalika, kulizuia mawanda ya ukaguzi wangu.

Ninashauri kuwa Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori ya Pasiansi iimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani na kuwasilisha viambatisho vilivyokosekana kwa ajili ya uhakiki; vinginevyo, madeni hayo yaondolewe kwenye vitabu.

Mkopo usiorejeshwa Shilingi 280,136,218

Katika ukaguzi wa Shirika la Uzalishaji mali la Magereza (Prison Corporation Sole), nilibaini kuwa shirika lililipa mkopo wa shilingi 280,136,218 kwa Kamishna wa Magereza Makao Makuu kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kawaida za ofisi. Fedha hizi zililipwa kwa kipindi kati ya tarehe 8/7/2015 hadi 20/06/2016. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hadi kufikia Januari 2017, fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa.

Ilibainika kuwa hakuna sera au muongozo wa namna ya kukopa au kurejesha fedha hizo; vilevile, hakukuwa na maelezo na sababu za malipo hayo kutokurejeshwa.

Kutokurejesha mkopo huo kunaashiria kuwa shirika linaweza kushindwa kujiendesha na kutekeleza majukumu yake.

Nilishauri kuwa uongozi wa Shirika la Uzalishaji la Magereza uongeze juhudi za kuhakikisha kuwa fedha hizo zinarejeshwa ili kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Madeni yasiyolipwa Shilingi 14,933,537,786.54

Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016 nilibaini kuwa Taasisi 15 zilikuwa na madeni ya Shilingi 14,933,537,786.54. Kati ya madeni hayo, madeni ya shilingi 10,614,191,293.06 (71%) yalikuwa hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12, na shilingi

4,319,346,493.48 (29%) ndani ya miezi 12. Ninatoa rai kuwa madeni haya yanaweza kutia doa sifa nzuri ya Taasisi hizi kwa Wazabuni.

Orodha ya taasisi ambazo zina madeni yasiyolipwa ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali 58: Madeni yasiyolipwa

Na.	Taasisi	Kiasi ndani ya miezi 12	Kiasi zaidi ya miezi 12
		Kiasi (shilingi)	Kiasi (shilingi)
1	Shule ya Sheria Tanzania	225,259,580.93	358,824,741.17
2	Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi	43,774,524.61	146,129,636.04
3	Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika	65,490,097.71	90,015,539.30
4	Chuo cha Mafunzo serikali za Mitaa Hombolo	374,033,937.52	1,000,589,641.40
5	Kituo cha Teknolojia ya Uundaji wa Magari Tanzania	111,548,992.30	145,204,000.00
6	Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru	110,467,555.00	263,000.00
7	Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela	254,882,108.00	1,465,353,138.00
8	Shirika la Uzalishaji Magereza	484,192,118.04	1,989,562,632.15
9	Kampuni ya Ulinzi ya SUMA	192,013,000.00	120,387,000.00
10	Taasisi ya utafiti wa Mifugo Tanzania	836,600,918.00	-
11	Shirika la Uzalishaji Mali pekee JKT 2014/2015	-	1,942,571,000.00
12	Taasisi ya rasilimali Madini	733,256,614.76	359,413,929.00
13	Taasisi ya Maji	107,287,925.00	438,996,036.00
14	Taasisi ya Uhasibu Tanzania	780,539,121.61	-
15	SUMA JKT-Idara ya Kilimo na Viwanda	-	2,556,881,000.00
	Jumla	4,319,346,493.48	10,614,191,293.06

Nashauri kuwa Maafisa Masuuli watengeneze bajeti inayokidhi kulipa mahitaji kwa wakati.

Dosari kwenye matumizi ya fedha

Katika mwaka wa ukaguzi, nilibaini dosari sita kwenye matumizi ya fedha; hivyo, sikuweza kuthibitisha usahihi na utaratibu wa matumizi hayo. Dosari hizo ni hizi zifuatazo: Matumizi yenye nyaraka pungufu (shilingi 206,521,652),

Kukosekana kwa stakabadhi za mashine za kielekitroniki (EFD) (shilingi 1,481,679,250) Kutokukata kodi zuio (shilingi Shilingi 69,443,677), malipo yaliyofanyika bila kukata kodi zuio (shilingi 36,589,303). Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti (shilingi 107,307,565.14), Masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu (shilingi 10,575,687.30) Malipo yaliyofanyika kwenye vifungu visivyostahili (shilingi 304,116,358.50).

Orodha ya Taasisi pamoja na dosari hizo ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali la hapo chini:

Jedwali 59: Dosari kwenye matumizi ya fedha

Kigezo	Matokeo ya ukaguzi	Taasisi	Kiasi (shilingi)
Kanuni ya 24 ya Sheria ya Kodi ya mapato (Stakabadhi za mashine za kielektroniki) ya 2012	Kushindwa kuwa na stakabadhi za mashine za kielektroniki	Taasisi ya Kuthibitisha Mbegu Tanzania	11,944,710.00
		Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi	355,830,350.03
		Taasisi ya rasilimali Madini	28,661,150.00
		Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania(MKURABITA)	24,054,288.24
		Shirika la Uzalishaji Mali JKT	65,874,820.00
		Kituo cha Teknolojia ya Uundaji wa Magari	67,127,631.00
		Shirika la Uzalishaji Magereza	372,066,550
		Taasisi ya Maji	307,095,714
		Taasisi ya Uongozi	38,184,400
		SUMA Matrekta ya Kilimo	21,614,000
		SUMA JKT-Idara ya Kilimo na Viwanda	108,097,040
		Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa	81,128,597
		Jumla	1,481,679,250
Kanuni ya 46 (3) ya Kanuni za Fedha za 2001, iliyorekebishwa 2004.	Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa	Taasisi ya Kuthibitisha Mbegu Tanzania	107,307,565.14
		Jumla	107,307,565.14
Kifungu cha 83 cha sheria ya Kodi ya mapato ya 2008	Malipo bila kukata kodi zuio	Taasisi ya Kuthibitisha Mbegu Tanzania	2,547,301.20
		Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania	8,511,041.47
		Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania(MKURABITA)	25,530,960
		Jumla	36,589,303
	Kodi zuio ambayo haikukatwa	Kituo cha Teknolojia ya Uundaji wa Magari	4,662,852
		Taasisi ya Maji	13,165,432
		Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam	42,825,005
		Taasisi ya Uongozi	402,432
		Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa	8,387,956
		Jumla	69,443,677
Kanuni 95(4) ya kanuni za fedha	Malipo yasiyo na viambatisho	Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi	19,108,400
		Medical Radiology and Imaging Professional Council	2,760,000
		Taasisi ya Uongozi	9,200,000
		SUMA Matrekta ya Kilimo	37,117,012
		Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania	15,428,642
		Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa	122,907,598
		Jumla	206,521,652
Kanuni 103 (5) ya Kanuni za Fedha 2001 zilizorekebishwa 2004.	Masurufu yasiyorejeshwa	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania(MKURABITA)	5,900,367.30
		Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa	4,675,320.00
		Jumla	10,575,687.30
Kifungu cha 9 cha Sheria namba 24 ya Taasisi zisizo za Serikali za 2002 zilizorekebishwa 2005	Malipo yaliyofanyika kwenye vifungu ambavyo sio sahihi.	Bodi ya Usimamizi wa Taasisi zisizo za Serikali	304,116,358.50
		Jumla	304,116,358.50

Chanzo: Taarifa za ukaguzi kwa menejimenti

Kuhusu malipo yenye nyaraka pungufu, nashauri uongozi wa taasisi za serikali kuzingatia matakwa ya vifungu 86(1) na 95(4) vya Kanuni za Fedha za 2001 kwa kuweka mifumo ya udhibiti ili kuhakikisha kuwa nyaraka husika zinatunzwa ipasavyo.

Kuhusu malipo yasiyo na stakabadhi za mashine za kielektroniki, nashauri serikali kutoa muongozo na kusisitiza kuzingatia kwamba Wazabuni wanaopewa Zabuni ni wale wanaotoa stakabadhi za kielektroniki.

Kuhusu malipo yaliyofanyika bila kukata kodi ya zuio, natoa wito kwa Maafisa Masuuli husika kuhakikisha kuwa Sheria ya kodi inazingatiwa.

Kuhusu masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu naishauri Taasisi husika zizingatie Kanuni za Fedha kwa kurejesha masurufu baada ya kukamilika kwa kazi zilizokusudiwa.

Kuhusu masurufu yasiyorejeshwa, nashauri Taasisi husika zizingatie Kanuni za Fedha kwa kurejesha masurufu baada ya kazi zilizokusudiwa kumalizika.

Nilishauri uongozi wa Taasisi husika kuhakikisha kuwa matumizi yanayofanyika yanazingatia bajeti au yapate kibali kutoka mamlaka husika.

Nilishauri Bodi ya kuratibu taasisi zisizo za Kiserikali kuzingatia kifungu cha 9(3) na (4) cha sheria namba 24 ya Taasisi zisizo za kiserikali ya 2002 iliyorekebishwa 2005 kuwa makisio ya mwaka yanafanyika na malipo yote yanayofanyika yanakuwa ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Bodi ya kuratibu Taasisi zisizo za Kiserikali.

8.3.19 Matokeo ya ukaguzi wa Mifuko Maalumu ya Fedha

Kwa mujibu wa kifungu 12(1) cha Sheria ya Fedha, 2001, Waziri anaweza kutoa tamko kwenye Gazeti la Serikali, kuanzisha Mifuko Maalumu ambayo haitakuwa sehemu ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Na, mapato yake kila mwisho wa mwaka wa fedha hayatalipwa Mfuko Mkuu wa Serikali, bali

fedha hizo zitabakishwa kwenye mfuko husika kwa matumizi yaliyokusudiwa wakati wa uanzishaji wa mfuko huo. Kila tamko katika kifungu 12(1) litaweka bayana lengo la kuanzisha Mfuko husika na kuteua Afisa Masuuli atakayewajibika kwenye uendeshaji wa Mfuko huo.

Katika sehemu hii, ninawasilisha mambo muhimu yatokanayo na utendaji wa mifuko maalumu 14 niliyoikagua. Yafuatayo ni mambo muhimu yatokanayo na ukaguzi:

Madai yaliyofikia muda wake na Hayajarejeshwa shilingi 1,345,206,622

Ukaguzi wa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ulibaini kuwa uongozi ulilipa shilingi 3,342,970,002 (mtaji pamoja na riba) kwa wateja mbalimbali katika wilaya za Dodoma. Nilibaini kuwa kiasi cha shilingi 1,997,763,380 (60%) kilirejeshwa, na kiasi cha shilingi 1,345,206,622 (40%) hakijarejeshwa. Orodha ya madai hayo ni kama inavyooneshwa katika Jedwali hapo chini.

Jedwali 60: Madai yasiyorejeshwa

Na.	Wilaya	Madai yaliyofikia muda wake (Mtaji na riba) (Shilingi)	Kiasi kilichorejeshwa (Shilingi)	Kiasi ambacho hakijarejeshwa(Shilingi)
1	Manispaa ya Dodoma	820,832,289	452,198,525	368,633,764
2	Kongwa	778,582,131	398,662,735	379,919,396
3	Chamwino	522,992,820	272,723,700	250,269,120
4	Bahi	14,999,940.00	12,125,700	2,874,240
5	Kondoa	1,123,532,097	810,775,720	312,756,377
6	Chemba	12,025,125	1,840,000	10,185,125
7	Mpwapwa	70,005,600	49,437,000	20,568,600
	Jumla	**3,342,970,002**	**1,997,763,380**	**1,345,206,622**

***Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016*

Kushindwa kurejesha mikopo ndani ya muda uliokubalika kunaweza kuzuia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo kushindwa kufikia malengo yake.

Ninaishauri kwa menejimenti ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo kuhakikisha kuwa madai yote (Mtaji na riba) yarejeshwe kwenye Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ili kuwezesha Mfuko kutokupata hasara inayoweza kutokea.

Usimamizi wa madai ya mikopo usioridhisha

Ukaguzi wa madai ya mikopo iliyotolewa na Mfuko wa Rais wa Udhamini (Presidential Trust Fund) ulibaini kuwa mkopo wa kiasi cha shilingi 479,545,924 na riba ya shilingi 18,579,600 ulilipwa kwa wanufaikaji wa Kilosa, Kanda ya kusini na Kituo cha Kibaha. Mkopo wa kiasi cha shilingi 439,802,799 na riba ya shilingi 18,579,600 hakijarejeshwa kutoka kwa wakopeshwaji kwa tangu mwaka 2010 hadi 2015.

Kushindwa kurejesha mikopo kunaashiria kuwa Mfuko unaweza kushindwa kutoa mikopo kwa wanufaikaji wengine.

Ukaguzi ulibaini kuwa katika Kituo cha Ubena tawi la Makambako kuna mnufaikaji mmoja aliyepewa mkopo wa shilingi 6,000,000 (uliokuwa na riba ya shilingi 1,800,000) mnamo mwaka 2008. Hadi wakati wa Ukaguzi, mwezi Agosti 2016, mkopo huo haukurejeshwa kwa sababu mkopaji alikataa baada ya kubainika kuwa mkopo ulitolewa kwa mnufaikaji mwingine.

Kituo cha Kidugalo kilitoa mkopo wa kiasi cha shilingi 6,000,000 kwa wanufaikaji wawili tangu tarehe 10/07/2007. Ukaguzi ulibaini kuwa mnufaikaji mmoja alikataa kuwa hakuchukua mkopo; na mwingine analipia mkopo wake kupitia Mahakama ya Mwanzo.

Ni dhahiri kwamba, vilivyotajwa hapo juu ni viashiria kuwa kuna usimamizi usioridhisha, hivyo kuweka Mfuko katika hatari kifedha.

Ninashauri Mfuko wa Rais wa dhamana uimarishe mifumo ya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa madai yanarejeshwa kwa wakati. Aidha, uongozi wa Mfuko ubainishe wanufaikaji ambao hawajarejesha mikopo hiyo na kuchukua hatua stahiki za kisheria.

Mikopo iliyotolewa kinyume na malengo yaliyokusudiwa Shilingi 1,098,566,332.69

Mfuko wa Hazina wa Ukopeshaji (Treasury Advance Fund) ulianzishwa na Bunge kwa Azimio Namba 4 la 2011 kwa lengo la msingi la kuboresha maslahi ya watumishi wa Umma wa Serikali kuu kwa kutoa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri, vyombo vya nyumbani, na utengenezaji wa vyombo ya usafiri.

Ukaguzi wa Mfuko huu uliabaini kuwa kiasi cha shilingi 1,098,566,332.69 kilibainika kutokurejeshwa. Nilibaini kuwa kiasi hiki kililipwa Fungu 23 kwa ajili ya matumizi ambayo hayaendani na malengo ya mfuko huu kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali 61: Mikopo iliyotolewa kinyume na malengo yaliyokusudiwa

Tarehe	Maelezo	Kiasi (Shilingi)
26/10/2015	Bara Construction Co (1994) ltd – Ujenzi Simiyu	57,888,102.69
18/11/2015	Fungu 53 Ufuatiliaji wa michanganuo ya Usimamizi wa mifumo ya ulipaji.	179,760,000.00
29/12/2015	Fungu 23 Mhasibu Mkuu - Kutengeneza Taarifa ya Fedha jumuifu - Bunju	548,223,000.00
27/01/2016	Uchapishaji	22,397,230.00
31/12/2015	Fungu 23 Kutengeneza muingiliano wa mifumo kati ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Mapato.	199,056,000.00
26/01/2016	Fedha kwa ajili ya wanafunzi (usafiri, shajara na chakula)	77,790,000.00
24/02/2016	Anfield investment	13,452,000.00
	Jumla	**1,098,566,332.69**

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Hali kadhalika, kwenye Mfuko wa Uwezeshaji wa Wanawake, nilibaini kuwa kiasi cha shilingi 11,740,000 kililipwa kwa ajili

ya shughuli mbalimbali zisizokuwa za Mfuko husika; kiasi cha shilingi 8,740,000 kwa ajili ya kulipia tiketi za ndege na kiasi cha 3,000,000 kililipwa kwa watumishi wawili.

Kutumia fedha kinyume na malengo yaliyokusudiwa kunaashiria kwamba waombaji wa mikopo kutoka katika Mfuko hawatanufaika kama ilivyokusudiwa.

Ninashauri uongozi wa Mfuko wa Hazina wa Ukopeshaji kuhakikisha kuwa kiasi cha shilingi 1,098,566,332.69 kinarejeshwa kutoka Fungu 23. Pia, Mfuko wa Uwezeshaji wa Wanawake urejeshe fedha hizo pamoja na kuhakikisha kuwa malengo ya uanzishwaji wa mifuko yanazingatiwa.

Madeni yasiyolipwa shilingi *888,349,824*

Ukaguzi wangu wa mwaka 2015/2016 ulibaini kwamba mifuko maalumu ilikuwa na madeni yasiyolipwa kiasi cha shilingi 888,349,824. Kati ya madeni hayo, kiasi cha shilingi 490,416,536.08 kilikuwa hakijalipwa kwa muda zaidi ya miezi 12 wakati kiasi cha shilingi 397,933,288 kwa kipindi ndani ya miezi 12. Orodha ya mifuko maalumu yenye madeni yasiyolipwa ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini:

Jedwali 62: Madeni yasiyokusanywa

Na.	Taasisi	Deni ndani ya miezi 12 (Shilingi)	Deni baada ya miezi 12(Shilingi)
1	Mfuko wa maji (Maji Central)	337,584,266	464,920,879.2
2	Mfuko wa Pembejeo za Kilimo	0	25,495,656.88
3	Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake	60,349,021.62	0
	Jumla	**397,933,288**	**490,416,536**

Nashauri kuwa Maafisa Masuuli watengeneze bajeti inayokidhi kulipa mahitaji.

Mapungufu kwenye matumizi

Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu manne katika mifuko maalumu minne kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.

Jedwali na.58: Mapungufu kwenye matumizi

Kigezo	Taasisi	Matokeo ya ukaguzi	Kiasi (shilingi)
Kanuni 95(4) ya kanuni za Fedha za 2001(zilizorekebishwa 2004)	Mfuko wa Uwezeshaji wa Maendeleo ya Madini	Malipo yenye nyaraka pungufu	35,420,104.00
	Mfuko wa Rais wa Dhamana		28,985,043.00
		Jumla	**64,405,147.00**
Kanuni ya 24 ya kanuni ya kodi ya Mapato (Mashine za kielektroniki) 2012	Mfuko wa Maji	Malipo yaliyofanyika bila kudai stakabadhi za mashine za kielektroniki	23,654,400
	Mfuko wa SELF		619,912,264
	Baraza la Madaktari wa Macho		3,000,000
		Jumla	**646,566,664**
Kifungu cha 83 cha sheria ya kodi ya mapato ya 2008	Mfuko wa Pembejeo za Kilimo	Kodi zuio isiyokatwa	1,400,866.96
Kanuni 103 ya Kanuni za Fedha za 2001(iliyorekebishwa 2004)	Mfuko wa Hifadhi Wanyamapori Tanzania	Masufuru yasiyorejeshwa	76,748,200

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Kuhusu Malipo yenye upungufu wa nyaraka, ninashauri uongozi wa Taasisi husika kuzingatia kifungu 95(4) cha Kanuni za Fedha 2001 kwa kuhakikisha kuwa mfumo wa uthibiti unaimarishwa na kuwa na nyaraka stahiki kwenye malipo yanayofanyika.

Kuhusu malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki, ninashauri Serikali itoe miongozo kwa Taasisi hizi ili kuhakikisha kuwa malipo yanakuwa na stakabadhi za kielektroniki inavyostahili.

Kuhusu masurufu yasiyorejeshwa, nashauri mifuko maalumu kuzingatia Kanuni ya Fedha za Umma kwa kuhakikisha kuwa masurufu yanarejeshwa baada ya kukamilika kwa lengo.

Kutokuzingatia Sheria za Manunuzi ya Umma

Katika sampuli za miamala kutoka Mfuko wa SELF, nilibaini kuwa manunuzi ya shilingi 223,357,466 katika mwaka wa Fedha 2015/2016 yalifanyika bila kuwa na Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi na Mpango wa Manunuzi kinyume na Kifungu cha 31(1) na 37(1) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 na Kanuni 70 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2013.

Udhaifu kwenye mifumo ya manunuzi unaweza kusababisha kupata bidhaa zenye kiwango kisichoridhisha na kwa bei isiyo na tija.

Nashauri uongozi kuzingatia sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 na Kanuni zake za 2013 kwa kuunda Bodi za Zabuni, Kitengo cha Manunuzi na kuandaa mpango kazi kila mwaka.

Madeni yasiyokusanywa shilingi 2,454,739,443

Katika Ukaguzi wa mwaka 2015/2016, nilibaini kuwa mifuko maalumu mitano ilikuwa na madeni yasiyokusanywa kiasi cha shilingi 3,954,533,192. Kati ya kiasi hiki, shilingi 2,034,192,487 (51%) zilikuwa hazijarejeshwa kwa zaidi ya miezi 12 wakati kiasi cha shilingi 1,920,340,705 (49%) ndani ya miezi 12. Kiasi hiki kikubwa cha madeni yasiyokusanywa kinapunguza ukuaji na uwezo wa mifuko hii kutekeleza majukumu yake. Orodha ya mifuko yenye madeni yasiyorejeshwa ni kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali 63: Mapato yasiyokusanywa

Na.	Mfuko	Mapato ndani ya miezi 12	Mapato zaidi ya miezi 12
1	Uwezeshaji wa maendeleo ya madini	93,431,632	-
2	Maji	30,740,000	361,804,003.8
3	Pembejeo za Kilimo	234,180,510	2,329,883
4	Maendeleo ya Wanawake	727,532,407	1,004,721,007
5	Maafa	834,456,156	665,337,593
	Jumla	**1,920,340,705**	**2,034,192,487**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Ninatoa rai kwa mifuko maalumu kufuatilia kwa karibu mapato yote yasiyokusanywa bila kuchelewa ili kuwezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Fedha zilizokusanywa na wakala kutokupelekwa benki Shilingi 56,967,688

Ukaguzi wangu wa mifuko maalumu ulibaini kuwa, vituo vya Iringa na Mafinga vilikuwa na mikopo isiyorejeshwa kiasi cha shilingi 56,967,688 mwaka 2011/2012. Ili kukusanya mikopo hiyo, Mfuko wa Rais wa Udhamini (Presidential Trust Fund) uliingia mkataba na kampuni ya ukusanyaji wa madeni ya Makalu. Ilibainika kuwa kampuni hii haikurejesha fedha hizo ambazo zilikusanywa tangu mwaka 2012. Ukaguzi ulibaini kuwa kampuni hiyo ilitokomea na kubadili aina ya biashara.

Kukusanya fedha bila kuwasilisha kunaashiria kuwa kazi iliyofanyika inaweza kuwa na vitendo vya udanganyifu.

Ninashauri kuwa uongozi wa Mfuko wa Rais wa Udhamini uchukue hatua za kisheria kwa wakala husika na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa.

Mauzo ya mahindi ya msaada yasiyowasilishwa kwenye akaunti husika Ofisi ya Waziri Mkuu Shilingi 44,666,300

Mwaka huu wa Ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri za Wilaya tano na Halmashauri ya Manispaa moja zilitakiwa kurejesha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kiasi cha shilingi 44,666,300 kutokana na mauzo ya mahindi ya msaada. Hata hivyo, hadi kufikia 30/06/2016 fedha hizo zilikuwa hazijawekwa kwenye akaunti husika katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Orodha ya Taasisi hizo ni kama inavyoonekana hapo chini;

Jedwali 64: Fedha zilizokusanywa ambazo hazikuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu

Na.	Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	6,762,100
2	Halmashauri ya Wilaya ya Iramba	4,500,000
3	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	13,500,000
4	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	8,479,000

Na.	Taasisi	Kiasi (Shilingi)
5	Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma	11,425,200
Jumla		**44,666,300**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Kutokuwasilisha fedha za mauzo ya mahindi kwa wakati kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha.

Naushauri uongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu uweke utaratibu wa namna ya kufuatilia na kukusanya Fedha zinatokana na mauzo ya mahindi kwenye shehemu husika.

Fedha zilizowekwa akaunti isiyohusika Shilingi 10,530,000

Ukaguzi wangu ulibaini kwamba Halmashauri ya Iramba ilitakiwa kuwasilisha kiasi cha shilingi 10,500,000 kwenye akaunti namba 9921151001 ya Maafa; hata hivyo kiasi hicho kiliwekwa kwenye akaunti namba 9921141201 Benki Kuu ya Tanzania. Kuna vihatarishi kwamba fedha hizi zinaweza kutumika kinyume na malengo.

Ninashauri uongozi kufuatilia suala hili na kuhakikisha fedha hizo zinawekwa kwenye akaunti husika.

Matumizi yasiyofaa ya mifuko ya uwezeshaji 1,427,515,995

Ukaguzi wa mwaka 2015/2016 ulibaini kuwa mwaka 2010/2011 kiasi cha shilingi 615,218,931 kilitumwa kutoka akaunti ya Uwezeshaji kwenda Mfuko wa Rais wa Dhamana (Presidential Trust Fund) kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya ofisi. Kati ya kiasi hicho, shilingi 159,550,206 (25%) ni mtaji. Hii ni kinyume na malengo ya akaunti ya uwezeshaji yanayohitaji riba ndiyo itumike kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya ofisi; mtaji ubaki kwenye Mfuko wa uwezeshaji. Pia, nilibaini kuwa muamala huu haukuwa na kibali cha Bodi ya Wadhamini kinyume na sura 13.1(6) ya Kanuni za Fedha za Mfuko wa Rais wa Udhamini.

Pia, nilibaini kuwa mwaka 2011/2012 hadi 2014/2015 kiasi cha shilingi 797,987,064.20 kililipwa kutoka akaunti ya Uwezeshaji kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile manunuzi ya mafuta ya magari, mafao ya kuachisha

wafanyakazi, mishahara ya watumishi, malimbikizo ya mishahara, makato ya mishahara kinyume na Sura 13.1(2) ya Kanuni za Fedha za Mfuko wa Rais wa Udhamini.

Kwa dosari hii, Mfuko wa Rais wa Udhamini unaweza kuwa kwenye hatari ya kutokufikia malengo yake kwa kufanya matumizi kinyume na madhumuni ya Mfuko.

Ninashauri kuwa uongozi wa Mfuko wa Rais wa Udhamini uboreshe mifumo ya udhibiti kwenye matumizi ya Mfuko huu kwa kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

8.3.20 Matokeo muhimu ya Ukaguzi wa Mabonde

Mabonde yalianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi ya Maji namba 42 ya mwaka 1974 pamoja na marekebisho yaliyofuata, sheria ya Matumizi ya Rasilimali ya Maji namba 42 ya 2009. Ukaguzi wangu ulijikita kwenye Mabonde yote 11 na yafuatayo ni matokeo muhimu:

Upungufu wa watumishi

Katika ukaguzi wa Usimamizi wa rasilimali watu, nilibaini kuwa Mabonde sita yalikuwa na upungufu wa watumishi 457 katika nafasi za Idara mbalimbali. Hii ni sawa na asilimia 56 ya mahitaji. Upungufu wa watumishi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

Upungufu wa watumishi unaathiri utendaji wa Mabonde haya.

Jedwali 65: Upungufu wa watumishi

Na.	Taasisi	Mahitaji	Idadi iliyopo	Upungufu
1	Bodi ya Mfereji wa Kati	112	39	73
2	Bodi ya Bonde la maji ziwa Viktoria	178	48	130
3	Bodi ya Bonde la mto Rufiji	168	60	108
4	Bodi ya Bonde la Maji ya Ruvuma na Pwani na	144	112	32

Na.	Taasisi	Mahitaji	Idadi iliyopo	Upungufu
	Kusini			
5	Bodi ya bonde la ziwa Tanganyika	134	40	94
6	Mamlaka ya Majisafi Wanging'ombe	72	52	20
	Jumla	**808**	**351**	**457**

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Nashauri bodi za Mabonde yote wakishirikiana na Tume ya Ajira kuhakikisha kuwa nafasi zilizo wazi zinajazwa.

Mishahara iliyolipwa kwa watumishi wasiokuwa kwenye utumishi wa Umma Shilingi 20,916,000

Ukaguzi wa rasilimali watu na Mishahara Bonde la mto Rukwa ulibaini kuwa Maafisa wawili walilipwa mshahara wa shilingi 20,916,000 ilhali hawakuwa watumishi wa Umma. Watumishi hao walilipwa shilingi 13,260,000 kwa miezi 10 na shilingi 7,656,000 kwa miezi 23. Hii ni kinyume na Kanuni ya 113 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001(zilizorekebishwa 2004) zinaelekeza kuwa Maafisa Masuuli watunze kumbukumbu za watumishi ili watumishi walipwe kwa siku walizofanya kazi.

Kulipa Mishahara kwa watumishi wasiokuwa kwenye utumishi wa Umma ni hasara kwa serikali.

Ninashauri Bodi ya Bonde la mto Rukwa kuhakikisha kuwa Mishahara iliyolipwa kwa watumishi wasiokuwa utumishi wa Umma inarejeshwa Wizara ya Fedha na Mipango.

Kuchelewa kukamilisha Ujenzi wa jengo la ofisi

Ukaguzi ulibaini kuwa tarehe 15/10/2013 Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliingia mkataba na Associated Investment & Services LTD wenye kumbukumbu namba ME-011/2012-13 wenye kiasi cha shilingi 2,632,033,365 kwa ajili ya ukarabati na Ujenzi wa Ofisi na maabara ya maji makao makuu ya Bonde la Ziwa Tanganyika Kigoma na Ofisi ndogo ya Kahama na Tabora.

Ukaguzi ulibaini kuwa kazi ya Ujenzi ilipaswa kukamilika baada ya wiki 52 na kuanza siku 28 baada ya kusaini mkataba, ambayo ni Novemba/Disemba 2014 lakini hadi Oktoba 2016 bado kazi zilikuwa hazijamalizika.

Kushindwa kukamilisha mradi kwa wakati kunaashiria kuwa malengo yaliyotarajiwa hayawezi kufikiwa kwa wakati. Ninashauri kuwa uongozi uimarishe usimamizi wa miradi ili iweze kukamilka kwa wakati; hali kadhalika, kuzingatia masharti ya mikataba.

Utekelezaji wa mpango wa manunuzi usioridhisha

Ukaguzi wangu wa Mabonde matatu ulibaini kuwa manunuzi ya vifaa na huduma vya shilingi 228,790,840 hayakujumuishwa kwenye mpango wa manunuzi kinyume na Kifungu 49(2) na (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 7 ya 2011 kinachohitaji kuwa mpango wa manunuzi uzingatie bajeti. Aidha, Taasisi nyingine za Mabonde zisizokuwa na mpango wa manunuzi ni Bonde la Rufiji shilingi 198,312,900 (87% ya mpango wa manunuzi), Mamlaka ya Usambazaji na Usafishaji Makonde shilingi 25,850,000 (11% ya mpango) na Mamlaka ya Usambazaji na Usafishaji ya Wanging'ombe 4,627,940 (2% ya mpango).

Ninashauri kuwa Mabonde yazingatie Mpango wa Manunuzi na Uongozi uzingatie kuongeza ufanisi kwenye uandaaji wa mahitaji na utafiti wa masoko ili kipata taarifa za kutosha kuwezesha mpango na utekelezaji wa manunuzi wenye tija.

Mapungufu kwenye matumizi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:

Katika mwaka wa ukaguzi, nilibaini dosari sita kwenye matumizi ya fedha, hivyo sikuweza kuthibitisha usahihi na utaratibu wa matumizi hayo. Dosari hizo ni kama zifuatazo: Matumizi yenye nyaraka pungufu (Shilingi 53,862,324), Kukosekana kwa stakabadhi za mashine za kielekitroniki (EFD) (Shilingi 283,408,496); Kutokukata kodi zuio (Shilingi 45,057,351.09), malipo yasiyostahiki shilingi 12,290,200.

Jedwali na.62: Mabonde na yaliijyojitokeza kwenye ukaguzi.

Kanuni	Taasisi	Matokeo ya ukaguzi	Kiasi (shilingi)
Kanuni 95(4) ya kanuni za Fedha za 2001(zilizorekebishwa 2004)	Bodi ya Mfereji wa Kati	Malipo yenye nyaraka pungufu	18,734,324
	Mamlaka ya Maji Handeni		30,418,000
	Mamlaka ya ugavi na usafishaji wa Maji Mugango-Kiabakari		4,710,000
		Jumla	**53,862,324**
	Bodi ya Bonde la ziwa Nyasa	Malipo yasiyostahiki	12,290,200
Kanuni ya 24 ya kanuni ya kodi ya Mapato (Mashine za kielektroniki) 2012	Bodi ya Bonde la ziwa Nyasa	Malipo yasiyo na stakabadhi za mashine za kielektroniki	9,945,000
	Bodi ya Bonde la ziwa Rukwa		90,623,470
	Bodi ya Bonde la ziwa Rufiji		8,692,000
	Bodi ya Bonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini		160,500,000
	Bodi ya Maji ya Wami- Ruvu		5,702,650
	Mamlaka ya Majisafi Wanging'ombe		7,945,376
		Jumla	**283,408,496**
Kifungu cha 83 cha sheria ya kodi ya mapato ya 2008	Bodi ya Bonde la ziwa Viktoria	Kodi zuio isiyokatwa	5,514,773
	Bodi ya Bonde la ziwa Rufiji		1,163,820.32
	Bodi ya Maji ya Wami- Ruvu		868,740
	Bodi ya Bonde la ziwa Tanganyika		37,510,017.77
		Jumla	**45,057,351.09**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016*

Kuhusu malipo yenye upungufu wa nyaraka, ninashauri Uongozi wa Taasisi husika kuzingatia kifungu 95(4) cha Kanuni za Fedha 2001 kwa kuhakikisha kuwa mfumo wa uthibiti unaimarishwa na kuwa na nyaraka stahiki kwenye malipo yanayofanyika.

Kuhusu malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki, Ninashauri Serikali itoe miongozo kwa Taasisi hizi ili kuhakikisha kuwa malipo yote ya manunuzi yanakuwa na stakabadhi za kielektroniki.

Kuhusu malipo yasiyokatwa kodi zuio, nashauri Maafisa Masuuli wahakikishe kuwa sheria ya kodi inazingatiwa kwa kukata kodi zuio na kuwasilisha Mamlaka ya Mapato.

Mapato yasiyokusanywa shilingi 3,735,127,782

Ukaguzi wangu wa mwaka 2015/2016 ulibaini kuwa Mabonde 13 yalikuwa na mapato yasiyokusanywa kiasi cha shilingi 3,735,127,782. Kati ya mapato hayo, kiasi cha shilingi 2,121,401,359 (57%) yalikuwa hayajakusanywa kwa kipindi zaidi ya miezi 12 wakati shilingi 1,613,726,423 (43%) ndani ya miezi 12.

Kiasi hiki kikubwa cha madai yasiyokusanywa kinapunguza ukuaji na uwezo wa kujiendesha na kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Ninaushauri uongozi wa Mabonde ufuatilie kwa ukaribu madai ambayo hayajalipwa ili kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Ukosefu wa hatimiliki kwa ardhi inayomilikiwa na mabonde

Uhakiki wa nyaraka za umiliki ulibaini kuwa ardhi inayotumiwa na kumilikiwa na bodi za mabonde ulibaini kuwa ardhi hazina hati miliki. Kwa ukosefu wa nyaraka za umiliki, sikuweza kuthibitisha kama mali hizo zinamilikiwa kisheria na Taasisi husika.

Hii inaashiria kwamba Taasisi hizo hazimiliki mali hizo kisheria; na endapo kutakuwa na shauri serikali inaweza kushindwa. Orodha hapo chini inaonesha taasisi hizo.

Na.	Taasisi	Sehemu
1	Internal Drainage Basin Water Board	Manispaa ya Singida
		Babati
		Mto wa Mbu
2	Bodi ya Bonde la ziwa Tanganyika	Manispaa ya Kigoma
		Manispaa ya Tabora
		Kahama
3	Mamlaka ya ugavi na usafishaji wa Maji Mugango-Kiabakari	Mugango, Kiabakari and Butiama

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa menejimenti 2015/2016

Ninashauri kuwa bodi za mabonde zikishirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa

Taasisi husika zinakuwa na nyaraka za umiliki ili kulinda mali za serikali.

Madeni yasiyolipwa shilingi 2,556,054,723.54

Ukaguzi wangu wa mwaka 2015/2016 ulibaini kuwa mabonde 10 yalikuwa na madeni ya shilingi 2,556,054,723.54. Kati ya madeni hayo, kiasi cha shilingi 2,295,412,580.90 (90%) yalikuwa hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12 na shilingi 260,642,142.64 (10%) ndani ya miezi 12.

Nashauri kuwa Maafisa Masuuli watengeneze bajeti inayokidhi kulipa madeni na mahitaji mengine.

USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

9.1 Utangulizi

Manunuzi ya bidhaa na huduma ni muhimu katika utendaji wa taasisi na mara nyingi yanahusisha kiasi kikubwa cha fedha. Matukio mengi yaliyopita ya rushwa yalibaini kuwa Manunuzi ndiyo eneo hatarishi kwa rushwa na ufujaji wa fedha. Matukuo ya rushwa katika manunuzi si tu kwamba husababisha hasara, bali husababishakuharibu taswira ya taasisi katika eneo la uaminifu katika kutoa huduma kwa jamii.

Manunuzi ya Umma ni nguzo muhimu ya kimkakati katika utoaji huduma Serikalini. Kutokana na Manunuzi ya Umma kutumia kiasi kikubwa cha fedha za Serikali, usimamizi wake ni muhimu katika kukuza ufanisi wa sekta ya Umma. Manunuzi ya Umma yanaongozwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni za Ununuzi wa Umma GN 446 ya 20 Desemba 2013 pamoja na marekebisho ya sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2016 ambazo kwa pamoja zinatoa mfumo wa kisheria unaoongoza taasisi na taratibu za manunuzi katika sekta ya umma. Licha ya kuwapo kwa sheria, baadhi ya Wizara / Sekretarieti za Mikoa pamoja na Balozi bado hazizingatii kikamilifu sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013.

Katika kuhakikisha kuwa taratibu za Manunuzi zinafuatwa nchini Tanzania, Kifungu na 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinaeleza bayana kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya tathmini na kutoa taarifa katika Ripoti yake ya mwaka kuwa Taasisi iliyokaguliwa kama imezingatia au kutozingatia Sheria za Manunuzi na Kanuni zake.

Sura hii inaonyesha matokeo ya mapitio ya taratibu za Manunuzi ya Umma na usimamizi wa mikataba kutokana na kaguzi za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka huu wa fedha husika. Katika ripoti yangu nimejumuisha ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti ya Manunuzi ya

Umma na Taarifa ya Divisheni ya Kurugenzi ya Uhakiki mali za Serikali.

9.2 Manunuzi Yaliyofanyika bila Ushindanishi Sh. 24,216,625,390

Katika Ukaguzi wa Taasisi za Serikali Kuu 122 zilizokaguliwa, imebainika kuwa taasisi za Serikali Kuu kumi na tano (15) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 24,216,625,390 bila kuzingatia Kanuni ya 163 &164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inazozitaka Taasisi zinazofanya Manunuzi kuzingatia upatikanaji wa nukuu za bei zisizopungua tatu kutoka kwa Wazabuni/Wakandarasi tofauti. Vilevile, nilibaini matumizi ya njia za manunuzi isivyostahili kama vile kutoka chanzo kimoja au kushindanisha wazabuni wachache kinyume na kanuni ya 159 ya kanuni za manunuzi ya umma za mwaka 2013. Orodha ya Taasisi ambazo hazikufuata Kanuni hizi ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho 9.1**.

Manunuzi ya bila ya kufuata njia ya ushindanishi katika taasisi za Serikali Kuu yamepungua kutoka Sh.27.12 bilionii hadi Sh.24.22 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya taasisi Tisa zilihukisika ikilinganishwa na taasisi kumi na nne zilizokaguliwa katika mwaka huu wa fedha.

Kutokana na kutofuata taratibu za ushindanishi, taasisi za Serikali kuu huwenda hazikulipa bei stahiki katika manunuzi zilizofanya. Nazishauri taasisi za Serikali Kuu kuzingatia kikamilifu sheria ya manunuzi ya Umma katika ushindani ili kupata thamani ya fedha kwa ajili ya bidhaa na huduma. Vile vile nasisitiza taasisi kuepuka kutumia njia za manunuzi kama vile kutoka kwa Mzabuni mmoja au Zabuni zisizo za wazi katika hali ambayo njia hizi zitashindwa kutibitishwa na kanunu ya 159 ya kanuni za Manunuzi ya umma ili kupata thamani ya fedha.

9.3 Mapungufu Yaliyobainika katika Usimamizi wa Mikataba na Miradi

Kanuni ya 114 ya kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi ya Umma kusimamia manunuzi yoyote ya bidhaa, huduma au kazi pamoja na:

(a) Kufuatilia gharama na upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa muda na ubora uliyoainishwe kwenye mkataba;
(b) Kufuatilia maendeleo na kukamilika kwa wakati wa kazi kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba;
(c) Kuchukua hatua za kusahihisha mapungufu yalijitokeza katika kutekeleza masharti ya mkataba
(d) Kuhakikisha majukumu yaliyobainishwa kwenye mikataba yanatekelezwa yote.

Kinyume na kanuni hii, nilibaini mapungufu katika usimamizi wa Mikataba/Miradi, ambapo mikataba/miradi nane (8) yenye thamani ya Sh 63,254 milioni na Dola za Kimarekani milioni 1,000 milionii katika taasisi nane (8) za Serikali Kuu zilizokaguliwa haikusimamiwa vizuri. **Kiambatisho 9.2** kinaonesha taasisi zilizoshindwa kusimamia mikataba/miradi vizuri.

Ikilinganishwa na mwaka wa ukaguzi 2014/2015 idadi ya Taasisi za Serikali kuu zilizokuwa na mapungufu katika usimamizi wa mikataba imepungua kwa asilimia 60% kutoka
taasisi ishirini (20) mwaka 2014/2015 hadi taasisi nane katika mwaka huu wa fedha; Hata hivyo kiasi cha fedha kilibadilika kutoka Sh. 109,683.40 milioni hadi kufikia Sh 63,254 milion na Dola za Kimarekani Milioni 1,000 hali inayoonesha uzingatiwaji hafifu wa sheria hii.

Kwa ujumla, menejimenti ya Wizara, Idara na taasisi za Serikali kuu hazina budi kubadili mtazamo katika usimamizi wa mikataba mbalimbali inayoingia na wakandarasi/wazabuni na kuzingatia masharti ya mkataba.

9.4 Kuchelewa Kukamilika kwa Miradi ya Ujenzi Sh. 23,328,603,706

Jumla ya Wizara, Idara na Sekretatieti za Mikoa kumi na nne (14) ziliingia katika makubaliano ya Mikataba na Wakandarasi katika ujenzi wa miradi mbalimbali. Nilibaini kuchelewa kukamilika kwa miradi hii yenye thamani ya Sh. 23,328,603,706 kinyume na muda uliyoainishwa kwenye mikataba. **Kiambatisho 9.3** kinaonesha taasisi, miradi husika na muda uliocheleweshwa.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi/mikataba kunaweza kusababisha Serikali kuingia gharama zisizo za lazima zinazotokana na mfumuko wa bei pamoja na kuongezeka kwa gharama za vifaa. Menejimenti za taasisi husika zinashauriwa kuzingatia matakwa ya kanuni ya 114 ya PPR, 2013 katika usimamizi wa mikataba ya manunuzi.

Menejimenti inashauriwa kusimamia kikamilifu mikataba inayoendelea ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati bila kuchelewa. Nazishauri Taasisi ziendelee kufanya juhudi za ufuatiliaji rasilimali fedha kutoka Hazina ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa katika bajeti. Nashauri pia miradi yenye fedha kidogo itekelezwe kwa hatua ili kurahisisha usimamizi wa miradi na ulipaji wake. Vile vile, zihakikishe hakuna cheti cha malipo kinachobakia bila kulipwa.

9.5 Manunuzi Yaliyofanyika bila Idhini ya Bodi ya Zabuni Sh. 2,485,411,529

Mapitio ya uzingatiwaji wa Kifungu na35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni na 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inayotaka Manunuzi kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni nilibaini kuwa jumla ya Taasisi za Serikali Kuu kumi(10) zilifanya Manunuzi yenye thamani ya Sh. 2,485,411,529 bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Taasisi mbalimbali zilizofanya Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni husika zimeorodheshwa kwenye **Kiambatisho 9.4.**

Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa ziliendelea kufanya vibaya kati uzingatiaji wa sheria hii. Jumla ya manunuzi ya Sh.2,485,411,529 sawa na ongezeko la asilimia 403 ikilinganishwa na yaliyobainika mwaka jana katika taasisi tatu ya jumla ya Sh.494,395,890

Kufanya manunuzi yasiyoidhinishwa na bodi ya Zabuni kunaweza kusababisha kazi kutolewa kwa wazabuni/wakandarasi wasiokuwa na uwezo; hivyo, kusababisha uwazi, ufanisi na tija kukosekana katika manunuzi.

Kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 35 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, nashauri menejimenti ya taasisi husika zizingatie kikamilifu ushiriki wa bodi ya zabuni

katika kuidhinisha manunuzi ili kuepuka manunuzi yasiyo kuwa na tija au mikataba isiyo tekelezeka.

9.6 Manunuzi ya Kazi za Ujenzi, bidhaa na Huduma bila ya Kuwapo kwa Makubaliano ya Mkataba Sh.11,253,346,373 & Dola 29,606,100

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilibaini kutozingatiwa kwa sheria za manunuzi ambapo Jumla ya taasisi za Serikali Kuu kumi (10) zilizokaguliwa zilifanya manunuzi ya kazi za ujenzi,bidhaa na huduma yenye thamani ya Sh. Sh.11,253,346,373 na Dola 29,606,100 bila ya kuwapo kwa makubaliano katika hali ya Mikataba. Hii ni kinyume na Kanuni ya 10 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 ambayo inatamka bayana kwamba, taasisi za Umma zitahakikisha kwamba malipo kutokana na mzabuni yanafanywa vizuri na mara moja kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba wa ununuzi iliyoingia. Taasisi mbalimbali zilizofanya Manunuzi bila ya kuwapo kwa mkataba zimeorodheshwa kwenye jedwali hapa chini

Jedwali 66: Manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa na huduma bila ya kuwapo kwa makubaliano ya mkataba

Na	Maelezo	Kiasi (Sh)
1	**Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa**	
	Malipo ya kazi mbalimbali za ujenzi bila ya kuwapo kwa makubaliano ya Mkataba	1,536,803,523
2	**Fungu 44: Wizara ya Viwanda, Biashara na uwekezaji**	
	Kutokuwapo kwa Mikataba ya huduma za Ulinzi na Usafi.	93,088,130
3	**Fungu 38: Jeshi la Wananchi wa Tanzania**	
	Kutokuwapo kwa Mkataba wa ujenzi Uwanja wa ndege wa NAB.	3,086,847,327
4	**Fungu 14: Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**	
	Malipo ya kukomboa magari ya Zimamoto bandarini bila kuwapo kwa mkataba.	45,661,399
5	**Fungu 28: Jeshi la Polisi**	
	Kukosekana kwa Makubaliano ya Mkataba	USD 29,606,100

Na	Maelezo	Kiasi (Sh)
	katika ununuzi wa Magari	
6	**Fungu 70: Sekretarieti ya Mkoa Arusha**	
	Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimali bila ya kuwapo ya Mikataba midogo	269,351,705
7	**Fungu 93: Idara ya Uhamiaji**	
	Kukosekana kwa mkataba wa Makubaliano kwajili ya ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Kamishna wa Uhamiaji-Msasani, Dar es Salaam.	309,428,942
8	**Fungu 61: Tume ya Taifa ya Uchaguzi**	
	Mapungufu katika ununuzi wa mihuri	944,000,000
9	**Fungu 61: Tume ya Taifa ya Uchaguzi**	
	Manunuzi ya karatasi za nyongeza za kupigia kura bila ya Mkataba	1,938,943,835
10	**Fungu 61: Tume ya Taifa ya Uchaguzi**	
	Manunuzi ya shajala kwa ajili ya uchaguzi kabla ya kuingia kwa mkataba.	3,029,221,512
Jumla		**11,253,346,373**

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2015/2016

Nimebaini kuongezeka kwa kiasi kikubwa katika manunuzi yanayofanyika bila ya mkataba ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo taasisi tano za Serikali kuu zilifanya manunuzi ya Sh 5.21 bila ya mikataba. Hatua hii inaonesha kwamba hapakuwa na mabadiliko katika kuzingatia sheria hii.

Ni muhimu Manunuzi ya Umma yakaambatishwa na nyaraka za kutosha za mikataba; ili kama kutatokea mmoja kushindwa kutimiza makubaliano ziweze kukubalika mbele ya Sheria. Nashauri Taasisi zizingatie Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake kwa kuingia makubiliano ya mikataba inayokubalika mbele ya Sheria.

9.7 Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa Sh. 7,395,231,560

Kanuni Na.131 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka, 2013 inaeleza bayana taratibu za kununua bidhaa na huduma kutoka kwa Wazabuni walioidhinishwa na Wakala wa manunuzi ya Serikali (GPSA). Pia Kanuni Na.137 ya PPR, 2013 inaelekeza

namna ya kufanya matengeno ya Magari ya Serikali kupitia TEMESA. Vile vile Kanuni za 139-141 za manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 zinatoa mwongozi kwa taasisi za Serikali kununa madawa kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD). Hata hivyo, nilibaini katika Ukaguzi jumla ya taasisi za Serikali kuu kumi na nne(14) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 7,395,231,560 kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa na TEMESA, GPSA na MSD.

Jedwali 67: Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa

Na	Maelezo	Kiasi(Sh)
1	**Fungu 42: Bunge**	
	Magari ya Serikali yaliyofanyiwa matengenezo kwenye karakana za watu binafsi bila idhini ya TEMESA.	36,240,792
2	**Fungu 9: Bodi ya Mishahara**	
	Matengenezo ya Magari yasiyofuata taratibu	5,477,500
3	**Fungu 26: Ofisi ya Makamu wa Rais - Ofisi Binafsi.**	
	Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)	3,674,437
4	**Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	259,698,748
5	**Fungu 73: Sekretarieti ya Mkoa Iringa**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	84,929,934
6	**Fungu 81: Sekretarieti ya Mkoa Mwanza**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	10,743,740
7	**Fungu 38: Jeshi la Wananchi wa Tanzania**	
	Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa	6,498,215,788
8	**Fungu 52: Wizara ya Afya**	

	Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)	25,542,567.80
9	**Fungu 89: Sekretarieti ya Mkoa Rukwa**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	9,652,020
10	**Fungu 70: Sekretarieti ya Mkoa Arusha**	
	Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa	6,134,601
11	**Fungu 75: Sekretarieti ya Mkoa Kilimanjaro**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	61,773,440
12	**Fungu 86: Sekretarieti ya Mkoa Tanga**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	171,873,302
13	**Fungu 93: Idara ya Uhamiani**	
	Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)	154,757,690.30
14	**Fungu 79: Sekretarieti ya Mkoa Morogoro**	
	Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	66,517,000
Total		**7,395,231,560**

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2015/2016

Nimebaini maboresho katika uzingatiaji wa kanuni hii kwenye taasisi za Serikali Kuu zilizokaguliwa; ambapo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 taasisi kumi na sita(16) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh.8,556.82 milioni kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa, hii ni sawa na maboresho ya asilima 13%

Ninashauri Menejimenti ya Taasisi husika izingatie kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ili Taasisi ziweze kupata thamani halisi ya fedha zilizotumika katika Manunuzi.

9.8 Mapungufu Yaliyobainika katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka Sh. 980,345,532

Kifungu cha 49(2&3) cha Sheria ya Manunuzi Na.7 ya mwaka 2011 kinaelekeza mamlaka ya bajeti kuidhinisha mpango wa manunuzi wa mwaka wa taasisi ya kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa. Kifungu hiki kinafafanua kuwa, taasisi ya manunuzi inapaswa kufanya manunuzi kwa mujibu wa mpango wa mwaka wa manunuzi na manunuzi yoyote ambayo hayakupangwa yanapaswa kupata barua ya idhini ya Afisa Masuuli wa taasisi ya Umma.

Katika kupitia mchakato wa manunuzi wa Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Balozi nilibaini manunuzi yenye thamani ya Sh. 980,345,532 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi kinyume na kifungu tajwa hapo juu.

Jedwali 68: Mapungufu yaliyobainika katika mpango wa Manunuzi wa mwaka

Na	Maelezo	Kiasi (Sh)
1	**Fungu 34: Wizara ya mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki**	
	Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali nje ya mpango wa Manunuzi wa mwaka	268,996,148
2	**Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Raisi**	
	Ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais nje ya mpango wa manunuzi	116,695,863
3	**Fungu 27: Msajili wa Vyama vya Siasa**	
	Manunuzi ya vifaa vya Ofisi nje ya mpango wa Manunuzi	18,954,533
4	**Fungu 70: Sekretarieti ya Mkoa Arusha**	
	Kutokuandaliwa kwa mpango jumuifu wa manunuzi wa mwaka	544,168,988
5	**Fungu Dogo: 2005 Ubalozi wa Tanzania Abuja**	
	Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi wa mwaka	31,530,000
Jumla		**980,345,532**

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2015/2016

Nimebaini kuendelea kuimarika kwa uzingatiaji wa sheria hii katika taasisi za Serikali Kuu. Manunuzi yaliyofanyika kinyume na Mpango wa Manunuzi yamepungua kwa asilimia 35%, kutoka Sh.8,462,110,917 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 hadi Sh.980,345,532. Nazishauri Taasisi husika zizingatie kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ili kuweza kuboresha mchakato mzima wa manunuzi katika taasisi za Umma.

9.9 Mapungufu katika Utunzaji wa Nyaraka za Mchakato wa Manunuzi Sh.12,576,421,680

Utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi ni takwa la kisheria kama lilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 61(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011. Kutokana na Kifungu hiki Taasisi za Umma zinapaswa kutunza kumbukumbu za mchakato wa manunuzi pamoja na maamuzi yaliyofanyika kwa kipindi kisichopungua miaka mitano toka kukamilika kwa mchakato wa mkataba. Vilevile kumbukumbu hizi ziweze kuwasilishwa kwa Waziri na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale zitakapokuwa zinahitajika. Pia kumbukumbu zinatoa ushahidi wa maamuzi yaliyofanyika na kuwezesha mchakato wa ukaguzi na uhakiki uwazi, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa(Fungu 57) haikuzingatia sheria ya Manunuzi ya Umma; ambapo, manunuzi yenye thamani ya Sh. 12,576,421,680 yalifanyika bila ya utunzaji wa nyaraka/kumbukumbu za manunuzi kinyume na Sheria tajwa hapo juu.

Ufanisi katika utunzaji wa kumbukumbu ni muhimu katika kuhakikisha uhifadhi, usalama, uadilifu na siri za taarifa.

Nashauri shughuli zote za manunuzi kuidhinishwa kwa usahihi na kuwa na viambatisho vya kutosha kwa ajili ya marejeo ya baadaye.

9.10 Mikataba Isiyohakikiwa (Vetting) na Mwanasheri Mkuu wa Serikali Sh.491,047,500

Kanuni Na.59 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inaeleza bayana kuwa Mikataba inayotokana na Zabuni zinazozidi kiasi cha Shilingi milioni hamsini inatakiwa kufanyiwa uhakiki (vetting) na Mwanasheri Mkuu wa Serikali kabla ya pande husika hazijaingia kwenye makubaliano ya Mkataba. Hata hivyo, nilibaini katika ukaguzi wangu kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji (Fungu 49) iliingia makubaliano ya mkataba wenye thamani ya Sh. 491,047,500 na Mkandarasi MS. International LTD kwa ajili ya kuleta mtambo wa kusafisha maji unaohamishika-Hanang bila ya Mkataba kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mikataba isiyohakikiwa (vetting) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaweza kuleta changamoto za kisheria endapo patatokea kutoelewa kwa pande mbili za mkataba.

Nazishauri Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kufanya kazi kwa pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha Mikataba inahakikiwa kabla ya kusaini.

9.11 Mapokezi ya Vifaa Visivyofanyiwa Ukaguzi Sh.2,315,756,038

Katika mwaka huu wa ukaguzi, jumla ya taasisi tisa (9) zilifanya manunuzi ya vifaa vyenye thamani ya Sh. 2,315,756,038 bila ya kukaguliwa na kupokelewa kinyume na Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 ambayo inaelekeza kuwa manunuzi yote yanayofanywa na taasisi yanapaswa kukaguliwa ili kuweza kubaini kama yamefikia vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba. Vile vile, Kanuni ya 245 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inamtaka Afisa Masuuli kuteua Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya vifaa ambayo itawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea pindi zinaponunuliwa kutoka kwa Wazabuni. Katika kuangalia utekelezaji wa Sheria hii, nilibaini kuwa taasisi za Serikali Kuu tisa (9) kati ya 122 zilizokaguliwa ukaguzi wa ubora wa vifaa venye thamani ya Sh. 2,315,756,038 haukufanyika. Katika sehemu nyingine, Maafisa Masuuli hawakuunda Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya Vifaa ambavyo ina wajibu wa kukagua, kuthibitisha ubora wa huduma na vifaa vilivyopokelewa kutoka kwa watoa huduma. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali 69: Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa Ukaguzi

Na	Maelezo	Kiasi(Sh)
1	**Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**	
	Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya vifaa haikuteuliwa na Afisa Masuuli	1,579,144,248
2	**Fungu 83: Sekretarieti ya Mkoa Shinyanga**	
	Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi	32,381,848
3	**Fungu 38: Jeshi la Wananchi wa Tanzania**	
	Manunuzi ya vifaa vya ujenzi IKOLA-Det bila ya kufanyiwa ukaguzi	78,408,000
4	**Fungu 14: Idara ya Zimamoto na Uokoaji**	
	Manunuzi ya sare bila ya kufanyiwa ukaguzi.	70,387,000
5	**Fungu 70: Sekretarieti ya Mkoa Arusha**	
	Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa ukaguzi	8,000,000
6	**Fungu 75: Sekretarieti ya Mkoa Kilimanjaro**	
	Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa ukaguzi	51,393,887
7	**Fungu 86: Sekretarieti ya Mkoa Tanga**	
	Mapungufu yaliyobainika kwenye ununuzi wa Gari la Wagonjwa.	17,818,148
8	**Fungu 93: Idara Uhamiaji**	
	Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya vifaa haikuteuliwa na Afisa Masuuli	417,323,907
9	**Fungu 78:Sekretarieti ya Mkoa Mbeya**	
	Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa ukaguzi	60,899,000
Jumla		**2,315,756,038**

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2015/2016

Nimebaini kuendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa katika uzingatiaji wa sheria hii ambapo, jumla ya Taasisi za Serikali Kuu kumi na sita (16) zilifanya manunuz yenye thamani ya Sh. 15,361,328,135 katika mwaka wa Ukaguzi uliopita bila ya kufanyiwa ukaguzi.

Kupokea vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na Kamati ya Ukaguzi, Mapokezi ya Vifaa na Huduma kunaweza kukatoa fursa kwa taasisi za umma kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango vya ubora au zisizofuata mahitaji muhimu ya Manunuzi.

Ili kuweza kukabiliana na matukio ya ukiukwaji wa Sheria za Manunuzi katika Taasisi za Serikali Kuu, Nazishauri Wizara, Idara Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuzingatia kikamilifu sheria ya Manunuzi ya Umma.

9.12 Vifaa na Huduma Zilizolipiwa Hazikupokelewa Sh. 3, 452,112,838

Katika Taasisi za Serikali Kuu nane (8) nilizokagua, nilibaini manunuzi ya vifaa na huduma yenye thamani ya Sh. 3,452,112,838 viliyoagizwa na kulipiwa lakini havikupokelewa; hivyo, thamani ya fedha haikupatikana. Bila ya kupata thamani ya fedha zilizotumika, manunuzi yatahesabika kama yamepotea. Hii ni kinyume na Makubaliano ya Mikataba kati ya Wazabuni na Taasisi za Manunuzi ambayo inataka malipo kufanyika baada cheti cha kazi kutolewa, bidhaa kuletwa au huduma kutolewa. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye Jedwali hapo chini.

Jedwali 70: Vifaa na huduma zilizolipiwa hazikupokelewa

Na	Maelezo	Kiasi (Sh)
1	**Fungu 36: Sekretarieti ya Mkoa Katavi**	
	Malipo ya awali kwa ajili ya bidhaa na huduma lakini havijapokelewa.	585,354,650
2	**Fungu 14: Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.**	
	Vipuri vilivyoagizwa havijapokelea	54,506,998
3	**Fungu 28: Jeshi la Polisi**	
	Malipo kwa Mzabuni M/S GIVA Justice System Ltd kwa ajili ya kuleta na kufunga mfumo wa taarifa kwa waliokamatwa na kuwekwa kizuizini lakini kazi haikufanyika.	798,789,242
4	**Fungu 40: Mahakama**	
	Malipo yamefanyika lakini magari manne hayakupokelewa	572,579,293

Na	Maelezo	Kiasi (Sh)
5	**Fungu 46: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**	
	Malipo yamefanyika lakini magari matano hayakupokelewa	360,221,920
6	**Fungu 99: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**	
	Malipo kwa ajili ya ujenzi wa malambo mkoa wa Mbeya lakini hayajajengwa.	561,660,735
7	**Fungu 99: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**	
	Malipo yamefanyika lakini magari hayakupokelewa	83,000,000
8	**Fungu 93:Idara ya Uhamiaji**	
	Malipo yamefanyika lakini magari hayakupokelewa	436,000,000
Jumla		**3,452,112,838**

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2015/2016

Ikilinganishwa na mwaka wa Ukaguzi 2014/2015, Taasisi za Serikali Kuu zilizobainika na mapungufu haya zimeongezaka kwa asilimia 100% kutoka Taasisi nne(4) zilizoripotiwa mwaka 2014/2015 hadi Taasisi nane(8) zilizoripotiwa mwaka huu. Hata hivyo kiasi kiliongezeka kutoka Sh.3,253.65 milioni hadi Sh.3,452.84 milioni ikionyesha maboresho kidogo katika kufuata na sheria hii.

Nashauri kwamba menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu zinapaswa kufuatilia uletwaji wa vifaa vyote. Na inaposhindikana kuhakikisha, fedha zilizolipwa zirejeshwe kutoka kwa Wazabuni na Wakandarasi, na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale walioshindwa kuleta vifaa na huduma.

9.13 Taarifa ya PPRA-Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni Zake za 2013

Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) ni Mamlaka iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011. Mamlaka hii ina majukumu ya kudhibiti na kusimamia manunuzi yote yanayofanywa na Taasisi za Serikali.

Malengo ya Mamlaka ni pamoja na kufuatilia uzingatiaji wa Taasisi wa Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, kutobaguliwa na thamani ya fedha katika manunuzi.

Hapa chini yamebainishwa baadhi ya matokeo ya Ukaguzi kutoka katika Ripoti ya PPRA, ya Tathimini ya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ambayo nimeona ni muhimu kujumuishwa katika Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka huu.

9.14 Matokeo ya Ukaguzi ya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi

Mamlaka ilifanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi kwa kutumia vigezo saba kama ifuatavyo; Kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi na utendaji kazi wake, kuandaa na kutekeleza Mpango wa Manunuzi wa mwaka, usahihi katika mchakato wa Zabuni, usimamizi wa Mikataba, Utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi, kutumia mifumo iliyoanzishwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma; ufuatiliaji wa Malalamiko.

9.14.1 Kiasi cha manunuzi yaliyokaguliwa

Idadi ya Mikataba ya Manunuzi iliyokaguliwa ilikuwa Ishirini na Moja Elfu, mia tatu kumi na mitatu (21,313) yenye thamani ya Sh. 1,051.78 bilioni. Ukaguzi ulijumuisha mikataba ya kazi mia nane arobaini na mitano (845) yenye thamani ya Sh. 698.67 bilioni sawa na asilimia 66.4% ya thamani yote, Mikataba ya bidhaa elfu saba mia moja sabini na Tisa (7179) yenye thamani ya Sh. 158.89 bilioni au 15.1% na mikataba ya huduma ya Ushauri mia moja na tatu (103) yenye thamani ya Sh. 100.28 bilioni sawa na asilimia 9.5%

9.14.1 Viwango vya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi

Uchambuzi ulionesha kuwa wastani wa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ulikuwa wa kiwango cha asilimia 71% sawa na ongezeko la asilimia mbili juu ya wastani wa mwaka jana. Hata hivyo, wastani huu ulikuwa chini ya lengo la 2015/2016 la asilimia 78%. Wastani wa uzingatiaji wa sheria kwa Taasisi za Serikali umeongezaka toka asilimia 69 ya mwaka jana hadi asilimia 75 ya mwaka huu.

Uchambuzi unaonesha vilevile kuwa Wizara, Wakala na Idara za Serikali zilizingatia kwa kiwango kinachoridhisha kwenye kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi na utendaji kazi wake (80%). Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Manunuzi wa mwaka (78%). Taasisi za Serikali kuu zilifanya kwa kiwango kinachoridhisha katika kigezo cha Zabuni kufuata utaratibu. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalifanyika chini ya kiwango kilichowekwa usimamizi na utekelezaji wa mikataba na utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi. Uchambuzi unaonesha pia Taasisi za Serikali Kuu zilifanya vibaya katika utekelezaji wa mifumo ya manunuzi iliyoandaliwa na PPRA (52%)

9.13.3 Tathimini ya Viashiria vya Rushwa

Katika ukaguzi wa tathimini ya uzingatiaji sheria,kiwango cha uwezekano wa kuwapo kwa rushwa katika Mikataba kiliweza kubainishwa. Taasisi zilizopata asilimia 20% na zaidi katika viashiria vya rushwa zilikisiwa kuwa na rushwa. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali 71: Tathimini ya Viashiria vya Rushwa.

Taasisi	Awamu kabla ya Zabuni (%)	Awamua ya Tathimini na kutoa Zabuni (%)	Awamu ya Usimamizi wa Mkataba (%)	Wastani (%)
Wizara ya Maji na Umwagiliaji	18	23	27	23
Makumbusho ya Taifa	22	25	45	30
Wakala wa Usafiri wa Mwendokasi Dar es Salaam	21.32	25.59	29.57	25.91
Bunge	28.56	36.74	15	27.96

9.14.4 Mfumo wa Utunzaji wa Taarifa za Manunuzi Kielekroniki (PIMS)

Mfumo wa Utunzaji wa taarifa za Manunuzi kielekroniki hurahisisha uwasilishaji wa taarifa za Manunuzi kwa njia ya Mtandao PPRA. Katika kipindi hiki, Mfumo huu umeboreshwa kwa kujumuisha vitu vipya na matakwa ya kisheria. Ili kuweza kuhakikisha kuwa Mfumo huu unaenezwa, mafunzo mbalimbali yalifanyika Mkoani Dodoma kwa Maafisa 194 kutoka Taasisi 129 za Serikali Kuu.

9.14.5 Uchunguzi wa Tuhuma, Malalamiko pamoja na Taarifa Zinazowasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti na Manunuzi ya Umma kutokana na Manunuzi yenye Mapungufu

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinatoa Mamlaka kwa PPRA kufanya uchunguzi inapotokea tuhuma za Manunuzi yenye mapungufu. Uchunguzi unaweza kufanywa na PPRA kwa kutumia juhudi binafsi au kupitia tuhuma zilizowasilishwa kwa Mamlaka. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka ya Manunuzi na Udhibiti wa Umma ilifanya chunguzi katika taasisi zifuatazo kama ilivyooredheshwa kwenye **Kiambatisho 9.5** kwenye ripoti hii.

9.15 Mapungufu katika Manunuzi na utunzaji wa bohari/ stoo kama yalivyoanishwa kwenye taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki Mali za Serikali

Ikiwa ni sehemu ya majukumu yangu nimepokea taarifa ya Mhakiki Mali na kujumuisha katika taarifa yangu ya ukaguzi ya mwaka huu kama Kanuni 239-249 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka, 2001 ambayo inamtaka Mhakiki Mali kuwasilisha nakala moja ya taarifa ya uhakiki mali kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kumbukumbu zake. Mapungufu yaliyobainika katika taarifa ya Mhakiki Mali yameorodheshwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali 72: Mapungufu yaliyobainika katika taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki mali za Serikali

Na	Hoja	Kiasi(Sh)
1	Bakaa ya vifaa isiyohamishwa	137,802,887.00
2	Mapokezi ya vifaa vya bohari bila maelezo	856,933,936.50
3	Ugawaji wa vifaa usio na nyaraka za kutosha	257,348,998.81

Na	Hoja	Kiasi(Sh)
4	Samani na vifaa visivyoingizwa kwenye daftari la Mali.	368,321,500.00
5	Vifaa vilivyobakia kwa mkopo	47,633,200.00
6	Vifaa vilivyopokelewa bila kuhakikiwa	590,402,748.00
7	Ugawaji wa vifaa bila kuingizwa katika leja ya vifaa	183,261,210.18
8	Mafuta yasiyoingizwa kwenye daftari la bohari	290,349,957.56
9	Vifaa vilivyotolewa bohari bila ya kuingizwa kwenye vitabu.	324,894,074.25
10	Vifaa vyenye mapungufu	124,757,015.00
11	Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani	29,288,569.00
12	Vifaa visivyopokelewa	250,170,472.00
13	Manunuzi ya vifaa vya bohari bila kutolewa maelezo	2,770,444,669.77
14	Mafuta yasiyoingizwa kwenye daftari la kuratibu safari za gari	310,191,721.20
15	Matengenezo ya magari yasiyoidhinishwa na TEMESA	11,223,428.00
16	Uhamishaji wa mali bila idhini	665,000,000.00
17	Manunuzi ya Vifaa yenye mashaka	2,140,000.00
18	Mafuta yaliyoidhinishwa kutoka bohari yenye mashaka	1,815,000.00
19	Vifaa visivyotumika Bohari kwa muda mrefu.	544,334,450.00
20	Miradi isiyofanya kazi	212,980,149.24
21	Malipo yasiyokuwa na risiti.	92,652,211.00
22	Vifaa kutolewa bohari bila utaratibu	102,389,050.00
23	Upotevu wa vifaa vya bohari	865,000.00
24	Mahindi yaliyokwisha muda wake kabla ya kutumika	4,152,984,500.00
25	Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni	64,622,408.77
Jumla Kuu		**12,392,807,156**

Chanzo: Taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki mali za Serikali ya 2015/16

Kwa maelezo zaidi kuhusu Wizara/Idara na Sektretarieti za Mikoa zilizohusika, angalia **Kiambatisho 9.6**

Ninapendekeza kuwa, Maafisa Masuuli waimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani katika Manunuzi ili vifaa na mafuta yanayonunuliwa yaweze kuingizwa kwenye vitabu vya stoo.

USIMAMIZI WA MATUMIZI

10.1 Utangulizi

Sura hii inahusisha matokeo niliyobaini katika ukaguzi wa matumizi ya fedha yaliyofanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Balozi na Sekretarieti za Mikoa (RSs) katika mwaka wa fedha 2015/2016. Muhtasari wa matokeo muhimu ya Ukaguzi na Mapendekezo niliyoyatoa ni kama ifuatavyo:

10.2 Matumizi Yasiyokuwa na Manufaa - Shilingi 1,460,570,913

Ukaguzi wa hati za malipo na viambatisho vyake ulibaini kuwa Taasisi sita (6) zilifanya malipo kiasi cha Shilingi 1,460,570,913 ambayo yalifujwa na hayakuwa na manufaa yoyote kwa Serikali; ambapo, hasara hiyo ingeepukwa laiti hatua stahiki zingefuatwa kwa umakini kabla matumizi hayo kufanyika kama inavyoainisha katika Kanuni 21 ya Kanuni za Fedha, 2001. Jedwali lenye Taasisi zilizolipa malipo yasiyokuwa na manufaa linaonekana kwenye **Kiambatisho 10.1**

Ulinganisho na mwenendo wa Taasisi zilizofanya malipo yasiokuwa na manufaa kwa miaka minne iliyopita:

Kielelezo 16: Mwenendo wa miaka minne (4) wa malipo yasiyokuwa na manufaa



Ulinganisho kwenye chati hapo juu unaonesha kupungua kwa malipo yasiyokuwa na manufaa kutoka Shilingi Bilioni 53.017 kwa mwaka 2014/2015 hadi Shiling bilioni 1.461 kwa mwaka huu 2015/2016. Pia, idadi ya Taasisi zilizohusika zimepungua kutoka 8 hadi 6 mwaka huu. Pia, mwenendo kwa ujumla kwa miaka minne iliyopita unaonesha kupungu kwa tatizo hili hivyo kuashiria kuimarika kwa udhibiti wa ndani na umakini kabla ya malipo kufanyika. Ninapendekeza kuwa Manejimenti za Wizara husika & Sekretarieti za Mikoa waimarishe mifumo yao ya udhibiti wa ndani kukabili changamoto hii.

10.3 Hasara iliyotokana na makato ya NHIF yaliyokataliwa- Shilingi 569,994,807

Katika kupitia madai ya Hospitali za Serikali wanayoidai NHIF yatokanayo na huduma za matibabu walizowapatia wanachama wa Mfuko huo nilibaini kuwa, Mfuko huo aidha ulipunguza au uliyakataa kuyalipa madai ya kiasi cha Shilingi 569,994,807 kwa mujibu wa Kanuni ya 27(2) ya Sheria ya NHIF ya Mwaka 1999 kutokana na hospitali husika za Serikali kukiuka bila sababu za msingi taratibu, Kanuni, sheria na mikataba walioingia, hivyo kwa kushindwa kurejeshewa fedha hizo kumesababisha hospitali hizo kupata hiyo hasara.

Kwa sehemu kubwa mapungufu yametokana na ujazwaji fomu za NHIF zikiwa na mapungufu kama vile kukosekana kwa sahihi za daktari ama mgonjwa, kukosekana kwa taarifa ya uchunguzi wa kitabibu na matibabu yaliyotolewa, utoaji tiba na dawa zilizo nje ya wigo ulioruhusiwa na NHIF, utoaji wa huduma kwa wagonjwa ambao uanachama wao umekoma, madai zaidi ya mara mbili, idadi isiyo sahihi ya siku za kulazwa, kukosekana kwa maelezo sahihi ya tiba zilizotolewa n.k. Taasisi zilizokutwa na mapungufu hayo ni kama jedwali linavyoonesha hapa chini:

Jedwali 1: Taasisi zenye madai yaliyokataliwa na NHIF

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu 52)	348,290,003

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
2	72	Sekretarieti ya Mkoa - Dodoma	115,888,673
3	73	Sekretarieti ya Mkoa - Iringa	11,802,653
4	87	Sekretarieti ya Mkoa - Kagera	10,905,918
5	77	Sekretarieti ya Mkoa - Mara	4,416,430
6	85	Sekretarieti ya Mkoa - Tabora	9,925,289
7	70	Sekretarieti ya Mkoa - Arusha	39,448,225
8	75	Sekretarieti ya Mkoa - Kilimanjaro	5,847,762
9	86	Sekretarieti ya Mkoa - Tanga	2,239,075
10	84	Sekretarieti ya Mkoa - Singida	21,230,779
		Jumla	**569,994,807**

***Chanzo**: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016*

Jedwali la hapo juu linaonesha Taasisi zenye kiwango kikubwa cha hasara ya shilingi milioni 348.29 ni Wizara ya Afya (Fungu 52) huku Sekretarieti ya Mkoa-Tanga ikwa na kiasi cha chini cha Shilingi 2,239,075 kilichokataliwa.

Maoni yangu ni kwamba, endapo hatua mahususi za kurekebisha kasoro hizi hazitatatuliwa, hospitali hizi zitaelemewa na mzigo mkubwa wa hasara ya gharama za kutibu wanachama wa Mfuko wa NHIF bila mfuko huo kuzirejesha fedha hizo.

Nazishauri Wizara zinazohusika kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa NHIF, kuwa katika hospitali zote kubwa za Serikali kuwe na angalau mtumishi mmoja wa NHIF ambaye pamoja na majukumu mengine, atakuwa akisimamia utekelezaji wa udhibiti wa ndani na pamoja na kuzikagua na kuhakiki uanachama na kuhakikisha kuwa fomu zimekidhi viwango kabla ya matibabu kutolewa.

10.4 Malipo Yaliyokosa Mchanganuo wa Matumizi-Shilingi 6,575,397,008

Kanuni ya 116 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inahitaji malipo yote yafanyike kwenye hati za malipo zikiwa na viambatisho vinavyokidhi na vyenye maelezo yakutosha kuhusu jinsi gani fedha zimetumika. Hii ni katika kuhakikisha Maafisa wanawajibika ipasavyo katika kutekeleza na kukamilisha majukumu yao.

Nilibaini wakati wa ukaguzi kuwa takriban Taasisi Nne (4) zilifanya malipo ya kiasi cha Shilingi 6,575,397,008 ambayo yanakosa viambatisho na mchanganuo namna yalivyotumika; hivyo, kunizuia kujiridhisha kujua kama zimetumika kwa tija na manufaa ya malengo yaliyokusudiwa. Orodha ya Taasisi zilizofanya matumizi yasiyo na mchanganuo wa matumizi na aina ya matumizi husika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 10.2**

Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unakuwepo, ninapendekeza Menejimenti za Taasisi husika kuhakikisha kuwa zinawasilisha mchanganuo wa matumizi ya kiasi cha Shilingi 6,575,397,008.

10.5 Malipo Yaliyolipwa Zaidi Ya Kiwango Stahiki-Shilingi 77,480,956

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu 2015/16, nilibaini malipo ya kiasi cha Shilingi Shilingi 77,480,956 yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki yakihusisha Taasisi nne (4) za Serikali kuu. Fedha zilizolipwa zaidi ya kiasi kinachostahili au kwa kazi ambazo hazijafanyika zinasababisha kutofanikisha kwa shughuli nyingine zenye manufaa kwa Umma. Malipo zaidi ya kiasi kilichostahili ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapa chini:

Jedwali 73: Taasisi zilizolipa zaidi ya malipo ya stahiki

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi(Shilingi)
1	82	Sekretarieti ya Mkoa-Ruvuma	12,090,000
2	95	Sekretarieti ya Mkoa-Manyara	2,410,861
3	86	Sekretarieti ya Mkoa-Tanga	58,130,095
4	14	Kikosi Cha Zimamoto	4,850,000
		Jumla	**77,480,956**

Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa Taasisi yenye kiwango kikubwa cha malipo zaidi ya kiwango stahiki ni Sekretarieti Mkoa-Tanga cha Shilingi 58,130,095 na ya yenye kiasi kidogo

ikiwa ni Sekretariet ya Mkoa-Manyara yenye Shilingi 2,410,861 zikiwa zimelipwa zaidi ya kiwango stahiki.

Chati inayoonesha Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki kwa miaka sita (6) iliyopita ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo hapa chini:

Kielelezo 17: Mwenendo wa miaka sita (6) wa malipo zaidi ya Stahiki



***Chanzo**: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Chati ya hapo juu inaonesha kuwa ikilinganishwa na mwaka jana, kiasi cha malipo zaidi ya kiwango stahiki kwa mwaka huu 2015/2016 kimeshuka hadi Shilingi Milioni 77.481 ikilinganishwa na Shilingi Milioni 373.842 za mwaka jana. Aidha, mstari wenye doti unaonesha kuwa mwenendo kwa miaka sita iliyopita unaonekana kupungua. Nashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi zilizohusika waendelee kuimarisha udhibiti wa ndani ili kupunguza mianya inayosababisha tatizo hili. Pia, nawasihi Maafisa Masuuli kufuatilia kurejeshwa kwa malipo hayo yaliyolipwa zaidi ya kiwango.

10.6 Kukosekana kwa Hati za Malipo Shilingi 91,347,958,833

Katika mwaka huu wa fedha 2015/16, Taasisi takriban nane (8) zilishindwa kuwasilisha hati za malipo na nyaraka zake za kiasi cha Shilingi 91,347,958,833 kinyume na Kanuni 43 ya PAR, 2009 inayosema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na mamlaka isiyo na mipaka ya kupata na kuhifadhi taarifa kutoka kwa mtu yoyote, mamlaka yoyote au chombo chochote wakati ambapo kwa maoni yake taarifa hizo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.". Pia, kwa mujibu wa Kif. 47(1)(b) cha PAA, 2008 Afisa wa umma anatenda kosa kisheria kama atashindwa kutoa taarifa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu aliyeidhinishwa naye kama alivyoihitaji. Jedwali lifuatalo linaonesha Taasisi ambazo zimeshindwa kuwasilisha hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi:

Jedwali 74: Taasisi zenye malipo yasiyo na hati za malipo

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57)	91,261,040,310
2	94	Tume ya Utumishi wa Umma	11,740,377
3	36	Sekretarieti ya Mkoa- Katavi	2,666,933
4	89	Sekretarieti ya Mkoa- Rukwa	5,930,000
5	93	Idara ya Uhamiaji	38,418,826
6	71	Sekretarieti ya Mkoa- Pwani	8,093,866
7	88	Sekretarieti ya Mkoa-Dar es Salaam	9,403,521
8	61	Tume ya Uchaguzi	10,665,000
		Jumla	**91,347,958,833**

Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016

Kukosekana kwa hati za malipo na viambatisho vyake, kulisababisha kutoweza kubaini uhalali, uhalisia, aina na madhumuni ya matumizi hayo ya kiasi cha Shilingi 91,347,958,833. Kwa maoni yangu kitendo hiki kinaashiria kuzuia mawanda ya ukaguzi na kinaweza kusababisha kufanyika udanganyifu aidha fedha hizo zaweza kutumika kinyume cha sheria ama kufujwa.

Mwenendo wa matokeo ya malipo yasiyokuwa na viambatisho vya kutosha kwa kipindi cha miaka sita (6) yameainishwa hapa chini kwa ulinganisho:

Kielelezo 18: Kielelezo kifuatacho kinaonesha mwenendo wa malipo ambayo Hati zake za Malipo zilikosekana na Taasisi zake:



	2010-11	2011-12	2012-13	2013-14	2014-15	2015/16
TZS Milioni	1,788.64	922.97	70.20	125.16	361.79	91,347.9
Idadi ya Taasisi	3	2	3	4	6	8

***Chanzo**: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kutokana na kielelezo cha hapo juu, ikilinganishwa na mwaka jana, mwenendo unaonesha kuwa tatizo la hati za malipo kukosekana limeongezeka kutoka shilingi milioni. 361.8 kwa mwaka 2014/2015 hadi shilingi bilioni. 91.348 kwa mwaka huu 2015/2016. Pia, idadi ya Taasisi zenye mapungufu hayo zimeongezeka kutoka sita(6) hadi nane (8) kwa mfuatano huo. Aidha, mwenendo kwa ujumla kwa miaka sita (6) iliyopita ambao unaoneshwa kwa mstari wenye nuktanukta unabainisha kuwa udhibiti wa tatizo hili ulidhibitiwa kati ya mwaka 2014 hadi 2013, Ilipofika Mwaka wa fedha 2014/2015 hali imekuwa ya kutoridhisha.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 18(1)(f) & (2) ya PFR, 2001 kukosekana kwa hati za malipo ni sawa na hasara ya upotevu wa fedha. Hivyo itampasa Mhasibu Mkuu wa Serikali kuorodhesha malipo hayo kwenye Taarifa ya Hasara ya mwaka ili yachunguzwe kwa kina na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Nilitoa wito kwa Menejimenti za Taasisi husika kuziwasilisha hati za malipo zilizokosekana kwa ajili ya ukaguzi, ambapo kushindwa kufanya hivyo, hatua stahiki lazima zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake kutokana na kutangaza kupatikana kwa hasara inayofikia shilingi 91,347,958,833. Aidha, hatua za kufidia hasara hiyo

lazima zichukuliwe kwa mujibu wa Kanuni 24 ya Kanuni za Fedha, 2001 kutoka kwa maafisa waliohusika kusababisha

10.7 Fedha Kutumika kwa Shughuli Zisizokusudiwa Shilingi 3,830,032,676

Licha ya mapendekezo ninayoyatoa kila mwaka kupitia ripoti zangu zilizopita, bado kumekuwepo na malipo yaliyofanyika kwa shughuli zisizokusudiwa kinyume na Kanuni 115 ya PFR, 2001 ambayo inahitaji fedha kutumika kwa mujibu wa bajeti na madhumuni yaliyokusudiwa. Katika ukaguzi nilioufanya, nimebaini Taasisi takriban kumi na mbili (12) zimefanya malipo kwa shughuli zisizokuwemo katika bajeti iliyoidhinishwa yenye thamani ya Shilingi 3,830,032,676; ambapo matokeo yake, malengo yaliyokusudiwa, yamkini, hayakufikiwa. Taasisi zilizohusika ni kama zinavyoonesha kwenye **Kiambatisho 10.3**

Chati inayoonesha Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki kwa miaka mine (4) iliyopita ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo hapa chini:

Kielelezo 19: Chati ya ulinganifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka minne (4) iliyopita :



***Chanzo*:** *Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kutoka kwenye kielelezo hapo juu, inaonekana kuwa malipo kwa shughuli zisizokusudiwa yameongezeka kwa kiasi cha

Shilingi Milioni 2,041.151 ikilinganishwa na mwaka jana 2014/2015.

Menejimenti za Taasisi husika zinashauriwa kujiepusha kufanya malipo tofauti na madhumuni yaliyokusudiwa. Pia, nashuri kuimarishwa kwa mfumo wa udhibiti wa matumizi kwa mujibu wa bajeti kuanzia maandalizi yake hadi utekelezaji wake, ukiukwaji wowote utambuliwe na ushughulikiwe ipasavyo.

10.8 Hati za Malipo Zenye Nyaraka Pungufu Shilingi 12,504,754,476

Licha ya mapendekezo ninayoyatoa kila mwaka katika ripoti zangu zilizopita, ukaguzi wa hati za malipo umebaini kuwa Taasisi 29 zimeendelea kufanya malipo yenye jumla ya Shilingi 12,504,745,476 ambayo yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Kanuni 86 (1) ya Kanuni za Fedha, 2001; pia Kanuni 95 (4) & 18 (f) ya Kanuni za Fedha, 2001. Nyaraka za viambatisho zikikosekana inakuwa vigumu kuthibitisha pasipo shaka uhalali wa malipo hayo hivyo, kufanya mawanda ya ukaguzi kuwa finyu. Angalia **Kiambatisho 10.4.**

Muhtasari wa miaka sita (6) wa mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu ni kama inavyoonekana katika Kielelezo hapa chini:

Kielelezo 20: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu



***Chanzo**: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Ikilinganishwa na mwaka jana, chati ya hapo juu inaonesha kuwa kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 kiasi cha malipo yaliyo na nyaraka pungufu kimeongezeka kufikia shilingi bilioni. 12.505. toka shilingi bilioni 11.315 kwa mwaka uliopita 2014/2015 ambapo Taasisi zilizohusika na tatizo hili zimepungua kutoka 30 mwaka jana hadi 29 kwa mwaka huu. Mstari wenye doti unaonyesha kuwa kiasi kinachohusisha tatizo hili kinaongezeka. Hali hii inaonyesha kwamba, viongozi wenye dhamana hawajaweka mfumo thabiti wa udhbiti wa ndani wa kukabiliana na udhaifu uliopo.

10.9 Malipo Yaliyofanyika bila Kudai Risiti za Kielektroniki (EFD) Shilingi 7,790,299,407

Katika mwaka huu mwa fedha 2015/2016, Taasisi 39 zilifanya malipo ya kiasi cha Shilingi 7,790,299,407 bila Taasisi husika kudai stakabadhi za kieletroniki (EFD) kinyume na Kanuni 28(1) ya Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Mashine za Stakabadhi za Kielektroniki) ya mwaka 2012.

Aidha, kwa kutokudai stakabadhi hizo za kielektroniki kunamaanisha kuwa Taasisi hizo za Serikali zinawasaidia wafanyabiashara kukwepa kodi, na hivyo, kuisababishia Serikali hasara kwa kupoteza sehemu kubwa ya mapato ya kodi kila mwaka.

Taasisi zilizofanya malipo ya jumla ya Shilingi 7,790,299,407 kwa wauzaji wa bidhaa na huduma mbalimbali bila kudai Risiti za EFD na kiasi cha malipo kwa kila Taasisi ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho 10. 5**

Kielelezo 21: Mwenendo wa Kukosekana kwa EFD Stakabadhi kwa miaka minne (4)



***Chanzo**: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kwa mujibu wa kielelezo cha hapo juu, malipo yaliyokosa stakabadhi za kielektroniki yameongezeka kutoka shilingi bilioni 6.19 kwa mwaka 2014/2015 hadi Shilingi Bilioni 7.79 kwa mwaka huu 2015/2016.

Nashauri Serikali iendelee kutoa elimu juu ya utekelezaji wa hiari wa Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Electronic Fiscal Devices) za mwaka, 2012 kuhusu matumizi ya hiari ya mashine za EFD zitakazochangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya Serikali kama kila Manunuzi ya Serikali yataambatana na Stakabadhi.

Pia, ninapendekeza kwamba, Serikali isiendelee kufanya biashara na Wazabuni ambao hawatumii mashine EFD na kutoa Stakabadhi za kielektroniki.

10.10 Malipo katika Vifungu vya Bajeti Visivyostahili Shilingi 4,580,215,827

Katika kipindi cha ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini kuwa, Taasisi zipatazo 16 ambazo zilifanya malipo kinyume na vifungu vya bajeti hivyo kukiuka Kanuni 51 (1-8) Kanuni za

Fedha za Umma za mwaka 2001. Malipo yaliyofanywa na Taasisi hizo ambayo yalilipiwa kwa kutumia vifungu vya matumizi tofauti na vilivyoidhinishwa bila kupata idhini stahiki ya Mamlaka husika ni jumla ya shilingi 4,580,215,827.

Kitendo hicho kinaonesha kuwa Menejimenti za Taasisi zilizooneshwa katika jedwali la hapa chini zimeweka udhibiti usioridhisha unaosababisha kukosekana kwa nidhamu ya kufanya malipo na matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa:

Jedwali 75: Orodha ya Taasisi zilizolipa katika vifungu vya bajeti visivyostahili

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (Fungu 34)	43,155,259
2	9	Ofisi ya Rais-Bodi ya Mishahara	11,308,500
3	32	Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32)	17, 578,000
4	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	10,704,569
5	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	3,323,755,320
6	92	Tume ya Kudhibiti UKIMWI	2,280,678
7	49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji (Fungu 49)	63,720,000
8	62	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 62)	249,987,284
9	73	Sekretarieti ya Mkoa-Iringa	4,610,000
10	36	Sekretarieti ya Mkoa- Katavi	21,553,520
11	25	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	7,860,000
12	70	Sekretarieti ya Mkoa- Arusha	31,422,566
13	14	Kikosi cha Zimamoto	84,984,410
14	48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na	

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
		Maendeleo ya Makazi	701,598,893
15	71	Sekretarieti ya Mkoa- Pwani	6,974,837
16	84	Sekretarieti ya Mkoa- Singida	16,299,992
			4,580,215,827

Chanzo*: *Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016

Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili ni matumizi ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Mwenendo wa matumizi hayo kwa miaka sita ni kama inavyoonekana hapa chini:

Mwenendo wa Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili kwa miaka sita (6) ni kama inavyoonekana hapa chini:

Kielelezo 22: Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili



Chanzo*: *Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita

Kiwango cha malipo ya matumizi nje ya vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 kimeongezeka maradufu kutoka shilingi milioni. 887.012 (ikihusisha Taasisi 12) hadi shilingi bilioni. 4.580 (ikihusisha Taasisi 16). Ninashauri Maafisa Masuuli katika siku zijazo kujiepusha na kufanya matumizi nje ya vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa. Endapo italazimu, basi nashauri uhamisho wa fedha kutoka fungu moja kwenda lingine upate idhini ya Mamlaka husika kwa mujibu wa Kanuni 41 ya Sheria ya Bajeti, 2015.

10.11 Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa-Shilingi 4,997,961,964

Ukaguzi nilioufanya umebaini kuwa Taasisi takribani kumi na tano (15) za Serikali Kuu zilifanya matumizi ya kiasi cha Shilingi 4,997,961,964 kugharamia shughuli mbalimbali ambazo zilikuwa nje ya bajeti iliyoidhinishwa kinyume na Kanuni 46(3) ya PFR, 2001. Utendaji huu usipodhibitiwa, unaweza kuathiri shughuli zilizokusudiwa kutokutekelezwa kama ilivyoidhinishwa kwenye bajeti za Taasisi husika.

Jedwali la hapa chini linaonesha Taasisi zilizohusika kufanya malipo nje ya bajeti iliyoodhinishwa:

Jedwali 76: Taasisi zilizofanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa

Na.	Fungu Na.	Jina la Taasisi	Kiasi(Shilingi)
1	81	Sekretarieti ya Mkoa-Mwanza	28,181,300
2	36	Sekretarieti ya Mkoa- Katavi	8,082,800
3	2006	Ubalozi wa Tanzania-London	1,983,531,601
4	2007	Ubalozi wa Tanzania-Lusaka	22,563,990
5	2021	Ubalozi wa Tanzania-Kampala	23,892,131
6	2004	Ubalozi wa Tanzania-Kinshasa	125,903,056
7	2032	Ubalozi wa Tanzania-Kuala Lumpur	99,670,868
8	2010	Ubalozi wa Tanzania-New Delh	76,023,783
9	70	Sekretarieti ya Mkoa- Arusha	61,846,518
10	2005	Ubalozi wa Tanzania-Abuja	32,897,631
11	2003	Ubalozi wa Tanzania-Cairo	180,471,374
12	2016	Ubalozi wa Tanzania-Stockholm	1,329,740,344
13	2033	Ubalozi wa Tanzania-Hague	143,669,276
14	2011	Ubalozi wa Tanzania-New York	297,659,486
15	2018	Ubalozi wa Tanzania – Washington DC	583,827,806
			4,997,961,964

Chanzo*: *Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016

Mwenendo wa malipo yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa miaka mitano (5) ni kama inavyoonesha katika Kielelezo hapa chini;

Kielelezo 23: Chati inayoonesha Mwenendo wa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyooidhinishwa



***Chanzo**: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Uchambuzi kutokana na kielelezo hapo juu, unaonesha kwamba, idadi ya Taasisi za Serikali Kuu zilizofanya malipo nje ya bajeti kwa mwaka huu zimeongezeka kutoka kumi na tatu (13) mwaka jana 2014/2015 hadi kumi na tano (15) kwa mwaka huu 2015/2016. Aidha, kiasi kilichofanya malipo husika kimeongezeka kutoka Shilingi Bil. 1.298 kwa mwaka 2014/2015 hadi Shilingi Bil. 4.116 kwa mwaka huu 2015/2016 wa ukaguzi. Aidha, mwendendo kwa ujumla kwa miaka mitano iliyopita kwa wastani kiasi cha tatizo hili kimeanza kuongezeka (angalia mstari wenye nuktanukta)

Ninawasihi Maafisa Masuuli kudhibiti ufanyaji wa malipo ya bidhaa au huduma ambazo hazijaidhinishwa au kuzidi kiwango kilichoidhinishwa. Kwa anayekiuka, hatua kwa mujibu wa Kanuni 48 ya Kanuni za Fedha, 2001 hatua stahiki zichukuliwe kwa kiasi kilichotumika bila idhini.

10.12 Masurufu Yaliyokaa Muda Mrefu bila Kurejeshwa Shilingi 397,575,730

Kinyume na Kanuni 103 ya PFR, 2001 Taasisi zipatazo tisa (9) za Serikali Kuu zilifafanua malipo ya Masurufu yenye thamani ya Shilingi 397,575,730 ambayo hayakurejeshwa ndani ya muda stahiki baada ya shughuli husika kukamilika.

Masurufu yasiyorejesha kwa wakati yanaweza kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa. Taasisi za Serikali Kuu zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali 77 Taasisi zenye masurufu ya muda mrefu

Na.	Fungu.	Jina la Taasisi	Kiasi(Shilingi)
1	56	Ofisi ya Rais-TAMISEMI	30,092,000
2	57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57)	83,785,650
3	38	Ulinzi	28,930,000
4	28	Idara ya Polisi	140,618,330
5	40	Mahakama (Fungu 40)	21,523,000
6	89	Sekretarieti ya Mkoa-Rukwa	10,824,600
7	76	Sekretarieti ya Mkoa-Lindi	9,143,750
8	76	Sekretarieti ya Mkoa-Lindi	16,982,000
9	61	Tume ya Uchaguzi	55,676,400
			397,575,730

***Chanzo*:** *Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016*

Mwenendo wa miaka mitano wa masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ni kama inavyoonekana katika kielelezo cha hapa chini:

Kielelezo 24: Mwenendo wa Masurufu yasiyorejeshwa



Chanzo: *Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Ikilinganishwa na mwaka jana, chati ya hapo juu inaonesha kuwa kiasi cha masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa kimeongezeka kutoka Shilingi Mil. 232.695 kwa mwaka jana 2014/2015 hadi shilingi milioni. 397.576 kwa mwaka huu 2015/2016. Wakati huohuo, idadi ya Taasisi zilizohusika zimeongezeka kutoka 3 hadi 9 kwa mfuatano huo. Kwa ujumla, mstari wenye doti unaonesha kuwa mwenendo wa kiasi cha masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu kwa miaka sita (6) iliyopita unaonekana kuanza kuongezeka.

Nashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi zilizohusika kuendelea kuimarisha udhibiti wa ndani ili kupunguza mianya inayosababisha tatizo hili. Pia, nawasihi Maafisa Masuuli kufuatilia kurejeshwa kwa masurufu hayo yaliyokaa zaidi ya muda unaokubalika wa wiki mbili baada ya kukamilika shughuli husika vinginevyo masurufu hayo yarejeshwe kupitia mshahara wa mhusika kama Kanuni 103(2) ya PFR, 2001, inavyoagiza.

10.13 Malipo Yasiyokuwa na Stakabadhi za Mapokezi Shilingi 97,719,677

Uchunguzi wa Hati za malipo ulibaini kuwa malipo yenye thamani ya jumla ya Shilingi 97,719,677 ambayo yalifanywa na Taasisi 3 za Serikali Kuu hayakuwa na stakabadhi za kukiri

kupokelewa na walipwaji kwa mwaka huu wa ukaguzi. Hivyo sikuweza kuthibitisha kama malipo hayo yalilipwa kwa walengwa waliokusudiwa.

Kitendo tajwa hapo juu ni kinyume na Kanuni 93 (2) ya Kanuni za Fedha, 2001 ambayo inamtaka Mhasibu Mkuu kuhakikisha kuwa kila malipo yanayofanyika yanaambatishwa na stakabadhi ya kukiri kuyapokea. Maelezo yanayoonesha kiasi na Taasisi zinazohusika ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapa chini:

Jedwali 78: Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi(Shilingi)
1	43	Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika	18,357,433
2	68	Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Tecknolojia	8,242,320
3	80	Sekretarieti ya Mkoa- Mtwara	71,119,924
		Jumla	**97,719,677**

Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016

Chati inayoonesha mwenendo na ulinganisho wa miaka ya nyuma wa malipo yasiyoambatishwa na stakabadhi za kukiri mapokezi ni kama inavyoonekana hapa chini:



***Chanzo**: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016*

Kielelezo hapo juu kinaonesha kupungua kwa kiasi cha malipo yasiyoambatishwa na Stakabadhi kutoka shilingi milioni.

220.054 kwa mwaka 2014/2015 hadi shilingi milioni. 97.72 mwaka huu 2015/2016. Taasisi zilizohusika zimebakia kuwa tatu (3) kama mwaka wa fedha uliopita. Mwenendo kwa ujumla unaoneshwa na mstari wenye nuktanukta kuwa udhibiti wa tatizo hili umeimarika tangu mwaka 2014/2015.

Ningependa kuzikumbusha Menejimenti za Taasisi za Serikali Kuu zote kuwa ni jukumu lao la msingi kuhakikisha malipo yote yafanywayo yanaambatishwa na Stakabadhi za kukiri mapokezi.

10.14 Taasisi za Umma zisizotoza kodi ya Zuio-Shilingi 990,181,705

Katika mwaka huu wa fedha, nimebaini vitendo vya ukiukwaji wa matakwa ya Kif. 83(1) (b) cha Sheria ya Mapato, 2004 (Revised 2008) ya kutoza kodi ya zuio. Marekebisho ya Sheria yanazitaka Taasisi za Serikali kutoza kodi ya zuio ya asilimia 5 na 15 ya malipo kwa wauza bidhaa na watoa huduma wafayao biashara ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, mapitio ya hati za malipo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 yalibaini Kodi ya Zuio kiasi cha Shilingi 990,181,705 haikukatwa kama jedwali hapa chini linavyoonesha. Ukiukwaji huu unasababisha kuinyima Serikali mapato kwa ajili ya utoaji huduma na kuwaletea maendeleo Wananchi.

Jedwali 79: Taasisi ambazo hazikuwakata watoa huduma kodi ya zuio

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	9	Ofisi ya Rais-Bodi ya Mishahara	9,132,953
2	12	Tume ya sheria	10,809,000
3	91	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya	2,310,569
4	56	Ofisi ya Rais-TAMISEMI	13,199,425
5	38	Ulinzi	767,493,500
6	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	157,350,136
7	49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	15,435,945

Na.	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
8	75	Sekretarieti ya Mkoa-Kilimanjaro	6,862,591
9	61	Tume ya Uchaguzi	7,587,586
Jumla			**990,181,705**

***Chanzo**: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016*

Jedwali 80: Ulinganisho wa Taasisi na kiasi cha Kodi ya Zuio isiyokatwa kwa miaka miwili (2):

Financial Years	MDAs/RSs involved	Amount (Shilingi)
2015/16	9	**990,181,705**
2014/15	6	692,539,424

Chanzo: *Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti za Miaka iliyopita*

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa kuna ongezeko la kiasi cha kodi ya zuio kisichotozwa kutoka Shilingi Mil. 692.54 kwa mwaka 2014/2015 hadi Shilingi Mil. 992.4 kwa mwaka huu 2015/2016.

Ninazikumbusha Menejimenti za Taasisi zinazohusika kuhakikisha zinatekeleza matakwa ya kisheria (Kifungu 83(1)(b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, 2004 (Iliyorejewa 2008)) yanayowataka kuwakata watoa huduma Kodi ya Zuio wanapolipia huduma walizonunua.

10.15 Kulipwa Madeni ya Miaka Iliyopita Yasiyokwemo kwenye Hesabu za Miaka Husika Shilingi 1,379,900,030

Wakati wa ukaguzi, Taasisi nane (8) zimelipa jumla ya Shilingi 1,379,900,030 kwa wazabuni mbalimbali wa bidhaa na huduma. Aidha, nilibaini kuwa, matumizi haya yalikuwa ya miaka iliyopita ambayo yamekuja kulipwa katika mwaka huu wa fedha bila madeni hayo kuwamo katika hesabu za fedha zinazoishia tarehe 30 Juni, 2015 wala kuwako kwa fungu la bajeti lililotengwa kwa ajili hiyo.

Kufanya hivyo ni kukiuka Kanuni Na.41 (4) ya Kanuni za Fedha, 2001 ambayo inasema kwamba "hakuna malipo yanayopaswa

kulipwa nje ya vifungu vya bajeti vilivyoidhinishwa". Pia IPSAS 1.88 (k) (m) inataka Taarifa ya Mizania ya Hesabu kuonesha kiasi cha madeni ambayo yanatokana na Taasisi husika kukopa au kuuziwa bidhaa".

Jedwali la hapo chini linaonesha Taasisi zilizolipa madeni ambayo hayakuwemo kwenye Taarifa za Hesabu za Mwaka:

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi(Shilingi)
1	56	Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Fungu 56)	7,448,200
2	32	Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32)	40,059,395
3	48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	848,599,570
4	62	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 62)	57,196,698
5	47	Sekretarieti ya Mkoa- Simiyu	21,138,590
6	70	Sekretarieti ya Mkoa- Arusha	65,744,117
7	88	Sekretarieti ya Mkoa-Dar es Salaam	17,589,580
8	61	Tume ya Uchaguzi	322,123,880
		Jumla	**1,379,900,030**

***Chanzo**: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016*

Natoa wito kwa Mhasibu Mkuu kuupitia upya Mfumo wa Utunzaji Miamala ya Fedha na Utoaji wa Taarifa za Fedha wa EPICOR ili kuuwezesha Mfumo huo kuhifadhi miamala ya fedha na kutoa taarifa za fedha zinazoendana viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu za Umma (IPSAS accrual), kwa sasa Mfumo wa EPICOR hauruhusu uingizaji wa Ankara (LPOs) na Hati za Madai ya Wazabuni walioziuzia Taasisi za Serikali bidhaa au Huduma bila Taasisi hizo kuwa na fedha Taslimu kwa wakati huo.

Pia, ninamshauri Mhasibu Mkuu wa Serikali kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa wakati wa kuandaa makisio ya bajeti zao za matumizi ya kila mwaka kukumbuka kuombea katika bajeti hizo fedha kwa ajili ya kulipa madeni yao. Aidha, wakati wa kufanya malipo, yapasa Maafisa Masuuli kufanya malipo kupitia vifungu husika vya madeni ambavyo ni tofauti na vifungu vya matumizi vya mwaka husika.

USIMAMIZI WA MALI NA MADENI

11.1 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inakusudia kuonyesha muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi na mapendekezo husika kutokana na ukaguzi wa usimamizi mali na madeni kwa mwaka 2015/16.

11.2 Ukaguzi wa Usimamizi wa Mali za Kudumu

Serikali ina sera rasmi na taratibu zake zilizowekwa ili kuhakikisha udhibiti wa mali upo wa kutosha na wa uhakika kuhusiana na utunzaji wa kumbukumbu, kuthamini, kuripoti na kutunza mali za Umma. Mali hizo ni zile zinazotarajiwa kuzalisha faida za kiuchumi kwa serikali kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja. Mifano ya Mali, Mitambo na Vifaa (PP & E) ni pamoja na ardhi, majengo, mitambo na magari. Katika ukaguzi wa mwaka huu niliona maeneo yanayohitaji maboresho juu ya udhibiti wa Mali. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

11.2.1 Utekelezaji wa viwango vya Kimataifa katika kuripoti Mali za Kudumu kwenye vitabu vya hesabu

Matokeo ya ukaguzi na uhakiki uliofanywa ili kuthibitisha iwapo Maafisa Masuuli wameanzisha mkakati maalumu wa utekelezaji wa matakwa ya vigezo vya kimataifa (IPSAS – Accrual) katika kutoa taarifa za Mali, Mitambo na Vifaa na kuhakikisha Mali za Umma zinatumika na kutunzwa kikamilifu ili kuleta tija iliokusudiwa.

Serikali Kuu ilianza kutumia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma mwaka wa fedha 2012/13 kutoka mfumo wa IPSAS taslimu. Mfumo huu umeleta mabadiliko makubwa katika sera za kiuhasibu, ikijumuisha uundaaji wa taarifa za hesabu zenye mchanganuo na taarifa nyingi zaidi. Vilevile, mfumo huu umeleta mabadiko katika kuripoti mali na madeni kwenye vitabu vya hesabu.

Katika Ripoti zangu za miaka ya nyuma zilionyesha mapungufu yaliyoonekana katika kutekeleza mpango maalum wa kufikia

kutoa taarifa za Mali za Kudumu za Umma kwa viwango vya kimataifa na.
kutoa mapendekezo. Hata hivyo, ukaguzi huu umebaini mapungufu yaleyale kuhusiana na uandaaji wa taarifa za hesabu, utambuzi na uthamanishaji wa mali na madeni, udhibiti na mambo ya sera za mali zinazotakiwa kutekelezwa kabla ya kipindi cha mpito kinachoishia tarehe 30 Juni, 2017 kama ifuatavyo:

Kuwapo kwa Rejista ya Mali za Kudumu Isiyo Timilifu
Katika sampuli ya taasisi 69 zilizokaguliwa, nilibaini kuwapo kwa rejista za mali zisizoendana na wakati katika taasisi , zingine hakuna regista kabisa. Pia, nilibaini kuwa baadhi ya Rejista hazina taarifa za umuhimu kama vile eneo iliopo tarehe ya manunuzi, tarehe ilipoanza kutumika, na aina ya mali kina inavyooneka katika **kiambatisho 11.1.**

Mali za Kudumu za Umma ambazo Hazikuthaminishwa
Nilibainisha kuwa kuna kutokuzingatia sheria ya IPSAS 17 kwa kotofanyika kwa usahihi wa uthaminishaji wa mali za kudumu. Hii ni kwa sababu hakuna uthamini uliofanywa kwa lengo la utoaji taarifa za fedha juu ya mali za umma ingawa baadhi ya mali bado zinatumika licha ya kuripotiwa kutokuwa na thamani yeyote kwenye Taarifa za fedha.

Nilibainisha kuwa kuna kuchelewesha kwa michakato ya kuthamini Mali za kudumu miongoni mwa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi. Mtazamo wangu ni kwamba muda uliobaki kwa ajili ya Serikali Kuu kuandaa kikamilifu taarifa za fedha kufuata Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) isiyo ya msingi wa taslimu.

Hali hii ni dalili ya ukosefu wa mapitio ya kila mwaka ya muda wa matumizi ya mali husika pamoja thamani iliyobaki kama inavyotakiwa na aya ya 51 ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) No 17 kujua thamani ya mali husika katika taarifa za fedha. Nimebaini kuwa Wizara, Taasisi na Sekretarieti za Mikoa na Balozi (jumla yao 69) ambazo hazikuthaminisha mali zao kama zinavyoonyeshwa katika **kiambatisho 11.2.**

Kukosekana kwa Sera za Kusimamia Mali, Mitambo na Vifaa

Serikali inatakiwa kuwa na sera za kiuhasibu ya kusimamia namna ya kutoa taarifa ya Mali za Kudumu, ambazo ni kanuni, sheria na taratibu zinazotumiwa na Taasisi za Umma katika kuandaa taarifa za hesabu. Sera hizi za uhasibu ni pamoja na mbinu, mifumo inayotumika pamoja na taratibu za kuwasilisha taarifa za mali za kudumu kwenye hesabu. Nimebaini kuwa Serikali bado haijatayarisha sera ya uhasibu kwa mali za kudumu kupata asilimia ya uchakavu wa mali kwa mwaka, njia ya kutumia kupata kiwango kilichotumika kwa mwaka ili kuwa nz usawa katika Wizara na Idara za Umma.

Moduli za Usimamizi wa Mali Epicor Hazikutumika

Wakati wa kutathimini matumizi ya kutumia mfumo wa Epicor -upande wa usimamizi wa mali za kudumu, nilibaini kuwa moduli zipo katika mfumo EPICOR kwa ajili mahitaji ya taarifa za hesabu unaozingatia IPSAS upo lakini mfumo huo haukutumika.

Kutotenganisha thamani ya Ardhi na Majengo katika Taarifa za Fedha

Aya ya 17(74) ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) vinahitaji kutoa taarifa inayotenganisha thamani ya Jengo na Ardhi kwa sababu ardhi haina mwisho wa matumizi wakati jengo lina mwisho wa matumizi. Hata hivyo, katika ukaguzi wa mwaka huu niibaini kuwa taasisi zipatazo 69 bado zinaripoti Ardhi na Majengo pamoja kama zilivyoonyeshwa katika **kiambatisho 11.3.**

Kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kuweza kuandaa Taarifa za Hesabu za kifedha zinazozingatia kikamilifu mfumo mpya wa kuandaa Taarifa za Hesabu za kifedha katika Sekta ya Umma kwa muda ulipangwa. Kama nilivyopendekeza kwenye repoti zangu za awali, napendekeza Afisa Masuuli pamoja na Wizara ya Fedha kufanya yafuatayo:

a) Watengeneze sera maalumu ya kihasibu kuhusu Mali za Kudumu itakayotumika katika Taasisi zote ili kuhakikisha kuwa kunakuwapo na uhalali katika kuripoti Mali za Kudumu kwenye Taarifa za Fedha;
b) Wahakikishe kuwa mali zote ambazo thamani zake hazijulikani zinafanyiwa thamini na kuharakisha kufanya

uhakiki wa mali zilizopo ili kuhakikisha Mali za Kudumu kwenye Taarifa za Fedha zinakuwa timilifu na sahihi; na

c) Wahakikishe kuwa mfumo wa kompyuta wa Epicor unaotumika kuandaa Taarifa za Fedha na unakidhi mahitaji ya kuandaa taarifa za Mali za Kudumu kulingana na matakwa ya viwango vya kimataifa. Pia watumishi wajengewe uwezo kwa njia ya mafunzo katika kutumia mfumo wa kompyuta.

11.2.2 Magari Mabovu Yasiyotumika ambayo Hayafanyiwi Matengenezo wala Hayauzwi

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa menejimenti za taasisi mbalimbali zilizokaguliwa hazikuchukua hatua za kutathmini mali za kudumu ambazo hazitumiki kuona kama kuna faida kuendelea kuwa nazo au kuziuza mali ambazo zinahitaji matengenezo makubwa. Kufuatia ukaguzi uliofanyika kwenye sampuli ya taasisi 26 nilibaini magari 1272 hayakufanyiwa taratibu za kuyaondosha kwa mujibu wa kanuni Na.254 (1) ya kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001. Magari haya yanachukua nafasi katika majengo ya taasisi husika kwa muda mrefu kama zilivyoonyeshwa katika **jedwali hapo chini.**

Jedwali 81: Magari Mabovu Yasiyotumika ambayo Hayafanyiwi Matengenezo wala Hayauzwi

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Idadi
1	24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika	2
2	28	Idara ya Polisi	1092
3	35	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka	2
4	48	Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi	1
5	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	13
6	54	Sekretarieti ya Mkoa Njombe	2
7	58	Wizara ya Nishati na Madini	4
8	59	Tume ya Marekebisho ya Sheria	6
9	62	Wizara ya Uchukuzi	6
10	70	Sekretarieti ya Mkoa Arusha	3
11	71	Sekretarieti ya Mkoa Pwani	3
12	72	Sekretarieti ya Mkoa Dodoma	4
13	73	Sekretarieti ya Mkoa Iringa	4
14	75	Sekretarieti ya Mkoa Kilimanjaro	5
15	76	Sekretarieti ya Mkoa Lindi	3

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Idadi
16	78	Sekretarieti ya Mkoa Mbeya	4
17	79	Sekretarieti ya Mkoa Morogoro	1
18	86	Sekretarieti ya Mkoa Tanga	10
19	87	Sekretarieti ya Mkoa Kagera	11
20	89	Sekretarieti ya Mkoa Rukwa	7
21	93	Idara ya Uhamiaji	2
22	94	Tume ya Utumishi wa Umma	6
23	95	Sekretarieti ya Mkoa Manyara	23
24	99	Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi	54
25	2027	Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi, United Arab Emirates	2
26	2009	Ubalozi wa Tanzania Moscow	2
Jumla			**1272**

Kama nilivyopendekeza katika ripoti zangu za nyuma, kwa mara nyingine ninapendekeza kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, itoe mwongozo/maelekezo mahsusi kwa Taasisi zote kuhusu taratibu za kuziondoa Mali za Umma zilizomaliza muda wake wa matumizi. Uongozi wa taasisi zinazohusika unashauriwa kuonyesha thamani ya ardhi tofauti na ya majengo kwenye vitabu vya hesabu.

11.2.3 Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo ya Umma

Nilibaini kuwapo kwa taasisi za umma ambazo hazina nyaraka za umiliki wa baadhi ya mali walizonazo. Tatizo kubwa lilibainishwa katika ukosefu wa hati miliki ya ardhi inayomilikiwa na taasisi nyingi za umma. Nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo yanayomilikiwa na taasisi 11 zikiwemo Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi za nje ya nchi hadi sasa hazina nyaraka za umiliki licha ya mapendekezo yangu ya awali. Jedwali lifuatalo linaonesha orodha ya taasisi ambazo hazijapata hati miliki kutoka kwa Mamlaka husika za Serikali. Kutokana na kukosekana kwa hati miliki za kisheria taasisi zinaweza kupoteza haki na wajibu juu ya mali hizo

Na	Fungu	Jina la Taasisi
1	28	Jeshi la Polisi
2	35	Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Serikali
3	40	Mahakama

Na	Fungu	Jina la Taasisi
4	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
5	99	Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi
6	54	Sekretarieti ya Mkoa Njombe
7	85	Sekretarieti ya Mkoa Tabora
8	77	Sekretarieti ya Mkoa Mara
9	93	Idara ya Uhamiaji
10	2010	Ubalozi wa Tanzania New Delhi
11	2003	Ubalozi wa Tanzania Cairo

Mkurugenzi wa Usimamizi ya Mali za Umma chini ya Wizara ya Fedha nashauri ahakikishe kuwa nyaraka za umiliki zinapatikana kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi na pia kutoa maelekezo ya ziada mahsusi kwa ajili ya kulinda Ardhi na Nyumba za Serikali. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa inakuwa na nyaraka za umiliki wa kisheria wa mali zake.

11.2.4 Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa katika vitabu- Shilingi 12,818,718,047

Kanuni ya 198 na 203 ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 zinahitaji kupokea bidhaa, kutoa bidhaa na kiasi cha bidhaa kilichobaki stoo kwa kila aina ya bidhaa taarifa zake zionyweshwe kwenye kurasa tofauti katika leja za stoo. Wakati wa ukaguzi wangu, nilishindwa kuthibitisha matumizi ya bidhaa zenye thamani ya shilingi 12,818,718,047 zilizonunuliwa na taasisi 8 zilizokaguliwa kutokana na kutokuwepo na kumbukumbu sahihi katika leja za stoo baada ya kupokelewa.

Orodha ya taasisi zenye bidhaa ambazo hazikuingizwa katika vitabu zimeoneshwa katika Jedwali hapa chini:

Jedwali 82: taasisi zenye bidhaa ambazo hazikuingizwa katika vitabu

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (shilingi)
1	38	Jeshi la Wananchi wa Tanzania	12,496,126,711
2	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	80,072,400
3	74	Sekretarieti ya Mkoa Kigoma	17,552,118
4	75	Sekretarieti ya Mkoa	21,593,800

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (shilingi)
		Kilimanjaro	
5	86	Sekretarieti ya Mkoa Tanga	4,999,318
6	79	Sekretarieti ya Mkoa Morogoro	24,871,877
7	84	Sekretarieti ya Mkoa Singida	7,893,344
8	61	Tume ya Uchaguzi	165,608,479
Jumla			**12,818,718,047**

Kukosekana kwa kumbukumbu za stoo na nyaraka, sikuweza kufuatilia manunuzi na matumizi ya bidhaa/mali zilizolipiwa.

Kutokana na kuwapo kwa kiasi kikubwa cha fedha za umma zilizotumika kununua bidhaa ambazo hazikurekodiwa popote, napendekeza kwamba rekodi ya mali/bidhaa kwa wakati katika leja kuimarishwe ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali katika kutoa huduma kwa wakati kwa watumiaji wa vifaa stoo.

11.2.5 Mapato ambayo Hayajapokelewa Shilingi 151,575,367,323

Katika kipindi kinachoishia Juni 30, 2016 taasisi kumi na nane (18) ikiwa ni pamoja na Wizara kumi na mbili (12), Sekiretarieti za Mikoa (6) zilikuwa na mapato yasiyokusanywa kiasi cha shilingi151,575,367,323. kiasi kikubwa ni kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi asilimia 87 ya mapato yasiokusanywa, pili ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi asilimia 8 ya jumla ya mapato kama zilivyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali 83: kiambatisho Taasisi ambazo zina mapato yasiyokusanywa

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (shilingi)
1	29	Idara ya Huduma za Mahakama	1,778,256,290
2	32	Ofisi ya Rais, Menegimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	12,717,920
3	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	10,000,000
4	44	Wizara ya Wiwanda, Biashara na Uwekezaji	8,645,500

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (shilingi)
5	48	Wizara ya Ardhi, Nyuma na Maendeleo ya Makazi	12,480,192,710
6	52	Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	134,184,300
7	53	Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	137,295,000
8	54	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe	557,945,038
9	58	Wizara ya Nishati na Madini	2,877,896,241
10	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	1,383,874,504
11	70	Sekretarieti ya Mkoa Arusha	2,970,000
12	71	Sekretarieti ya Mkoa Pwani	39,025,764
13	72	Sekretarieti ya Mkoa Dodoma	2,026,170
14	77	Sekretarieti ya Mkoa Mara	20,446,607
15	87	Sekretarieti ya Mkoa Kagera	15,407,754
16	93	Idara ya Uhamiaji	107,111,438
17	96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	59,614,956
18	98	Wizara ya Ujenzi	131,947,757,132
		Jumla	**151,575,367,324**

Mapato ambayo bado hayajakusanywa kutoka kwa wateja yanapelekea ucheleweshwaji wa mapato.

Nashauri Wizara na Sekiretarieti za Mikoa kuja na mkakati maalum katika kukusanya mapato ndani ya muda muafaka. Bila kukusanya mapato hayo inaweza kusababisha taasisi zinazohusika kushindwa kutoa huduma iliyokusudiwa kwa umma.

11.2.5.1 Ukarabati wa Majengo na kuendeleza Viwanja vya Serikali katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

Kama nilivyobainisha katika ripoti yangu ya mwaka 2014/15 Serikali haikuchukua hatua za kutosha na kwa wakati kukarabati majengo ya ofisi na makazi katika Balozi za Tanzania nje ya nchi. Baadhi ya majengo ni chakavu na yako katika hali mbaya. Hayajafanyiwa matengenezo au ukarabati kwa muda mrefu. Pia, Serikali inamiliki viwanja kwenye balozi

mbalimbali ambavyo bado havijaendelezwa kwa muda mrefu. Kati ya Balozi 34, kumi na mbili (12) zilizokaguliwa zina majengo 37 chakavu ambayo yanahitaji ukarabati na matengenezo makubwa. Zaidi ya hayo, balozi 10 zilikuwa na viwanja ambavyo havijaendelezwa. Maelezo yapo katika **kiambatisho Na.11.4** Tathmini yangu imebainisha kuwa kuna tatizo la kujua ni nani mwenye jukumu la kufanya matengenezo na ukarabati katika majengo yaliyoharibika vibaya kwenye balozi zetu. Naona kwamba hakuna mtu au ofisi iliyopewa wajibu/jukumu hilo.

Kwa mfano London, ukaguzi ulibainisha kuwa ubalozi wa Tanzania unamiliki maeneo yenye majengo 9, ambapo mengi kati ya hayo kwa ujumla yana hali mbaya pia kuna kesi ya jengo lilipo mtaa wa 9 Denewood ambapo, imeamriwa na mamlaka husika jengo livunjwe kutokana na ubovu.

Taarifa iliyopo ni kuwa licha ya juhudi za Mabalozi Nje ya Nchi kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali ili kuendeleza majengo na viwanja, idhini lazima itoke Dar es Salaam ambayo inachukua mda mrefu Hivyo ucheleweshaji huo unasababisha majengo na viwanja kuachwa kukarabatiwa/ kuendelezwa kwa miaka mingi. Kwa mfano, London hakuna majibu yaliyotolewa kutoka Wizarani na baada ya miaka michache mimea isiyohitajika imeota na kupelekea Halmashauri ya Jiji London kutoa taarifa kwa ubalozi kuondoa mimea hiyo, na mtaalamu wa kuondoa mimea hiyo utaugharimu ubalozi kiasi cha Paundi 50,000.

Ni maoni yangu kwamba ucheleweshaji katika kuidhinisha au kuchukua hatua juu ya kuendeleza, ukarabati na matengenezo ya majengo na viwanja vya Balozi nje ya nchi kunasababisha kuongezeka kwa gharama za matengenezo ya majengo na kama tunashindwa kuendeleza kwa wakati viwanja na majengo inawezekana viwanja na majengo yakachukuliwa na nchi wenyeji. Zaidi ni kwamba, kuchelewa kwa utoaji wa vibali inaonekana ni kutokana na ukosefu wa kitengo kinachowajibika moja kwa moja kwa ajili ya maendeleo ya majengo na viwanja katika balozi zetu.

Kwa mujibu wa aya M1, Sehemu M, nyumba na samani katika Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma 2009, Serikali ina

wajibu wa kuwezesha na kutoa nyumba/malazi kwa watumishi wa umma ambao masharti ya ajira ni pamoja na haki ya makazi ya bure. Pia, katika M2 nyumba za Serikali zitasimamiwa katika kuweka madaraja, kukodisha au kuuza na Wakala wa Majengo Tanzania na kupitishwa na Katibu Mkuu anayewajibika na Nyumba za Serikali zinamilikiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na wizara nyingine zenye maslahi kama Wizara ya Ujenzi (Tanzania Building Agency) na Katibu Mkuu-Utumishi wa Umma.

Kuna haja ya kuanzisha kitengo chenye wajibu wa usimamizi wa mali na majengo ya umma nje ya nchi; na kuwa na uelewa wa pamoja kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa mali hizi za serikali ambaz

Hivyo, napendekeza kwamba kikosi kazi kiundwe kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Mambo ya Nje kupata muafaka juu ya kuwa na kitengo kitakachohusika na masuala yote yanayohusu uendelezwaji na ukarabati katika viwanja na majengo yaliyopo nje ya Nchi.

11.2.6 Mali za Kudumu ambazo Hazina Alama za Utambulisho

Alama za utambulisho kwenye vifaa inarahisisha mfumo wa ufuatiliaji wa Mali, ufuatiliaji kujua hali ya kifaa na kama kuna uhitaji wa kukibadilisha, na uwezekano wa kukiweka kinapohitajika. Pia husaidia kuzuia wizi wa mali. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa baadhi ya taasisi hazitoi kipaumbele suala la kuweka alama za utambulisho kwenye vifaa kama hatua za kudhibiti upotevu na wizi. Wakati wa ukaguzi nimebaini taasisi 10 ambazo zina Mali zilivyoripotiwa kwenye vitabu vya kumbukumbu ya mali bila kua na alama za utambulisho kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini

Jedwali 84: Mali za Kudumu ambazo Hazina Alama za Utambulisho

Na	Fungu	Jina la Taasisi
1	33	Ofisi ya Rais Tume ya Maadili

Na	Fungu	Jina la Taasisi
2	40	Mahakama
3	41	Wizara ya Katiba na Sheria
4	54	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe
5	71	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani
6	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma
7	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora
8	94	Public Service Commission
9	2001	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa.
10	2005	Ubalozi wa Tanzania Abuja

Chanzo: Vitabu vya mali

Napendekeza kwa serikali kuhakikisha kwamba mali zote ziwekewe alama za utambulisho.

11.3 Usimamizi wa Madeni

IPSAS 1 kwenye Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha inasema kwamba Madeni ni wajibu wa sasa wa taasisi kutokana na matukio ya zamani. Malipo yake yanatarajiwa kusababisha uondoshaji wa rasilimali za taasisi zenye faida za kiuchumi au uwezo wa huduma". Mwaka huu nilibainisha mapungufu yafuatayo katika usimamizi wa madeni kwenye taasisi zilizokaguliwa:

11.3.1 Madeni tarajiwa (Kesi ambazo hazijafanyiwa maamuzi)

Madeni tarajiwa ni matarajio ya wajibu wa kulipa utakaotokana na matokeo tarajiwa.

Wakati wa ukaguzi, taasisi zilizokaguliwa zilikuwa na kesi zenye thamani ya shilingi 850,740,035,053 ambazo hazijaamuliwa kutoka kwa makampuni mbalimbali na watu binafsi. kesi hizi zitakuwa na athari kubwa kifedha katika uendeshaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa. Baadhi ya kesi ziko katika hatua za kusikilizwa, nyingine hatua ya upatanishi mahakamani. Kati ya taasisi 207 zilizokaguliwa, Wizara na Sekretarieti za Mikoa 15 zilikuwa na madeni tarajiwa ya shilingi 850,740,035,053 yanayotokana na kesi mahakamani ambazo hazijahukumiwa.

Taasisi zenye kesi za kisheria ambazo hazijatolewa hukumu ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapa chini.

Jedwali 85: Madeni tarajiwa

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (shilingi)
1	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	8,728,170,711
2	43	Wizara ya Kilimo, Chakula na Maendeleo ya Ushirika	5,851,314,597
3	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	1,189,624,889
4	48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	67,439,500,000
5	58	Wizara ya Nishati na Madini	660,767,521,003
6	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	24,774,534,809
7	98	Wizara ya Ujenzi	78,295,901,881
8	99	Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi	42,109,407
9	62	Wizara ya Uchukuzi	317,824,034
10	89	Sekretarieti ya Mkoa Rukwa	50,000,000
11	85	Sekretarieti ya Mkoa Tabora	114,000,000
12	86	Sekretarieti ya Mkoa Tanga	39,582,422
13	87	Sekretarieti ya Mkoa Kagera	90,000,000
14	77	Sekretarieti ya Mkoa Mara	13,429,300
15	80	Sekretarieti ya Mkoa Mtwara	3,026,522,000
Jumla			**850,740,035,053**

Kuna hatari ya kuingia katika matumizi yasiyo na manufaa kwa Wizara / Sekiretarieti za Mikoa kutokana na faini au adhabu ambayo inaweza kuamriwa na mahakama kama Wizara / Sekretarieti za Mikoa zitashindwa kesi hizi. Kwa kuongezea, kuna gharama ambazo hutokana na ufuatiliaji wa kesi hizi.

Kwa kuzingatia mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma, nazidi kupendekeza serikali kufanya mkazo juu ya kila taasisi kuwa na mikakati thabiti ya usimamizi wa vihatarishi ili

kuhakikisha kwamba kila taasisi ina sera ya usimamizi wa vihatarishi vya upotevu wa fedha ili kuhakikisha vinapunguzwa.

11.3.2 Malimbikizo ya madeni shilingi 1,979,323,563,821

Mpaka kufikia Juni 30, 2015 taasisi 92 zilikuwa na madeni kiasi cha shilingi 1,979,323,563,821 kama zilivyoonyeshwa kwenye taarifa za fedha za taasisi husika, ikilinganishwa na mwaka uliopita ulikuwa na madeni yaliyofikia shilingi 1,443,168,096,360. Kuna ongezeko kubwa la madeni la kiasi cha shilingi 536,155,467,461.67 sawa na ongezeko la asilimia 37. Mwenendo wa madeni kwa kipindi cha miaka minne yameonyeshwa katika kielelezo hapa chini:



Sehemu kubwa ya deni inatoka Jeshi la Polisi ambalo lina deni sawa na asilimia 37 ya jumla deni lote; ya pili ni Wizara ya Ujenzi ikiwa na asilimia 14 ya jumla ya deni ikifuatiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikiwa na asilimia 13 ya jumla ya deni lote kama ilivyoonyeshwa kwenye kielelezo hapo chini.

Kielelezo 25: Malimbikizo ya madeni



Deni lililoripotiwa linajumuisha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikiwa ni madai ya matibabu kwa Serikali kutoka hospitali za India ambapo Serikali ilipeleka wagonjwa kwa matibabu.Deni la matibabu linalodaiwa kwa mwaka unaoishia 30 Juni, 2016 lina jumla ya shilingi 19,192,661,032 ukilinganishwa na deni lililopita la shilingi 16,940,392,204 ikiwa ni ongezeko la shilingi 2,252,267,829. Hosipitali zinazodai ni kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali 86: Hosipitali zinazodai

Na	Jina la Hospitali	Kiasi (shilingi)
1	Ahmedabad	2,056,191,663
2	Bangalore	548,323,232
3	Chennai	6,164,240,402
4	Madras	5,274,465
5	Hyderabad	2,594,310,144
6	New Delhi	7,824,321,126
Jumla		**19,192,661,032**

Orodha ya taasisi zenye madeni ya Serikali ya muda mrefu zimeonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 11.5.

Ongezeko kubwa la deni bila kuonyesha juhudi za kulilipa linavuruga uhusiano mzuri uliokuwepo kati ya taasisi za umma na watoa huduma na kwa watumishi linaweza kusababisha

utoaji huduma kwa umma usioridhisha. Wizara, Wakala, Idara na Sekiretarieti za Mikoa zinaweza kushitakiwa kwa kosa la kushindwa kulipa deni kwa wakati. Napendekeza yafuatayo kwa Serikali:

- Madai yote kuingizwa kwenye bajeti ya mwaka ujao ili yaweze kulipwa yote ili kuepuka mgogoro na wauzaji na wadau wengine. Katika siku zijazo, fedha zitolewe kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti ili kuepuka athari za madai na kudumisha uaminifu.
- Kupitia upya mchakato wa maandalizi ya bajeti ili kuhakikisha bajeti ianyoandaliwa inaendana na uhalisiai.

11.3.3 Madeni ambayo hayana nyaraka shilingi 41,634,353,231

Madeni ni wajibu wa kulipia bidhaa au huduma iliyopokelewa au iliyotolewa kabla, na kupokea ankara au uwepo wa makubaliano kabla. Kwa mujibu wa mapitio yaliyofanywa kwa sampuli ya taasisi 3 zilishindwa kutoa udhibitisho wa madai yaliyoripotiwa mwisho wa mwaka. Orodha ya taasisi na madeni ambayo hayana vithibitisho zimeonyeshwa katika jedwali hapo chini:

Jedwali 87: Madeni ambayo hayana nyaraka

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (shilingi)
1	94	Tume ya Utumishi wa Umma	448,288,838
2	38	Jeshi la Wananchi wa Tanzania	41,129,424,819
3	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	56,639,574
Jumla			**41,634,353,231**

Kutokana na kukosekana kwa nyaraka za kuthibitisha madai yaliyopo kwenye taarifa za fedha, kuna uwezekano wa kuwepo madai ambayo si halisi yalioandaliwa na mtumishi asie mwaminifu.

apendekeza kuwa Maafisa Masuuli wanaohusika waweke mifumo ya udhibiti ilyo madhubuti ili kuhakikisha madai yote yanakuwa na nyaraka na madai yawe yanathibishwa na mtu mwingine tofauti kabla ya kuingizwa kwenye vitabu vya hesabu. .

KAGUZI MAALUM NA UKAGUZI WA VYUAMA VYA SIASA

12.0 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2008 na Kanuni Na.79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kutokana na maombi kutoka kwa Afisa masuuli au mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara,
Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vyombo vingine.
Kanuni pia inampa CAG mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum pale anapoona inafaa. Katika mwaka husika, kaguzi maalum mbili (2) zilifanyika. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum ni kama ifuatavyo:

12.1 Ukaguzi Maalumu Katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mnamo tarehe 08 Machi, 2016 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alianza Ukaguzi Maalumu katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kutokana na ombi la Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia barua yenye Kumb. Na. SAB 365/439/01/60 ya tarehe 01 Februari 2016 kwa kuzingatia Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 na Kanuni Na.78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009.

Ukaguzi huu ulihusu tuhuma dhidi ya Menejimenti ya Mamlaka kuhusu matumizi ya fedha kwa ajili ya utengenezaji wa vitambulisho ambapo kiasi cha jumla ya Sh.179.6 Bilioni kilitumika katika manunuzi na malipo mbalimbali. Ukaguzi ulipitia mikataba ya ununuzi wa mitambo ya kutengenezea vitambulisho, mchakato wa kutengeneza vitambulisho, mchakato wa upatikanaji wa vibarua na gharama za kusafirisha vifaa na mitambo ya kusajili raia kwa kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Juni 2016.

Ukaguzi ulibaini kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2015/16 Mamlaka ilipokea jumla ya kiasi cha

Sh.189,764,035,764 na kutumia jumla ya Sh.183,043,117,014 toka mwaka 2012/2013 hadi 2015/2016. Ukaguzi huu Maalum ulibaini mambo yafuatayo;

(a) Ubadhirifu katika Malipo ya Bima za Magari ya Mradi na vifaa vya Usajili na Utambuzi wa Jumla ya Sh.1,236,978,426

Jumla ya kiasi cha Sh.1,236,978,426 kililipwa kwa huduma za bima zilizolipiwa kupitia dalali wa Bima M/s Aste Insurance Brokers Company Limited. Kiasi hiki kililipwa zaidi ya gharama halisi isivyostahili. Huduma hizi zilipaswa kugharimu jumla ya Sh. 450,184,450 (gharama halisi) ambapo Mamlaka ililipa jumla ya Sh.1,687,162,876.

Ubadhirifu mwingine ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Manunuzi ya Bima ya Vifaa vya Usajili na Magari yaliyotumika katika mradi wa vitambulisho vya Taifa ya jumla ya Sh. 494,000,779 yalifanyika bila kukihusisha Kitengo cha Manunuzi.

- Kadhalika, dalali wa Bima M/s Aste Insurance Brokers Company Limited alitumia Akaunti za Biashara (Current Accounts) katika kupokelea fedha za malipo ya bima ya jumla ya Sh.1,687,162,876 badala ya Akaunti ya Amana (Trustee Account), isivyostahili.

- Mamlaka ilinunua vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh.76,672,200 kwa ajili ya shughuli za Wizara ya Mambo ya Ndani. Aidha, uhakiki wa leja za Mafuta ulibainisha kuwa Lita 1,110 za mafuta ya dizeli yenye thamani Sh.2,217,720 zilitumika kwa shughuli zisizo za Mamlaka. Vilevile, Wizara ya Mambo ya Ndani ilikopa jumla ya kiasi cha Sh. 455,280,000 sawa na USD 280,000 kutoka katika Mamlaka kwa ajili ya ununuzi wa magari manne (4) mwaka 2014 ambazo hadi Ukaguzi Maalum unakamilika mnamo Oktoba, 2016 fedha hizo hazikuwa zimerejeshwa.

(b) Utengenezaji wa Fomu zenye "Barcode" na Utengenezaji wa "Postal Codes" ambazo hazikutumika

Uhakiki wa fomu zenye 'Barcode' zilizotengenezwa kupitia mpiga chapa binafsi M/s MFI Solution ulibaini kuwa fomu 7,762,907 zenye thamani ya Sh. 2,484,130,240 zilizopokelewa na Mamlaka hazikutumika.

Kadhalika, ilibainika kuwa fomu 8,220,000 zenye thamani ya Sh.519,588,870 zilizochapishwa tangu mwaka 2011/2012 hadi 2013/2014 hazikutumika; hivyo, kutelekezwa katika stoo za TANITA. Hali hii ilitokana na Mamlaka kutokuwa na Mpango Kazi, hivyo kuingia hasara ya Sh.932,838,470 (gharama za fomu 8,220,000 Sh. 519,588,870 na gharama za wino ambao haujatumika Sh.413,249,600)

Pia, mnamo mwaka 2013/2014 baada ya Mamlaka kuamua kutumia Taasisi za Serikali za uchapishaji pekee, Taasisi ya Malindi Printing na Dar es Salaam University Press (DUP) zilichapa jumla ya fomu 22,000,000 zenye thamani ya Sh. 7,040,000,000; ambapo, fomu 658,650 zenye thamani ya Sh. 210,768,000 zililipiwa ila hazikupokelewa na Mamlaka.

Kwa mwaka 2013/2014 Mamlaka iliagiza fomu za Usajili 18,000,000 na "Postal code" 90,000 za thamani ya Sh. 7,286,940 kutoka Dar es Salaam University Press (DUP). DUP haikuwa na uwezo wa kufanya kazi hizo kutokana na kuwa na mitambo chakavu. Hivyo ilimpa M/s Guyella Investment zabuni hiyo. Aidha , M/s Guyella Investment, kampuni ambayo imesajiliwa na BRELA kufanya biashara ya vifaa vya ujenzi, ilimpa M/s Jayant Printers LLP ya nchini India sehemu ya kazi hiyo bila idhini ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

(c) Ubadhirifu Katika Utengenezaji wa Magari na Malipo

- Ukaguzi ulibaini malipo ya Sh. 42,631,736 yaliyofanyika zaidi ya madai stahili kutokana na udanganyifu wa kuongeza tarakimu katika hati za madai na kutumiwa kwa hati moja ya madai zaidi ya mara moja katika malipo ya kuanzia Mwaka 2012/2013 hadi 2015/2016.

- Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 mpaka 2015/2016 Mamlaka ilifanya matengenezo ya magari kupitia gereji binafsi yaliyogharimu jumla ya Sh.1,288,746,869; ambapo, matengenezo yaliyogharimu jumla ya Sh. 1,091,574,749 yalifanyika na kulipwa na Mamlaka bila kufanyika ukaguzi wa awali (Pre- inspection) unaothibitisha kuwapo kwa ubovu wa gari na mahitaji ya matengenezo husika.Na matengenezo yaliyogharimu jumla ya Sh. 197,172,120 yalifanyika na kulipiwa na Mamlaka bila kufanyika ukaguzi wa awali wala ukaguzi baada ya matengenezo (Pre and post inspection).

- Pia, ilibainika kuwa yalifanyika matengenezo mfululizo ya magari yaliyoigharimu Mamlaka jumla ya Sh. 410,649,047; ambapo, magari yamekuwa yakitengenezwa kila baada ya siku 2 hadi 18 tangu matengenezo ya awali kufanyika. Aidha, kampuni ya Nduvini Auto Works iliwasilisha hati za madai zinazofanana za Sh.61,845,570 ambazo hazikuthibitika uhalali wake.

Ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma

(a) Katika Mikataba ya Ukodishaji wa Nyumba kwa ajili ya Matumizi ya Ofisi

- Mamlaka ilitoa zabuni ya kuipangisha Ofisi ya Mamlaka kwa Ms. Mary Salome Mwema kupitia barua ya maombi ya tarehe 06.05.2012 ambapo tangazo la zabuni husika ni la tarehe 25.05.2012 baada ya tarehe ya kuomba. Zabuni husika haikupitia Kitengo cha Manunuzi na haikuwa imeidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Aidha, mzabuni wa upangishaji wa jengo la ofisi Mr & Mrs. John Masenga wa S.L.P 11729 hakujumuishwa kwenye mchakato wa tathmini ya kitaalam licha ya kukidhi vigezo.

- Pia, Mamlaka ilipanga katika jengo la BMTL lililopo maeneo ya Victoria Dar es salaam kwa ajili ya Ofisi bila kushirikisha Kitengo cha Manunuzi.

- Hali kadhalika, katika uhakiki wa Majengo ya ofisi ilizopanga Mamlaka, ilibainika kuwa majengo matatu (3) kati ya matano (5) yaliyokaguliwa hayakukidhi vigezo vya ofisi vilivyohitajika

kama kutokuwa na eneo la kuegeshea magari zaidi ya 50 na jenereta la dharura (Stand by Generetor).

(b) Udanganyifu katika ushindanishi wa wazabuni katika Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA

Mamlaka ilifanya manunuzi ya Ipad zenye thamani ya Jumla Sh. 63,383,700 zilizonunuliwa kutoka kwa M/s Elite computers baada ya kuonekana kukidhi vigezo vya ushindani na kupewa zabuni saba (7) tofauti.

Taarifa za wazabuni ambao waliainishwa kuwa washindani katika zabuni hii M/s Prudent Enterprise na M/s Morex General Enterprise zilighushiwa na wazabuni hawa hawakuhusishwa wala kutoa nukuu za bei.

(c) **Ukiukwaji wa Sheria na Vigezo katika Mchakato wa Upatikanaji wa Mzabuni M/s Gwihotolo Implex**

Uhakiki wa mkataba kati ya M/s Gwiholoto na GIPSA ulionesha kuwa M/s Gwihotolo Implex Limited alitoza gharama za huduma ya Wakala wa forodha kinyume na Mkataba kati yake na GPSA. Ilibainika M/s Gwihotolo Implex iliitoza Mamlaka gharama za vibarua "consolidation fee" na "documentation fee" kinyume na makubaliano ya kwenye mkataba hivyo kusababisha Mamlaka kulipa kiasi cha Sh. 48,389,920 nje ya mkataba.

Pia Mamlaka ilimlipa M/s Gwihotolo Implex Limited kiasi cha Sh.45,515,961 zaidi katika madai iliyowasilisha ya Sh.91,036,928 kama gharama za kutolea mizigo. Ilibainika kuwa Mamlaka ililipa kiasi cha Sh. 113,703,471 zaidi kutokana na Wakala M/s Gwihotolo Limited kughushi mkataba Na.0010589 alioingia na Wakala wa Manunuzi (GPSA) unaotoza 1.5% ya gharama halisi ambapo mkataba halisi unaainisha gharama za 1.2% ya gharama.

(d) Ubadhirifu na Mapungufu Katika Ununuzi wa Tiketi za Ndege

Manunuzi ya tiketi yenye thamani ya Sh.613,263,302 kutoka Sykes Travel Agent na Kearsley Travel and Tours yalifanywa bila kukishirikisha Kitengo cha Manunuzi.

Aidha, Mamlaka ilifanya malipo ya Sh.5,979,600 kwa M/s Skyes Travel Agent mara mbili (double payments) katika malipo ya safari za watumishi na ilimlipa jumla ya Sh. 106,925,050 kwa ajili ya tiketi za ndege kupitia "Proforma invoice" . Pamoja na kumlipa wakala huyu, kiasi cha Sh.3,333,000 kama gharama ya kufuta tiketi (cancellation) ambapo haikuthibitika kama Mamlaka ilikata tiketi husika. Vile vile, Mamlaka ililipa jumla ya Sh.1,360,000 kama gharama za kufuta tiketi ya ndege kwenda Dar-Doh-Kora-Doh-Dar ya Mshauri Elekezi kutoka M/s Gotham Inernational Limited; safari ambayo ilithibika kuwa ilifanyika na haikuwa imeahirishwa.

Vile vile, Mamlaka ililipa gharama za tiketi za ndege zenye thamani ya Sh.2,432,000 kwa wasafiri wasiokuwa watumishi wa Mamlaka.

(e) Mapungufu katika Mchakato wa Kumpata Mshauri Elekezi wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa na Utekelezaji wa Mkataba

Ukaguzi ulibaini ukiukaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 katika kumpata Mshauri Elekezi wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa M/s Gotham International Limited. Aidha Sh. 930 milioni zililipwa kwa M/s Gothan International Limited kwa kazi ya upembuzi yakinifu (Feasibility Study) bila ya mkataba wa Makubaliano (MoU).

Pia, Mamlaka ililipa Sh.108,684,450 kama nyongeza ya malipo ya awali kutokana na makosa yaliyofanyika kwenye kiwango cha kubadilishia fedha, malipo ambayo yalifanyika bila kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka kinyume na Kanuni za Fedha za Mamlaka za Mwaka 2009.

Kadhalika, Mamlaka, kupitia M/s Gotham International Limited , ilichapisha vitabu vya Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) 200 kwa gharama ya Sh.30,000,000 ambapo vitabu 105 (sawa na Sh. 15,750,000) havikuwa vikihitajika na vimehifadhiwa katika stoo ya Mamlaka tangu Mwaka 2010.

(f) **Mapungufu katika Kumpata Mzabuni na Utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Mfumo wa Kutengeneza Vitambulisho vya Taifa**

Tarehe 21.04.2011 Mamlaka iliingia Mkataba na M/s IRIS Corporation Berhad juu ya utekelezaji wa kujenga Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa; ambapo ilibainika kuwa mzabuni aliwasilisha ongezeko la gharama la jumla ya USD 230,000 kwa maelezo kuwa tathmini ya awali ya Dola za Kimarekani USD 149,726,303 ilikosewa. Licha ya ongezeko hilo kuwasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha Bodi ya Zabuni, uhakiki wa "Financial Proposal" zilizowasilishwa na kukubalika awali za jumla ya USD 149,726,303 hazioneshi msingi wa ongezeko la gharama kwa maelezo ya kukosewa kwa makadirio.

Vilevile, Mamlaka iliilipa jumla ya Sh.1,025,343,729 ikiwa ni gharama za forodha kwa ajili ya kuingiza vifaa vya usajili na mitambo; ambapo, kwa mujibu wa makubaliano, malipo hayo yalipaswa kugharamiwa kwa usawa baina ya pande zote mbili (NIDA na IRIS Corporation Berhad). Hivyo, Mamlaka imelipa zaidi kiasi cha jumla ya Sh. 512,671,865.

(g) Ajira za muda na za kudumu

Ukaguzi ulibaini ukiukwaji wa Sheria katika Ajira za Muda na za Kudumu zilizofanywa na Mamlaka; ambapo, kuanzia mwaka 2012 hadi 2015 vibarua wapatao 1,071 walipatikana kwa kupigiwa simu bila kutangaza mahali popote kinyume na Sera ya Rasilimali Watu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na Kanuni zake za Mwaka 2011.

Mamlaka iliomba na kupatiwa vibarua kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Chuo cha Utumishi wa Umma wapatao 415. Baada ya kupatiwa watumishi/vibarua hao, Mamlaka haikuweza kuwatumia na kubainisha kwamba wangetumiwa siku za baadae. Hata hivyo,, Mamlaka iliamua kuajiri vibarua wengine wapatao 882 tofauti na watumishi 415 ambao walikwisha patiwa bila kutangaza mahali popote.

Pia, tarehe 01.09.2015 Mamlaka iliajiri jumla ya watumishi 213 licha ya kibali cha kuajiri kutoka Utumishi kuisha tarehe 20.04.2015. Hali kadhalika, tarehe 25.06.2013 Mamlaka ilifanya malipo ya Sh. 16,627,500 ya kiinuo mgongo kwa vibarua kinyume na mkataba wa ajira ya muda na Sheria Namba 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004.

(h) Udhaifu katika udhibiti wa ndani

Kutothibitika kwa Matumizi ya Mafuta ya 'Diesel' na Petrol yaliyonunuliwa na Mamlaka yenye Thamani ya Sh. 2,349,748,595

Mafuta yenye thamani ya Sh. 2,349,748,595 yaliyotolewa kwenye magari na majenereta hayakuthibitika matumizi yake kutokana na sababu mbalimbali kama ifuatavyo:

Mafuta/Lita	Uhakiki/Mzabuni	Sababu	Thamani (Sh.)
Diesel/14,330	Leja za mafuta/ GPSA	Magari na Majenerata hayakuainishwa	29,059,100
	Leja za mafuta /GPSA na Wazabuni wengine	Kukosekana vitabu vya matumizi (log books)	2,195,120,350
Diesel/6,160	Leja za mafuta/GPSA	Kiwango cha lita za mafuta ni zaidi ya uwezo wa ujazo wa tenki za magari husika	12,320,000
Diesel/6,115	Leja za mafuta/GPSA	Magari yaliyoainishwa yalikuwa gereji	12,487,230
Diesel na Petrol/50,726	Taarifa kutoka Total Tanzania Limited	Magari hayakuainishwa	100,761,915
Jumla			**2,349,748,595**

Upotevu wa Vifaa vyenye Thamani ya Jumla ya Sh. 93,662,000

Ukaguzi maalum ulibaini upotevu wa vifaa vyenye thamani ya Sh.93,662,000 katika stoo ya Mamlaka. Pia, hakukuwa na taarifa rasmi kutoka kwa Mtunza Stoo juu ya upotevu huo licha ya kufahamu kuhusu upotevu wa vifaa hivyo.

Hali kadhalika, vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh.991,406,974 havikutumika tangu kununuliwa kwake katika vipindi tofauti kuanzia Machi 2013 hadi Oktoba 2016.

Mapendekezo

- M/s Aste Insurance Company irejeshe Sh.1,246,341,080 zilizolipwa zaidi isivyostahili;
- M/s Aste Insurance Broker irejeshe jumla ya Sh.1,236,978,426 na hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Bw. Astery Ndege na kampuni hii kwa kufanya udanganyifu na kujipatia fedha toka Mamlaka;
- Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika katika udanganyifu uliobainishwa na kutozingatia sheria za manunuzi ya umma na kuisababishia Mamlaka gharama zisizo na tija sanjari *na* kuhakikisha kuwa wahusika wanafidia hasara iliyopatikana, kisha, kuhakikisha udhibiti wa vifaa.

- Menejimenti ya M/s Gwiholoto Implex Ltd irejeshe kiasi cha jumla ya Sh 48,389,920 kilichotozwa kwa Mamlaka kinyume na mkataba na gharama iliyoongezeka ya Sh.787,187,557 sambamba na kuchukuliwa hatua stahili dhidi ya TAFFA na M/s Gwiholoto Impex Ltd. Hali kadhalika Mamlaka ihakikishe kuwa M/s Gwiholoto Implex Ltd anarejesha jumla ya Sh.113,703,471 ili kufidia hasara iliyopatikana kwa kugushi bei elekezi.

- Menejimenti ya Mamlaka ihakikishe kuwa kiasi cha Sh. 5,979,600 kinarejeshwa kutoka kwa M/s Sykes Travel Agent.
- Nduvini Auto Works ichukuliwe hatua kwa mujibu wa mkataba baina yake na TEMESA kipengele Na.5 na 6. Pamoja na Sheria ya Ununuzi ya Umma.
- Wajumbe wa Bodi ya Zabuni waliohusika kupitisha ongezeko la bei ya mkataba kwa kiasi cha USD 230,000 wawajibishwe

kwa kutotimiza wajibu wao ipasavyo na hivyo kuisababishia Mamlaka hasara

- Menejimenti ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ihakikishe kiasi fedha za gharama za forodha zilizolipwa kwa niaba ya IRIS zinarejeshwa kikamilifu

- Serikali iimarishe Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili nyaraka zote za serikali ziweze kupigwa chapa katika ofisi hizo.

12.1.2 Ukaguzi Maalum wa Fedha Za GAVI Alliance kwa Ajili ya Chanjo ya Surua Rubella

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari mambo muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi huu maalum katika Halmashauri za Wilaya na Ofisi za Waganga Wakuu wa Mikoa. Timu ya ukaguzi maalum ilibaini mambo na mapungufu mbalimbali ambayo maelezo ya kina yametolewa katika aya husika. Mambo muhimu na mapungufu yaliyojitokeza ni haya yafuatayo:

(a) Fedha zilizopokelewa na Wizara ya Fedha na kupelekwa Wizara ya Afya

Jumla ya Sh.20,936,782,798 sawa na (USD 12,791,693) zilipokelewa na Wizara ya Fedha kutoka GAVI Alliance, na kiasi hicho chote kilipelekwa Wizara ya Afya kwa ajili ya zoezi la chanjo ya Surua Rubella. Kati ya kiasi hicho, jumla ya Sh. 19,095,020,382 zilitolewa kwa ajili ya zoezi la chanjo, ambapo Sh. 18,369,444,799 zilitumika Tanzania Bara na Sh. 725,575,583 kupelekwa Zanzibar. Pia kiasi cha Sh. 1,003,339,008 kilitumika kama gharama za uendeshaji na hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2014 kulikuwa na bakaa ya Sh. 838,423,408.

(b) Fedha zilizopokelewa na Mikoa na kupelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kiasi cha Sh.17,333,760,792 kilitumwa katika mikoa na kuingizwa kwenye akaunti za Kifua Kikuu na Ukoma "TB & Leprosy" zinazosimaiwa na Waganga Wakuu wa Mikoa husika isipokuwa Dar es Salaam. Fedha hizo zilitolewa benki na

kugawanywa zikiwa taslimu kwa mafisa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao walikuwa wakihusika na zoezi la chanjo. Aidha kiasi cha SH 1,035,684,000 kililipwa kama masurufu kutoka Wizara ya Afya kwa ajili ya zoezi la chanjo Mkoa wa Dar es Salaam. Ufuatiliaji wa fedha zilizotumwa mikoani umeonyesha kuwa:

- Kiasi cha Sh.13,134,813,258 kimethibitika kupokelewa na maafisa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

- Kiasi cha Sh.1,077,167,188 kilichopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hakikuthibitika kupokelewa. Aidha, maafisa wa Serikali za Mitaa walikana kufahamu ujio wa fedha hizo na nyaraka za mapokezi yake.

- Kiasi cha Sh. 2,153,289,221 kilibaki chini ya usimamizi wa maafisa wa Wizara ya Afya ambao walitumwa mikoani kwenda kusimamia zoezi la chanjo. Hatukuweza kupata sababu zilizopelekea kubaki na kiasi kikubwa hivyo cha fedha wakati wao walikuwa ni waratibu tu wa zoezi la chanjo.

- Nyaraka zenye jumla ya Sh. 968,491,799 kwa Wilaya zote na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na Wilaya za Same, Hai na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro hazikuweza kupatikana kwa ukaguzi.

(c) Malipo ya posho hewa kwa kutumia nyaraka za kughushi Sh.1,204,625,500

Kiasi cha Sh.1,204,625,500 kililipwa kama posho kwa kutumia nyaraka za kughushi. Mahojiano yaliyofanywa na timu ya ukaguzi maalum yalibaini kuwa walioonekana kulipwa posho, wasimamizi wa vituo na baadhi ya Waganga Wakuu wa Wilaya hawayatambui malipo hayo.Na kwa baadhi ya Halmashauri, Waganga Wakuu wa Wilaya na Maafisa Utumishi waliyakana majina ya waliolipwa katika fomu hizo kuwa sio watumishi wa Halmashauri zao.

(d) Malipo kwa watumishi hewa ambao hawakuhusika katika zoezi la chanjo Sh. 293,950,500

Jumla ya Sh.293,950,500 zililipwa kwa watu ambao hawakuhusika katika zoezi la chanjo. Aidha, ukaguzi wa kina ulibaini kuwa waliolipwa hawakuwa watumishi wa Halmashauri husika, wala hawakuweza kujulikana kada zao na mahala pao pa kazi. Hata baada ya timu ya ukaguzi kufanya juhudi za kuwajua ni kina nani na mahali walipo, hawakuweza kupatikana.

(e) Watumishi waliofanya kazi ya chanjo bila kulipwa Sh.82,725,000

Timu ya ukaguzi maalum ilibaini kuwepo kwa watumishi waliohusika moja kwa moja katika zoezi la kutoa chanjo ya Surua-Rubella lakini hawakulipwa jumla ya Sh.82,725,000 licha ya bajeti kwa ajili ya malipo yao kuwepo. Waathirika katika kadhia hii kwa asilimia kubwa, walikuwa ni madereva na watendaji wa kata.Na waliahidiwa wangelipwa endapo fedha zingekuja lakini hadi wakati wa ukaguzi huu walikuwa hawajalipwa.

(f) Malipo ya huduma hewa ya chakula kwa kutumia nyaraka za kughushi Sh.316,292,995

Nyaraka za matumizi ya Sh.316,292,995 zinahusiana na huduma ya chakula ambayo haikutolewa. Nyaraka hizo zilikuwa ni za kugushi na zilikataliwa na watoa huduma wenyewe kwa maelezo kuwa hazikuwa zao au hawakuziandika wao. Ukaguzi ulibaini kuwa nyaraka hizo zilikuwa za kughushi kutokana na kuwapo kwa kasoro mbalimbali ikiwa ni pamoja na mihuri iliyotumika kutofautiana na mihuri halisi tuliyoipata kutoka kwa watoa huduma hao. Saini zilizotumika kwenye nyaraka hizo hazifanani na saini halisi zinazotumika kwenye vitabu vya wazabuni hao. Muonekano halisi wa nyaraka za mzabuni unatofautiana na ule wa hati zilizoambatishwa kwenye marejesho ya matumizi. Baadhi ya nyaraka za kughushi zinamtambua Katibu Mkuu Wizara ya Afya kama mhusika aliyepatiwa huduma wakati huduma zikitolewa katika Halmashauri.

(g) Manunuzi na matumizi ya mafuta yaliyofanywa kwa udanganyifu Sh.248,034,893

Mafuta yenye thamani ya Sh.248,034,893 yalionekana kununuliwa kwa ajili ya shughuli za chanjo. Hata hivyo, madaftari ya kuratibu safari za magari yaliyopewa mafuta hayo yamebainisha kuwapo kwa taarifa zisizo na uwiano na hivyo kubainisha kuwa mafuta hayo yalitolewa kwa udanganyifu kutokana na kutokuwapo kwa mtiririko wa namba za stakabadhi. Stakabadhi hizo zimepewa namba tofauti na mtiririko wa tarehe husika. Mahojiano na baadhi ya madereva yamebainisha kwamba, mafuta hayo hayakuwa halali na katika maelezo yao wamekana kuyatambua mafuta ambayo yanasemekana kutumika kwenye magari yao. Madaftari ya kuratibu safari za gari hayakujazwa kwa usahihi, kwani hayakuwa na taarifa ya jina la afisa aliyekuwa anatumia gari, kiasi cha mafuta yaliyotumika, mahali gari lilipokwenda wala shughuli ya safari hiyo.

(h) Mafuta ambayo hayakuthibitika matumizi yake Sh. 372,398,769

Kiasi cha Sh.372,398,769 kilitumika kulipia mafuta wakati wa zoezi la Surua-Rubella katika Mamlaka za Serikali za mitaa 55. Ambapo, ufuatiliaji wa matumizi ya mafuta hayo ulibaini kuwa mafuta yote hayakuingizwa kwenye leja ya mafuta, hivyo kutokuweza kuthibitisha matumizi halisi. Hii ni kinyume na Agizo la 54 (3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mtaa ya mwaka 2009. Pia vitengo vya manunuzi vya Halmashauri husika havikuwa na taarifa yeyote kuhusiana na ununuzi wa mafuta hayo na havikuhusishwa hata kidogo katika ununuzi wake.

(i) Kutohakikiwa kwa mafuta yaliyotumika katika magari Sh 364,884,950

Agizo la 89 (3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaagiza kila gari la Halmashauri kuwa na daftari la kuratibu safari, kuweka kumbukumbu za gari kwa kila safari ya gari na kuweka kumbukumbu ya mafuta yaliyopokelewa na gari husika. Kinyume na matakwa haya, ukaguzi maalum umeshindwa kupata uhalali wa matumizi ya mafuta yaliyogharimu kiasi cha Sh. 364,884,950 yaliyotumika katika kutekeleza zoezi la chanjo kutokana na ama daftari la

kuratibu safari za gari kutowasilishwa kwa ukaguzi (Sh.230,652,189) au kutoonesha kiasi cha mafuta kinachosemekana kununuliwa na kuwekwa kwenye gari husika (Sh.134,232,761). Hiki ni kiashiria kuwa mafuta hayo hayakutumika kwa shughuli zilizokusudiwa.

(j) Matengenezo ya magari yasiyothibitishwa Sh. 137,743,754

Kiasi cha Sh.137,743,754 kilitumika kwa ajili ya kutengeneza magari mbalimbali yaliyotumika katika zoezi la chanjo. Hata hivyo, uhalali wa matengenezo hayo haukuweza kuthibitishwa, kwani baadhi ya karakana hazikuwemo kwenye orodha ya karakana zilizoteuliwa kufanya matengenezo hayo. Aidha, wamiliki wa karakana walikataa kuyatambua matengenezo hayo huku madereva kwa upande wao walikana kuyafahamu matengenezo yaliyodaiwa kufanywa kwenye magari waliyokuwa wanayaendesha kipindi cha chanjo.

Mapendekezo

Mfumo wa udhibiti wa ndani uimarishwe ili kuhakikisha kuwa malipo ya huduma yanafanyika tu pale huduma inapokuwa imetolewa. Pia hatua za kinidhamu na za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika waliotajwa kufanya marejesho ya matumizi kwa kutumia nyaraka za wazabuni za kughushi na kiasi cha fedha kilicholipwa kwa huduma isiyotolewa kirejeshwe na wahusika waliotajwa.

Mapendekezo

Mamlaka husika iwachukulie hatua stahiki wote waliohusika kufanya matengenezo hewa ya magari kwa malipo ya Sh. 137,743,754 na kuhakikisha fedha zilizotumika bila manufaa kwa Serikali zinarejeshwa. Aidha, karakana (M/s Buhi Auto Garage na Eckernford Working Group) za Tanga zilizoshirikiana na watumishi kufanya matengenezo hewa zichukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria

Mamlaka za uchunguzi hasa Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai ifuatilie kwa karibu uhalali wa matumizi ya fedha mbazo zilionekana kulipwa kwa Maafisa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao walikanusha kuyafahamu malipo hayo.

12.2 Muhtasari wa Masuala yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi wa Taarifa za fedha za Vyama vya siasa

Nilifanya taratibu za ukaguzi ilikupata ushahidi kama Vyama vya Siasa vinazingatia Sheria husika kuhusu mambo ya fedha, usimamizi wa fedha na mambo mengine. Matokeo ya ukaguzi wangu juu ya kutozingatia masuala maalum katika Sheria husika yameoneshwa hapo chini:

(a) **Miamala isiyo na uhalisia**

Nimebaini uandaaji duni wa vitabu vya msingi vya hesabu kama vile mizani ya majaribio, daftari za fedha taslimu, kitabu cha kila akaunti na vitabu vikuu ambavyo hutoa taarifa za kuaminika katika kuwasilisha taarifa za fedha, hivyo taarifa nyingi za fedha zilikosa nyaraka na kupunguza mtiririko wa hatua za ukaguzi (Audit trail), usahihi, uwazi na kuaminika kwa taarifa. Sikuweza kuthibitisha kama vitabu vya kutunza hesabu viliandaliwa. Vyama vya Siasa vilivyoathirika ni pamoja na Chama cha Alliance for Tanzania Farmers, ACT Wazalendo,Tanzania Democratic Alliance-TADEA), Chama Cha Kijamii, Alliance for Democratic Change Tanzania-ADC, Chama cha Demokrasia (Democratic Party), Demokrasia Makini, Chama Cha Sauti ya Umma (SAU), National League for Democracy na United Democratic Party.

*Ili kuwa na ufanano wa kumbukumbu za uandaaji wa Hesabu, nimeona ni muhimu kwa Wizara ya Fedha na Mipango (Mhasibu Mkuu) kwa kushirikiana na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (*NBAA*), kutunga sheria, kusimamia namna ya kutunza vitabu vya fedha za vya vyama vya siasa na kuanzisha kanuni za kutambua mapato, gharama, mali, Madeni na vyanzo vya fedha*

Kuna mapungufu na Uandaaji duni wa kumbukumbu za Uhasibu yaliyoonekana kwenye baadhi ya vyama vya Siasa. Baadhi ya taarifa za fedha zilitofautiana na misingi ya Uhasibu na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Muundo na mwaka wa Hesabu vinatofautiana na havioneshi taarifa muhimu juu ya msingi wa uandaaji wa taafira za fedha, pia kutokuwepo kwa sera za uhasibu na maelezo ya ziada kwenye taarifa za fedha kulizuia mawanda ya ukaguzi. Vyama vilivyoathirika ni chama cha Alliance for Tanzania Farmers, ACT-Wazalendo, Tanzania Democratic Alliance (TADEA), Chama cha Kijamii, Alliance for Tanzania Democratic Change, Democratic Party, Demokrasia Makini, National League for democracy, Chama cha Sauti ya Umma (SAU), na Chama cha United Democratic

Ni muhimu kwa vyama vya siasa vilivyokaguliwa kutumia mfumo wa udhibiti wa ndani wenye ufanisi ili kuhakikisha utii wa sheria, usimamizi wa gharama na Mafanikio ya usimamizi wa rasilimali za fedha na mali nyingine, na kuongeza kiwango cha uelewa na Wajibu wa watu wanaohusika *katika shughuli za chama cha Siasa*

Kukosekana kwa Mfumo wa uandaaji wa Hesabu za Vyama tisa (9) vya siasa vilivyokaguliwa kwa sababu taarifa zilizowasilishwa zilikuwa ni taarifa za mapato na matumizi na taarifa hazikujumuisha habari za jumla kuhusu chama na maelezo ya ziada kwenye taarifa za fedha. Mfumo bora wa kuandaa hesabu ni kiungo muhimu kwa ajili ya kukuza uwajibikaji na uwazi. Mfumo hutoa dhana na vigezo vya uandaaji wa hesabu. Kutokana na kukosekana kwa taarifa za mfumo wa fedha, sikuweza kutambua vipimo, utambuzi, uandaaji na uoneshaji wa vitu vyote muhimu katika Taarifa za fedha. Mbali na hiyo, watumiaji wa Taarifa za fedha wasingeweza kutafsiri habari zilizomo katika Taarifa za fedha.

Namshauri Msajili wa Vyama vya *Siasa, kwa kushirikiana na Mhasibu Mkuu wa Serikali na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi, kuanzisha uoanishaji unaofanana wa mfumo wa uandaaji wa Hesabu.*

(b) **Kutowasilishwa kwa Taarifa za Fedha**

Katibu Mkuu wa kila chama cha Siasa ana jukumu la kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa ajili ya ukaguzi. Kifungu cha 14 cha Sheria Na.5 ya

Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (Iliyorejewa 2015) inataka kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kutunza vitabu sahihi vya fedha na mali za chama na kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya fedha ya kila mwaka ya chama cha siasa iliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na kutoa maoni juu ya Hesabu hizo.Pia kuwasilisha na tamko la kila mwaka la mali zote zinazomilikiwa na Chama.
Vyama vinne (4) vyenye usajili wa kudumu kati ya kumi na tisa (19) vilivyokaguliwa havikuwasilisha taarifa za fedha za kila mwaka kama inavyotakiwa na Kifungu cha 14 (1) (i) cha Sheria Na.5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (illiyorejewa 2015). Vyama hivyo ni National Reconstruction Party (NRA), United Peoples Democratic Party (UPDP)), Chama cha Ukombozi wa Watu (CHAUMMA) na Umoja for Multiparty Democracy (UMD).

Mbali na hiyo ukaguzi wa Vyama viwili vya siasa ulikuwa bado haujahitimishwa kama ifuatavyo

	Jina la chama	**Mwaka**	**Maoni**
1	Chama cha Wananchi-CUF	Miezi sita kuanzia Januari 2015 hadi Juni 2015	Mgogoro unaoendelea Miongoni mwa viongozi wa kisiasa umesababisha tushindwe kufanya kikao cha kumaliza kazi
2	NCCR-MAGEUZI	2013/2014	Uongozi ulijikita zaidi kwenye shughuli za kisiasa na kushindwa kujibu barua za mapungufu ya Ukaguzi; matokeo yake tulishindwa kufanya kikao cha Kumaliza kazi

Namshauri Msajili wa Vyama vya Siasa kuwawajibisha viongozi wa vyama vilivyoshindwa *kuwasilisha kwa wakati taarifa za fedha kwa ajili ya Ukaguzi*

(c) **Kukosekana kwa Taariza za Akaunti ya Benki**

Vyama vitatu (3) kati ya kumi na tatu (13) vilivyokaguliwa havina akaunti za benki kama inavyotakiwa katika kifungu cha 15 cha Sheria Na.5 ya vyama vya Siasa ya mwaka 1992(Iliyorejewa 2015). Vyama hivyo ni Demokrasia Makini, Chama cha Kijamii na Chama cha Alliance for Democratic Change-ADC.

Uzingatiaji wa Sheria inayoongoza Vyama vya Siasa ni jambo la lazima. Nashauri Vyama vya Siasa kufuata sheria na kanuni

(d) **Mapungufu katika usimamizi wa rasilimali watu**

Ukaguzi wangu wa majalada ya wafanyakazi wa Vyama vya siasa umebaini kuwa vyama vingi vya siasa vina wafanyakazi wa kujitolea isipokuwa Makatibu Wakuu .Na hakuna mikataba ya ajira yenye nguvu za kisheria inayoeleza majukumu,uwajibikaji na malipo ya wafanya kazi, Zaidi ya hayo,Nimebaini kuwa wakuu wa vitengo vya Fedha hawana uwezo wa kitaalamu wa nafasi zao.

Majukumu ya Idara ya fedha kwa ajili ya usimamizi wa masuala ya fedha yanajumuisha kuanzisha na kuandaa taarifa za fedha na mifumo ya udhibiti, kusimamia fedha na kutumia hizo taarifa na kuzichambua ili kushauri uongozi kuhusu mipango, sera na Uwekezaji wa mitaji. Wadau wote wanashauriwa kushiriki katika kuunda sera za usimamizi wa rasilimali watu kwa Vyama vya Siasa.

(e) **Kutotenganishwa kwa Ardhi na Majengo**

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IAS 16), Ardhi ni mali isiyochakaa, na hivyo, kuna haja ya kuiandika katika kundi lake ili kuitofautisha na mali nyingine. Mapitio ya Taaffa za Fedha za Chama cha Mapinduzi(CCM) na majedwali ya Mali, Mitambo na Vifaa, ilibainika kuwa thamani za Ardhi na majengo havikutenganishwa kama inavyotakiwa na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu.

Kutotambua thamani ya ardhi ambayo ina asili ya kupanda thamani kunachangia kwa kiasi kikubwa kushusha thamani mpaka sifuri kwenye vitabu vya chama na kusababisha

uandaaji wa mizania ya Hesabu usioakisi hali halisi. Nashauri uongozi wa chama kufanya tathimini ya ardhi kwa kuitofautinsha na majengo.

(f) **Kutokuwepo Kwa rejista ya Mali za kudumu**

Tumebaini kuwa Chama na matawi yake hawana rejista ya Mali za Kudumu. Hii inakinzana na matakwa ya kanuni ya 7.1.3 ya Kanuni za fedha na mali za mwaka 1997. Tunasisitiza pendekezo letu kwa uongozi wa chama kuanzisha rejista ya mali ili kuimarisha udbibiti wa mali za Chama. Mapitio ya sampuli yetu yamebaini maeneo ambayo hayaandai rejista. Maeneo hayo ni CCM-Makao makuu,CCM Dar es Salaam,CCM Kinondoni, CCM Ilala, CCM Temeke,Jumuia ya Wanawake, Jumuiya ya Vijana, Uhuru publication, PMCL

(g) **Kutoandaa kwa rejista ya vitabu vya fedha (Counterfoil Register)**

Katika matawi ya CCM na Taasisi zake kuna mwenendo wa uandaaji warejista za vitabu vya fedha kwa ajilii ya kuandikia nyaraka za uwajibikaji kwa malengo ya udhibiti kama vile kitabu cha hundi, kitabu cha stakabadhi n.k. Nyaraka hizi zisipoandikwa vizuri zinaweza kutumika kwa maslahi binafsi. Mapitio ya sampuli yamebaini kuwa CCM Dar es Salaam, CCM Temeke, Jumuiya ya Vijana, shirika la uchapishaji la Uhuru na Shirika la Habari, hawaandai rejista ya vitabu vya fedha.

(h) **Kutoandaliwa kwa taarifa za usululishi wa Benki**

Udhibiti wa ndani unaohusiana na usululishi wa salio kwenye kitabu cha fedha taslimu na salio kwenye taarifa za benki haukutekelezwa ipasavyo. Taarifa za fedha zilizoandaliwa na Vyama vya Siasa zinaweza kuwa zinapotosha. Wakati wa Ukaguzi nilibaini kuwapo kwa utofauti wa salio katika vitabu vya fedha taslimu na salio la benki. Hata hivyo,tulishindwa kupata maelezo ya hizo tofauti na hapakuwepo na taratibu mbadala ambazo zingetumika kutambua asili ya hizo tofauti. Vyama vya Siasa vilishindwa kusululisha salio katika vitabu vya fedha taslimu na salio katika taarifa za benki ikiwemo CCM Dar es Salaam, CCM Ilala,Jumuiya ya Wanawake, Jumuiya ya Vijana, Jumuia ya Wazazi , Shirika la Habari na Kikundi cha kwaya(Tanzania One Theater), chama cha Alliance for Tanzania Farmers Party, ACT-Wazalendo, Tanzania Democratic Alliance (TADEA), Chama cha Kijamii, Alliance for

Tanzania Democratic Change, Democratic Party, Demokrasia Makini, Chama cha Sauti ya Umma (SAU), National League for democracy na United Democratic Party havikuandaa usululishi wa benki.

Napendekeza kuwa tofauti zilizoonekaza zichunguzwe na taarifa za usululisho wa benki kwa kila Mwezi ziandaliwe Kama tofauti haiwezi kutatuliwa , kiasi hicho kirejeshwe tena.

(i) **Mapendekezo**

Ili kuongeza uwazi, uwasilishaji na ulinganisho wa ufanisi wa Vyama vya Siasa, vyama vinapaswa kuandaa taarifa za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu. Utumiaji wa mfumo unaofanana katika kuandaa Hesabu utasababisha kutobadilikabadilika na kufanana wa kuandika miamala na kuandaa taarifa za fedha za vyama vya siasa.

Vyama vya Siasa vinapaswa kuandaa taarifa za fedha katika namna ambayo inafanana na tamko la kiufundi la Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi ya mwaka 2009 inayoeleza kuwa Tanzania imeanza kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhanndaaji wa Hesabu (IFRS) na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma (IPSAS) kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 na kila Taasisi iwe ndogo au kubwa zinapaswa kuandaa taarifa za fedha kulingana na IFRS au IPSAS kwa kadri itakavyowezekana

(j) **Changamoto**

Kifungu cha 14 (1) cha Sheria Na.5 ya mwaka 1992 kinanitaka kukagua vyama vya Siasa. Hatahivyo, wakati wa ukaguzi nimekumbana na changamoto juu ya ukaguzi wa hela zisizo za umma zilizokusanywa na Vyama vya Siasa. Kulingana na majukumu ya kikatiba chini ya ibara ya 143(2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napaswa kukagua fedha na rasilimali za Umma.

Namsihi Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa na mpango wa kujenga uwezo utakaoongeza uwezo kwa Vyama vya Siasa kuzingatia mahitaji ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2009 (Iliyorejewa 2015) pamoja na kanuni zake.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

13.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo ya jumla kwa masuala yaliyojitokeza kwenye taarifa hii. Mapendekezo hayo yanahitaji mpango kazi na kushughulikiwa na Serikali, Bunge pamoja na Menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu. Mapendekezo haya kwa sehemu kubwa yametokana na taarifa za Ukaguzi za taasisi husika zilizowasilishwa kwa kila Afisa Masuuli wakati wa ukaguzi pamoja na maswala mengine ya muhimu ambayo umma unapaswa kuyafahamu.

Kwa ujumla, Wizara, Idara, Wakala na taasisi nyingine za Serikali zinashauriwa kuanzisha mfumo na utaratibu ambao unaweza kushughulikia masuala ya maslahi ya umma pamoja na usimamizi makini wa raslimali za umma kwa ufanisi bila kuathiri ubora wa huduma zinazotolewa na Serikali.

Napenda kutoa mapendekezo ya ujumla kuhusu matokeo ya Ukaguzi wa Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Wakala wa Serikali, Mifuko Maalum na Taasisi nyingine kama ifuatavyo:

13.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya yaliyopita

Ili kuongeza faida kamili zinazotokana na utekelezaji wa mapendekezo ya awali ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali na malengo ya jumla ya ukaguzi, natoa ushauri wa dhati kwa Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuuli kuweka juhudi zaidi katika kuhakikisha kwamba mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali yanafanyiwa kazi ipasavyo.

Mapendekezo mengi ama utekelezaji wake unaendelea au haujafanyika kabisa na kusababisha kujirudia kwa hoja za miaka ya nyuma ikiwa ni ishara kwamba mapendekezo yangu na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali hayachukuliwi kwa uzito unaotakiwa na Maafisa Masuuli. Hivyo, Mlipaji Mkuu wa Serikali anashauriwa kuendelea kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuhuli kuchukua hatua za lazima kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani,ambayo ni vyanzo

vikuu vinavyochangia kuchelewa kutekeleza mapendekezo yangu na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali.Maafisa Masuuli pia wanashauriwa kutunza vizuri kumbukumbu za mipango kazi yao ili kuwongoza juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu za Hesabu za Serikali na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali. Mpango kazi utafanua muda, mtu na namna ya kutekeleza mapendekezo.

13.3 Usimamizi Wa Fedha Za Umma

Makusanyo ya mapato ya ndani yameonesha mwenedo chanya katika kipindi cha miaka minne mfululizo. Pamoja na makisio ya mapato kuongezeka na ukusanyaji wa mapato kukua, bado kumekuwa na changamoto kama vile bajeti kupunguzwa, fedha nyingi kutolewa mwishoni mwa mwaka wa fedha na kutofikia malengo ya makusanyo kusudiwa.

Bila ya kuwa na bajeti halisi, malengo ya uendeshaji na ya kimkakati ya Taifa kwa ujumla yatafikiwa kwa kutumia mikopo ya ndani, nje na kwa kutegemea misaada ya wahisani ambayo, kwa upande mwingine ina madhara katika ukuaji wa uchumi.

Mikopo ya Ndani hutumika zaidi katika kusaidia bajeti na kulipa amana za Serikali zilizoiva (Rollovers). Kuendelea kutegemea washirika wa maendeleo ambao wanatoa fedha kwa masharti na wakati mwingine, hawatoi kabisa kunaweza kuchelewesha matokeo tunayotegemea kwa wakati. Katika mwaka wa fedha 2015/16 tulitegemea kupokea kutoka Akaunti ya Changamoto za Milenia Tanzania (MCA (T)) kiasi cha shilingi bilioni 347.80, lakini hawakutoa fedha yeyote. Pia tulitegemea kiasi cha shilingi bilioni 660.34 kutokana na misaada na mikopo yenye masharti nafuu ya kibajeti ila kilipatikana kiasi cha shilingi bilioni 291.38 (sawa na asilimia 44 ya lengo kusudiwa). Hii ina maana shughuli zote za maendeleo zilizopangwa kutekelezwa kwa kutumia fedha hizo hazikutekelezwa.

Ninapendekeza Serikali itafute vyanzo mbadala vya mapato ya ndani na kuendelea kuziba mianya mbalimbali inayotumika kukwepa kulipa kodi. Serikali, kupitia mamlaka ya nidhamu niwanashauri kuchukua hatua za kinidhamu, dhidi ya wafanyakazi wasio waadilifu pamoja na kuboresha udhibiti wa

ndani katika mifumo ya ulipaji kodi ambayo itasaidia wafanyabiasha na kufanya kazi zao kwa uhuru na kulipa kodi kwa hiari. Pia, kuhakikisha matumizi bora ya mifumo wa kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kupunguza upotevu wa mapato. Udhibiti na uhamasishaji zaidi juu ya matumizi ya vifaa vya kieletroniki katika kukusanya mapato, kwani wengi wamekuwa hawatumii vifaa hivyo kwa madai ya matatizo ya kimtandao. Matokeo zaidi yanapatikana katika sura ya nne ya taarifa hii.

13.4 Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara

Usimamizi wa rasilimali watu na mishahara umeendelea kuwa na changamoto kadhaa katika Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Taasisi zingine. Dosari ambazo zimeendelea kujitokeza ni: kulipa mishahara kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma, makato mbalimbali ya kisheria yaliyokatwa kwenye mishahara ya watumishi ambao sio watumishi wa Umma, kuchelewa na kutokupeleka makato ya kisheria ya watumishi kwenye taasisi husika, watumishi kukaimu nafasi zaidi ya muda unaokubalika kisheria, posho ya kukaimu nafasi mbalimbali kutokukatwa kodi, upungufu wa watumishi, baadhi ya taasisi kushindwa kufanya tathmini na kupima utendaji wa watumishi, dosari katika utunzaji wa kumbukumbu za watumishi, kutokulipa stahili mbalimbali za watumishi na baadhi ya waajiri kushindwa kutekeleza sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kadri kifungu cha 20 kama kilivyorekebishwa mwaka 2007 kinavyotaka waajiri kuijulisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuhusu wanufaikaji na kuanza kuwakata na kuwasilisha makato hayo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mapungufu katika usimamizi wa rasilimali watu yanaathiri ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya serikali. Hivyo, naendelea kupendekeza kuwa Serikali ihakikishe na kuzingatia matumizi bora ya rasilimali watu pamoja na kuipatia miongozo ili kupunguza mapungufu yaliyobainika katika taarifa yangu kwa ajili ya kulinda maslahi ya waajiri na waajiriwa ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

13.5 Wakala wa Serikali, Taasisi nyingine na Mifuko Maalum

Matokeo ya Ukaguzi ya Wakala wa Serikali, Taasisi nyingine pamoja Mifuko Maalum yanaonesha kuendelea

kutozingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba. Hali hii inaashiria kuwa Maafisa Masuuli, Watendaji Wakuu na Menejimenti kwa ujumla hawazingatii ushauri ninaokuwa nikiutoa kwao. Menejimenti za Wakala wa Serikali, Mifuko ya Fedha, Taasisi nyingine na Bodi za Maji zihakikishe utunzaji unaostahiki wa nyaraka na unaozingatia Sheria.

Miongoni mwa mapungufu niliyoyabaini wakati wa ukaguzi ni pamoja na kufanya matumizi kwa shughuli zisizokusudiwa. Aidha, kuwapo kwa malipo ambayo yalikosa mchanganuo wa namna yalivyotumika. Taasisi zilizohusika na mapungufu haya ni ALAT, Mfuko wa Rais wa Udhamini, Wakala wa Majengo, SUMA Agri Machinery, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza, Mfuko wa Mikopo wa Hazina ambazo Maafisa Masuuli wake wanapasa kuwajibika kwa matumizi hayo mabaya ya Fedha.

Ninashauri Maafisa Masuuli kutathmini mara kwa mara ili kubaini viashiria hatarishi vya matumizi mabaya ya fedha pamoja na kutenga bajeti ya kutosha ya kulipa madeni. Aidha, Menejimenti za Taasisi husika zishirikiane na Wizara husika ili kuwepo uwezeshaji kwa wakati wa utoaji fedha za kulipa madeni kwa wakati.

Ninashauri Wakala za Serikali kuhakikisha kuwa zinafanya ufuatiliaji wa karibu kwa wafanyabiashara wasio tii sheria bila shuruti matakwa ya sheria inayowahitaji kutumia mashine za EFD ikiwa pamoja na kuwachukulia hatua wakiukwaji.

13.6 Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Ukaguzi nilioufanya umeniwezesha kubaini endapo Vyama vya Siasa vimezingatia Sheria za fedha na kanuni zake katika masuala yahayohusu usimamizi wa fedha. Sura ya kumi na mbili (12) ya ripoti hii imefafanua kwa kina mapungufu niliyobaini wakati wa ukaguzi ambayo yametokana na ukiukwaji wa sheria na mapendekezo ambayo nimekuwa nikiyatoa.

Mapungugu hayo ni pamoja na uandaaji usioridhisha wa Taarifa za Hesabu za Fedha kama Mizani ya Hesabu za Fedha, Daftari la Mapato na Matumizi, Leja za Akaunti, Leja kuu na kutowasilisha Taarifa za Hesabu za Fedha kwa CAG.

Mapungufu mengine ni kutokuwa na Akaunti rasmi za benki, Kutoandaa Daftari la kurejista Nyaraka Muhimu za Fedha, Rejista ya Mali za Kudumu, Kutofanya usuluhishi wa Daftari la Mapato na Matumizi dhidi ya Akaunti ya Benki na kutoandaa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya hesabu za Umma (IPSAS Acrual).
Kuhusu uandaaji wa hesabu kwa viwango vinavyofanana, ninamshauri Mhasibu Mkuu kwa kushirikiana ana Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) kutoa Mwongozo wa kuratibu namna sahihi ya uandaaji wa Hesabu za Vyama vya Siasa ikiwa ni pamoja na Kanuni za Utunzaji wa Taarifa za Mapato na Matumizi, Mali za Kudumu, Madeni, na Vyanzo vya Mapato.

Ninamshauri Msajili wa Vyama vya Siasa aandae utaratibu wa kuwajengea uwezo watendaji wa Vyama vya Siasa ili waweze kuboresha utendaji wao wa kazi uendane na matakwa ya Kanuni na Sheria ya Vyama vya Siasa,2009 (Iliyorekebishwa 2015).

13.7 Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

Kama ilivyoelezwa awali, Manunuzi ya Umma yanatumia kiasi kikubwa cha Rasilimali za Serikali ili kutekeleza shughuli zilizopangwa. Hivyo Serikali inatakiwa kuboresha uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni za Ununuzi wa Umma GN 446 ya 20 Desemba 2013 pamoja na marekebisho ya sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2016 ili kuepuka kujirudia kwa Mapungufu yaliyobainika. Mapendekezo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa ili kuweza kuboresha uzingatijia wa Sheria:

i) Serikali kupitia Wizara ya Fedha itenge fedha za kutosha kuweza kugharamia miradi ambayo haijakamilika kutokana na kukosa fedha za kutosha.

ii) Serikali itekeleze Miradi Mikubwa kwa awamu ili kuepuka gharama za ziada zinatokana na tozo za kuchelewesha Malipo kwa Wakandarasi.

iii) Serikali iboreshe uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa rasilimali watu na fedha ili iweze kuhakiki mikataba yote kikamilifu kabla haijasainiwa na Taasisi za Manunuzi. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itahusika na usimamizi wa mikataba yote yenye maslahi ya Taifa; na inapobainika mikataba kutokuwa na maslahi kwa Taifa, Afisa aliyehusika kuhakiki atawajibishwa.

iv) Serikali kupitia PPRA, kuendesha Mafunzo ya kujenga uwezo ya mara kwa mara kwa Kitengo cha Manunuzi, bodi ya Zabuni,Afisa Masuuli na Watumia huduma ili kuweza kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni za Ununuzi wa Umma GN 446 ya 20 Desemba 2013

v) Mfumo wa Utunzaji wa taarifa za Manunuzi kielekroniki kufanya kazi kwa ufanisi. Mfumo huu upo chini ya PPRA. Hivyo, PPRA inatakiwa kuhakikisha Mfumo huu unakuwa rafiki kwa watumiaji ili Taasisi za Serikali Kuu kuweza kutumia katika kuboresha ufanisi taratibu za manunuzi.

13.8 Mapungufu katika usimamizi wa matumizi ya Taasisi za Serikali Kuu

Licha ya ushauri ninaotoa mara kwa mara katika ripoti zangu zilizopita, tathmini yangu katika usimamizi wa matumizi bado inaonesha kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali Kuu zimeendelea kuwa na udhibiti wa ndani usioridhisha wa usimamizi wa matumizi. Hivyo, kusababisha ukaguzi kubaini mapungufu kama Matumizi yasiyokuwa na manufaa – Sh. bilioni 1.461; Hasara iliyotokana na makato ya NHIF yaliyokataliwa-Sh. Milioni 569.99; Malipo yaliyokosa mchanganuo wa matumizi-Sh. bilioni 6.575; Malipo yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki-Sh. Milioni 77.48; Kukosekana kwa hati za malipo – Sh. bilioni 91.348; Fedha kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa-Sh. bilioni 3.83.

Mapungufu Mengine ni kama Hati za malipo zenye nyaraka pungufu -Sh. Bilioni 12.5; Malipo yaliyofanyika bila kudai risiti za kielektroniki (EFD)- Sh. bilioni 7.79; Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili-Sh. bilioni 4.56; Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa Sh. Milioni 397.5; Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa-Sh. bilioni 4.998; Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi-SH. Milioni

97.72; Taasisi za Umma zisizotoza kodi ya Zuio-Sh. Milioni 990.18; Kulipwa madeni ya miaka iliyopita yasiyokwemo kwenye hesabu za miaka husika -Sh. bilioni 1.379. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye Sura ya Kumi ya Ripoti hii.

Nawashauri Afisa Masuuli wa Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Balozi waendelee kuboresha Mifumo ya ndani ya udhibiti, vile vile wawajengee uwezo Wafanyakazi. Mbali na hayo, utunzaji wa nyaraka unatakiwa kuboreshwa pamoja na uzingatiwaji wa Kanuni.

Kwa upande wa kutozingatiwa matumizi ya EFD na Kodi ya Zuio, narejea mapendekezo yangu kwa Serikali kusitisha kufanya biashara na wazabuni wasiotoa risiti za kielektroniki. Aidha, nazikumbusha Menejimenti za Taasisi za Serikali Kuu kuhakikisha zinatimiza wajibu wa kisheria wa kutoza kodi ya zuio kwa malipo yote wafanyayo kwa wazabuni wa bidhaa na huduma.

Natoa wito kwa Mhasibu Mkuu kuupitia upya Mfumo wa Utunzaji Miamala ya Fedha na Utoaji wa Taarifa za Fedha wa EPICOR ili kuuwezesha Mfumo huo kuhifadhi miamala ya fedha na kutoa taarifa za fedha zinazoendana na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu za Umma (IPSAS accrual). Kwa sasa, Mfumo wa EPICOR hairuhusu uingizaji wa Ankara (LPOs) na Hati za Madai ya Wazabuni walioziuzia Taasisi za Serikali bidhaa au Huduma bila Taasisi hizo kuwa na fedha Taslimu kwa wakati huo.

Pia, ninamshauri Mhasibu Mkuu wa Serikali kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa wakati wa kuandaa makisio ya bajeti zao za matumizi ya kila mwaka kukumbuka kuombea katika bajeti hizo fedha kwa ajili ya kulipa madeni yao. Aidha, wakati wa kufanya malipo, yapasa Maafisa Masuuli kufanya malipo kupitia vifungu husika vya madeni ambavyo ni tofauti na vifungu vya matumizi vya mwaka husika.

13.9 Mapungufu katika usimamizi wa Mali za Kudumu

Usimamizi wa Mali za Kudumu ni muhimu kwa taasisi katika kutekeleza shughuli zake ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa umma. Mapungufu katika usimamizi wa Mali za

Kudumu kunasababisha kuripoti mali kimakosa kwenye taarifa za hesabu, matumizi mabaya au kupotea na huweza kusababisha utoaji wa huduma duni kwa umma.

Dosari zilizobainika katika ripoti hii ni pamoja na: Kukosekana kwa sera ya Mali za Kudumu, magari ambayo hayatumiki, kutokufanyika kwa zoezi la kuthaminisha mali za kudumu, kutokuwa na rejista ya mali za kudumu iliyoboreshwa, ukosefu wa mikakati ya kuendeleza viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya Nchi na ukarabati wa majengo katika balozi za Tanzania nje ya nchi; kutokutenganisha thamani ya ardhi na majengo na arthi na majengo ya Serikali kukosa nyaraka za umiliki.

Nilipendekeza katika ripoti yangu ya mwaka uliopita juu ya kasi ndogo ya utekelezaji wa kuelekea kutambua mali za kudumu na kuzitolea taarifa chini ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu Sekta za Umma (IPSAS accrual) katika maeneo yafuatayo; tathmini ya Mali za Kudumu, Regista ya Mali za Kudumu, kutokuwepo kwa Sera ya Mali za Kudumu. Nazidi kusisitiza mapendekezo yangu kwa Kurugenzi ya Usimamizi wa Mali za Kudumu za Serikali chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kuwa na utaratibu wa ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba Wizara, Idara na Wakala za Serikali pamoja na Sekretarieti za Mikoa wanatekeleza maelekezo yaliyotolewa. Zaidi ya hayo, nashauri Serikali kuhakikisha kuwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali pamoja na Sekretarieti za Mikoa zinapata nyaraka za umiliki ili kulinda mali za Serikali. Nashauri pia Serikali kuchukua hatua muafaka kuhusiana na magari ambayo yamepaki bila kutumika na ambayo hayatengenezwi tena kwa ajili ya matumizi ya Serikali yanauzwa/kutolewa kulingana na sheria na kanuni zilizopo ili kuokoa thamani ambayo inaweza kupatikana. Taratibu kali zinapaswa kuwekwa katika kupunguza muda wa kukusanya mapato ambayo hayajakusanywa au kulipa madeni kwa kuwa na sera ya madeni na madai na ili kuhakikisha kiasi kinachodaiwa kinalipwa ndani ya muda mfupi iwezekanavyo.

Nilibainisha madeni ya muda mrefu katika Taasisi 97 yanayofikia kiasi cha Sh. trilioni 1.979 ambalo ni ongezeko la Sh. trilioni 0.536 kukiwa na ongezeko la asilimia 37

ikilinganishwa na Sh. 1.443 katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015.

Madeni yaliyoripotiwa ni pamoja na kiasi cha shilingi bilioni 19.192 yakiwa ni madeni ya matibabu kwa wagonjwa ambao wamekuwa wakitibiwa katika hospitali za rufaa nchini India.

Pia, nilibaini kesi za kisheria zenye jumla ya madai yanayofikia Sh. bilioni 850.740 katika taasisi 15 zilizokaguliwa, kesi hizo zinasubiri uamuzi wa mahakama dhidi ya makampuni mbalimbali na watu binafsi.

Katika suala la madeni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu, nashauri Serikali kutenga fungu katika bajeti za miaka ijayo ili kulipa madeni hayo na kuepuka migogoro na wazabuni, watumishi na wadau wengine.

Katika upande wa madeni tarajiwa; nashauri Serikali kuelekeza kila Taasisi kuwa na mikakati sahihi ya usimamizi wa vihatarishi ili kuhakikisha kwamba Taasisi zinajikinga kikamilifu katika kupunguza kesi.

13.10 Matokeo ya Kaguzi Maalum

Ukaguzi umejiridhisha kwamba,uongozi,wafanyakazi na watoa huduma na wazabuni wameshiriki kwa namna moja au nyingine katika ubadhirifu na udanganyifu kwenye matumizi ya fedha katika mradi wa kuboredha Vitambulisho vya Taifa unaojumuisha mikataba ya manunuzi ya vifaa vya kuboresha Vitambulisho vya taifa, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kama vile ipad, programu na Vifaa vya kompyuta,upatikanaji wa vibarua,bima za magari na gharama za kusafirisha na kufunga vifaa vya kusajili raia ambapo shilingi bilioni 4.5 zilikuwa na udanganyifu

- Zaidi ya hayo, hali ya usajili na kutoa vitambulisho vya taifa kuwa mpya ilisababishwa na maandalizi hafifu kwa uongozi wa Mamlaka juu ya kuamua jinsi ambavyo mfumo ungeweza kutumika vizuri kulingana na uwezo wa Mamlaka.Hali hiyo ilisababisha mabadiliko ya maelekezo yaliyoigharimu Serikali kupitia manunuzi yasiyo na tija na wakati huo huo, wadanganyifu kutumia

mianya iliyopo kujinufaisha wenyewe kinyume na taratibu

- Mamlaka za kiuchunguzi zichunguze viashiria vya udanganyifu vilivyotambuliwa kama ilivyoelezwa kwenye ukaguzi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya Wahusika.

13.11 Ukaguzi maalum za fedha zilizopokelewa Wizara ya Fedha kutoka "GAVI Alliance"

Masuala mbali mbali yaliyojitokeza katika ukaguzi Maalum kuhusu fedha kutoka GAVI Alliance yanaashiria udanganyifu. Nayo ni kama vile; kukosekana kwa viambatisho katika malipo, kutothibitika mapokezi ya fedha na matumizi yake, malipo hewa ya chakula na posho za mafunzo, matengenezo hewa ya magari na kutozingatia taratibu za manunuzi ya umma.

- Maafisa ambao wamehusika kufanya mgawo wa fedha kinyume na bajeti watakiwe kueleza ni vigezo gani walivitumia katika kugawa fedha hizo kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe kwa maafisa ambao walihusika kufanya mgao wa fedha kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kufuata bajeti na bila kushirikisha Kamati ya Afya ya Mkoa.
- Mamlaka za uchuguzi, hasa Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) zifuatilie kwa karibu uhalali wa fedha zilizoonekana kulipwa kwa Maafisa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao walikanusha kuyafahamu malipo hayo.

13.12 Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na Utawala Bora

Tathmini yangu ya mifumo ya udhibiti na Utawala Bora ililenga utendaji wa Kamati za Ukaguzi, utendaji wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, TEHAMA, usimamizi wa vihatarishi pamoja na utendaji wa Bodi za Uongozi. Kwa ujumla nilibainisha mapungufu katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali pamoja na Sekretarieti za Mikoa juu ya udhibiti wa mifumo ya ndani na utendaji wa Bodi za Uongozi kama yalivyoonyeshwa katika sura ya sita.

Maafisa Masuuli wanawajibika kwa kuanzisha mifumo madhubuti ya Udhibiti wa Ndani ili kufuatilia shughuli za Taasisi na kufanya mabadiliko / hatua za marekebisho ya mifumo wakati uhitaji ukibainika. Huu ni mchakato endelevu wa kuelekeza nguvu katika kuimarisha Udhibiti wa Ndani ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Viambatisho Sura ya Kwanza

Kiambatisho 1.1: Kazi ambazo hazikufanyika kutokana na ukosefu wa fedha

	Kazi/Taasisi	Maelezo
1.	Uaguzi wa SADC	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilitakiwa kuchangia kiasi cha shilingi 400,000,000 kwa ajili ya Ukaguzi wa Sakretariati ya SADC lakini kutokana na uhaba wa fedha kiasi hicho cha fedha hakikutolewa na hivyo kushindwa kushiriki kwenye ukaguzi.
2.	Ukaguzi wa vyama vya siasa	Kati ya vyama vya siasa 14 vilivyoleta taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi ni chama kimoja tu ambacho hakikugaliwa. (CHADEMA).
3.	Kipindi cha Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC).	Ufuatiliaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Serikali Kuu (PAC) mikoani haukufanyika.
4.	Kaguzi maalum	Kaguzi maalum 15 zilizokuwa zimeombwa kufanyika hazikufanyika.
5.	Ofisi za Mahakama za Mikoa	Ofisi za Mahakama za Mikoa (Mahakama Kuu 25, mahakama za mwanzo 113 na mahakama za Wilaya 131); ni Mahakama za Mikoa 4 tu kati ya 25 ziliweza kukaguliwa.
6.	Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi	Vyuo vya Ualimu Tanzania 30 na Ofisi 11 za Kanda za Ukaguzi wa shule hazikukaguliwa.

	Kazi/Taasisi	Maelezo
7.	Shughuli za Uchaguzi	Halmashauri za wilaya 13 kati ya 166 ndizo zilizokaguliwa – Tume ya Taifa ya Uchaguzi.
8.	Ofisi ya Waziri Mkuu	Mfuko wa Maafa wa Taifa – Ofisi 6 za Mikoa hazikukaguliwa.
9.	Jeshi la Ulinzi Tanzania	Kati ya vituo vya malipo 43, vituo 20 tu vilikaguliwa, Hospitali za Jeshi 8 na Shule za Sekondari 6 hazikukaguliwa.
10.	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu 53)	*Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake* - (Mwanza, Mtwara, Mara, Tanga, Ruvuma, Iringa, Mbeya na Arusha) ni vyuo 11 kati ya 50 vilivyokaguliwa.
11.	Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu	CMA – Mikoa 25 TAESA – Mikoa 8 (Mwanza, Kagera, Arusha, Dodoma, Mtwara, Lindi, Mbeya & Iringa) Mikoa 4 tu kati ya 25 ilikaguliwa
12.	Idara ya Huduma za Magereza	(Magereza 9, Bukoba Magereza 11, Musoma Magereza 9, Magereza Tabora, Tanga, Mtwara, Moshi, Singida na shirika la pekee la (Tabora, Bukoba na Musoma) ni mikoa 4 tu ilikaguliwa kati ya Mikoa 25.
13.	Idara ya Jeshi ya Kujenga Taifa	Kambi 11 kati ya 15 zilikaguliwa
14.	Idara ya Uhamiaji	Ofisi 9 za uhamiaji za Mikoa hazikukaguliwa
15.	Wizara ya Nishati na Madini	Vituo 6 vya uchimbaji vya Mikoa havikukaguliwa

	Kazi/Taasisi	Maelezo
16.	Wizara ya Kazi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 98)	i. TANROAD na TEMESA – ni Mikoa 4 tu ilikaguliwa kati ya 10 iliyopangwa kukaguliwa. ii. Mizani zote hazikukaguliwa iii. Barabara kuu za - Dodoma –Singida; daraja la Sibiti; daraja la Kilombero, barabara ya Magore –Turiani na barabara ya KIA-Mererani hazikukaguliwa.
17.	Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi	Mikoa 23 haikukaguliwa (Chuo cha Ardhi Tabora na Morogoro, Mtwara, Lindi, Mbeya, Njombe, Iringa, Morogoro & Morogoro. Mahakama ya Aridhi Nyumba na Makazi)
18.	Idara ya Polisi	Vituo vyote vya Polisi vya nje ya ji havikukaguliwa
19.	Idara ya Zima moto na Uokozi	Vituo vyote vya Polisi vya nje ya ji havikukaguliwa

Viambatisho Sura ya Pili

Kiambatisho 2.1: Orodha ya Taasisi zilizopata hati Zinazoridhisha.

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
	Wizara		
1	4	Ofisi ya Rais Idara ya Usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali.	Inayoridhisha
2	5	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	Inayoridhisha
3	6	Ofisi ya Rais Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Kipaumbele	Inayoridhisha
4	9	Ofisi ya Rais-Bodi ya Mishahara	Inayoridhisha
5	12	Tume ya sheria	Inayoridhisha
6	13	Kitengo cha Uchunguzi wa fedha	Inayoridhisha
7	14	Kikosi Cha Zimamoto	Inayoridhisha
8	15	Tume ya Usuluhishi na Upatanishi	Inayoridhisha
9	16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu	Inayoridhisha
10	20	Ofisi ya Rais-Ikulu	Inayoridhisha
11	21	Hazina	Inayoridhisha
12	23	Idara ya Mhasibu Mkuu	Inayoridhisha
13	24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika	Inayoridhisha
14	25	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	Inayoridhisha
15	26	Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais	Inayoridhisha
16	27	Masajiri wa Vyama vya Siasa	Inayoridhisha
17	28	Idara ya Polisi	Inayoridhisha
18	29	Huduma za Magereza	Inayoridhisha
19	30	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	Inayoridhisha
20	35	Kurugenzi ya mashitaka ya umma	Inayoridhisha
21	36	Sekretarieti ya Mkoa- Katavi	Inayoridhisha
22	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	Inayoridhisha
23	38	Ulinzi (TPDF)	Inayoridhisha
24	39	Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)	Inayoridhisha
25	40	Mahakama	Inayoridhisha
26	41	Wizara ya Katiba na Sheria	Inayoridhisha
27	42	Ofisi ya Bunge	Inayoridhisha
28	44	Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji	Inayoridhisha
29	47	Sekretarieti ya Mkoa- Simiyu	Inayoridhisha
30	49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	Inayoridhisha
31	50	Wizara ya Fedha	Inayoridhisha

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
32	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	Inayoridhisha
33	54	Sekretarieti ya Mkoa Njombe	Inayoridhisha
34	55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	Inayoridhisha
35	56	Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Inayoridhisha
36	59	Tume ya Marekebisho ya Sheria	Inayoridhisha
37	61	Tume ya Uchaguzi	Inayoridhisha
38	62	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	Inayoridhisha
39	63	Sekretarieti ya Mkoa Geita	Inayoridhisha
40	65	Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Welemavu.	Inayoridhisha
41	66	Ofisi ya Rais Tume ya Mipango	Inayoridhisha
42	67	Sekretariati ya Ajira	Inayoridhisha
43	68	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	Inayoridhisha
44	71	Sekretarieti ya Mkoa- Pwani	Inayoridhisha
45	72	Sekretarieti ya Mkoa- Dodoma	Inayoridhisha
46	73	Sekretarieti ya Mkoa -Iringa	Inayoridhisha
47	76	Sekretarieti ya Mkoa Lindi	Inayoridhisha
48	77	Sekretarieti ya Mkoa -Mara	Inayoridhisha
49	79	Sekretarieti ya Mkoa -Morogoro	Inayoridhisha
50	80	Sekretarieti ya Mkoa -Mtwara	Inayoridhisha
51	83	Sekretarieti ya Mkoa -Shinyanga	Inayoridhisha
52	84	Sekretarieti ya Mkoa -Singida	Inayoridhisha
53	88	Sekretarieti ya Mkoa -Dar es Salaam	Inayoridhisha
54	91	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya	Inayoridhisha
55	92	Tume ya Kudhibiti UKIMWI	Inayoridhisha
56	93	Idara ya Uhamiaji	Inayoridhisha
57	96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	Inayoridhisha
58	97	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	Inayoridhisha
59	98	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	Inayoridhisha
60	31	Ofisi ya Makamu wa Rais	Yenye masuala ya msisitizo

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
61	32	Ofisi ya Rais,TAMISEMI, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Yenye masuala ya msisitizo
62	33	Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Maadili ya Umma	Yenye masuala ya msisitizo
63	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	Yenye masuala ya msisitizo
64	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	Yenye masuala ya msisitizo & mengine
65	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	Yenye masuala ya msisitizo
66	53	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	Yenye masuala ya msisitizo
67	58	Wizara ya Madini na Nishati	Yenye masuala ya msisitizo
68	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	Yenye masuala ya msisitizo
69	86	Sekretarieti ya Mkoa -Tanga	Yenye masuala ya msisitizo & mengine
70	99	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi	Yenye masuala ya msisitizo
71	70	Sekretarieti ya Mkoa -Arusha	Yenye masuala mengine
72	74	Sekretarieti ya Mkoa- Kigoma	Yenye masuala mengine
73	75	Sekretarieti ya Mkoa- Kilimanjaro	Yenye masuala mengine
74	95	Sekretarieti ya Mkoa -Manyara	Yenye masuala mengine
75	82	Sekretarieti ya Mkoa -Ruvuma	Yenye masuala mengine
76		Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	
	Ofisi za Balozi		
1	2001	Ubalozi wa Tanzania, Addis Ababa, Ethiopia	Inayoridhisha
2	2002	Ubalozi wa Tanzania, Berlin, Ujerumani	Inayoridhisha
3	2004	Ubalozi wa Tanzania Kinshasa, Congo-	Inayoridhisha

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
4	2006	Ubalozi wa Tanzania – London	Inayoridhisha
5	2007	Ubalozi wa Tanzania – Lusaka	Inayoridhisha
6	2008	Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji	Inayoridhisha
7	2009	Ubalozi wa Tanzania, Urusi	Inayoridhisha
8	2010	Ubalozi wa Tanzania - New delhi-India	Inayoridhisha
9	2013	Ubalozi wa Tanzania Paris, Ufaransa	Inayoridhisha
10	2014	Ubalozi wa Tanzania Beijing, China	Inayoridhisha
11	2015	Ubalozi wa Tanzania Rome, Italy	Inayoridhisha
12	2016	Ubalozi wa Tanzania Stockholm, Sweden	Inayoridhisha
13	2017	Ubalozi wa Tanzania Tokyo, Japan	Inayoridhisha
14	2021	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	Inayoridhisha
15	2022	High commission of Tanzania – Harare	Inayoridhisha
16	2023	Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya	Inayoridhisha
17	2024	Ubalozi wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia	Inayoridhisha
18	2025	Ubalozi wa Tanzania Pretoria, South Africa	Inayoridhisha
19	2026	Ubalozi wa Tanzania Kigali, Rwanda	Inayoridhisha
20	2027	Ubalozi wa Tanzania Abu dhabi, United Arabia Emirates	Inayoridhisha
21	2028	Ubalozi wa Tanzania Bujumbura, Burundi	Inayoridhisha
22	2029	Ubalozi wa Tanzania Muscat	Inayoridhisha
23	2030	Ubalozi wa Tanzania Lilongwe	Inayoridhisha
24	2031	Ubalozi wa Tanzania Brasillia	Inayoridhisha
25	2032	Ubalozi wa Tanzania - Kuala Lumpur	Inayoridhisha
26	2033	Ubalozi wa Tanzania Hague, Netherlands	Inayoridhisha
27	2012	Ubalozi wa Tanzania-Ottawa Kanada	Inayoridhisha
27	2034	Ubalozi wa Tanzania Moroni, Comoro	Inayoridhisha
28	2005	Ubalozi wa Tanzania – Abuja	Yenye masuala ya msisitizo
29	2019	Ubalozi wa Tanzania Brussels, Belgium	Yenye masuala ya msisitizo
30	2020	Ubalozi wa Tanzania wa Kudumu UN	Yenye masuala

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
		– Geneva	ya msisitizo
31	2018	Ubalozi wa Tanzania Washington, DC, Marekani	Yenye masuala mengine
32	2011	Ubalozi wa Tanzania wa Kudumu UN- New York	Yenye masuala mengine
	Wakala		
1	*Wakala*	Wakala wa Mbegu za Killimo Tanzania	Inayoridhisha
2	*Wakala*	Wakala wa Usajili Lesseni na Biashara	Inayoridhisha
3	*Wakala*	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam	Inayoridhisha
4	*Wakala*	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	Inayoridhisha
5	*Wakala*	Wakala wa Serikali wa Mtandao	Inayoridhisha
6	*Wakala*	Chuo cha Mafunzo ya Twakwimu Afrika Mashariki.	Inayoridhisha
7	*Wakala*	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo	Inayoridhisha
8	*Wakala*	Wakala wa Utafiti wa Miamba	Inayoridhisha
9	*Wakala*	Wakala wa Maabara za Serikali	Inayoridhisha
10	*Wakala*	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo	Inayoridhisha
11	*Wakala*	Chuo cha Mafunzo ya Mifugo	Inayoridhisha
12	*Wakala*	Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA)	Inayoridhisha
13	*Wakala*	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	Inayoridhisha
14	*Wakala*	Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi	Inayoridhisha
15	*Wakala*	Tanzania Employment Service Agency	Inayoridhisha
16	*Wakala*	Tanzania Global Learning Agency (TaGLA)	Inayoridhisha
17	*Wakala*	Wakala wa Ndege za Serikali	Inayoridhisha
18	*Wakala*	Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa	Inayoridhisha
19	*Wakala*	Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania	Inayoridhisha
20	*Wakala*	Chuo cha Utumishi wa Umma	Inayoridhisha
21	*Wakala*	Wakala wa Mbegu za Miti	Inayoridhisha
22	*Wakala*	Wakala wa Maabara za Mifugo	Inayoridhisha

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
23	*Wakala*	Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji	Inayoridhisha
24	*Wakala*	Wakala wa Vipimo	Inayoridhisha
25	*Wakala*	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu	Yenye masuala ya msisitizo
26	*Wakala*	Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi	Yenye masuala ya msisitizo
27	*Wakala*	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania	Yenye masuala ya msisitizo
28	*Wakala*	Wakala wa Barabara Tanzania	Yenye masuala ya msisitizo
29	*Wakala*	Chuo cha Taifa cha Utalii	Yenye masuala ya msisitizo & mengine
30	*Wakala*	Wakala wa Majengo Tanzania	Yenye masuala mengine
31	***Wakala***	Taasisi ya Uhasibu Tanzania	Yenye masuala mengine
	Bodi za Mabonde ya Maji na Mamlaka za Maji		
1	BWB	Internal Drainage Basin Water Board	Inayoridhisha
2	BWB	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji	Inayoridhisha
3	BWB	Bonde la Maji la Ziwa Rukwa	Inayoridhisha
4	BWB	Bodi ya Bonde la Maji la Ruvuma na Pwana ya Kusini	Inayoridhisha
5	BWB	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Viktoria	Inayoridhisha
6	BWB	Bodi ya Bonde la Maji la Pangani	Inayoridhisha
7	BWB	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika	Inayoridhisha
8	BWB	Bodi ya Bonde la Maji ya Wami/Ruvu	Inayoridhisha
9	NWSSA	Handeni Trunk Main Water Supply and Sanitation (HTM)	Inayoridhisha
10	NWSSA	Mugango/Kiabakari/Butiama	Inayoridhisha
11	NWSSA	Makonde Plateau Water Supply and Sanitation Authority	Inayoridhisha
12	NWSSA	Wanging'ombe (WSSA)	Inayoridhisha
	Mifuko		
1	Mfuko	Mfuko wa Pembejeo za Kilimo	Inayoridhisha
2	Mfuko	Mfuko wa Usimamizi na Ukaguzi wa vyama vya Ushirika.	Inayoridhisha

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
3	Mfuko	Mfuko wa Uwezeshaji Maendeleo ya Madini	Inayoridhisha
4	Mfuko	Mfuko wa Maji	Inayoridhisha
5	Mfuko	Mfuko wa Taifa wa Maafa	Inayoridhisha
6	Mfuko	Mfuko wa Misitu Tanzania	Inayoridhisha
7	Mfuko	Mfuko wa Hifadhi ya Wanyama Pori	Inayoridhisha
8	Mfuko	Mfuko wa Self-Microfinance	Inayoridhisha
9	Mfuko	Mfuko wa Mikopo ya Hazina	Inayoridhisha
10	Mfuko	Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake	Inayoridhisha
11	Mfuko	Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.	Inayoridhisha
12	Mfuko	Mfuko wa Maendeleo ya Nishati Vijijini.	Yenye masuala ya msisitizo
	Taasisi Nyingine		
1	*Taasisi Nyingine*	Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA)	Inayoridhisha
2	*Taasisi Nyingine*	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	Inayoridhisha
3	*Taasisi Nyingine*	Wakala wa Maabara za Mifugo	Inayoridhisha
4	*Taasisi Nyingine*	Taasisi ya kuthibitisha ubora wa Mbegu	Inayoridhisha
5	*Taasisi Nyingine*	Uongozi Institute	Inayoridhisha
6	*Taasisi Nyingine*	Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika	Inayoridhisha
7	*Taasisi Nyingine*	Taasisi ya Rasilimali ya Madini	Inayoridhisha
8	*Taasisi Nyingine*	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)	Inayoridhisha
9	*Taasisi Nyingine*	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania	Inayoridhisha
10	*Taasisi Nyingine*	Kituo cha Kuunda Mitambo na Magari Tanzania	Inayoridhisha
11	*Taasisi Nyingine*	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania	Inayoridhisha
12	*Taasisi Nyingine*	Baraza la Wakunga na Manesi Tanzania	Inayoridhisha
13	*Taasisi Nyingine*	Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru	Inayoridhisha
14	*Taasisi*	Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi	Inayoridhisha

Na	Kundi	Jina la Taasisi	Hati
	Nyingine		
15	*Taasisi Nyingine*	Baraza la Madaktari wa Macho	Inayoridhisha
16	*Taasisi Nyingine*	Baraza la Madawa Tanganyika	Inayoridhisha
17	*Taasisi Nyingine*	Shirika la Uzalishaji Mali Polisi	Inayoridhisha
18	*Taasisi Nyingine*	Baraza la Wataalamu wa Mionzi na Picha	Inayoridhisha
19	*Taasisi Nyingine*	Bodi ya Usimamizi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali	Inayoridhisha
20	*Taasisi Nyingine*	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Technolojia ya Nelson Mandela	Inayoridhisha
21	*Taasisi Nyingine*	Baraza la Watoa Huduma za Maabara.	Inayoridhisha
22	*Taasisi Nyingine*	Bodi ya Maabara Binafsi za Afya	Inayoridhisha
23	*Taasisi Nyingine*	SUMA-Idara ya Ulinzi	Yenye masuala ya msisitizo
24	*Taasisi Nyingine*	Mamlaka ya Mapato Tanzania	Inayoridhisha
25	*Taasisi Nyingine*	Shule ya Sheria Tanzania	Yenye masuala ya msisitizo
26	*Taasisi Nyingine*	SUMA – Makao Makuu (JKT HQ)	Yenye masuala mengine

Chanzo: Ripoti kwa Menejimenti ya mwaka 2015/16

Kiambatisho Na. 2.2: Taasisi na vigezo vya Hati zenye shaka

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
1. Tume ya fedha ya pamoja (Fungu 10)
Mizania ya Taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2016 inaonesha bakaa ya Vifaa vya Ofisi vyenye thamani ya Sh. 319.55 Milioni na samani zenye thamani ya Sh. 69.50 Milioni. Hata hivyo, uhakiki pamoja na ukaguzi wa Daftari la Mali za kudumu ulibaini kwamba, vifaa vya Ofisi vyenye thamani ya Sh. 63.7 Milioni na samani zenye thamani ya Sh. 5.90 Milioni viliingizwa kwenye Taarifa za Fedha wakati havikuwa vinatumika tena, na vilikuwa kwenye hali mbaya. Mapungufu kwa ujumla yalikuwa na thamani ya Sh.69 Milioni.
2. Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94)
Kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016, Tume iliripoti madeni yenye thamani Sh.1,177,483,777.21 kwenye Taarifa za Hesabu. Hata hivyo ni madeni yenye thamani ya Sh. 729, 194,938.99 tu yalikuwa na Nyaraka za kutosha na madeni yenye thamani ya Sh.448, 288,838.22 hayakuwa na nyaraka za kutosha hali iliyosababisha kushindwa kuthibitisha uhalali wake. Hati za malipo zenye thamani ya Sh. 11, 740,377 hazikuweza kupatikana wakati wa Ukaguzi. Hati za Malipo zenye thamani ya Sh. 53, 538,100 hazikuwa na nyaraka za kutosha kuthibitisha matumizi kinyume na Kanuni ya 86(1),95(4) & 116 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. Mapungufu haya yamepunguza mawanda ya Ukaguzi ya kujiridhisha kuhusu uhalali wa matumizi haya.
3. Shirika la Mzinga
Wadaiwa wenye thamani ya Sh.18,673,675 hawakuingizwa kwenye taarifa za fedha za Mwaka. Mwezi Juni, 2015 Shirika la Mzinga lilichukua mkopo wenye thamani ya Euro 32,588,376 kwa ajili ya manunuzi ya boti. Hata hivyo, yalibainika yafuatayo; i. Mkopo pamoja na manunuzi ya boti hayakuingizwa kwenye Taarifa za Fedha; ii. Nyaraka za ununuzi wa boti hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi; iii. Kwa mujibu wa mkataba, mapato ya kulipa mkopo yatatolewa na kulipwa kwa dola, kwa akaunti ya Escrow, wakati mkopo ulichukuliwa kwa Euro. Hii inaweza kulifanya Shirika la Mzinga

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
kuwa katika hatari kutokana kubadilika kwa viwango vya kubadilisha fedha ingawa hakuna mikakati wa kujikinga dhidi ya hatari hii. iv. Mchanganuo wa mapato kwa ajili ya kuweka kwenye akaunti maalumu (escrow) haukuwekwa bayana kwa ukaguzi.
4. Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Nyasa
Taarifa ya usuluhishi wa fedha za benki ulionesha salio la fedha taslimu kiasi cha Sh. 14,067,033 wakati Mizania ya Taarifa za Fedha ilionesha bakaa ya fedha Taslimu kiasi cha Sh.5,400,460; hivyo, kusababisha tofauti ya Sh. 8,666,573. Mizania katika Taarifa ya Fedha ilionyesha mali za kudumu zenye thamani ya Sh.772,209,394 lakini mchanganuo ulioambatanishwa na Taarifa ya Fedha (Note 18) ulionyesha thamani ya Sh.1,889,278,442. Hali hii ilisababisha tofauti ya Sh. 1,117,069,048 isiyokuwa na maelezo. Ilibainika tofauti ya Ziada (Surplus) ambapo taarifa ya ufanisi wa fedha(Statement of financial performance) ilionesha Ziada (Surplus) ya Sh. 276,082,352 wakati Taarifa ya Mizania (Statement of financial position) ilionesha Ziada ya Sh. 846,043,306 Marekebisho yalifanyika kwenye mali za kudumu yenye thamani ya Sh. 664, 896,148.96. Hata hivyo, marekebisho haya vile vile yalipaswa kufanyika kwenye Kiambatisho cha Orodha ya Vifaa(Note 23-Inventory) lakini hayakufanyika, hivyo kusababisha tofauti ya Shs. 664, 896,148.96 katika Taarifa ya hesabu.
5. Taasisi ya Mafunzo ya Wanyama Pori ya Pasiansi
Ilibainika kuwa kuna wanafunzi 809 waliodahiliwa na kuhitimu kozi mbalimbali za Wanyamapori; ambapo kila Mwanafunzi alipaswa kulipia ada ya cheti ya Sh 5,000 ili kufanya jumla ya Sh. 4,045,000. Hata hivyo taasisi ilionesha Sh. 180,000 kama mapato na kuacha Sh. 3,865,000 bila kutambuliwa. Taarifa za ziada Na.24 kwenye taarifa ya Mizani ya Fedha ilijumuisha madeni ya shilingi 189,904,160. Hata hivyo, hapakuwepo nyaraka toshelevu na majedwali yaTaarifa za fedha . Kutokuwapo kwa nyaraka toshelevu na majedwali, kunafanya usahihi wa hicho kiasi kutoweza kutambuliwa.

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
Pia, matumizi ya Shilingi 19,108,000 yaliyooneshwa kwenye Taarifa ya Ufanisi wa fedha hayakuwa na nyaraka muhimu kama vile hati za madai, risti, hati za kupokelea bidhaa kinyume na kanuni Na 86 na 6(1), 95 (4) na 116 ya Kanuni za Fedha za Umma. Kutokuwepo kwa nyaraka toshelezi kunafanya usahihi wa hicho kiasi kutoweza kutambuliwa.
6. Sekretariati ya Mkoa wa Kagera
Kiasi cha Shilingi 1,805,674,761 kilichojumuishwa kwenye bakaa ya fedha taslimu na fedha linganifu (Cash and cash equivalent) kwenye Raarifa za Mtiririko wa fedha na Taarifa za mizani ya Hesabu hakikuweza kudhibitika kama ni kiasi muhimu, kwani hapakuwepo na Taarifa za Usululishi wa benki zilizowashilishwa na Mkuu wa Hazina ili kudhibitisha salio hilo kinyume na kanuni ya 162 ya kanuni za fedha za umma za mwaka
7. Sekretariati ya Mkoa wa Mwanza
Kiasi cha shilingi 1, 602,627,200 kilichojumuishwa kwenye bakaa ya fedha taslimu na fedha linganifu(Cash and cash equivalent) na Mizani ya Hesabau hakikuweza kudhibitika kwa sababu ya kutoandaa taarifa za usululisho wa benki ambao ungethibitisha hilo salio kinyume na kanuni ya 162 ya Kanuni za fedha za Umma za mwaka 2001. Mlinganisho wa fedha zilizopokelewa ambayo ni msingi wa uandaaji wa hiki kiasi kwenye Taarifa za fedha) na kiasi halisi kilichopokelewa ulibaini kuzidishwa kwa shilingi 37,836,170 ambazo hazikufanyiwa usululisho. Hapakuwepo na maelezo ya kina kutoka kwa uongozi juu ya kilichosababisha huo utofuti.
8. Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora
Mapitio ya Taarifa za Mizani ya Hesabu ya Sekretariati ya Mkoa wa Taboa yalibainika kuwa Shilingi 274,255,792.04 zilioneshwa kama salio la amana kwenye madeni ya muda mfupi; kiasi hicho kilipaswa kuoneshwa kama mapato yaliyopokelewa kabla ya muda wake. Kiasi hicho kilijumuisha salio la msaada wa mradi wa Miombo Woodland, Fedha za TASAF, Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Miradi ya Maendeleo, Programu ya Miradi ya Mendeleo ya Maji na Tume ya Kuzuia UKIMWI. Palikuwepo na upotoshaji wa Shilingi 1,072,048,360 ambao haukurekebishwa katika mwaka uliotangulia. Hivyo, kiasi hicho kiliendelea

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
kuoneshwa kwenye Taarifa za fedha za Mwaka 2015/16. Mapato ya Serikali yalioneshwa chini ya kiwango halisi shilingi 176,616,458,376. Kiasi hiki kinatofautiana na taarifa ya utoaji wa fedha (ukurasa 60-62) wa Shilingi 176,646,458,376 na kusababisha kiasi kilichopokelewa kuoneshwa chini wa kiasi halisi kwa shilingi 30,272,094. Taarifa za ufanisi wa fedha wa Ujira, mishahara na maslahi ya wafanyakazi zilionesha Shilingi 6,809,234,980. Kiasi hiki kilijumuisha makato ya shilingi 842,639,916 badala ya shilingi 875,642,038. Hivyo kupelekea kupungua kwa makato kwa shilingi 33,002,121
9. Wakala wa Manunuzi na Huduma za Ugavi (GPSA)
Salio la kuanzia la Magari mpaka 1 Julai, 2015 lilikuwa shilingi 3,343,920 na hapakuwapo na nyongeza katika mwaka husika.Hata hivyo kiasi cha uchakavu kilichooneshwa cha shilingi 1,247,561,850,shilingi 530,700,093 zilikuwa za magari.Kwa sababu hiyo hatukuweza kutambua msingi ambao ulitumika kutoza uchakavu uliokuwa Zaidi ya thamani hasili ya magali. KAtika mwaka wa Ukaguzi,Wakala ulinunua 7,920 za shajala na kalenda zenye thamani ya shilingi 129,903,840 na shilingi 10,800,000 kwa kufuatana kwa ajili ya kuuzwa kwa Taasisii za Serikali.Mpaka mwisho wa mwaka 2015/16 jumla ya shajala 3138(40%) na kalenda 1263(42) zilibaki bila kuuzwa kwenye ofisi za mikoani na kuonekana kama Bifdhaa mfu.Bakaa za vifaa haikutathiminiwa kwa gharama ya chini na thamani ya uuzaji wa mali kinyume cha aya ya 15 ya IPSAS 12
10. Ubalozi wa Tanzania Cairo, Misri
Taarifa za Mizani wa Hesabu zilionesha fedha za Walipa kodi za shilingi 770,151,462 na limbikizo la faida la shilingi 17,460,522 ambazo zilitofautiana na fedha za Walipa Kodi za shilingi 785,755,656 na limbikizo la Faida la shilingi 38,645,354 zilizooneshwa kwenye Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji Pia hasara ya mabadilikoo ya thamani ya fedha ya shilingi 7,164,855 hayakuoneshwa kwenye Taarifa za Ufanisi wa fedha,Hivyo Faida iliyooneshwa ilizidishwa
11. Shirika Hodhi la Mzinga
Madai ya shilingi 2,022,418,232 hayakuoneshwa kwenye Taarifa za

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.

fedha.Kwa sababu hiyo,madai yalioneshwa chini ya kiasi halisi kwa kiwango sawa

Pia tulibaini marejesho ya masurufu ya shilingi 382,144,314. Hatahivyo maelezo ya urejeshwaji wake haukupatikana kwa ajili ya Uhakiki wa Ukaguzi.Kutokuwepo kwa nyaraka toshelezi za marejesho ya masurufu kumefanya tushindwa kuhitimisha usahii wa hayo marejesho.

Ukaguzi wa Taarifa za fedha na Vitabu vikuu vya fedha vilivyowasilishwa kwa mwaka 2015 ilibainika kuwa kiasi kilichooneswa kama deni la muda mrefu shilingi 2,660,739,357 hakikulingana na kiasi kilichokokotolewa upya kutoka kwenye vitabu vikuu vya fedha shilingi 2,286,109,904. Hivyo kuingizwa juu ya kiwango halisi kwa shilingi 374,629,453.

Kutofanana (kuzidishwa) kwa shilingi 270,930,750; kwani, mradi wa ujenzi ulionesha katika Taarifa za ziada za Taarifa Na.9.1 na Taarifa za fedha shilingi 11,017,676,599 zilitofautiana na gharama zilizokokotolewa kutoka kwenye Vitabu vikuu vya fedha kwa shilingi 746,745,849

Ilibainika kwamba,tarehe 2 Mei,2016 Shirika Hodgi la Mzinga lilipata mkopo usio na riba kuoka Shirika la Mzinga shilingi 126,132,771. Hata hivyo, hicho kiasi cha mkopo ama hakikuoneshwa kwenye taarifa za fedha zinazoishia 30 Juni,2016 au hapakuwapo na idhini ya Bodi.

12. Deni la Taifa (Fungu 22)

Kati ya makubaliano ya mikopo kumi na nne (14) kutoka BADEA, Makubaliano tisa (9) sawa na asilimia (64.3%) yalikuwa na riba isiyolipwa ya Sh. 3.764 bilioni ambayo haikuoneshwa kwenye Taarifa za Madeni. Hivyo, kupelekea Deni la Taifa kuonekana lina upungufu kwa kiasi hiki kwa mwaka unaoishia tarehe 30/6/2016.

Taarifa ya Madeni ya Fungu 22 kwa Mwezi Juni, 2016 inaonesha kuwa Deni la Taifa ni Sh.41,039.387 bilioni. Hata hivyo, Deni hili halikujumuisha deni la Mifuko ya Hifadhi ya jamii lenye thamani Sh.2,991.4 bilioni na dhamana ambazo zimepita muda wake na ambazo masharti yamekiukwa zenye thamani ya Sh. 225.6 bilioni chini ya Msajili wa Hazina; hivyo, kufanya jumla ya Sh. 3,217 bilioni.

Kwa upande mwingine, Serikali ilikuwa na Madeni ya Sh.934 bilioni ambayo

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.

yalikuwa chini ya migogoro na mchakato wa uthibitisho. Kwa maoni yetu, Madeni haya kwa mifuko ya pensheni yenye thamani ya Sh. 934 bilioni yalipaswa kuingizwa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka 2015/16 kama madeni ambayo hayajathibitishwa (Contingent liabilities).

Taarifa za Fedha kwa Mwaka 2015/2016 ziliripoti bakaa ya fedha taslimu (Cash and Cash Equivalent) kiasi cha Sh. 378.9 bilioni , Hata hivyo Taarifa ya usuluhishi wa kibenki ilibaini kuwa kiasi halisi ni Sh.154 bilioni hivyo kusababisha tofauti ya Sh.224.9 bilioni.

Katika Taarifa ya Fedha ya Mwaka 2015/2016 tathimini ya uwezo wa kulipa mafao kwa mifuko ya hifadhi ya jamii (Actuarial valuation of the pension provision) ilikuwa na thamani ya Sh. 393,478,520,000. Hata hivyo, ripoti ya Tathmini hii haikuweza kupatikana ili kujiridha na uhalisia wake kinyume na (IPSAS 25)

13. SUMA – Idara ya Kilimo na Viwanda

Mapitio ya Taarifa za fedha ya SUMA JKT XVI Mgambo yalionesha madeni yenye thamani ya Sh.74,751,259 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi kudhibitisha usahihi wa hilo salio. Kiasi kilichooneshwa kinaathiri taarifaa za Fedha Jumuifu za SUMA –Idara ya Kilimo na Viwanda

14. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu 43)

Katika mwaka wa fedha 2014/15 tulibaini kuwa mali za kudumu zenye thamani ya Shilingi 6,484,994,624 hazikuingizwa katika rejista ya mali za kudumu; hivyo, kutooneshwa kwenye taarifa ya fedha ya mwaka husika. Katika mwaka wa fedha 2015/16, taarifa za fedha zilionesha mali za kudumu zenye thamani ya shilingi 29,521,111,584 kwenye taarifa ya mizania; wakati mwaka uliopita walionesha mali zenye thamani ya shilingi 29,196,805,351 ikiwa na maana kuwa kulikuwa na ongezeko kwenye mali za kudumu la kiasi cha shilingi 324,306,233 ambazo uchakavu haukotozwa kwa sababu ya kipindi cha mpito cha miaka mitano kilichoruhusiwa na Viwango vya Kimataifa visivyo vya misingi ya taslimu 17 (IPASA 17).

Hii inaonesha kuwa kiasi cha shilingi 6,486,994,624 hakikuoneshwa kwenye taarifa za fedha za mwaka uliopita na mwaka huu wa ukaguzi hivyo kupelekea mali za kudumu kutolewa taarifa kwa pungufu ya kiasi tajwa.

Pia, nilibaini kuwa rejista ya hasara haiendani na wakati, kwani kuna

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
hasara ambazo zimeshafungwa tangu mwaka 2010 (Upotevu wa fedha taslimu kiasi cha shilingi 134,959,775 na gari lililoibwa) lakini zimeendelea kuonekana kwenye rejista ingawa zimeshafungwa.
15. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48
Kwenye taarifa za fedha za Wizara noti 52 (Noti 52) ilionesha mali zilizonunuliwa zitumike katika mwaka wa fedha ambazo hadi mwisho wa mwaka wa fedha zilikuwa hazijatumika (inventories) zenye thamani ya shilingi 874,168,355. Hata hivyo, hatukuweza kuthibisha uwepo wa mali hizo. Hati za malipo zenye thamani ya shilingi 5,015,366,196 hazikuwa na zimeambatanishwa na nyaraka muhimu za kuhalalisha malipo hayo kinyume na Kanuni ya 86(1), 95(4) na 116 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001. Kutokana na mapungufu hayo, ukaguzi haukweza kuthibisha uhalali wa malipo hayo. Kinyume na Kanuni ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001, malipo ya posho ya saa za ziada, honoraria na posho za vikao yenye thamani ya shilingi 701,598,893 yalirekodiwa katika kifungu kisichostahili hivyo kuleta upotoshwaji kwenye taarifa za fedha.
16. Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi
Taarifa za Fedha za Wakala noti 3 (a&b) (Noti 3a&b) inaonesha mali zilizonunuliwa zitumike kwa mwaka wa fedha ambazo hadi mwishoni mwa mwaka zilikuwa hazijatumika zenye thamani ya shilingi 55,243,417. Hata hivyo ukaguzi haukuweza kuthibisha kuwepo kwa mali hizo. Pia, kiasi hicho cha mali hizo kinatofautiana na kilichokuwepo kwenye ripoti ya mali zilizohesabiwa mwishoni mwa mwaka (annual stock taking report) za shilingi 106,928,790. Noti 5A ya taarifa za fedha inaonesha masurufu yasiyorejeshwa ya thamani ya shilingi 491,236,919. Hata hivyo, nilibainisha kuwa masurufu yenye thamani ya shilingi 611,376,730 yalitolewa na yalikuwa hayarejeshwa katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi. Pia kiasi cha shilingi 256,746,097 hayakurejeshwa katika mwaka wa fedha 2014/15; hivyo, kufanya kiasi cha masurufu yasiyorejeshwa kufikia shilingi 868,122,827 badala ya shilingi 491,236,919. Hii ilisababisha masurufu kuripotiwa kwa pungufu ya shilingi

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
376,885,908. Noti ya 11 ya taarifa za fedha inaonesha mapato yaliyovushwa mwaka (Deferred income) ya kiasi cha shilingi 48,671,294; hata hivyo, kiasi hicho hakikuoneshwa katika uso wa taarifa za fedha.
17. Idara ya Ujenzi ya SUMA
Ilionekana kuwa mapato yanayotokana na mikataba ya ujenzi ilikuwa inatambuliwa kwenye vitabu pale yanapopokelewa; na sio kwa kila kiasi cha kazi kilichofanyika au kwa kiasi cha mkataba kilichotekelezwa. Hii ni kinyume na aya ya 30 ya Viwango vya Kimataifa visivyo vya misingi ya taslimu namba 11. (IPSAS 11 para 30). Kadhalika, gharama zinazohusiana na mkataba kwa ujumla wake hazikugawanywa kwa usawa kulingana na mikataba husika kinyume na Viwango hivyo Namba 11 aya ya 23. (IPSAS 11 Para 23). Taarifa za fedha zilionesha kiasi cha mali zilizonunuliwa hazikutumika zenye thamani ya Shilingi 2,657,611,230. Hata hivyo hatukuweza kuthibisha kuwapo wa mali hizo. Nilibaini madai yatokanayo na kesi yenye thamani ya shilingi 292,153,750 kama yalivyokuwa katika rejista ya kesi lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye taarifa za fedha.
18. Shirika la uzalishaji mali la Jeshi la Magereza
Katika orodha ya madeni kulikuwa na deni linalotokana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi lenye thamani ya shilingi 621,092,622. Hata hivyo, wakati wa kuhakiki madeni tuliwasiliana na Wizara husika ambao walikiri kuwa hawajafanya mauzo yoyote kwa shirika hilo la Magereza.
19. Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (LDF)
Menijimenti ilifuta katika taarifa za Mali zenye thamani ya Sh. 359,622,792 lakini hazikuoneshwa kwenye Taarifa za Fedha.
20. Shirika la uzalishaji mali zana za kilimo-SUMA
Noti namba 32 ya taarifa za fedha ilionesha kuwa mali zilizonunuliwa

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
zitumike katika mwaka wa fedha ambazo hazikutumika (Inventories) kiasi cha shilingi 8,678,156,000 zikiwa ni kwa ajili ya vipuri, zana na matrekta. Hata hivyo hatukuweza kuhakiki usahihi wa kiasi hicho kwa sababu hatukuweza kupata ripoti ya mali zilizohesabiwa mwishoni mwa mwaka (Stocktaking report).
21. Chama cha UDP [MWAKA WA FEDHA 2016]
UDP hawakuwa wametengeneza vitabu vya hesabu kama leja ya akaunti binafsi za chama, leja ya jumla, kitabu cha fedha na mali za chama kama inavyotakiwa na Kifungu cha 14(1), 14(b)(ii) ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na.5 ya mwaka 1992 (iliyorekebiswa mwaka 2015). Vitabu hivi hutumika kama chanzo cha kutegemewa kwenye maandalizi ya taarifa za fedha, hivyo taarifa zao za fedha zimekosa uwazi, uhakika na haziwezi kuaminika wakati wa kufanya maamuzi. Kiasi cha shilingi 24,600,000 zililipwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za chama; hata hivyo, hazikuwa na nyaraka za kutosha kuweza kuthibisha uhalali wa malipo hayo kinyume na Kanuni ya 86 (1), 95 (4) na 116 ya Kanuni ya Fedha za Umma yam waka 2001. Ukaguzi ulishindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
22. Chuo cha Uongozi wa Serikali za Mitaa (Hombolo)

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.

Kiasi cha shilingi 139,628,305 kimeoneshwa katika ukurasa wa 23 wa taarifa za fedha. Ambayo inajumuisha kiasi cha shilingi 6,512,750 ambazo ni mikopo kwa watumishi na masurufu yaliyozaliwa ndani ya mwaka na kiasi cha shilingi 2,929,060,672. Kinatokana na ada za wanafunzi zimeoneshwa katika ukurasa huo huo ikijumuisha kiasi cha fedha kilichokuwa hakijakusanywa kwa mwaka uliopita cha shilingi 11,305,300 ambacho kilikuwa kimeshaoneshwa kama mapato katika mwaka husika.

Gharama za matengenezo zilikuwa kiasi cha shilingi 256,008,980 zikiwa zimeripotiwa kwa pungufu ya shilingi 1,158,500 ambayo yalikuwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya nishati ya jua. Pia, gharama nyinginezo zilikuwa kiasi cha 2,927,102,913 zikiwa zimeripotiwa zaidi kwa kiasi cha shilingi 124,019,150 ambazo ni masurufu ambayo yaliwekwa kama matumizi wakati yalikuwa hayajarejeshwa. Ilibidi yaonekane kama sehemu ya mali za sasa ambazo hazijapokelewa.

Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya shilingi 33,940,000 zilizolipwa kwa ajili ya vikao vya bodi ya wadhamini na vikao maalumu, hata hivyo kiasi cha shilingi 19,835,000 zilizolipwa hazikuwa na nyaraka za kuweza kuthibisha uhalali wake.

Malipo ya kiasi cha shilingi 122,907,598 yalikosa baadhi ya nyaraka kama stakabadhi, barua za mialiko na risti ya malipo. Hivyo, kuzuia mawanda ya ukaguzi. Pia, chuo kilishindwa kutoa hati za malipo zenye thamani ya shilingi 3,427,150.

Katika kupitia mapato, nilibaini kuwa kiasi cha shilingi 26,787,290 kilikusanywa lakini haukuwepo ushahidi kuwa fedha hizo zilipelekwa benki kinyume na Kanuni ya 78 (1&2) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

23. Mamlaka ya Mapato Tanzania-Mapato

Makusanyo ya kodi ya mafuta kutoka nje ya nchi yasiyo na nyaraka Shilingi 2,418,400,472

Ukaguzi wangu wa mafuta yaliyoingizwa kutoka nje ya nchi kuanzia 1 Januari 2016 hadi 30 June 2016 ulibaini kuwa kiasi cha mafuta lita

Jina la Taasisi na Vigezo vya Hati zenye shaka.
3,234,420 yenye kodi kiasi cha shilingi 2,418,400,472 yaliingizwa na makampuni 24 ya masoko ya mafuta na kuwafikia wamiliki. Sikuweza kupata ushahidi kuwa kodi itokanayo na mafuta hayo ililipwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Dosari hii pia ilikuwa kwa mafuta yote yaliyoagizwa na kuingizwa kutoka nje ya nchi kuanzia 1, Julai hadi 31 Desemba 2015 ambapo pia sikupata nyaraka kwa sababu wakati huo Mamlaka ya Mapato ilikuwa inahama kutoka mfumo wa Asycuda++ kwenda TANCIS. Hivyo, ilikuwa vigumu kuthibitisha kuwa kodi ya mafuta kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Mapato kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2016 ilikuwa kamili na sahihi. **Kodi ya Mafuta yaliyoagizwa kutoka nje ya Nchi kushindwa kuthibitishwa kukusanywa Sh 2,452,616,541** Ukaguzi wa kiasi cha mafuta kilicholetwa na meli 86 toka nje ya nchi dhidi ya kiasi cha mafuta yaliotumika nchini,kiasi kilichoa samehewa kodi,kiasi kilichosafirishwa nje ya nchi kilibaini tofauti ya lita 3,874,263 katika meli moja ambapo thamani ya Kodi ya Sh. 2,452,616,541 ilishindwa kuthibitika kukusanywa. Nyaraka za Kodi zinazohusu kiasi hiki cha Mafuta pamoja na taarifa ya usuluhisho hazikuweza kupatikana wakati wa Ukaguzi. Hivyo kushindwa kuthibitisha ukamilifu na usahihi wa kiasi cha Kodi katika Taarifa za Mapato za TRA kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.
24. Msajili wa Hazina (Fungu 7)
Ukaguzi ulishindwa kuhakiki uhalisia wa kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa za mizani ya hesabu kwenye mali za muda mrefu kama uwekezaji katika ubia, Uwekezaji katika mshirika na uwekezaji katika hisa kwa kiasi cha shilingi 22,565,538,152,418.50. Hii imesababishwa na ukokotoaji kwa kutumia msingi wa mwaka uliotangulia.

Kiambatisho 2.3: Taasisi na Mambo yaliyopelekea Kupata Hati Mbaya kwa Hesabu za Miaka iliyopita.

Demokrasia Makini [FY: DEC 2015]
Katika ukaguzi wa mwaka huu tulibaini kuwa Demokrasia Makini hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015. Rekodi hutoa taarifa za muhimu wakati wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha, Hivyo, taarifa zao zilikosa vyanzo vya taarifa ambayo ilipunguza usahihi, uwazi na uegemezi (reliability) wa taarifa. Pia, chama hakitumii mfumo wa taarifa za fedha kama inavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA) Tangazo namba 3 la mwaka 2009; na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo ni taarifa ya mapato na matumizi peke yake iliandaliwa. Bila kuwepo mifumo inayokubalika na sera za uhasibu, hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa za fedha. Ilibainika kuwa Demokrasia Makini hawana akaunti ya benki kama inavyotakiwa na Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Vile vile vitabu vya fedha (Cash book) havikuwa vimetunzwa vizuri; hivyo, ukaguzi ukashindwa kuelewa miamala iliyofanyika katika mwaka husika.
Chama cha ADA-TADEA [Mwaka wa Fedha Disemba 2015]
Katika ukaguzi wa mwaka huu tulibaini kuwa ADA-TADEA hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha. Tulibaini kuwa mapato ya shilingi 56,448,200 na matumizi ya shilingi 55,545,000 hayakuingizwa kwenye vitabu vya hesabu. Kukosa vitabu vya hesabu ilizuia mawanda ya ukaguzi. Pia, chama cha ADA TADEA hakitumii mfumo wa taarifa za fedha kama inavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA) Tangazo namba 3 la mwaka 2009 na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa za fedha.

Chama cha (ADC) [Mwaka wa Fedha JUNI 2015]

Katika ukaguzi wa huu tulibaini kuwa ADC hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Kukosa vitabu vya hesabu ilizuia mawanda ya ukaguzi.

Pia chama cha ADC hakitumii mfumo wa taarifa za fedha kama unavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA) Tangazo namba 3 la mwaka 2009 na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha; hivyo hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa za fedha. Katika mwaka wa ukaguzi ADC waliweza kutengeneza taarifa ya mapato na matumizi peke yake.

Tulibaini kuwa malipo ya shilingi 62,405,100 kwa watu mbalimbali ambao walifanya shughuli za chama hata hivyo hati za malipo hayo hazikutolewa kwa ukaguzi pamoja na viambatisho vyake kinyume na Kanuni ya 86 (1), 95(4) na 116 ya Kanuni ya Fedha za Umma yam waka 2001. Mawanda ya ukaguzi yalizuiliwa kwa kushindwa kuhakiki uhalali wa malipo hayo.

Chama cha DP [Mwaka wa Fedha JUNI 2015]

Katika ukaguzi wa mwaka huu tulibaini kuwa DP hawakutunza vitabu vya uhasibu ipasavyo ikijumuisha vitabu vya mapato, kitabu cha fedha, vitabu vya leja na rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kudhibiti na kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kinyume na Kifungu cha 14(1) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Kukosa vitabu vya hesabu kulizuia mawanda ya ukaguzi.

Pia, chama cha DP hakitumii mfumo wa taarifa za fedha kama unavyotakiwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taifa (NBAA) Tangazo namba 3 la mwaka 2009. Na hakuna sera za uhasibu walizoandaa kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha. Hivyo, hatukuweza kubaini misingi iliyotumika kuandaa taarifa za fedha.

Viambatisho Sura Ya Tatu

Kiambatisho 3.1 : Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa miaka iliyopita kwa kila Mkaguliwa (Mafungu na Balozi)

Fungu	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yaliyo katika utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea matukio mengine	Jumla
5	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	8	9	9	0	26
6	Ofisi ya Raisi usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Kipaumbele	4	0	0	1	5
7	Ofisi ya Msajili wa Hazina	4	4	3	0	11
9	Ofisi ya Rais Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma	2	0	1	0	3
10	Tume ya Fedha ya Pamoja	2	1	0	0	3
12	Tume ya Huduma ya Mahakama	3	5	0	0	8
13	Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha	4	4	3	0	11
14	Jeshi la zimamoto na Uokoaji	13	1	0	0	14
15	Tume ya Usululishi na Uamuzi	3	4	0	0	7
16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	3	7	0	0	10
20	Ofisi ya Rais Ikulu	3	2	0	0	5
21	Idara ya Hazina	17	18	2	0	37
22	Idara ya Deni la Taifa	8	20	7	0	35
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	9	17	0	0	26
24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika	5	7	0	0	12
25	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	0	0	1	0	1
26	Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais	6	10	0	0	16
27	Msajili wa Vyama vya Siasa	2	2	6	0	10
28	Jeshi la Polisi Tanzania	35	11	6	0	52
29	Idara ya Huduma za Magereza	10	9	8	0	27
30	Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	3	2	0	0	5
31	Ofisi ya Makamu wa Rais	7	9	0	0	16
32	Ofisi ya Rais, Managementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	5	4	0	0	9
33	Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili	0	9	0	0	9
34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	10	7	2	1	20
35	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka	4	8	4	0	16
36	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	7	7	11	0	25

Fungu	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yaliyo katika utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea matukio mengine	Jumla
37	Ofisi ya Waziri Mkuu	3	5	3	0	11
38	Jeshi la Wanachi wa Tanzania	3	26	2	3	34
39	Jeshi la Kujenga Taifa	7	7	6	8	28
40	Mfuko wa Mahakama	8	4	0	2	14
41	Wizara ya Katiba na Sheria	13	6	1	2	22
42	Bunge	12	0	5	0	17
43	Wizara ya Kilimo, Usalama wa Chakula na Ushirika	23	8	3	0	34
44	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji	7	4	8	0	19
46	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	11	18	2	1	32
47	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	20	14	2	8	44
48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makzi	3	21	12	0	36
49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	6	5	1	0	12
50	Wizara ya Fedha na Mipango	2	23	0	0	25
51	Wizara ya Mambo ya Ndani	12	3	1	0	16
52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	1	4	12	0	17
53	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	3	14	1	2	20
54	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe	12	0	4	0	16
55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	5	13	2	0	20
56	Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	6	22	7	1	36
57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	4	25	1	6	36
58	Wizara ya Nishati na Madini	6	8	0	3	17
59	Tume ya Kurekebisha Sheria	3	7	3	0	13
61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	4	11	2	0	17
62	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilano	3	1	1	0	5
63	Sekretarieti ya Mkoa wa Geita	1	19	10	0	30
65	Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu	4	1	0	1	6
66	Tume ya Mipango	0	7	0	0	7
67	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Utumishi wa Umma	1	3	0	0	4
68	Wizara ya Kazi, Uchukuzi na	15	7	1	6	29

Fungu	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yaliyo katika utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea matukio mengine	Jumla
	Mawasiliano					
69	Wizara ya Mali Asili na Utalii	2	6	5	2	15
70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	4	5	17	0	26
71	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	8	0	7	0	15
72	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	24	3	7	0	34
73	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	14	12	2	6	34
74	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	12	4	9	12	37
75	ekretariati ya Mkoa wa Kigoma	24	20	10	0	54
76	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	10	18	11	0	39
77	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	6	7	2	7	22
78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	28	2	15	0	45
79	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	0	13	16	0	29
80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	2	4	21	3	30
81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	18	7	10	5	40
82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	7	18	37	0	62
83	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	27	3	13	28	71
84	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida	0	22	1	14	37
85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	1	17	28	8	54
86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	23	2	6	0	31
87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	8	10	8	14	40
88	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam	0	3	0	0	3
89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	18	6	37	0	61
91	Tume ya Kuzuia Madawa ya Kulevya	4	2	0	0	6
92	Tume ya Kuzuia UKIMWI	2	3	1	0	6
93	Idara ya Huduma ZA Uhamiaji	10	20	13	0	43
94	Ofisi ya Rais,Tume ya Utumishi wa Umma	3	0	0	0	3
95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	21	3	10	0	34
96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	16	16	4	0	36
97	Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki	3	0	3	4	10
98	Wizara ya Kazi, Uchukuzi na Mawasilino	4	2	0	0	6
99	Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi	23	12	0	0	35
2001	Ubarozi wa Tanzania, Addis Ababa	1	3	4	2	10
2002	Ubalozi wa Tanzania, Berlin	0	1	5	0	6
2003	Ubalozi wa Tanzania, Cairo	2	1	4	0	7
2004	Ubalozi wa Tanzania, Kinshasa	5	0	11	1	17

Fungu	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yaliyo katika utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea matukio mengine	Jumla
2005	Ubalozi wa Tanzania, Abuja	3	4	4	1	12
2006	Ubalozi wa Tanzania, London	3	8	3	0	14
2007	Ubalozi wa Tanzania, Lusaka	10	7	12	0	29
2008	Ubalozi wa Tanzania, Maputo	10	9	11	6	36
2009	Ubalozi wa Tanzania, Moscow	0	5	4	0	9
2010	Ubalozi wa Tanzania, New Delhi	3	2	0	0	5
2011	Ubalozi waTanzania- New York	8	7	6	0	21
2013	Ubalozi wa Tanzania, Paris	5	2	6	1	14
2014	Ubalozi wa Tanzania, China	13	15	1	3	32
2015	Ubalozi wa Tanzania, Rome	5	0	6	0	11
2016	Ubalozi wa Tanzania, Stockholm	3	2	7	1	13
2017	Ubalozi wa Tanzania, Tokyo	2	4	6	2	14
2018	Ubalozi wa Tanzania, Washington DC	2	5	5	0	12
2019	Ubalozi wa Tanzania, Brussels	6	6	0	0	12
2020	Ubalozi wa Kudumu katika Umoja wa Mataifa	2	0	1	5	8
021	Ubalozi wa Tanzania, Kampala	18	8	2	0	28
2022	Ubalozi wa Tanzania, Zimbabwe	1	0	5	0	6
2023	Ubalozi wa Tanzania, Nairobi	14	12	0	0	26
2024	Ubalozi wa Tanzania, Saudi Arabia	0	0	0	0	0
2025	Ubalozi wa Tanzania, Pretoria	8	8	3	4	23
2026	Ubalozi wa Tanzania, Kigali	5	11	0	1	17
2027	Ubalozi wa Tanzania, Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu	7	6	0	0	13
2028	Ubalozi wa Tanzania, Bujumbura	4	7	2	3	16
2029	Ubalozi wa Tanzania, Muscat	23	6	0	0	29
2030	Ubalozi wa Tanzania, Lilongwe	2	3	7	1	13
2031	Ubalozi wa Tanzania, Brasilia	2	5	0	0	7
2032	Ubalozi wa Tanzania, Kuala Lumpur	2	1	0	0	3
2033	Ubalozi wa Tanzania, The Hague	2	1	1	4	8
2034	Ubalozi wa Tanzania, Moroni	15	14	8	0	37
	Jumla	**883**	**866**	**570**	**183**	**2502**

Kiambatisho 3.2: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguiwa (Wakala)

Na	Jina la Wakala	Yaliyotekelezwa	Yaliyo katika utekelezaii	Ambayo	Yanayotegemea	Jumla
1	Wakala wa Mbegu za Kilimo	5	26	4	0	35
2	Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu	2	9	3	1	15
3	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni	12	14	0	0	26
4	Wakala wa Mabasi ya Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART)	10	14	4	0	28
5	Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa	8	2	2	0	12
6	Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki	10	3	1	0	14
7	Wakala wa Serikali Mtandao	1	0	0	0	1
8	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo	3	0	0	0	3
9	Wakala wa Utafiti wa Miamba	1	5	4	0	10
10	Wakala wa Maabara za Kemia za Serikali	8	11	2	0	21
11	Wakala wa Hududuma za Ugavi na Manunuzi	10	20	4	0	34
12	Wakala wa Mafunzo wa Mifugo	10	0	1	0	11
13	Chuo cha Taifa cha Utalii	4	1	4	0	9
14	Wakala wa Nyumba na Tafiti za Majengo	7	1	3	0	11
15	Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini	11	4	0	0	15
16	Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini	18	16	0	1	35
17	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania	3	5	0	0	8
18	Wakala wa Majengo Tanzania	39	15	0	0	54
19	Wakala wa ufundi wa Mitambo na Umeme	7	11	2	0	20
20	Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania	7	1	0	0	8
21	Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa Tanzania	3	1	0	0	4
22	Wakala wa Ndege za Serikali	0	3	2	0	5
23	Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania	7	2	0	0	9
24	Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania	2	3	2	7	14
25	Wakala wa Barabara	88	29	8	0	125
26	Wakala wa Kudhibitisha Mbegu Tanzania	2	0	3	0	5
27	Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania	13	2	0	0	15
28	Wakala wa Huduma za Ndege Tanzania	3	4	3	0	10
29	Wakala wa Maabara za Kilimo	4	0	0	0	4
30	Taasisi ya Maji	7	2	1	0	10
31	Wakala wa Vipomo	11	1	3	0	15
32	Taasisi ya Uhasibu Tanzania	10	15	2	0	27
	Jumla	**326**	**220**	**58**	**9**	**613**

Kiambatisho 3.3: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguliwa (Taasisi nyingine)

Na	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yalioy katika Utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea Matukio Mengine	Jumla
1	Taasisi ya Kujenga Uwezo ya Afrika	5	1	0	3	9
2	Mpango wa kujitathimini katika nchi za Afrika	2	3	1	1	7
3	Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo	12	5	1	0	18
4	Chama cha Alliance for Demokratic Change(ADC)	2	0	4	0	6
5	Umoja wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania	2	0	3	0	5
6	Chama cha Sauti ya Umma (SAU)	4	0	0	6	10
7	Shirikisho la Bunge yla Jumuia ya Madola-Sekretariett ya Ukanda wa Afrika	0	0	3	0	3
8	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo	6	6	4	0	16
9	Mamlaka ya Maji safi na Taka Dar es Salaam (DAWASA)	3	3	0	0	6
10	Mfuko wa Kuwezesha Maendeleo ya Madini	1	0	1	1	3
11	Mamlala ya Maji safi na Taka Handeni	1	2	0	0	3
12	Baraza la Maabara za Afya	0	2	5	0	7
13	Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika	0	3	0	0	3
14	Chuo cha Utumishi wa Mahakama	2	6	1	2	11
15	Bodi ya Bonde la Maji ya Mfereji wa Kati	2	0	2	0	4
16	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	7	9	0	0	16
17	Mamlaka ya Maji Safi na Taka Mugango-Kiabakari	2	5	4	1	12

Na	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yalioy katika Utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea Matukio Mengine	Jumla
18	Shirika la Mzinga	19	18	20	5	62
19	Kampuni Hodhi ya Mzinga	1	32	6	0	39
20	Bodi ya Maji ya Ziwa Nyasa	4	5	8	4	21
21	Bonde la Maji la Ziwa Rukwa	2	3	3	4	12
22	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika	3	1	1	0	5
23	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Viktoria	2	2	2	2	8
24	Taaasisi ya Sheria kwa Vitendo	15	6	0	2	23
25	Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo	0	2	0	0	2
26	Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (HOMBOLO)	4	36	4	1	45
27	Mfuko wa Maji	6	0	2	0	8
28	Baraza la Madawa Tanganyika	2	0	5	0	7
29	Balaza la Wataalamu wa Miyonzi na Picha	1	0	2	0	3
30	Taasisi ya Rasilimali ya Madini	3	0	2	0	5
31	Mfuko wa Taifa wa Maafa	0	2	1	0	3
32	Shirika la Uzalishaji Mali (SUMA)-Makao makuu	4	5	1	1	11
33	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa	6	1	19	0	26
34	Baraza la Wataalamu wa Macho	0	0	2	0	2
35	Bodi ya Bonde la Maji la Pangani	3	4	1	0	8
36	Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi	0	0	11	0	11
37	Mfuko wa Rais wa Udhamini wa Kujitegemea	8	1	0	1	10
38	Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza	4	4	7	0	15
39	Bodi ya Maabara Binafsi za Afya	2	3	3	0	8
40	Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi	0	0	6	0	6
41	Mpango wa Kurasimisha Mali na Biashara	11	5	4	0	20

Na	Jina la Taasisi	Yaliyotekelezwa	Yalioy katika Utekelezaji	Ambayo hayajatekelezwa	Yanayotegemea Matukio Mengine	Jumla
	za Wanyonge Tanzania					
42	Bodi ya Mfuko wa Barabara	8	0	4	0	12
43	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji	0	2	4	0	6
44	Bodi ya Bonde la Maji la Ruvuma na Pwana ya Kusini	1	4	1	1	7
45	Mfuko wa Fedha wa SELF	6	4	0	0	10
46	SUMA JKT-Ulinzi	4	4	2	2	12
47	SUMA JKT-Matrekta ya Kilimo	11	11	1	3	26
48	SUMA JKT-Idara ya Kilimo na Viwanda	8	13	0	7	28
49	SUMA JKT-Idara ya Ujenzi	2	3	2	7	14
50	Kituo cha Teknolojia ya Magari Tanzania	6	8	1	4	19
51	Mfuko wa Misitu Tanzania	11	4	3	0	18
52	Chama cha Tanzania Labour Party (TLP)	0	0	9	0	9
53	Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania	0	0	10	0	10
54	Taasisi ya Kuthibitisha Mbegu Tanzania	2	0	3	0	5
55	Mfuko wa Kuifadhi Wanyama Pori Tanzania	4	2	1	0	7
56	Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru	6	7	2	0	15
57	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Technolojia ya Nelson Mandela	8	6	6	4	24
58	Baraza la Mitishamba na Tiba Mbadala	0	0	2	0	2
59	Mfuko wa Mikopo ya Hazina	1	6	0	0	7
60	Baraza la Mifugo Tanzania	4	0	0	0	4
61	Bodi ya Bonde la Maji la Wami	1	8	6	0	15
62	Mamlaka ya Maji ya Wanging'ombe	4	4	4	0	12
63	Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake	1	3	6	2	12
64	Mfuko wa Maendeleo ya Vijana	1	1	8	0	10
65	**Jumla**	240	265	214	64	783

Kiambatisho 3.4: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguli

Fungu au Na	Majina ya Wakaguliwa	Yaliyotekel	Yaliyo	Ambayo	Yanayoteg	Jumla
Fungu	**MAFUNGU NA BALOZI**					
5	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	0	4	4	4	12
14	Jeshi la zimmoto na Uokoaji	0	9	0	0	9
16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	1	1	0	0	2
21	Idara ya Hazina	0	4	1	0	5
22	Idara ya Deni la Taifa	0	2	0	0	2
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	1	2	0	0	3
28	Jeshi la Polisi Tanzania	4	0	6	0	10
29	Idara za Huduma ya Magereza	1	3	4	0	8
30	Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	1	3	4	0	8
32	Ofisi ya Rais,Managementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	1	1	0	0	2
34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika MASHARIKI	10	10	0	0	20
36	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	1	0	3	0	4
37	Ofisi ya Waziri Mkuu	5	0	1	0	6
38	Jeshi la Wanachi Tanzania	1	3	0	0	4
39	Jeshi la Kujenga Taifa	3	1	0	0	4
41	Wizara ya Katiba na Sheria	5	0	1	0	6
42	Bunge	4	0	0	0	4

Fungu au Na	Majina ya Wakaguliwa	Yaliyotekel	Yaliyo	Ambayo	Yanayoteg	Jumla
43	Wizara ya Kilimo, Usalama wa Chakula na Ushirika	1	0	6	0	7
44	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji	1	3	0	0	4
46	Wizara ya Elimu, Sayansi na Kujitegemea	0	0	4	0	4
47	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	5	0	0	0	5
48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	0	4	0	0	4
49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	3	0	0	0	3
50	Wizara ya Fedha na Mipango	2	0	3	8	13
51	Wizara ya mambo ya ndani	0	0	2	0	2
55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	1	1	4	4	10
58	Wizara ya Nishati na Madini	0	0	5	0	5
59	Tume ya Kurekebisha Sheria	4	0	1	0	5
61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	2	0	4	0	6
69	Wizara ya Maliasili na Utalii	3	0	3	0	6
70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	1	2	3	0	6
72	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	0	0	4	0	4
74	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	5	9	1	0	15
75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	0	0	5	0	5
77	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	0	0	1	0	1
78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	5	0	0	0	5
80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	1	1	4	0	6

Fungu au Na	Majina ya Wakaguliwa	Yaliyotekel	Yaliyo	Ambayo	Yanayoteg	Jumla
81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	2	4	0	0	6
82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	1	1	0	0	2
83	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	5	0	1	0	6
85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	0	1	0	0	1
86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	2	0	2	0	4
87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	0	2	3	0	5
89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	1	1	0	0	2
93	Idara ya Huduma za Uhamiaji	5	0	0	0	5
95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	0	0	5	0	5
96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	1	0	0	0	1
98	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	2	3	0	0	5
	Jumla ndogol (A)	**91**	**75**	**85**	**16**	**267**
Na	**WAKALA**					
1	Wakala wa Huduma za Ufundi wa Mitambo na Umeme	1	0	0	0	1
2	Wakala wa Barabara	5	4	0	0	9
3	Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania	1	6	0	0	7
	Jumla ndogo (B)	**7**	**10**	**0**	**0**	**17**
Na	**TAASISI NYINGINE**					
1	Shirika la Uzalishaji Mali (SUMA JKT-Makao Makuu)	4	0	0	0	4

Fungu au Na	Majina ya Wakaguliwa	Yaliyotekel	Yaliyo	Ambayo	Yanayoteg	Jumla
2	Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (HOMBOLO)	0	2	0	0	2
	Jumla Ndogo (C)	**4**	**2**	**0**	**0**	**6**
	Jumla Kuu (A+B+C)	**102**	**87**	**85**	**16**	**290**

Kiambatisho 3.5: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	2006/2007		
1	**Mapungufu katika usimamizi wa dhamana za serikali** Wizara inashauriwa kupitia Sheria na Kanuni kwa kufanya marekebisho kwenye sheria ya dhamana na Kanuni zake ili kuendana na hali ya sasa	Marekebisho yamefanyika kwenye Sera ya madeni na Mikopo ya Serikali na Sheria ya dhamana na mikopo Na. 30 ya 1974. Marekebisho hayo yatapelekwa bungeni kwa uidhinishaji hivi karibuni. Mkakati wa madai umerekebishwa	**Utekelezaji haujakamilika** Marekebisho ya sheria ya mikopo ya Serikali, dhamana na ruzuku Na.3 ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004) na mapitio ya Mkakati wa Deni la Taifa (NDS) yanasubiriwa
2	**Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo hazijarudishwa Serikalini** Tunaendelea kusisitiza kwamba Wizara ifanye juhudi ikishirikiana na mkusanyaji wa madeni ya Serikali kusisitiza makusanyo ya kiasi kilichobaki cha JPY 16,699,499,858 na kuwasilisha maendeleo yaliyofikiwa kwa ajili ya ukaguzi.	Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali iliizuia Serikali kutochukua hatua yoyote mpaka pale maelekezo juu ya suala hili yatakapo tolewa.	**Utekelezaji haujakamilika**
	2008/2009		
3	**Kutoandika kwa usahihi mikopo**	Makubaliano hayo yaliyofikiwa baina ya Serikali	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	iliyotolewa na serikali kama dhamana Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilisha makubaliano hayo yaliyofikiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Makampuni hayo ya maua, ratiba ya ulipaji mikopo pamoja na vielelezo vingine vinavyoonyesha kuanza kulipwa kwa mkopo.	na Makampuni ya maua pamoja na vielelezo vingine vya msingi vitawasilishwa ofisi ya ukaguzi kwa ajili ya uhakiki.	
	2010/2011		
4	**Madeni na Miadi** Mamlaka ya mapato Tanzania inatakiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato, na Hazina ihakikishe kuwa fedha zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwenye bajeti	Serikali itaendeleza jitihada za kuongeza mikakati ya kurahisisha utekelezaji wa bajeti kwa kuendelea kurasimisha sekta zisizo rasimi ili kuijumuisha kwenye wigo wa kodi	**Inategemea matukio mengine**
5	**Mali zisizoingizwa katika daftari la kudumu la mali** Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuonyesha hatua (ratiba) za utekelezaji wa ushauri huu. Daftari la mali za kudumu linatakiwa kuwa tayari kabla ya mwaka 2016/2017 ambapo serikali itakuwa inatumia viwango vya kufunga Hesabu vya kimataifa (IPSAS)	Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inashughulikia suala la daftari la kudumu la Mali ambalo litajumuisha mali zote za serikali	**Hoja iko katika utekelezaji** Tunaendelea kusisitiza utumiaji kamili wa Uandaaji wa hesabu katiba viwango vya kimataifa usiofuata taslim
	2011/2012		

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
6	**Deni la Shirika la ndege (ATCL)** Ninapendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya waliohusika katika kuiingiza serikali katika biashara zisizozaa matunda,na ambazo zimesababisha serikali kudaiwa limbikizo la deni la dola za Marekani 41,466,177.16 kuanzia 26/10/2012; na Kuanzia tarehe 26/10/2012 deni limekuwa likiongezeka mpaka kufikia dola za Marekani 41,466,177.16 kutoka dola 39,000,000 .Serikali inapaswa kujadili hili deni na kampuni ya Wallis kama kuna uwezekano wa kulifuta kwa vigezo kwamba serikali haikufaidika na biashara hiyo.	Suala hili liko katika uchunguzi na TAKUKURU. Uongozi utawasiliana na Wakaguzi juu ya hatua zilizo chukuliwa baada ya TAKUKURU kukamilisha uchunguzi. Taarifa inayoonesha gharama za uendeshaji wakati ndege inafanya kazi na baada ya kutofanya kazi iko tayari na itawasilishwa kwa Wakaguzi kwa ajili ya uhakiki. Andiko linaandaliwa kwa ajili ya kupitisha na Baraza la Mawaziri. Kwa sasa kamati ndogo ya IMTC inajadiliana na wadai wa ATCL ili wapunguze deni kabla ya kuomba kibali cha baraza la Mawaziri	**Iko katika utekelezaji** Suala hili bado liko katika uchunguzi na TAKUKURU. Hata hivyo tunasisitiza kuwa Mlipaji mkuu wa Serikali afanye majadiliano na kampuni ya kibiashara ya Wallis juu ya suala hili
7	**Malipo ya matibabu nje ya nchi yasio na nyaraka za viambatisho kiasi cha Sh. 448,144,343** Afisa Masuuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii anatakiwa kuboresha udhibiti wa ndani katika matumizi ya wizara na kuhakikisha kwamba nyaraka zote	Matumizi haya yanahusiana na malipo yaliyolipwa kwa Balozi mbalimbali kwa ajili ya matibabu ya wateule wa urais, ankra, orodha ya wagonjwa waliotibiwa nje ya nchi na stakabadhi za kukiri kutoka kila Ubalozi husika yalitolewa na Wizara ya Mambo ya Nje	**Iko kwenye utekelezaji** Tunasubiria nyaraka zinazohusiana na hayo malipo

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	zinazohusiana na matibabu ya nje zinawasilishwa kwa ukaguzi.		
	2012/2013		
8	**Usimamizi wa manunuzi** Ukaguzi ulibaini mapungufu yanayojirudia katika shughuli za manunuzi. Hivyo, ninapendekeza: Serikali kupitia Mamlaka ya udhibiti wa manunuzi ya umma (PPRA) Kuendesha semina kadhaa kwa lengo la kujenga uwezo kwaenye kitengo cha manunuzi, Bodi ya Zabuni, Maafisa Masuuli na Idara ya watumiaji juu ya umuhimu wa kutekeleza Sheria ya Manunuzi na kanuni zake Pia, ni muhimu kuwa na mfumo wa usimamizi wa taarifa za manunuzi katika kufanikisha shughuli za manunuzi. Mfumo huu unasimamiwa na Mamlaka ya udhibiti	Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2011 imeipa mamlaka PPRA kujenga uwezo wa kitengo cha manunuzi, Bodi ya Zabuni, Afisa Masuuli na idara ya mtumiaji juu ya kufuata Sheria. PPRA imepitia Mfumo wa Taarifa za manunuzi na kuanza kutumia mfumo ulioboreshwa mwezi Juni, 2015 kwa kuwashirikisha wadau	**Inategemea matukio mengine** Tathimini endelevu juu ya utekelezaji utafanyika katika ukaguzi ujao

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	wa manunuzi ya umma. Mamlaka hii inatakiwa kuhakikisha kwamba mfumo huu ni rafiki kwa watumiaji wa mwisho ili Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa watumie mfumo huu kwa urahisi katika kuboresha shughuli za manunuzi.		
9	**Kutofanyiwa kazi kwa changamoto ya upungufu wa nguvu kazi katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa** Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa wa wafanyakazi ikilinganishwa na ikama ya watumishi katika taasisi. Kwa hiyo, ninapendekeza: Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM) ipitie upya ikama za Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa na kuja na mapendekezo halisi ya idadi ya watumishi wanaohitajika. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa wanapaswa kuhakikisha kwamba wana idadi ya kutosha ya watumishi wenye sifa stahiki. Uhaba wa watumishi unapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka husika ikiwa ni	Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Managementi ya Utumishi wa Umma ilitoa miongozo kwa waajiri juu ya mishahara ya Watumishi kwa mwaka wa fedha 2014/15 kwa kuendelea kuomba nguvukazi kulingana na mahitaji. Kwa kipindi cha kati year wa fedha 2008/09 na 2013/15 nafasi mpya 373,280 zilitolewa kwa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na halmashauri .	**Haijatekelezwa kikamilifu** Utekelezaji hauko katika kiwango kinachotakiwa

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	pamoja na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM).		
10	**Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa** Ili kuepuka upotevu kama huu katika siku zijazo, Maafisa Masuuli katika Wizara, Idara na Mikoa husika wanapaswa kuangalia taarifa za mishahara ya watumishi wao mara kwa mara na kuthibitisha uhalali wa watumishi wote kabla ya malipo. Mawasiliano pia lazima yaimarishwe ili kuhakikisha kwamba majina ya wastaafu, watoro/walioacha kazi au walioachishwa kazi yanafutwa katika taarifa za wafanyakazi mara moja. Mbali na hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha mishahara isiyolipwa kwa watumishi ambao muda wao wa utumishi umekoma kwa sababu moja au nyingine inarudishwa Hazina kwa wakati kulingana na maagizo. Zaidi ya hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa kutunza taarifa za watumishi (HCMIS-	Serikali imeanzisha Mfumo wa kusimamia Taarifa wa Watumishi .Hii imewezesha jumla ya wafanyakazi wa 61,136 kufutwa kutoka kwenye orodha ya mishahara kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kifo na kustaafu,	**Haijatekelezwa kikamilifu** Kazi ya kuondoa watumishi hewa linapaswa kuwa endelevu

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	LAWSON) unafanya kazi na unatumika kikamilifu ili kupata thamani ya fedha tarajiwa.		
11	**Utendaji katika Balozi** Balozi husika zikishirikiana na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa (MFAIC) zinatakiwa kusitisha malipo ya posho kwa maafisa wastaafu na kufanya utaratibu wa kuwarudisha nyumbani haraka pindi utumishi wao unapokoma. Napendekeza mamlaka husika iangalie ni jinsi gani zitakavyoweza kurudisha fedha zilizolipwa kwa maafisa wasiostahili wa Balozi. Menejimenti ya Balozi iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya kuwarejesha majumbani watumishi waliomaliza utumishi wao ambao bado wanaendelea kuishi ubalozini na wale ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu wabadilishwe. Hii itakuwa chachu katika utoaji wa huduma kwa balozi zetu. Menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje	Uongozi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje inatathmini uwezekano wa kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kufanya diplomasia ya kiuchumi na kukuza kivutio cha utalii ambayo itategemea upatikanaji wa rasilimali	**Haijatekelezwa kikamilifu**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na Ushirikiano wa Kimataifa ione uwezekano wa kuanzisha mfuko katika bajeti yake kwa ajili ya kufanya shughuli za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio vya utalii, kwa kuzingatia kwamba hii ni kazi muhimu kwa uchumi wa nchi.		
12	**Uendeshaji wa Hospitali Teule na Hospitali za Rufaa** Wizara ya Afya inapaswa kuhakikisha kuwa fedha zote zinapohamishwa kwenda hospitali mbalimbali zinaambatana na mchanganuo wa matumizi yake badala ya utaratibu wa sasa usioainisha malengo ya fedha hizo kama ilivyodhihirika wakati wa ukaguzi. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Hazina ni muhimu waboreshe mawasiliano na menejimenti za Hospitali husika kuhakikisha kuwa watumishi hewa wanafutwa kwa wakati katika mfumo wa ajira serikalini Nasisitiza Hospitali teule zizingatie makubaliano ya mkataba kati yao na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	Wizara imewasiliana na hospitali zote teule nchini kwa barua yenye kumbukumbu Na. HC.209/320/01 ya tarehe 30 Oktoba, 2013 na kuwataka kurejesha Wizara ya fedha mishahara yote haikustaili kulipwa.	**Haijatekelezwa** Ushahidi wa mishahara iliyorejeshwa kutoka hospital teule na hospitali za rufaa unapaswa kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Ninapendekeza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na menejimenti za Hospitali husika ihakikishe ya kwamba, wanafungua akaunti ya benki inayojitegemea mahususi kwa ajili ya fedha za ruzuku za Serikali badala ya hali ya sasa ya kuchanganya fedha hizi za Serikali na fedha za matumizi mengine ya hospitali. Aidha, Menejimenti za hospitali zinapaswa kuwajibika kutoa taarifa za mara kwa mara za matumizi ya fedha hizo kwa Wizara husika.		
13	**Ununuzi wa Kivuko cha Misungwi** Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wa umma walioshindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi. Na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mzabuni M/S Sinnautic international ambaye alishindwa kutekeleza kazi zote za kuleta vipuri vya thamani ya Euro 41,140 za kivuko cha Misungwi kwa mujibu wa mkataba.	Hatua zimeshachuliwa dhidi ya maafisa wa umma ambao walishindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi, Wizara ikishirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaangalia utaratibu wa kuchukua hatua zaidi za kisheria dhidi ya Mkandarasi	**Haijatekelezwa kikamilifu** Vipuri muhimu kwa ajili ya kivuko bado havijapokelewa. Taratibu za kisheria zinapaswa kufuatwa
14	**Utayari wa Serikali katika utekelezaji wa IPSAS, yaani Viwango vya Kimataifa**	Tathimini ya mali katika Serikali za Mitaa inasubiria mapitio ya Sheria ya fedha za Umma	**Haijatekelezwa kimamilifu** Kasi ya utekelezaji haiendani na

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	vya Uhasibu kwa Taasisi za Umma Usio taslim Kuanzisha kamati ya kitaifa ya kuratibu utekelezaji wa IPSAS ambayo itashirikisha Wahasibu/Wakaguzi wenye weledi na wataalam mbalimbali ambao watakuwa wasimamizi wa jukumu hili kwa miaka mitano ili kuhakikisha kila hatua inatekelezwa kwa umakini na kwa wakati. Mhasibu Mkuu wa Serikali anapaswa kuwa mwenyekiti wa hiyo Kamati Mhakiki mali wa Serikali anapaswa kufanya kazi kwa karibu na wadau ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango wa kuhamia IPSAS isiyo taslimu unazingatia IPSAS 17, pia kufanya mabadiliko muhimu katika taarifa za fedha yanayohusu kutenganisha ardhi na majengo makundi mawili tofauti, Kuuboresha mfumo wa EPICOR na wa bajeti ili uweze kumudu kutengeneza ripoti za mwaka zinazokidhi matakwa ya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu,	ambayo itatoa mamlaka ya kisheria Idara ya Serikali ya Usimamizi wa Mali katika Serikali za Mitaa Wizara ya Fedha iko kwenye mchakato wa kuratibu jitihada za pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Ujenzi(Wakala wa Majengo ya Serikali) kuhakikisha uandaaji wa hati miliki kwa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha moduli za Mfumo Jumuifu wa Usimamizi wa Fedha unaamshwa na kufanya kazi ipasavyo Kwa sasa, Serikali inakamilisha kuweka sawa Mfumo Jumuifu wa Usimamizi wa Fedha ili kendana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu usio Taslim. Pia nimpango wa Serikali kuamsha moduli zilizosalia kwenye mfumo kama vile orodha ya mali na mali za kudumu Mafunzo ya toleo jipya la 9.05 limefanyika kwa Wahasibu Wakuu wote, Wahasibu wa Mikoa, Wakuu wa Hazina Ndogo, Waingiza takwimu na Waandaaji wa taarifa za fedha wa Wizara,	muda uliobaki

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Serikali inashauriwa kuanzisha mchakato wa kutengeneza ripoti ya fedha ya mwaka iliyounganisha taarifa za fedha za taasisi zake zote zikiwemo Serikali za Mitaa na vyombo vingine vilivyo chini yake, Mlipaji Mkuu wa Serikali ahakikishe Sheria ya Fedha ya Umma iliyorekebishwa inaanza kutumika, Serikali ihakikishe hati miliki za ardhi na majengo yanayomilikiwa na wizara, idara, wakala na sekretarieti za mikoa zinafuatiliwa mara moja ili kuwa na ushahidi wa umiliki wa mali hizo, Napendekeza kwamba menejimenti za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa kwa kushirikiana na Hazina ihakikishe kwamba modull zote za IFMS zinarekebishwa na zinatumika kikamilifu. Pia, mafunzo,= yafanyike pale inapohitajika hasa wakati kuna waajiriwa wapya au kunapokuwa na maboresho mapya katika mfumo wa kihasibu, Serikali itoe mafunzo jinsi ya kutumia EPICOR 9.05 na viwango vya uhasibu vya	Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa. Zaidi ya hapo mafunzo yatakuwa endelevu Mafunzo ya utumiaji wa Epicor 9.5 uliratibiwa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15 (Moduli ya Usimamizi wa Mali) Serikali itaendelea na mageuzi mbalimbali ya kifedha yaliyosababishaa kupitia Sheria ya Fesha za Umma 2001 (iriyorekebishwa 2004) ili kujumuisha changamoto zinazotokana na hayo Mageuzi Kwa sasa,rasimu ya pili imewasilishwa Mamlaka za juu kwa ajili ya mapitio na mapendekezo.	

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kimataifa visivyo vya taslimu, Kuanza kutumika kwa viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu kabla ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Umma Na. 6 ya 2001 (iliyrekebishwa 2004). Hivyo, Sheria ya Fedha ya Umma inakinzana na falsafa ya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu		
15	**Kubadilisha Hati za Ukwasi kugharamia nakisi ya bajeti** Nashauri Serikali kujiepusha na kubadili hati za ukwasi ili kuepuka uwezekano wa kuwa na deni kubwa lisilolipika siku za usoni. Iko haja ya Serikali kuchukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), kupunguza matumizi, na makadirio ya bajeti yenye ufanisi.	Serikli inakubalianana mapendekezo ya Wakaguzi ili siku za usini ijiepushe na kubadili hati za ukwasi kufidia naksi ya bajeti labda pawepo na mahitaji muhimu ya kufanya hivyo.Kwa ajili ya udhibiti, ubadilishaji wa Hati za ukwasi lazima uidhinishwe na Mamlaka za Juu za Serikali.	**Haijatekelezwa**
16	**Kutolewa migao ya fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha** Ili kukabiliana na changamoto ya fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati, Nashauri Serikali kutengeneza makisio	Kutolewa kwa fedha mwishoni mwa mwaka inatokana na changamoto ya kutekeleza busget	**Inategemea matukio mengine**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	yake ya mwaka yakishabihiana na makusanyo ya mapato ili kuzuia kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa.		
17	**Ulipaji wa kodi ya kupanga ofisi Sh. 7,895,872,337** Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, nyumba na maendeleo ya makazikwa kushirikiana na Wakala wa majengoTanzania (TBA) watafute maeneo ambayo Serikali inaweza kujenga ofisi za wizara, idara na wakala wake. Serikali ifanye majadiliano na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili waweze kupata mkopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali. Serikali pia ifanye mazungumzo na washirika wa maendeleo kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Dunia ili waweze kupata mikopo/misaada kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa ofisi hizo.	Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mamlaka ya Kustawisha Mji mkuu wameanza kutenga maeneo kwa ujenzi wa majengo ya Serikali	**Haijatekelezwa kikamilifu**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Nia ya Serikali ya ujenzi wa majengo inapaswa pia kuelekezwa kwenye Balozi Zetu kwani ni gharama sana kupangisha ofisi na nyumba za wafanyakazi		
18	**Changamoto zinazokabili huduma ya magereza Tanzania** Mahakama ya Tanzania iharakishe kutoa maamuzi juu ya kesi zilizopo. Kuna idadi kubwa ya mahabusu katika magereza ambao wanasubiri kesi zao kusikilizwa na haki kutolewa na mahakama. Kukamilisha kesi zinazowakabili mahabusu kutasaidia kupunguza idadi ya mahabusu katika magereza, Serikali inaweza kuchagua kutumia njia nyingine ya kuwaadhibu wafungwa baada ya kupatikana na hatia. Serikali inaweza kuchagua kutumia njia mbadala kama wafungwa kutumikia kifungo cha nje cha kuanzia mwaka mmoja mpaka miwili chini ya uangalizi wa mkuu wa wilaya au mkoa huku akijushughulisha na shughuli za jamii kama usafi maofisini bila malipo (*extra Mural labour*), kifungo cha nje chini ya	Serikali kupitia Sheria ya Huduma za Jamii, Sheria ya kifungo mbadala (Parole act) na Magereza (Kinga ya ziada ya kifungo cha nje) Kanuni na Sheria zote hizi zinafanya kazi lakini idadi ya wafungwa ambao wanastahili ni wachache sana kutokana na masharti husika. Jitihada zinafanyika ili sheria zilizotajwa kufanyiwa marekebisho ili wafungwa wengi waweze kustahili. Hadi Aprili, 2015 jumla ya wafungwa 4,402 waliandikishwa chini ya kifungo mbadala (Parole) Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge (PAC) wataalikwa kutembelea Magereza na kuona hali halisi ili waweze kuendelea kutoa ushauri juu ya uboreshaji wa Idara ya Magereza.	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	uangalizi cha miaka minne na kuendelea kutokana na makosa madogo madogo kwa wafungwa ambao tayari wametumikia theluthi moja (1/3) ya kifungo chao gerezani huku wakishughulika na huduma za jamii bila malipo (Parole).Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi ya mahabusu na wafungwa katika magereza, Kwa ajili ya wahalifu wadogo na wanaokiuka sheria ni bora kulipa faini , na kama wao wakishindwa kulipa faini, wanapaswa kupelekwa kwa uongozi wa miji yao, au wilaya na kupewa kazi za jamii (*communal based labour*), Kuwahudumia mahabusu na wafungwa kunasababisha gharama kubwa kwa Serikali. Kuwalisha, kuwapa mavazi na matibabu ni ghali. Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kuboresha shughuli zao za uzalishaji kama useremala, shughuli za kilimo, ushonaji, ujenzi wa nyumba na mafundi mitambo na magari. Baada ya hapo, watafute soko la bidhaa zao. Hii itawawezesha kuwa na		

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	uwezo wa kujilisha na kujinunulia mavazi wenyewe, Idara ya huduma ya Magereza inahamasishwa kuandika juu ya mapendekezo kadhaa ya maendeleo na kutafuta wahisani mbalimbali kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), nk ambao watatoa fedha kwa ajiri ya kupanua na kuboresha magereza, Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kutoa wito kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Serikali Kuu (PAC) na viongozi wengine wa Serikali kutembelea magereza na kuona hali halisi katika magereza. Hii itawasaidia kufanya maamuzi sahihi juu ya mgao wa rasilimali.		
19	**Ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Siasa** Ili kuboresha utoaji wa taarifa, uwasilishwaji na ulinganifu wa utendaji wa vyama vya siasa, vyama vinatakiwa kuandaa taarifa za hesabu kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vya kimataifa. Kuanza kutumika kwa mfumo mmoja wa	Office ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa wanashughulikia namna ya marekebisho ya Sheria na. 5 ya Vyama vya Siasa (Iliyorekebishwa 2009) na kutoa miongozo ambayo itajumuisha uandaaji wa taarifa za fedha za Vyama vya Siasa	**Utekelezaji haujakamilika** Wadau bado wanaendelea na mazungumzo namna ya kupata mfumo wa uhandaaji wa Taarifa za fedha

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	taarifa za kihasibu utasababisha kufanana kwa taarifa za hesabu za vyama vya siasa. Hii inawezekana pale ambapo Msajili wa vyama vya siasa akishirikiana na Mhasibu Mkuu wakitoa mwongozo wa aina ya muundo wa taarifa za fedha utakaotumiwa na vyama vya siasa, Napendekeza Serikali irekebishe sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992 ili kutatua changamoto zilizopo.		
20	**Mapungufu katika mifumo ya misamaha ya kodi** Kuanzisha kitengo cha ufuatiliaji wa misamaha ambacho kitakuwa na wajibu wa udhibiti na kuhakikisha kuwa utoaji wa misamaha ya kodi unanakidhi matakwa ya kisheria na kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya misamaha hiyo ya kodi pamoja na kushirikiana na mamlaka zinazohusika na utoaji wa misamaha hiyo. Kufanya mapitio ya sheria za misamaha ya kodi kwa lengo la kupunguza mianya katika misamaha ya kodi. Aidha, serikali ihakikishe kwamba misamaha ya kodi	Serikali itaendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali juu ya misamaha ya kodi. Katika utekelezaji huo, mwaka 2014 Serikali ilifanya mapitio ya ushuru wa mafuta, ushuru wa bidhaa kwa kusitisha misamaha iliyokuwa imetolea na Wizara ya fedha kwa Wawekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji. Hatua hii imechukuliwa ili kupunguza mianya ya ukwepaji wa kodi kupitia misamaha ya kodi..	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	haizidi 1% ya Pato la Taifa au 5% ya mapato ya kodi yaliyokusanywa.		
21	**Kuchelewa katika kushughulikia rufaa za kodi** Naishauri Serikali kuongeza kasi ya kushughulikia hizo rufaa kwa kuzingatia umuhimu wake katika uchumi	TRA imefanikiwa kushughulikia kesi za kodi kupitia Bodi ya Rufaa ya Mapato, Baraza laUshururishi wa Mapato ya Kodi na Mahakama ya Rufaa .Aprili 2016, Bodi ya Rufaa ya Mapato ilikuwa na kesi 117 zenye thamani ya shilingi bilioni 116 . Katika kipindi cha Aprili na Septemba 2016 jumla ya kesi 63 zenye thamani ya shilingi bilioni 66 zilitolea maamuzi.. TRA ilishinda kesi 50 zenye thamani ya shilingi bilioni 58.TRA Ilishindwa Kesi 13 zenye thamani ya shilingi bilioni 8 (sawa na 12.5%). Kwa hiyo bado kuna kesi 54 zinazosubilia maamuzi ya mahakama	**Utekelezaji haujakamilika** Matokeo ya kesi ambazo hazijafanyiwa maamuzi hayawezi kujulikana kwa sasa. Hivyo tutafanya Ufuatiliaji katika kaguzi zijazo
22	**Udhaifu katika usimamizi wa mapato** Naishauri Mamlaka ya Mapato (TRA) kuyafanyia uchunguzi wa kina makampuni yote ya mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na makampuni ya kuchimba madini kutathmini kiwango cha ushuru wa forodha ambacho hakijalipwa na kuchukua hatua ili kilipwe, pia, katika siku zijazo, mamlaka ihakikishe ushuru huo unalipwa	Serikali kupita Mamlaka ya mapato (TRA) imefanya uchunguzi kwa makampuni ya gesi kama ilivyoshauriwa na Wakaguzi	**Inategemea matukio mengine**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na makampuni yote yanayopaswa kulipa.		
23	**Ukosefu wa Uwiano Sawia wa Ukomo katika Dhamana za Serikali** Napenda kuishauri serikali kuongeza ushindani katika soko la ndani la dhamana za serikali na hivyo kuongeza ushawishi wa ununuzi wa dhamana za muda mrefu.	Mara kwa mara Serikali imekuwa ikichukua hatua kuboresha taratibu za ushiriki wa masoko ya dhamana za Serikali kwa kuwashawishi wawekezaji katika dhamana za Serikali za muda mrefu pamoja na kutoa misamaha ya kodi kwenye riba kutoka miaka miwili ya kuiva kwa dhamana za Serikali	**Utekelezaji haujakamilika**
24	**Usimamizi Usiotosheleza Kwenye Uwekezaji wa Serikali na Vipaumbele Vyake** Naishauri serikali kuandaa Mfuko wa Uwekezaji utakaowezeshwa kutoka katika makampuni amabyo inamiliki hisa chache kwenye gawio na mapato mbalimbali ili kunusuru hisa za serikali, na pia kuiwezesha serikali kuwekeza katika sekta zingine ambazo itaona zinahitaji ushiriki wake. Mwisho, naishauri serikali kupitia mara kwa mara ufanisi wa uwekezaji wake na malengo k	Utungaji wa sheria mpya ya Msajili wa Hazina uko katika hatua za mwisho. Kwa sasa andiko la Baraza la Mawaziri linapendekeza kutunga sheria ya Msajili wa Hazina linasubiri kujadiliwa na Mkutano wa Baraza la Mawaziri. Andiko limejumuisha mapendekezo yote ya IMTC	**Utekelezaji haujakamilika**
25	**Ucheleweshaji wa fedha na kutolewa kwa fedha pungufu** Ili kukabiliana na changamoto ya fedha	Ucheleweshaji wa fedha na kutolewa kwa fedha pungufu kunasababishwa na Sababu za Changamoto katika utekelezaji wa bajeti,	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	zilizoidhinishwa na Bunge kutolewa kwa kuchelewa, nashauri Serikali kuandaa makisio yake ya mwaka yanayoshabihiana na makusanyo ya mapato ili kuepuka kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa	Makusanyo ya mapato kutofikia malengo yaliyowekwa, Ucheleweshaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Mchakato mrefu au mchakato mgumu wa kupata mikopo ya mashariti nafuu Hata hivyo, Serikali inadhamiria kupunguza utegemezi kwa Asilimia tisa (9%).Msisitizo wa kutumia EFD na makubaliano ya mapema katika kupata mikopo yenye mashariti nafuu	
26	**Mapungufu katika Usimamizi wa rasilimali watu na malipo ya mishahara** Maafisa Masuuli wanashauriwa kutumia kwa ufanisi mfumo wa kompyuta wa Lawson na kuhakikisha kwamba kumbukumbu sahihi za wafanyakazi zinatunzwa na wakati huohuo maafisa waliostaafu wanafutwa kwenye mfumo huo kwa wakati, pia kuhakikisha kuwa mtumishi haidhinishiwi mkopo mpya kabla ya kulipa na kumaliza uliotangulia Menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa kusitisha mara moja malipo ya posho na kodi kwa watumishi waliostaafu walioko nje ya nchi	Katika mwaka 2012 Serikali ilianzisha Mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu (Lawson) ili kuhakikisha kwamba Malipo ya mishahara yanasimamiwa kupitia sheria za usimamizi wa rasilimali watu na kuendana na nyaraka za kiofisi zinazoambatishwa kwenye miamala katika mfumo kwa ajili ya kuidhinishwa. Pia Serikali imendelea kulipa waajiriwa waliostaafu katika Balozi na kuwarejesha nchini ambapo katika mwaka 2014/15 wafanyakazi kumi na sita walirejeshwa nchini	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na kufanya utaratibu kwa ajili ya kuwarejesha maafisa husika nyumbani mara tu muda wa utumishi wao unapokoma.		
27	**Mapungufu katika Usimamizi wa mali kwani kasi ya kutadhimini mali, kuandaa rejista ya mali na kuweka alama za utambulisho unaonekana kukwama** Mlipaji Mkuu wa Serikali aharakishe mchakato huo na ahakikishe changamoto zote zilizobainika zinashughulikiwa kabla ya mwaka 2016/2017 ambapo serikali inatakiwa iwe inatekeleza IPSAS kikamilifu, Mlipaji Mkuu wa Serikali atoe mwongozo wa namna ya kuweka kumbukumbu katika rejista ya mali za kudumu, msisitizo uwe katika jinsi ya kutathimini mali, kiwango cha uchakavu, kuweka alama za utambulisho na uboreshaji wa taarifa mara kwa mara katika rejista ya mali za kudumu, Kuzingatia matumizi ya mifumo ya kompyuta ambayo inaendana na	Mshauri mwelekezi aliyeazimwa na Wizara ya Fedha kupitia Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazikwa ajili ya kuhakikisha ardhi yote inayomilikiwa na Serikaliinapewa nyaraka za usimamizi wa Ardhi na si lazima hati miliki	**Utekelezaji haijakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kuingiliana na mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) kwa ajili ya kusimamia mali za serikali ili kuepuka uandaaji wa taarifa nyingi na vihatarishi vinavyotokana na kuhamisha taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine, Naishauri Serikali ihakikishe taarifa za kihasibu za Maafisa Masuuli zinatenganisha ardhi na majengo ili kupata thamani ya ardhi na kutoza uchakavu kwenye mali zinazochakaa. Pia, nashauri serikali ihakikishe Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa zinapata hati miliki ili kulinda mali zake, Nashauri serikali ichukue hatua stahiki kuweza kufuta ambazo zimechakaa na hazitengenezeki kwa mujibu wa kanuni za fedha za mwaka 2001.		
28	**Limbikizo la madeni** Ninaishauri serikali kuongeza makusanyo ya mapato, kupunguza matumizi ya serikali na hatimaye kutumia baki ya fedha kulipa madeni, zaidi ya hayo ninaishauri serikali kulipa umuhimu wa	Maelekezo kutoka kwa Katibu Mkuu kiongozi (Kumb.SAB/4857/0/23) ya Tarehe 24 Oktoba, 2013 NA Waraka wa Hazina Na.4 wa 2014/15 ulielekeza kila Afis Masuuli kuchukua hatua kali na tahadhali ya kutotengeneza madeni mapya. Kwa madeni ambayo hayajalipwa , Maafisa	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kipekee swala la kulipa madeni ya huduma za afya nje ya nchi.	Masuuli walielekezwa kuyaingiza kwenye bajeti inayofuata	
29	**Madeni yanayotegemea Matukio (Contingent Liabilities)** Maafisa Nasuuli wa kila Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa Kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wahakikishe ufuatiliaji wa karibu kuakikisha kesi ambazo hazijaamuliwa zinashughulikiwa mapema ili kuiondloea au kupunguza gharama zinazoweza kuotkana na kushindwa kesi	Serikali iko hatua za mwisho za kutoa muongozo kwa Maafisa Masuuli wote juu ya taratibu za kushughulikia kesi za kisheria ili kuwasaidia kuzifanyia kazi kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali , hasa kutoa taarifa sahihi kwa wakati ili kumsaidia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa mashtaka au kuandaa taarifa ya upande wa utetezi kadri ya kesi itakavyokuwa na kuanza mashhtaka katika mahakama husika	**Utekelezaji unaendelea**
30	**Ukaguzi maalum wa mradi wa manunuzi ya matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2014.** Serikali inapaswa kutathmini uwezo wa kifedha wa mradi, uwezo wa rasilimali watu na uwezo wa kiufundi ili kujua udhaifu uliopo na hatimaye kutoa msaada ipasavyo. Usimamizi wa mradi wa matrekta chini ya SUMA JKT uhakikishe mradi unatekelezwa	Serikali imeanza kuchukua hatua ili kuhakikisha mradi wa Matrekta chini ya SUMA JKT unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma ili kuhakikisha masharti ya pande zote mbili yanatekelezwa ipasavyo. Masharti yote yaliyotambuliwa kutotekelezwa yanapaswa kutekelezwa: vilevile, gharama zinazohusiana na Malipo kwa mwajiri. Zaidi ya hayo Serikali kupitia vyombo vyake kama Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Mkaguzi mkuu wa ndani na Ubia kati ya	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kwa kufuata Sheria na Kanuni husika za manunuzi ili kuhakikisha pande zote mbili katika mkataba zinatekeleza mkataba ipasavyo, majukumu yote ya kimkataba ambayo hayajatekelezwa inapaswa yatekelezwe au gharama husika zirejeshwe kwa mwajiri	sekta binafsi na umma wataendelea kufanya ukaguzi na usimamizi wa mikataba wa SUMA JKT kwa lengo la kuhakikisha masharti yote ya mikataba yanatekelezwa kulingana na makubaliano. Serikali kupitia SUMA JKT inakubali kwamba masuala ya fedha yanapaswa kufanyiwa tathimini na hasa madhara ya kushuka kwa dola juu ya mradi na kutambua hasara inayotokana na kushuka kwa dola.	
31	**Ukaguzi maalum wa mfumo mzima wa manunuzi wa pembejeo za kilimo katika sekta ya kilimo cha tumbaku chini ya WETCO – Tabora** Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inapaswa kuimarisha jukumu la usimamizi ili kuhakikisha kunakuwa na utawala bora katika uendeshaji wa vyama vya ushirika,	Ili kuhakikisha viongozi wa Vyama vya ushirika wanatimiza wajibu wao ipasavyo, Sheria Na.6 ya mwaka 2013 imeeleza kwamba kila mjumbe wa Bodi aliyeteuliwa anapaswa kuwa amefunzwa juu ya uongozi na ujuzi wa usimamizi wa vyama vya ushirika hasa utawala bora na kanuni za maadili. Mafunzo haya yanapaswa kufanyika kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao yaliyoainishwa.	**Imetekelezwa**
32	**Ukaguzi maalum juu ya utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili**	Kwa masuala ya ubunifu yanapaswa kupitiwa na mtaalamu mwenye uwezo, Wizara ya Maji inakubali juu ya umuhimu wa kumshirikisha Mshauri mwelekezi mwenye utaalam wa kupitia	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Wazabuni wapewe mikataba ya kazi inayolingana na uwezo wao na daraja la mkandarasi kwa mujibu wa Bodi ya Usajili wa wakandarasi (CRB) Usanifu wa miradi kama wa usambazaji wa maji Chalinze ni vema ukapitiwa kwa umakini kabla ya kutangazwa kwa zabuni, Taasisi zinazofanya manunuzi zinapaswa kuimarisha ufuatiliaji ili kuhakikisha wakandarasi wanafuatiliwa na wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa mkataba. Taasisi zinazofanya manunuzi zinatakiwa kuwa na hakika wa upatikanaji wa fedha kabla ya kuingia katika mikataba ili kuepuka gharama za ziada kama tozo zinazosababishwa na ucheleweshaji wa malipo.	ubunifu wa usanifu.Wizara ya Maji imekuwa ikiunda kikosi kazi kutathimini ubunifu kabla ya kutangaza zabuni.. Zaidi ya hayo, Wizara ya Majiinahakikisha kwamba ujenzi wa njia za usambazaji zinasimamiwa na kufuatiliwa na Mshauri mwelekezi kwa kila mkataba Nyongeza ya hapo ni kwamba menejimenti imekuwa ikiunda kikosi kazi cha kusimamia na Kufuatilia utekelezaji wa mikataba yote.	
33	**Ukaguzi maalum katika Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha Shilingi 252,975,000,000 za ujenzi wa barabara kutumika kulipia madeni nje ya utaratibu** Bajeti inapaswa iandaliwe kwa kuzingatia mahitaji halisi.	Serikali inakubali mapendekezo ya Wakaguzi juu ya kuhakikisha bajeti inaandaliwa kwa kuangalia shughuli halisi zitakazotekelezwa. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi itaandaa bajeti na kuanza kujenga barabara mpya kulingana na uwezo wa kifedha ili kuepusha ukuaji wa deni kwa siku za usoni	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Serikali isaini mikataba mipya ya ujenzi wa barabara baada ya kupima uwezo ilionao wa kulipa madeni ya wakandarasi waliopo ili kuzuia kukua kwa madeni katika siku zijazo		
34	**Ukaguzi maalum wa taarifa za fedha zilizotumika katika mkutano wa kimataifa wa SMART Partnership Dialogue (SPD) wa mwaka 2013 uliofanyika kwa miezi kumi na tisa kuanzia Julai, 2012 hadi Januari, 2014** Nashauri taasisi zinazofanya manunuzi ya vifaa, huduma na ujenzi zihakikishe manunuzi yote yanawekwa na kufanyika kwa mujibu wa mpango wa manunuzi. Taasisi zifanye manunuzi yenye tija kwa taifa kwani kiasi kikubwa cha fedha za serikali zinatumika katika kufanya manunuzi.	Mamlaka ya Udbibiti wa Manunuzi ya Umma imekuwa ikitoa mafunzo juu ya Sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake ili kuongeza uwezo kwa wadau mbalimbali. Mamlala ya Udbibiti wa manunuzi ya Umma hufanya ukaguzi kwenye Taasisi nunuzi pamoja na mambo mengine mpango wa manunuzi ya mwaka hufanyiwa tathmini	**Inategemea matukio mengine**
35	**Usimamizi wa bajeti usioridhisha** Ukomo wa bajeti unapaswa kuwa wa uhalisia na unapaswa kupitiwa mara kwa mara. Hatua zichukuliwe ili kupunguza ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka	Mhasibu Mkuu ameendesha warsha Mwezi Novemba, 2014 kwa kuwahusisha Wahasibu wakuu wote na kuweka msisitizo juu ya kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma katika michakato ya Malipo iliyofanyika. Juu ya hayo	**Inategemea matukio mengine**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Wizara ya Fedha. Miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya mipya wakati wa utengaji na ugawaji wa fedha. Kukuza ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kuongeza ulipaji kodi kwa hiari ili kukuza mapato, kuongeza vyanzo na kupanua wigo wa kodi. Nashauri Serikali itumie hati za manunuzi kutokana na mfumo wa EPICOR kuepuka kuwalipa wazabuni nje ya bajeti na kutoa kipaumbele kwa miradi inayoendelea na kuhakikisha uwepo wa fedha kabla ya kusaini mikataba. Serikali ianzishe utaratibu wa kutunza kumbukumbu za madeni mwishoni mwa mwaka na kuhakikisha kuwa malimbikizo hayo yanabajetiwa katika bajeti ya mwaka unaofuata. Mbinu hii itapunguza ukuaji wa madeni.	Mkutano wa Maafisa Mauuli ulifanyika Januari, 2015 ambapo mambo ya usimamizi wa bajeti yalijadiliwa.	
36	**Kutotumika kwa Mashine za kielektroniki za EFD kutokana na kutozingatia Kanuni Na. 24 ya Kanuni za Mapato (EFD) Kanuni za 2012,**	Serikali kupitia Wizara ya Fedha imetoa maelekezo kwa taasisi zote za Serikali kuacha kufanya biashara na wauzaji wasiotumia mashine za EFD	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Serikali itoe maelekezo kwa taasisi zote za Serikali kutojihusisha na wauzaji ambao hawatumii mashine za EFD. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya kodi nashauri elimu ya ulipaji kodi bila shuruti iendelee kutolewa mara kwa mara.		
	2014/15		
37	**Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi** Serikli kupitia kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuhli wanashauriwa kuweka jitihada ili kuhakikisha mapanekezo yote ya ukaguzi yaliyotolewa na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge yanashughulikiwa ipasavyo	The Ministry of Finance and Planning vide letter with Ref No CHA.114/4 Kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CHA.114/47/4/01756 ya tarehe 14/3/2016 Wizara ya Fedha Nna Mipango ilielekeza maafisa Masuhuli waote katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kuweka jitihada zaidi ili kuhakikisha maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge yanafanyiwa kazi iasavyo	**Utekelezaji haujakamilika**
38	**Usimamizi wa Fedha za Umma** Serikali inahamasishwa kutumia vyanzo mbadala vya mapato ya ndani	Hakuna majibu ya Serikali	**Haijatekelezwa**
39	**Mapato yaliyokusanywa chini ya kiwango Shilingi 1,091.27** Serikali inaombwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani. Jitihada zaidi zinahitajika kwa Serikali kuhakikisha	Serikali inatambua mapendekezo ya Mdibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Kupitia uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Serikali itaendelea kuanzisha hatua za kudhibiti ili kuboresha ukusanyaji wa mapato. hatua ni	**Utekelezaji haujakamilika** Tutafanya tathimini ya utekelezaji katika kaguzi zinazofuata

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	uzingatiaji wa sheria na kuchukua hatua juu ya limbikizo la madeni ya kodi kwa kuweka riba na adhabu, kuimarishaukaguzi wa kodi na vikosi vya uhakiki vya Mamlaka ya Mapato na idara ya uchunguzi wa Kodi kupunguza kuongezek kwa ukwepaji na mazoea ya kukwepa kodi na kuimarisha ukaguzi, udhibiti na mmbinu za usimmashineamizi wa mizigo na mafuta kutoka nje au iliyo njiani ili kupata kaodi zote kulingana na sheria zilizopo, kuongeza wigo wa kodi, kuboresha utii na ukusanyaji wa kodi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali	pamoja na ukusanyaji wa malimbikizo ya kodi kwa nguvu, kusululisha mapingamizi ya kodi, na ufuatiliaji wa kesi za rufaa. Hatua nyingine zitajumuisha ukaguzi wa kodi na uchunguzi	
40	**Kushindwa kurejesha pesa za Mpango wa kubakiza makusanyo kiasi cha Shilingi bilioni 21.04** Natoa wito kwa Wizara na Idara zilizo chini ya mpango wa kubakisha pesa kwa kukusanya mapato yasiyo ya kodi ili kufikia malengo yaliyowekwa, hii ni pamoja na kuwa na bajeti ya awali (zero budget) kwa ajili ya wale ambao walikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi	Kutorejeshwa kwa shilingi bilioni 21.04 chini ya mpango wa kubakiza makusanyo ilitokana na ukweli kwamba mapato yaliyokusanywa hayakutosheleza kulingana na vipaumbeli	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	bilioni moja kwa mfano (Idara ya Magereza na Wizara ya Maendeleo ya Jamii chini ya CDTI).		
41	**Ujumuishaji wa Taasisi zenye tarehe tofauti za kuripoti Hesabu bila kufanya marekebisho** Serikali kupitia Msajili wa Hazina ina jukumu la kuhakikisha ufuatiliaji wa karibu ili taasisi zinazopaswa kujumuishwa zinakuwa na muda unaofana wa kuandaa Hesabu	Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa Waraka Namba 11 ya mwaka 2014/15 tarehe 9 Januari 2015 na kukumbushia tena kupitia barua yenye Kumb. Na. CAN III / 372/01/05 ya tarehe 15 Oktoba 2015 iliyotolewa na Msajili wa Hazina juu ya mabadiliko katika mwaka wa fedha. Taasisi nyingi zilizingatia isipokuwa Taasisi za fedha za umma kama vile Benki ya Twiga, Benki ya Wanawake Tanzania, Benki ya Uwekezaji Tanzania, Benki ya Posta Tanzania n.k	**Utekelezaji haujakamilika**
42	**Utofauti Katika Uandaaji wa Taarifa za Mtiririko wa fedha (Cash Flows)** Ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa maelekezo yanayoongoza uandaaji wa hesabu yatolewe na Mhasibu Mkuu wa serikali kupitia kwa Katibu Mkuu Hazina ili kuondoa utata unaojitokeza wakati wa kuandaa Hesabu.	Tarehe 9 Januari, 2015 Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa Waraka wa Hazina Namba 11 ya mwaka 2014/15. Aidha, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, TAMISEMI na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu alikutana tarehe 10 Novemba, 2015 ili kujadili juu ya suala hilo. Azimio lililofikiwa lilitolewa na CAG kupitia barua ya tarehe 2015/10/11 yenye Kumb. Na CE.27 / 307/14	**Imetekelezwa**
43	**Kuandaa Hesabu za Majumuisho za Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala**	Serikali inatambua ukweli kwamba maandalizi ya taarifa za fedha hayatokani na mfumo	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	wa serikasli, Serikali za mitaa na Taasisi za Serikali zinazofanya biashara kwa Kutumia Mfumo Usiojiendesha Serikali inapaswa: Kuboresha mfumo wa Epicor unaojiendesha kujumuisha Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa na Taasisi zinazojiendesha kibiashara Kuongeza jitihada za kujumuisha Balozi za Tanzania katika mfumo wa ili kuongeza udhibiti wa bajeti na kuaminiwa kwa taarifa za fedha Kuoanisha mfumo wa kutunza taarifa(Database) wa Wizara,Idara ,Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa ili kuweza kujiendesha kutoa taarifa za fedha kutoka kwenye mfumo wa Epicor, na hatimaye, kuendeleza mfumo bora wa kujumuisha taarifa za fedha za Serikali kwa kutumia Epicor lakini mazingira ya utendaji yanasababisha utenganisho wa mifumo ya kuhifadhi taarifa.	unojiendesha. Taarifa jumuifu za fedha za Serikali zimeandaliwa kwa kutumia TEHAMA (ICT) kwa njia excel na si kwa mfumo wa EPICOR ambao ulijumuisha taasisi 553. Hata hivyo, uongozi unafanya mipango yote ili kuhakikisha kwamba kuoanisha/kushirikiana kwa programu mbalimbali ya kutumiwa na taasisi hizi baada ya utafiti wa kina juu ya jinsi muungano unaweza kufikiwa kwa kujiendesha wenyewe. Hivi sasa, uongozi unendelea na mchakato wa kuunganisha balozi katika EPICOR kwa majaribio ya Balozi saba. Wakati huo huo, utafiti wa jinsi programu mbalimbali ya kutumiwa na Taasisi za serikali unavyoweza kuunganishwa.	
44	**Kukosekana kwa vigezo vya uthaminishaji kwa ajili ya utoaji wa**	Uongozi unatafuta njia bora ya kufanya zoezi hili, wakati huo huo, maandalizi ya kutambua	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Pensheni za Serikali shilingi bilioni 597.4 Serikali kuzingatia IPSAS 25 juu ya uhasibu wa maslai ya wafanyakazi kwa kufanya tathimini ili kujua kiasi cha madeni ya wastaafu na Watumushi wa kudumu wanaoidai Serikali.	madeni ya pensheni katika taarifa za fedha badala ya thamani inayotokana na thathimini yamefanyika. Uzoefu huu hutumiwa na baadhi ya nchi za Afrika Mashariki. Hitimisho la utafiti huu litamshirikisha CAG.	
45	**Mali za kibaiolojia ambazo hazijabainishwa shilingi bilioni 83.993** Kuandaa taarifa ya mali za kibaiolojia kulingana na IPSAS 27 Kujumuisha taratibu za kutoa taarifa ya mali za kibiolojia kwenye miongozi ya taratibu za uhasibu ili kutoa mwelekeo kwa kila Taasisi namna ya kuhesabu na kuonesha mali za kibaiolojia	Mwaka 2015 Serikali kupitia Mhasibu Mkuu wa Serikali aliandaa na kusambaza mwogozo wa uhasibu. Sura ya kwanza kifungu cha 1.7 cha mwongozo kimetoa muda wa kubadilisha mwongozo kwenda na wakati, na kitabu cha muongozo aya 1.7. Aidha Serikali imetoa waraka wa hazina Na.3 wa tarehe 3 Juni, 2016 wa kufunga mwaka 2015/16 mbali na mambo mengine umetoa maelekezo kwa Taasisi zenye mali za kibaiolojia kuzingatia mahitaji ya IPSAS 27.	**Imetekelezwa**
46	**Usimamizi usiojitosheleza katika uwekezaji wa Serikali na maslahi yake** Serikali kuanzisha mfuko uliotayari kusubiri uwekezaji kutoka kwenye mapato yaliyopokelewa kutoka kwenye gawio na mapato mengine ili kujenga mfuko wa	Serikali inakubaliana na mapendekezo ya CAG na itaanzisha utaratibu ambao utamfanya Msajili wa Hazina kubakiza kiasi chote kilichopokelewa kama gawio au mapato mengine kutoka kwenye uwekezaji katika taasisi nyingine ili iwe rahisi kupata mitati pale itakapohitajika	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	uwekezaji wa mtaji ambao Serikali ina hisa ili kuwekeza tena au kushiriki katika kufungua njia nyingine za uwekezaji ambayo Serikali anataka kuwekeza. Hii inaweza kuhusisha serikali kuruhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kubakisha makusanyo yote kwa kipindi maalum (miaka minne hadi mitano) Serikali kupitia, Wixara ya Fedha, ianzishe mpango wa kubakiza mapato kwa ajili ya Ofisi ya Msajiri wa Hazina ili kuanzisha mfuko wa uwekezaji uliopendekezwa. jMpango huu utasaidia pia kama kipimo cha ufanisi kwa Msajili wa Hazina ambacho kitawezesha Serikali kufanya tathimini uwezo wa Msajili wa Hazina kuhamasisha mapato kutoka kwenye mapato ya uwekezaji wake		
47	**Ushiriki hafifu wa Msajili wa Hazina katika Mkutano Mkuu wa mwaka katika Taasisi ambazo kuna uwekezaji wa Serikali** Uongozi wa ofisi ya Msajili wa Hazina uanzishe mfumo utakaowezesha Serikali	Daima Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikishiriki katika mikutano mikuu ya mwaka katika makampuni ambayo Serikali imewekeza	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	iwe inawakilishwa ipasavyo na kushiriki katika kufanya maamuzi katika kampuni ambazo Serikali ina hisa kwa Faida ya umma.		
48	**Usimamizi wa Madeni yaliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina** Serikali huwa inapangilia upya na kutenga madeni yasiyo ya uwekezaji na muda wake wa dhamana kwenye Deni la Taifa na Huduma za jumla ili kuiwezesha Serikali kuwa muundo wa usimamizi na ulipaji. Hii inaweza kufanyika na Serikali kwa kutoa dhamana ambayo kutumika kama chombo cha utambulisho na kuhudumia madeni hayo chini ya fungu husika. Uongozi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina uweke sawa kumbukumbu za madeni yake na kila mwaka kuandaa bajeti ya kutosha kulipia madai yaliyobaki amabayo yanahusiana na kazi za uwekezeji pale yanapositahili kulipwa. Hii itaepusha kulimbikiza zaidi madeni.	Tayari Ofisi ya Msajili wa Hazina imewasiliana na PST kupitia baua yenye kumb. Na. CAN.15/36/02/02 juu ya kuamisha madeni yasiyohusu uwekezaji amabyo yanachukuliwa kuwa sehemu ya deni. Wizara ya Fedha na Mipango ilalifanyia kazi suala hili kupitia CPAD na Serikali iko makini kutekeleza ushauri wa Wataalam. Aidha, Uongozi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina umeandaa bajeti ya shilini bilioni 151 kwa mwaka wa fedha 2016/17 kulipia sehemi ya madeni yake.	**Utekelezaji haujakamilika**
49	**Mambo muhimu yaliyochangia kutofikia**	Kupunguza matumizi ya misamaha ya kodi. Kwa	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	malengo yaliyowekwa Serikali inapaswa kuendelea kupitia sera za kifedha na kodi kwa lengo la kuondoa ukarimu wa kodi.Hii inaweza kufanyika kupitia ukaguzi wa kina na udhibiti wa ukarimu/motisha wa kodi, kuongeza Ufuatiliaji na upekuzi juu ya matumizi ya motisha za kodi. Serikali iendelee kuongeza uwazi wa misamaha ya kodi kupitia matangazo ya misamaha na ukaguzi huru wa misamaha ya kodi kwa mwaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Srikali Serikali iimarishe usimamizi wa marejesho ya kodi na mfumo wa kupokea ufanyike kupitia efd na kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa marejesho ya kodi ili kupunguza madai hewa kutoka kwa wadai wa mtandao wa kodi ya ongezeko la thamani(VAT) Serikali iimarishe ukaguzi wa kodi, uchunguzi na kutumia hatua za kisheria kuzuia ongezeko la ukwepaji na mazoea ya kukwepa kodi.	kipindi cha kuanzia July 2015 to May 2016 misamaha ya kodi ilifikia shilingi milioni 1,487,137.0 sawa na 1.6% pato ghafi la Taifa (GDP). Hatua nyingine zinajumuisha kutunga sheria ya kodi la ongezeko ya thamani (VAT) ya 2014 ambayo, kwa kiasi kikubwa, imeondoa baadhi ya vitu kwenye sheria iliyotangulia.Zaidi ya hapo, Mamlaka imeimarisha udhibiti juu ya uhakiki wa matumizi kabla ya kurejesha hela iliyolipwa, kutembelea miradi ili kuhakiki uwepo wake na kuongeza mifumo ya udhibiti wa ndani (Kama ITAX,TANCIS, na EFDMS NK) ambazo zinaharakisha kugundua wafanya biashara hewa. Serikali imendeleza jitihaza za kuimarisha ukaguzi wa kodi na uchunguzi ili kuzuia ukwepaji wa kodi au makadirio yaliyo chini ya hali halisi. Zimekuwepo jitihada za kuwajengea uwezo Maafisa wa kodi na vitendea kazi ambayo vimerahisisha utambuzi wa ukwepaji wa kodi.. Pamekuwepo na ubadilishanaji wa taarifa katika Mamlaka za Mapato,udhibiti mkali wa forodha, Ufuatiliaji wa mizigo iliyo njiani, udhibiti wa maghara ya dhamana (Bonded ware	

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Serikali itangaze misamaha ya riba na adhabu juu ya kuonesha kwa hiari deni la kodi na malipo ya awamu ya madeni ya kodi kwa kutoa fursa kwa Walipa kodi ambao huamua kutubu na kuanza ukurasa mpya kwa kuwezesha walipa kodi kulipa kiasi wanachodaiwa bila kujumuisha riba na adhabu katika madeni ya nyuma. Serikali iimarishe ukaguzi na udhibiti wa taratibu za kutoa mizigo kutoka nje au iliyo njiani ili isitumike ndani ya nchi na kodi stahiki kukusanywa mara moja pale mizigo inapotumika ndani ya nchi. Serikali iendelee kufunga na kutumia mita sisizo na dhamana (off bond meters) na kupata/kujenga Hifadhi ya Taifa ya Mafuta katika kila bandari ya kuingia ili kiwango wa petroli itakayoingizwa nchini iwe na kumbukumbu sahihi na kutolewa kwake kudhibitiwa ipasavyo. Matumizi ya mita kati yake na Kisima cha hifadhi ya Mafuta itawezesha mamlaka husika kuwa na kumbukumbu sahihi ya mzigo uliopakuliwa na mafuta ya petroli	house) na Bandari kavu (ICDS) pamoja na kutoa zawadi kwa watoa taarifa wanaosaababisha ukusanyaji wa kodi iliyokwepwa . Kuoanisha mfumo wa ununuaji wa mafuta wa pamoja, kumewezesha Mamlaka kutambua mapema kiwango cha kodi kitakacholipwa.. Utekelezaji wa Mpaka mmoja wa forodha (Single Customs Territory) umeondoa fursa ya kutupa mizigo katika soko la ndani. Imekuwepo programU endelevu ya kutoa elimu kwa Walipakodi kuWelemisha Juu ya masuala mbalimbali ya kodi ikiwamo kudai risiti yz EFD na kuimarisha taratibu za uhakiki wa marejesho ya Kodi ya ongezeko ya dhamani (VAT) ili kuhakikisha madai sahihi ndo yanarejeshwa	

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	yaliyosambazwa. Hivyo, kuongeza mapato kutoka sekta ya mafuta ya petroli		
50	**Usimamizi wa Pingamizi za kodi na kesi za pingamizi za kodi za muda mrefu ambazo hazijafanyiwa maamuzi na Mamlaka ya Mapato** Usikilizaji wa rifaa za kodi unapaswa kuhakishwa na Bodi ya Rufaa, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Kwa utatuzi ulioshindikana kwa muda mrefu, Napendekeza Serikari kuunda Tume huru ya Malalamiko ili kuharakisha kushughulikia rufaa Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania uimarishe ukaguzi na uchunguzi ili kupunguza migogoro ya kodi kati ya Mamlaka na Walipakodi.	Idara ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato inafanya kazi kwa ukaribu na mahakama ili kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi mbalimbali za Rufaa pamoja na Tarehe 7/2/2017 siku ya Sheria, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, John Pombe Magufuli alimuagiza Jaji Mkuu, Othman Chande kuhakikisha usikilizaji wa kesi za kodi unaongezewa kasi.. Mahaakama ya Rufaa ya Tanzania imenza kusikiliza kesi ambazo hazijashughulikiwa. Kuanzisha Tume huru ya kushughulikia mlalamiko ni suala la sera litakaloshughulikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa maana hiyo TRA ina mradi wa majaribio katika Mkoa wa Manyara kwa kuanzisha mfumo wa utetezi wa WalipakodI (Taxpayer Advocacy System-TAS) kwa kusikiliza na kumshauri Kamishina Mkuu juu ya mapingamizi ya kodi ziliyotokea kwa Walipakodi wadogo na wakati ili kufapa	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
		sululisho la haraka la hiyo migogoro TRA ina taarifa za kila robo mwaka juu ya Kesi zilizoshughulikia na kutengeneza ripoti za kesi ambazo hazijashughulikiwa	
51	**Kasoro zilizoonekana katika mapingamizi ya Kodi na Mifumo ya ushawishi ya ulipaji Kodi** Kushughulikia maombi ya mapingamizi ya kodi kwa haraka ili kutatua hizo pingamizi. Hii inaweza kufanyika kwa kuongeza idadi wa Wafanyakazi hodari na wenye uzoefu na kuimarisha kitengo cha ufundi. Pia, kuimarisha mchakato wa kutathmini ili kupunguza idadi ya mapingamizi yaliyoweza kujitokeza Kuchunguza mahitaji ya sheria ya Kukusanya juu ya theludhi mona ya kodi iliyotathaminiwa au kiasi ambacho hakiko katika mgogoro kabla ya kupokea pingamizi la kodi na Kuokoa amana kutoka kodi iliyotathminiwa katika pingamizi	Uongozi unachukua hatua stahiki za kuhakikisha maombi ya migogoro ya kodi yanashughulikiwa mapema na kujumuisha mapingamizi ya kodi ambayo muda wake wa kulipwa umefika lakini hayajalipwa Shilingi 580,718,607,384. Hizi ni pamoja na hatua za muda mfupi kwa kuongeza muda wa kufanya kazi na hatua za muda mrefu zinajumuisha kutafuta wafanyakazi wenye ujuzi ili kuimarisha timu ya kushughulikia pingamizi .	**Utekelezaji haujakamilika**
52	**Usimamizi wa misamaha ya kodi** Serikali; Iendelee kufanya mageuzi ya usimamizi	Serikali inakubali mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Serikali itaendelea kupitia sera za fedha na kodi	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	wa motisha kwa lengo la kupunguza kiwango ch misamaha ya kodi mpaka 1% ya pato la Taifa au chini ya Pato la Taifa na kuchochea kiwango cha makusanyo ya mapato. Hili linaweza kufanyika kwa kufanya ukaguzi wa kina na kudhibiti mootisha za kodi, kuongeza usimamizi na upekuzi juu ya utumiaji wa motisha za kodi	kwa lengo la kuondoa motisha mbalimbali za kodi. Hii itafanyika kwa kufanya ukaguzi wa kina na kudhibiti motisha za kodi, kuongeza usimamizi na upekuzi juu ya motisha za kodi	
53	**Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizohifadhiwa katika maghala kabla ya kulipiwa ushuru wa forodha** Serikali ichukue hatua za haraka kuuza bidhaa zilizokaa kwenye maghala kwa muda mrefu kwa njia ya mnada ili kuepusha kushuka kwa thamani na kuharibika kwa bidhaa zilizokaa muda mrefu na kuisababishia Serikali hasara ya mapato Serikali iongeze usimamizi na mbinu za uhakiki wa maghala ili kuzingatia mahitaji ya kifungu cha 42(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.	Kati ya Kiasi kilichohojiwa, shilingi 77,872,535,125 (71%) zilihusiana na bidhaa zilizoingizwa kwenye Ukanda wa kuuza Bidhaa nje (Export Processing Zone), Kutengeneza bidhaa chini ya dhamana,maduka yaliyosamehewa ushuru, maghala yaliyo ya ushuru wa kodi na wauaji wa magari mapya ambayo hayahusiki chini ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Pia 87% ya bidhaa zililipiwa ushuru wa forodha na bidhaa zilizobaki zinasubiria mnada na kuahribiwa Kati ya shilingi 9,151,090,596.72 zilizohojiwa na Wakaguzi, shilingi 8,822,432,335.36 (96.4%) ni bidhaa iliyouzwa nje kupitia vituo mbalimbali katika mipaka na kiasi kilichobaki shilingi	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Serikali itoe ushahidi wa bidhaa zilizouzwa nje kwa kusamehewa ushuru wa forodha wa shilingi 9,151,090,597. Vinginevyo, itoe ushahidi wa kuokoa kiasi kilichohojiwa. Pia, kuongeza mbinu za udhibiti wa bidhaa zote zilizo njiani na kuuzwa tena nje kuepusha kutumia katika soko la ndani kinyume na sheria na kuisababishia Serikali mapato ya Serikali .	328,658,261.36 (3.6%) ya bidhaa hazijathibitishwa kama zimeuzwa nje. Jalada la hoja limepelekwa kwa Wakaguzi kwa uchunguzi na uhakiki	
54	**Mifumo isiyoridhisha ya Udhibiti wa mafuta yanayosafirishwa nje ya nchi na bandari kavu** Serikali iongeze uzingatiaji wa taratibu za kutoa bidhaa na kudhibiti mafuta yaliyo njiani na bandari kavu ili kuhakikisha makusanyo ya ushuru wa forodha. Serikali ichunguze mafuta yote ambayo hayajathibitishwa na kuokoa kodi kwa mafuta yaliyotumika soko la ndani	Serikali itaendelea kuongeza uzingatiaji wa taratibu zote za kutoa bighaa kama ilivyopendekezwa. Maingizo 139 yenye shilingi 11,937,625,883 yamefsnyiwa kazi na kuingizwa kwenye mfumo. Ushahidi wa maingizo 139 kwenye mfumoumetumwa mipakani ili kuingiza kwenye nyaraka kuu.Zaidi ya hayo, TRA itaendelea kuchunguza mafuta yote ambayo hayajathibitishwa na kuokoa kodi kwa mafuta yaliyotumika kwenye soko la ndani	**Utekelezaji haujakamilika**
55	**Kutokukusanywa kwa faini zilizotokana na ucheleweshwaji wa malipo ya dhamana zilizoisha (Cancelled bond) na kuchelewa kulipa kodi za mafuta**	TRA itahakikisha riba na faini zinatozwa kwa malipo yaliyocheleweshwa ya mafuta yaliyo njiani na kutumika katika soko la ndani na kuokoa kiasi ambacho hakikukusanywa kama	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	yaliyotumika nchini bila kulipa kodi kwa kisingizio cha kwamba yapo njiani kwenda nchi za nje. Serikali: Ihakikishe riba na faini zinatozwa kwa malipo yote yaliyocheleweshwa ya mafuta yaliyo njiani na kutumika katika soko la ndani na kuokoa shilingi 47,005,629 ambazo hazikukusanywa kulingana na kifungu cha 249 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 na; Kukusanya faini zote katika ucheleweshaji wa malipo ya dhamana zilizoisha zenye thamani ya shilingi 1,886,574,959.39 kama inavyotakiwa na kanuni ya 104 (17) ya Kanuni za Usimamizi wa kodi katika Jumuiya za Afrika Mashariki ya mwaka 2019.	kitakuwepo. Zaidi ya hapo, faini zote kwenye ucheleweshaji wa dhamana zilizoisha kama inavyotakiwa na kanuniya 104 (17 ya Kanuni za Usimamizi wa Ushuri wa Forodha katika Jumuia ya Afrika Mashariki ya mwaka 2010 zitakusanywa na kuwashirikisha Wakaguzi	
56	**Kutokukusanywa kwa Kodi na Ushuru wa forodha unaotokana na mafuta yaliyoingizwa nchini Sh.5,774,263,079** Serikali: Ichunguze utofauti wa mafuta kwa lengo la kutambua kama mafuta yalitumia	Serikaliimetekeleza mapendekezo ya CAG. Kiasi chote kilichoojiwa cha shilingi 9,463,254,713.80 kimefanyiwa kazi na ushahidi umewasilishwa kwa Wakaguzi kwa uchunguzi na kuangalia uwezekano wa kuifunga	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kinyume cha sheria katika masoko ya ndani na kuhakikisha kuwa ushuru wa forodha uliotathiminiwa pamoja na faini na riba unakusanywa Kuhakikisha udhibiti wa mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje unaimarishwa kwa lengo la kuzuia vitendo kama hivyo havitokei tena kwa siku za Usoni		
57	**Kodi zilizokokotolewa na kutokukusanywa kwa wakati TZS. 297,296,619,239** Serikali ianzishe hatua kali za kisheria kukusanya kodi ambazo hazijalipwa kutokana na tathmini iliyofanywa na Idara ya Uchunguzi wa Kodi,Kitengo cha Uhakiki na Tkaguzi wa Kodi	Kwa maana hiyo, Majibu ya hoja Na 32 (Temeke) ya shilingi 1,235,580,882.00; Hoja Na. 50 (Kinondoni) shilingi 6,860,707,985.43; Hoja Na. 120 (Ilala) shilingi 11,560,478,591.69 na Hoja Na. 148 (Mwanza) shilingi 1,259,233,015 yamewasilishwa kwa Wakaguzi kwa ajili ya uhakiki. Mpaka sasa tumeweza kukusanya shilingi 4,403,236,609.00. Mchakato wa ukusanyaji umebakiza shilingi 17,945,963,865.12 zitakazo kusanywa kabla ya Septemba 2016. Mchakato huu utawashirikisha Wakaguzi.	**Utekelezaji haujakamilika**
58	**Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi shilingi 43, 911,472,701** Kuboresha ukaguzi na uchunguzi	Uongozi wa TRA utaendelea kuweka jitihada za kuimarisha ukaguzi wa kodi na uchunguzi ili kupunguza madai hewa kutoka kwenye mtandao wa Kodi ya Ogezeko la Thamani na kukabiliana	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	wa ukokotoaji wa kodi ili kupunguza udanganyifu wa madai ya kodi zinazotokana na mauzo ya bidhaa kutoka kwa wafanyabiashara waliopo katika mfumo wa kodi ya ongezeko la thamani na kuzuia udanyanyifu wa utoaji wa taarifa zinazoonyesha makadirio ya chini ya mapato katika taarifa za mapato ya walipa kodi. Kufanya uchunguzi wa kodi zilizobainika kuwa pungufu katika ukokotoaji na kuhakikisha tofauti ya kodi hizo zinakusanywa pamoja na riba na tozo kama inavyotakiwa katika Sheria za Kodi.	na kutoa taariza za chini ya marejesho ya kodi Uongozi wa TRA utaendelea kuchunguza tathimini zilizo chini ya hali halisi na kuokoa kodi zote ambazo hazijalipwa pamoja na riba na faini kama inavyotakiwa na sheria za kodi.	

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
59	**Kuhudumia Deni na Uchambuzi wa Deni la Taifa** Serikali iongeze juhudi za ndani katika kukusanya mapato ili kupata fedha ya kutosha kulipia madeni kutokana na kukosekana kwa mkakati wa vyanzo vya mapato. Mkakati utawezesha kulipia deni badala ya kulipa deni kwa kukopa (rollover) kama ilivyo sasa. Serikali iweke mkakati wa matumizi bora ya raslimali fedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi na kukopa mikopo yenye masharti nafuu na usimamizi wenye ufanisi na kuratibu shughuli za kigeni nchini Serikali kupitia Mkakati wa Taifa wa Madeni ihakikishe Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Deni inatekelezwa	Serikali iko kwenye mchakato wa kupitia Sera ya Deni la Taifa na kurekebisha sheria iliyopo ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada sura 134 (iliyorekebishwa 2004) ili iendane na Idara ya Usimamizi wa Deni la Taifa iliyoanzishwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ili Sera ya ya Usimamizi wa Deni la Taifa iweze kufanya kazi	**Utekelezaji unaendelea.** Tutafanya tathimini ya utekelezaji wa majibu ya Serikali katika ukguzi ujao
60	**Kutoingizwa kwa dhamana za Serikali kwenye Deni la Taifa**	Serikali imeishaingia makubaliano na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na itatoa dhamana zisizo taslimu na Dhamana ambazo hazijalipwa baada ya kuhakikiwa zitatambuliwa kama Deni la Taida	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Serikali iharakishe marekebisho ya Sheria ya Dhamana, Mikopo na Misaada ya 1974 (Iliyorejewa 2004) ili kukabiliana na changamoto ya Usimamizi wa wa Deni la Taifa	kwenye fungu husika	
61	**Kukosekana kwa usuluhishi wa malipo kati ya Serikali na Benki Kuu** Serikali ihakikishe inafanya ulinganisho wa hesabu mara kwa mara na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka tofauti kama hizo katika siku zijazo.	Serikali itahakikisha ulinganisho na udhibitisho wa hali halisi na Benk Kuu unafanyika mara kwa mara ili kuepusha tofauti kwa siku za usoni	**Utekelezaji haujakamilika**
62	**Sheria ya Deni na Mpango Mkakati wa Deni la Taifa vilivyopitwa na Wakati** Serikali ipitie Mkakati wa Deni la Taifa na kuhakikisha Sera ya Usimamizi wa Deni la Taifa inafanya kazi. Pia Serikali Iharakishe marekebisho ya Sheria ya Dhamana za Serikali,Nikopo na Misaada ya 1974 (Iliyorejewa 2004) ili kukabiliana na changamoto za Deni la Taifa na Usimamizi wake	Serikali iko kwanye mchakato wa kupitia kuhakikisha Sera ya Usimamizi wa Deni la Taifa na kuhakikisha sera hiyo inatumika na kurekebisha Sheria ya Dhamana za Serikali, Mikopo na Misaada ya 1974(Iliyorejewa 2004) ili kukabiliana na changamoto za Deni la Taifa na Usimamizi wake	**Utekelezaji haujakamilka**
63	**Madeni Mfu Yasiyolipwa kwa Muda Mrefu Bilioni 2,090** Serikali IharakishE mazungumzo na Nchi	Mazungumzo na Klabu ya Ufaransa (Parish Club-PC VII) bilateral ya mpango wa unafuu wa deni kwa pande zote mbili kwa Wadai wa Klabu ya	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	husika kwa lengo la kutoa msimamo wa madeni husika na kuanza kuhudumia madeni hayo.	Ufaransa wale wasio wa Klabu ya Ufaransa: pale makubaliano yatakapo hitimishwa, akaunti ya deni mfu itakuwa imetatuliwa	
64	**Kuchelewesha Makato ya Kisheria ya Mafao na Kusababisha Adhabu ya Shilingi Bilioni 52.8** Serikali kutoa michango ya makato ya kisheria kwa Mifuko ya Pensheni kwa wakati muafaka ili kuepuka adhabu zisizo za lazima na kuzingatia matakwa ya sheria. Kwa kufanya hivyo, itaboresha ukwasi wa fedha na kuwezesha walengwa wa pensheni kulipwa kwa wakati.	Serikali inachukua hatua kadhaa kulipa maadhi ya madeni ya mafao. Pia Serikali inachukua jitihada kuboresha makusanyo ya mapato na kuimarisha hatua za ukusanyaji ili kuhakikisha fedha zinapatikana ili shughuli za Serikali fifanyike vizuri.	**Utekelezaji haujakamilika**
65	**Ukokotoaji Usio Sahihi wa Mafao ya Wastaafu** Maafisa Masuuli wahakikishe wanaoshughulikia Mafao wazingatie kanuni ya ukokotoaji na sheria na kuhakikisha wanawasilisha majalada ya mafao yaliyokamilika, kwa wakati na yakiwa na taarifa zahihi ili kuepusha ucheleweshaji wa malipo ya mafao. Mafunzo yatolewe kwa wanaoshughulikia mafao ili kuongeza uelewa wa sheria za	Hakuna jibu	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	mafao na mambo mengine		
66	**Ucheleweshwaji Usiokuwa na Tija katika Kuandaa Mafao ya Wastaafu** Serikali inashauriwa kuwasilisha michango ya kisheria ya makato kwenye Taasisi za mifuko ya Jamii ili kuepusha ucheleweshaji wa kushughulikia mafao na faini. Maafisa Masuhuli wahakikishe Wanaoshughulikia mafao wanazingatia sheria na kanuni.Wanapaswa pia kuwasilisha majalada ya mafao yaliyokamilika,kwa wakati na yawe na taarifa sahihi ili kuepusha ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya Wastaafu Serikali itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa Wanaoshughulikia mafao ili kuongeza uelewa wa sheria za mafao na mabo mengine	Hakuna jibu	**Haijatekelezwa**
67	**Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani katika Taasisi** Maafisa masuhuli wahakikishe kuna rasilimali za kutosha na kuwa na Kitengo	Serikali kupitia Mkaguzi Mkuu wa Ndani chini ya Wizara ya Fedha na Mipango itendelea kuimarisha uwezo wa Wakaguzi wa Ndani na kusimamia utendaji kazi wao ili kuhakisha	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	cha Ukaguzi wa ndani kinachofanya kazi na kuhakikisha majukumu ya kisheria ikijumuisha utambuzi wa mifumo ya ndani na kupendekeza ipasavyo hatua za marekebisho	uhalisia unatolea katika maeneo ya udhibit wa ndani, usimamizi wa majanga na utawala. Zaidi ya hayo, Maafisa Masuhuli wataelekezwa kuchukua hatia zote kurekebisha mapungufu yaliyoainishwa na Mkaguzi wa Ndani	
68	**Tathimini ya Kamati za Ukaguzi** Maafisa Masuuli wahakikishe kamati za Ukaguzi zinatimiza majukumu ya kisheria kulingana na Kanuni za fedha za Umma Ili kuchochea uwajibikaji na utoaji Huduma kwa kutoa usimamizi wa nazi ya juu ya ufanisi wa mifumo ya udbibiti wa ndani na kuzingatia Sheria na Kanuni	Serikali kupitia Mkaguzi Mkuu wa Ndani chini ya Wizara ya Fedha na Mipsngo itaendelea kufundisha wajumbe wa kamati za ukaguzi katika Wizara,Idara na Wakala wa Serikali kwa lengo la kuwaongezea ujuzi. Zaidi y hayo,Maafisa Masuuli wanakumbushwa kuhakikisha Kamati za Ukaguzi zinapewa ushirikiano wa kutosha ili kutekeleza majukumu ya kisheria kulingana na Kanuni za fedha za Umma na Miongozo ya kamati za Ukaguzi zilizotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango mwaka 2013	**Imetekelezwa**
69	**Mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi** **M**aafisa Masuuli wanashauriwa kuboresha taratibu za kusimamia na kudhibiti vihatarishi kwa kuhakikisha kuwapo kwa taratibu zilizoandikwa vizuri za kuzuia vihatarishi na kufikia malengo	Miongozo ya kuboresha na kutekeleza muundo wa usimamizi wa majanga umetolewa	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	yaliyowekwa..		
70	**Tathimini ya Mifumo ya TEHAMA** Serikali inapaswa kuangalia usiri, uaminifu na upatikanaji wa habari. Kutafsiri na kuweka katika mazingira rafiki muundo wa TEHAMA ili uendane na maamuzi ya kimkakati, uwekezaji na mipango kuhakikisha udhibiti wa teknolojia ya habari unasimamiwa ipasavyo Muundo uweke kipaumbele cha kanuni za kamati za kuendesha REHAMA, Mpango Mkakati wa TEHAMA NA Muundo wa kazi utakaowezesha malengo na mipango ya Taasisi	Mwaka 2012 Wizara ya Fedha na Mipango ilianzisha muongozo wa usalama wa TEHAMA ambao utekelezaji wa usalama ulifanyika. Hii inategemewa kutekelezwa na kila Wizara, Idara na Wakala wa Serikali Wizara ya Fedha na Mipango ilianzisha kamati tendaji ya TEHAMA ambayo inaongoza shughuli za TEHAMA. Kila Wizara, Idara na Wakala wa Serikali wanatakiwa kufuata Wizara ya Fedha na Mipango inajiandaa kuandaa mpango wa kudhiibiti majango katika Mfumo Jumuifu wa Fedha na mifumo mengine ya fedha ya kielektronic.Hii pia itatumika katika kila Wizara,Idara na Wakala wa Serikali. Katika Bajeti ya 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango imetenga fedha kwa ajili kujumuisha shughuli zote za Serikali katika mfumo wa Epicor	**Imetekelezwa**
71	**Tathmini ya Kugundua na Kuzuia Udanganyifu** Mambo yafuatayo yamegunduliwa;	Serikali kupitia Mkaguzi Mkuu wa Ndani chini ya Wizara ya Fedha amechukua hatua za kusaidia Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Serikali	**Implemented**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Kukosekana kwa sera ya usimamizi wa udanganyifu ambayo itaonyesha viashiria hatarishi. Tathmini ya vihatarishi hazikufanyika mara kwa mara Hakuna ushahidi wa maandishi wa kutambua udhibiti maalum ambao utasaidia kupunguza hatari ya makosa kutokana na udanganyifu. Hakuna tathmini yoyote ya usimamizi wa mifumo ya ndani iliyofanyika. Uelewa mdogo wa udanganyifu kutokana na ukosefu wa tathmini yoyote ya vihatarishi uliofanywa: **Mapendekezo ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali** Wizara, Idara na Wakala wa Serikali zianzishe mbinu za kugundua na kuzuia vitendo vya udanganyifu kwa kuweka vigezo vya ktambua udanganyifu ambavyo vitasaidia Wizara, Idara na Makala wa Serikali husika kupunguza na kuzuia masuala ya udanganyifu	za mitaa katika kubaliliana na udanganyifu na masuala ya udhiti wa ndani Hatua hizo ni kama : Kutoa miongozo ya kuendeleza na kutekeleza usimamizi wa udanganyigu na viatarishi. Miongozo inalenga kutoa maelekezo kwa vitendo kwaTaasisi za Serikali katika kuboresha na kutekeleza kushabihana kwa mifumo na programu za viatarishi vya udanganyifu Kutoa miongozo ya mifumo ya udhibiti wa ndani katika Taasisi za umma.Miongozo iliyoboreshwa inatoa kiwango cha chini katika kuboresha,kuendeleza na kuongeza mifumo ya udhibiti wa ndani Mafunzo kwa baadhi ya Wakuu wa Idara za Wizara, Idara, Wakala wa Serikalai na Serikali za Mitaa juu ya usimamizi wa viatarishi vya udanganyifu na uboreshaji wa udhibiti wa ndani na Serikali itaendelea kuangalia Maendeleo yake	
	Kutozingatia Sheria ya Bodi ya Mikopo ya	Serikali kupitia kwa Mlipaji mkuu wa Serikali,	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya 2004 kwa ajili ya malipo ya mkopo. Maafisa masuuli (Waajiri) kutoa taarifa Bodi ya Mikopo juu ya ariraya wanufaika wa mkopo na kulipa kila makato kutoka kwenye ujira au mshahara ndani yasiku kumi na tano baada ya mwisho wa kila Mwezi	Msajiri wa Hazina na Katibu Mkuu wa Wizar ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilitoa barua kwa Maafis Masuhuri (Waajiri) wa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Taasisi binafsi juu ya Waajiri kuzingatia mawasilisho ya taarifa ya Wahitimu wa Elimu ya Juu kutoa makato kwenye mishahara kupitia barua kumb.. Na. CBE.165/328/01/3 ya tarehe 10/3/ 2016 kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na FB.41/185/01A/82 na tarehe 8/4/, 2016 zimerejewa. Aidha, Serikali imeandaa rasimu ya marekebisho ya sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo imejumuisha kipengele cha malipo ya mkopo kuwa ya kisheria na makato ya mkopo kuwa tozo ya kwanza kabla ya makato mengine yasiyo ya kisheria. Rasimu itapelekwa Bungeni katika vikao vinavyofuata Septemba 2016.	
73	**Malipo kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye Utumishi wa Umma Shilingi 392,651,036** Maafisa Masuuli wahakikishe kiasi kilicholipwa kinarejeshwa Wizara ya fedha	Katibu Mkuu Utumishi kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CFC.26/205/01 "B"/44 alielekeza waajiri wote wawasilisheuwepo wa watumishi hewa na hatua zilizochukuliwa kuhakikisha mishahara iliyolipwa kwa Watumishi	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na Maofisa husika. Kwa nyongeza, Nawashauri Maafiss Masuhhli kuimarisha udhibiti kwa kuboresha kumbukumbu za watumishi kupitia mfumo wa LAWSON na kusafisha taarifa iwe shughuli endelevu kwa kila Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa	hewa inarejeshwa serikalini. Mpaka sasa kama waajiliwa 1,826 wanakadiriwa kurejesha shilingi 12,244,692,233.75	
74	**Upungufu wa Watumishi wa Umma** Maafisa masuhuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Managementi ya Utumishi wa Umma kuwa na idadi kamili ya nafasi zilizojazwa au kupitia nguvu kazi iliyopo kulingana na mahitaji halisi	Waajiri wana mamlaka ya kuomba idadi inayotoshelewa ya waajiliwa wapya katika mwaka wa fedha husika kupita HCMIC kulingana na ukubwa wa kazi na mipango mkakati.Waajil pia wamepewa mamlaka kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na vifo, kustaafu, kuachishwa kazi nk	**Haijatekelezwa**
75	**Wafanyakazi ambao hawajathibitiswa baada ya muda wa majaribio kumalizika** Maafisa Masuuli wahakikishe waajiliwa wanathibitishwa mara moja baada ya kumaliza muda wao wa majaribio na taarifa zao kuboreshwa kwenye mfumo wa LAWSON	Serikai imepokea mapendekezo ya CAG na Maafisa Masuhuli watakumbushwa kuwathibitisha waajiliwa wapya baada ya kukamilisha muda wa majaribio	**Utekelezaji unaendelea**
76	**Kukosekana kwa ushahidi wa kupima na kutathimini utendaji wa wafanyakazi**	Kulingana na Sheria Na.8 ya Utumishi w Umma ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kwa uwazi Maafisa Masuuli wafanye tathimini ya utendaji wa kazi kwa uwazi kwa wafanyakazi wao wote kulingana na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009	Na.18/2007 mfumo wa tathimini ya utendaji wa wazi ni jambo la kisheria. Maafisa Masuuli watakumbushwa kuzingatia matakwa ya sheria	
77	**Wakuu wa Vitengo kukaimu nafasi zilizo wazi kwa zaidi ya miezi sita** Maafisa masuhuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais managementya utumishi wa Umma ijaze nafasi muhimu kwa kuweka waajiliwa wenye uwezo	Serikali inakubaliana na mapendekezo ya CAG na mchakato wa kujaza nafasi za uongozi zinaendelea	**Utekelezaji unaendelea**
78	**Kuchelewa kutuma makato ya kisheria kwenye Mishahara - Shilingi 707,169,904** Serikli ihakikishe inawasilisha makato ya kisheria kulingana na sheria	Katika kushughulikia hili tatizo,Serikali katika mwaka wa fedha 2014/1 iliwasilisha michango wa waajiliwa kwenda kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ifuatavyo NSSF – Shilingi bilioni 21.3 , GEPF – Shilingi bilioni 28.4 , PSPF – Shilingi bilioni 424.7 , LAPF – Shilingi bilioni 135.7 , PPF – Shilingi 39.9 na NHIF – Shilinig bilioni 142.1.	**Utekelezaji unaendelea**
79	**Kodi ya Mapato kutolipwa kutoka kwenye posho za kukaimu Shilingi 78,187,048** Maafisa Masuhuli wahakikishe posho zote	Kulingana na kifungu cha 7(2) CHA Sheria ya Mapato ya mwaka 2008 posho zoteza waajiliwa zinapaswa kutozwa kodi ya mapato.Kwa sasa mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	za kukaimu zinatozwa kodi ya Lipa Kadri Unavyopata.Kwa nyongeza,Maafisa Masuhuli wahakikishe kodi ya mapato ambayo imelimbikizwa inalipwa Mamlaka ya Mapato Tanzania	Watu umewezeshwa kukata kutoka kwenye posho ya kukaimu	
80	**Watumishi walio na mikataba ubalozini hawakulipwa kiinua mgongo - Shilingi 17,980,539** Serikali ihakikishe kuwa viinua mgogo kwa wafanyakazi vinalipwa kulingana na mikataba	Wizara iliwasilisha shilingi 20,905,250.00 kwa lengo la kulipa kiinua mgongo kwamfanyakazi aliyeshikizwa Cairo katika Mwezi Desemba 2015	**imetekelezwa**
81	**Mishahara isiyolipwa ambayo haijarejeshwa Hazina - Shilingi 2,233,475,668** Maafisa Masuuli wazingatie kanuni 133(i)na (2) ya Kanuni za fedha za Umma za mwaka 2001.Na Zaidi ya hayo kuhakisha mishahara ambayo haikulipwa inarejeshwa Hazina	Maafisa masuuli watakumbushwa wanazingatia kanuni 133(i)na (2) ya Kanuni za fedha za Umma za mwaka 2001 ikijumuisha kurejesha mishahaya ambayohakulipwa inarudishwa na Mkuu wa Jeshi la Wananchi	**Haijatekelezwa**
82	**Watumishi wa umma kupokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria** Maafisa Masuuli kuimarisha udhibiti kwa kuthibitisha mikopo ya wafanyakazi wote	Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali Watu umewezeshwa kuzuia makato kwenye mishahara chini ya theluthi moja(1/3) kulinana na kifungu cha 3 cha Sheria ya Kukusanya madeni sambamba na waraka wenye kumb.	**imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na kuwaliliana na watoaji wa mikopo kiasi kwamba makato hayazid theluthi mbili ya mshahara wa kila Mwezi kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Makusanyo ya Madeni ya mwaka 1970 na waraka wenye kumbu Na.C/CF.45/271/01/1/87 of 19March,2009 kutoka kwa Katibu Mkuu-Ofisi ya Rais Management ya Utumishi wa Umma	Na.C/CF.45/271/01/1/87 of 19 Machi, 2009 kutoka kwa Katibu Mkuu-Ofisi ya Rais Menegementi ya Utumishi wa Umma	
83	**Watumishi waliostaafu kufanya kazi bila kuwa na mikataba ya ajira** Ofisi ya Raisi-Menegementi ya Utumishi wa Umma isiingie mikataba ya ajira na Wastaafu mpaka pesa ya kulipia uhamisho itakapokuwa tayari. Nyongeza ya hapo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iandae mpango endelevu kurahisisha kujaza nafasi za Wastaafu.	Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa imeuelekeza Ubalozi wa Tanzania wa Washntoni kulipa gharama za uhamisho na gharama nyingine kwa Wastaafu kupitia barua yenye kumb. Na FAP 2506/106 na FAP 2506 ya Tarehe 17th May,2016 na 16 Juni, 2016 kwa mfuatano. Baada ya kurejea kwa Mstaafu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tutapeleka mfanyakazi mwingine kujaza nafasi iliyoachwa wazi	**Utekelezaji unaendelea**
84	**Kufanya kazi ubalozini zaidi ya muda ulioidhinishwa** Afisa Masuuli wa Wizara ya Mambo ya Nje	Kwa mwaka wa fedha 2015/16 Maafisa waliozidisha muda walirejeshwa nchini. Aidha,Serikali inatafuta fedha ili kulipa gharama	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na Ushirikiano wa Kimataifa azingatie kanuni ya 31(1) na (2) ya Kanuni za Huduma ya mambo ya nje ya Tanzania ya mwaka 2013 ya kuamisha wafanyakazi	za mizigo kwa wale wote waliozidisha muda ili kuendana na Kanuni ya 31(2) ya Huduma za mambo ya nje ya Tanzania ya mwaka 2013	
85	**Utegemezi wa Ruzuku za Serikali** Serikali inashauriwa kuendelea mbinu zitakazosaidia Wakala kutegemea vyanzo vyao vya mapato badala ya ruzuku za Serikali	Serikali imeishaanza kuhakikisha Mashirika ya Umma na Wakala wanajiendesha bila kutegemea fedha kutokaSerikalini. Baaddhi ya hizi hatua ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa lengo la kuokoa fedha kwa ajili ya shughuli za msingi.Kwa kufanya hivyo, Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ametoa waraka Na.1 wa mwaka 2015 kuzuia Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine kulipa posho za vikao kwa Wajumbe wa ya mapatoBodi. Serikali pia imerekebisha Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 iliyoweka ukomo wa gharama za uendeshaji kutozidi Asilimia 60% ya mashirika ya Umma. Katika bajeti ya 2016/17 Serikali haikutenga fesha kwa ajili ya Matumie mengine kwa baadhi ta Mashirika ya Umma yanayoweza kutengeneza mapato yake kama njia ya kupunguza utegemezi kutoka bajeti ya Serkali	**Utekelezaji haijakamilika**
86	**Kuchelewa kuanza huduma ya usafiri wa mabasi**	Huduma ilianza kutolewa mayi,2016 baada ya kukamilisha sehemu ya kufunga na kufanya	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Uongozi wa Wakala wa usafiri wa mabasi yaendayo kasi unaelekezwa kufuata masharti yaliyowekwa kwenye mikataba ili kuepuka mikataba kuchelewa zaidi	majaribio ya mfumo wa AFCC. Uidhinishaji wa Leseni ya utendji naMradi wa Mabasi yaendayo Kasi kutoka SUMATRA ilitolewa Meyi, 2016 Ufungaji wa mifumo ya ITS bado unaendelea na unaweza kukamilika Septemba 2016	
87	**Ununuzi wa mabasi uliozidi mahitaji** Uongozi wa Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) uhakikishe kwamba uendeshwaji wa UDA-RT unazingatia kanuni na tararibu zilizoainishwa kwenye mkataba. Uwajibikaji wa ziada unapaswa kusimamiwa kwa malengo yaliyokusudiwa	Serikali anakubali kwamba ISP (UDA-RT) ina ilizonunuliwa mabasi 140 badala ya 76 kinyume na mkataba. Mabasi haya ya nyongeza yalnunuliwa bila makubaliano na Wakala na Serikali; Hata hivyo hii ililidhiwa Nyongeza No.1 iliyorekebishwa ili kuingiza ziada ya mabazi yote 140. Wakala pia uliwasiliana na UDART kuweka nembo kulingana na mkataba wa ISP. Adhabu itatozwa baada ya muiezi mitano ya uendeshaji kama kama hawatazingatia. Hivyo kwasababu ISP imeishapewa onyo juu ya ukiukwaji, tozo ya adhabu inaweza kutozwa mara tu baada ya muda uklio kwenye mkataba kuisha.	**imetekelezwa**
88	**Mapungufu ya ununuzi wa kivuko Shilingi 7,916,955,000** Uongozi uwasiliane naMzabuni kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa	Tarehe 25 Aprili, 2013 Wakala wa Ufundi wa mitambo na Umeme uliingia Mkataba na Johns. Gram Hansen Bergensgade 10 DK 2100 Copenhagen Oe Dermank kuleta Kivuko kipya	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	na kamati ya ukaguzi na upokezi yakijumuisha kasi ya juu na chini na mwishowe kutoa hati ta kupokea mizigo.Pia,Uongozi unashauriwa kuzingatia masharti ya mikataba na Sheria ya Manunuzi ya umma na kanuni zake za 2013.	kwa njia ya Dar Es Salaam na Bagamoyo .Kivuko kililetwa Novembar 2014. Wakati wa majaribio iligundulika kivuko hivyo hakikukidhi viwango vilivyowekwa vya kasi ya noti 20. Kamati ilipendekeza Mzabuni kurekebisha mapungufu.Mzabuni alikubali kupitia barua yenye kumbu. Na.JGH 285449 ya tarehe 9 Decemba, 2015. Mawasiliano Zaidi yamefanywa na Mzabuni kupitia barua yenye kumbu.Na. TMS/F/86/8 ya tarehe 2 Mei 2016 ikimtaka Mzabuni kuwasilisha kwa Wakala wa Ufundi wa Mitambo na Umeme ratiba inayojumuisha mpango uliopendekezwa kurekebisha kasi kama ilivyotolewa kwenye mkataba kwa ajili ya kuidhinishwa.Wakati wa kujibu Mzabuni aliboresha mpango kazi kwa barua Na.28549 ya tarehe 13 Mei, 2016 ambayo kwa sasa inasubilia kuidhinishwa na Wizara.Baada ya kukamilisha kurekebisha na kama kivuko kitafikia kasi iliyokubaliwa Wakala wa Ufundi wa Mitambo na Umeme utatoa hati ya kupokea mizigo.	
89	**Kuchelewa kukamilika kwa kazi ya ujenzi**	Wakati ukaguzi unafanyika kwenye miradi mwenendo wa mtiririko wa taslimu kwa Wakala	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Uongozi wa Wakala wa Barabara ufanye ufuatiliaji wa fedha kutoka Wizara ya Ujenzi n kuakikisha miradi inakamilika mapema. Utoaji wa mkataba ufanyike kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ili pasiwe na hati inayobaki bila kulipwa na hivyo kusababisha riba. Hii ingeisaidia Serikali kuzuia gharama ambazo zingekwepeka kukadiria mradi na muda. Uongozi wa Wakala wa Barabara kuweka jitihada Zaidi katika kusimamia miiradi/mikataba ili utekelezaji ufanyike ndani ya muda uliopangwa.	wa Barabara haukuwa toshelevu. Hatahivyo, tangu Desemba 2015 mtiririko wa taslim imeboreswa na baada ya kupokea hela kutoka Hazina kwa ajili ya malipo ya madeni yote ya Wakandarasi/Washauri ikijumuisha riba kwa kuchelewesha malipo. Kwa mwaka wa fedha 2015/16 kiasi cha shilingi 667,788,106,184 zililipwa kwa Wakala wa Barabara kutoka Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya kupilia madeni dhidi ya shilingi. 70,955,371,965.78 zilizotengwa kwenye miradi iliyocheleweshwa. Kiasi kilicholipwa kimepunguza riba zilizopaswa kulimbikizwa kwa sababu ya kuchelewesha malipo	
90	**Ongezeko la riba katika 15% mkopo Shilingi 12,723,218,833** RITA ilipe mkopo bila kuchelewa zaidi ili kupunguza mzigo kwa Serikali kutokana na riba inayozidi kuongezeka.	Serikali kupitia kwa katibu Mkuu kiongozi alielekeza Wizara husika (Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Katiba na Sheria, na Wizara ya Kazi) kuunda Kamati ya ufundi ili kushauri namna ya kutatua ukata.Timu iliundwa tarehe 4 Aprili, 2016. Hii timu inajumuisha wajumbe kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, RITA, NSSF, Wizara ya Fedha na Mipano na Wizara ya Kazi. Serikali inasublia ushauri kutoka kwenye hii timu na Serikali iko makini kutekeleza	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
91	**Mapato yasiyokusanywa kwenye Mauzo ya nyumba za Serikali shilingi 214,748,556** Uongozi wa Wakala wa Majengo ya Serikali uchukue hatua za kisheria dhidi ya wakwepaji na kuja na mikakati wa kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kulingana na makubalianao ya mkataba kwa pande zote ili kuepusha hasara ya mapato ya Serikali	Wakala wa Majengo ya Serikali umeingia makubaliano na Kampuni ya Minaya ya Yono Auction Mart kukusanya madeni katika mikoa yoteya Tanzania Bara na kuwafukuzia Wakwepaji wote walioshindwa kulipa madeni ndani ya kipindi cha notisi. Serikali imeishakusanya shilingi 129,269,979.83 ambayo ni 60% ya madeni yote ya shillingi. 214,748,556.00.	**Utekelezaji haujakamilika**
92	**Matokeo ya ujumla ya ukaguzi wa vyama vya siasa** Uongoi wa vyama vya siasa kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Sasa kuzingatia kifungu cha 14 cha Sheria Na.5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na kifungu cha 25(2) na (40 cha Sheria ya Fedha za umma ya mwaka 2001(Iliyorejewa 2004) na Kanuni na. 71 ya kanuni ya Ukaguzi wa Umma ya 2009 kwamba Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa	Msajili wa Vyama vya Siasa amefuata kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Vyama Vya Siasa kya mwaka 1992 kwa kuvitaka Vyama vyote vyenye usajili wa Kudumu kuwasilisha Hesabu zilizo kaguliwa kabla ya 27 Julai 2016 kupitia barua yenye kum.Na.AB.111/368/01/64 ya tarehe 15 Aprili, 2016 na AB.111/368/01/69 ya tarehe 7 Aprili, 2016. Vyama vyote vya Siasa kupitia barua yenye kumb.Na.HA.171/322/01/79 ya tarehe 30 Juni, 2016.	**Imetekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	hezabu za mwisho na kuwailisha kwa Mkaguzi na Mdhibiti na Mkaguzikwa ajili ya ukaguzi kabla ya 30 Septemba ya kila mwaka		
93	**Utendaji usioridhisha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** Serikali inashauriwa kuhakikisha vifaa vya kuzuia moto vinafanyiwa majaribio na kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara: pia kusaidia Idaza ya Zimamoto na Uokoaji wanakagua na kufundisha wafanyakazi namna ya kutimia vizuia moto	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea nz zoezi la ukaguzi wa usalama wa masuala ya moto nchi nzima na kutoa mafunzo Zaidi kwa Waajiriwa juu ya matumizi sahihi ya vizimia moto. Katika bajeti ya Mwaka 2016/17 Jeshi limebajeti shilingi 1.500,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa zabuni mbili kama njia ya ya kupunguz upungufu mkubwa katika nchi	**Utekelezaji haujakamilika**
94	**Ukaguzi Maalum wa Hesabu za Mpango wa pili wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP II D by D) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30/6/2013** Watekelezaji wenza kwa kushirikiana na Wenza wa Maendeleo kufanya uchunguzi wa kina juu ya mapungufu yaliyoonekana	Uchunguzi wa kina (Ukaguzi maalum) ulifanywa na PWC ulitoa hoja za ukaguzi wa matumizi mabaya ya shilingi 605,583,379 na ilipendekezwa kiasi hicho kirejeshwe kwa Wafadhili husika. Baada ya Uchunguzi wadau walikubaliana Kamba Serikali irejeshe hicho kiasi cha shilingi 605,583,329 kwa wafadhili	**Haijatekelezwa**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
95	**Kuhakiki na kuthibitisha fedha zilizotumwa kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi** Serikali ifanye uchunguzi wa kina kwa kurejea masuala yaha kwenye Mamlaka za Uchunguzi kwa lengo la kuchukua hatua na kuzuia kutokea tena katika Idara nyingine za Serikali Serikali kupitia kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kuna udhibiti toshelezi kwenye kuhaurisha fedha kwenda kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara Mama na kuanzisha mbinu za kusimamia na ufuatiliaji kwa lengo la usululisho na utoaji wa taarifa za fedha	Uchunguzi ulifanyika na Mwajiriwa aliyeiba hundi yuko katika Mahakama ya Kisheria na tunasubilia maamuzi ya mahakama. Kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Udhibiti umewekwa kuhakikisha Taasisi zinapewa Nyaraka za Kutuma hela(Warant of funds) Wizara iwe inaomba stakabadhi ya kukiri kupokea hela zilizohaulishwa kwenye Akaunti za Banki za Taasisi	**Utekelezaji unaendelea**
96	**Utekelezaji wa Sera ya mambo ya Nchi za Nje za Kiuchumi na Diplomasia** Huduma za kidiplomasia hazina utoshelevu na ujuzi wa watu wanaofaa kufanya hii kazi kwa ufanisi. Baadhi ya Balosi hazina wafanyakazi wa kutosha kulinganisha na mipaka yao ya kazi na kuwa chngamoto kutoa Huduma	Serikali inakubaliana na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya kupanga wafanyakazi katika balozi kulingana na ujuzi na maarifa katika maendeo ya Biashara, Uwekezaji , Utalii na Usimamizi wa Uchumi. Pia Serikali kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakatibila kuchelewa ili kuwezesha balozi kutimiza ankra zao kwa wakati kulingana na	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	katika kiwango kinachotakiwa Kwa miaka mingi Balozi zimekuwa hazitengewi bajeti toshelezi ili kutimiza malengo, matarajio na mipango yao japokuwa wanapaswa kushughulikia masuala ya kidiplomasia na matukio ya kiuchumi katika miji mikuu na majiji mengine katka nchi za Ulaya ya Mashariki na Kati ambazo zina muunganiko wa kihistoria na nchi yetu Kukosekana kwa uratibu na ufanisi wa mawasiliano wa Wizara za Kisecta unaweza kuzuia utendaji sahihi wa shughuli mbalimbali katika balozi mbalimbali.Pia shughuli nyingi zinazohusiana na biashara za kidiplomasia ziko mikononi wa sekta binafsi hivyo kuitaji ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na Sekta za biashara ili kufanikisha malengo ya sera ya Taifa **Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali** Mgawanyo wa Wafanyakazi katika Balozi uzingatie ujuzi na maarifa katika maeneo	upatikanaji wa fedha	

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	ya Biashara, Uwekezaji, Utalii na Usimamizi wa Uchumi ili kuhakikisha wafanyakazi hao wana uwezo wa kufanya kazi na matarajio ya Huduma yanaweza kufanyika kupitia mfumo maalumu wa mafunzo ya lazima ya kujenga uwezo Wafanyakazi wa nyongeza katika maeneo yenye mapungufu ili kufikia mahitaji ya kujaza nafasi zilizo wazi na wafanyakazi wenye sifa katka muda unaotakiwa Serikali itenge fedha za kutosha kupitia fungu maalumu kwa ajili ya Balozi Serikali ihakikishe utoaji wa fedha zinazotesheleza katika Balozi ili kukidhu mahitaji yao ya fedha. Aidha, Fedha zitolewe kwa wakati bila ucheleweshaji ili kuwezesha kutimiza ankra zao kwa wakati Serikali iwe na Kamati ya Uratibu itakayo wajibika kikamilifu kwa uratibu na mawasiliano mbalimbali yanayohusiana na Balozi.		
97	**Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba** Taasisi zinazonunua zinashauriwa kuhakikisha zinazingatia kikamilifu	Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma wataendelea kusimamia na kuzingatia sheria ya Manunuzi ya Umma ya	**Inatehemea matukio mengine**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	mahitaji ya sheria za manunuzi, hasa katika eneo la maandalizi na utekelezaji wa mpango wa mwaka wa manunuzi , Uidhinishaji wa Bodi ya Zabuni, Ukaguzi wa bidhaa na Huduma wa manunuzi yaliyofanyika na kufanya manunuzi kutoka kwa Wazabuni walioidhinishwa Kuhusu utunzaji wa nyaraka, nashauri Vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi wa Wizara,Idara na Wakala wa Serikali na Sekretariati za mikoa kuhakikisha wanatunza nyaraka za manunuzi Kuhusu ucheleweshaji wa kukamisha mikataba, Nahauri uongozi wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Sekretariati za mikoa kuangalia masharti na Vigezo ya mikataba na kuhakikisha hasara ya kuvunja mikataba inayotokana na kushindwa kukidhi kwa masharti na vigezo vya mikataba	mwaka 2011 na Kanuni zake, 2013 kwa Taasisi Taasisi zinazonunuaNyongea ya hapo, Mamlaka ya Udhibiti w Manunuzi ya Umma itaendelea kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi katika Taasisi zinazonunua ili kuongezauzingatiaji wa sheria ya manunuzi na kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa mikataba ya manunuzi.	
98	**Mapungufu katika uzimamizi wa matumizi** Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na	Serikali ilitoa waraka wa Hazina Na.1 wa tarehe 26 Januari, 2016 ukiwataka Maafisa Masuuli kutii taratibuna kanuni katika kutekeleza bajeti zao.	**Inategemea matukio mengine**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	Wakala wa Serikali na Balozi waendelee kuimarisha udhibiti wamifumo ya ndani ya Taasisizao pamoj na kujenga uwezo Serikaliitoe maelekezo kwa Taasisi nyingine za Serikali kuacha kufanya biashara na Wazabuni wasio na Mashine za EFD na kuendelea kutoa programu za uelewa ili kuamasisha utii usio na shuruti	Waraka ulisisitiza matakwa ya kufuata Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015	
99	**Udhaifu katika Usimamizi wa Mali** Mlipaji Mkuu wa Serikali aboreshe na kutekeleza mbinu za usimamizi kuhakikisha kwamba Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa wanazingatia maelekezoya Wizara ya Fedha ya kuanza kutumia kikamilifu Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu kwa misingi isiyo taslimu. Serikali kuhakikisha kwamba Wizara/Sekretariati za Mikoa zinapata umiliki wa nyaraka ili kulinda mali za Serikali.Serikali iwajibike katika kuhakikisha hatua zinachukuliwa kwa kuuza magari magari amabyo hayatengenezeki kwa kufuata sheria na	Tathmini na Tafiti za Ardhi na Majengo zinaendela. Kazi hii inashughulikiwa kwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makzai. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya magari 546, pikipiki 40, mitambo na mashine 68 na ndege 6 ziifutwa kwenye daftari la mali na kuuzwa kwa njia ya mnada wa wazi ambapo kiasi cha shilingi 2,137,195,351 kilikusanywa	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	kanuni ili kuokoa kiasi cha fedha kwenye uuzwaji wa mali z Serikali.		
100	**Kupungua kwa Uwekezaji wa Serikali** Serikali kupitia Wizara ya Fedha ianzishe mfumo wa kubakiza mapato katika Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kutenga fesha za Uwekezaji uliopendekezwa. Mfumo utasaidia kama kipimo cha ufanisi kwa Msajili wa Hazina kwa kuwezesha Serikali kutathmini uwezo wa Msajili katika kuhamasisha mapato kutoka kwenye uwekezaji	Katika bajeti ya mwaka 2016/17 serikali imeondoa mfumo wa kubakiza mapato na kutaka fedha zote kuingizwa kwenye mfuko wa Serikali Budget. Hatahivyo, Serikali inaangalia namna bora ya kuchangia katika Mashirka ya Umma ili kuhakikisha hisa za Serikali zinazingatiwa	**Utekelezaji haujakamilika**
101	**Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu** Maafisa masuuli wahakikishe waanoshughulikia mafao wanazingatia kanuni za ukokotoaji wa mafao na sheria na kuhakikisha uwasilishaji wa majalada	Serikali iliandaa mwongozo wa mafao utakaoelekeza watumiaji masuala yote yanayohusiana na ukokotoaji wa mafao. Katika bajeti ya 2016/17 setikali imetenga shilingi milioni 464 kuwafundisha Wahasibu juu ya masuala ya ukokotoaji wa mafao	**Utekelezaji haujakamilika**

Na.	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)
	ya mafao umekamilika, umewasilishwa kwa muda kwa kuwa na taarifa sahihi ili kuepusha ucheleweshaji wa malipo ya mafao. Mafunzo yafantanyike kwa Wanaoshughulikia Mafao ili kuongeza uelewa wa sheria za mafao na masuala mengine		
102	**Deni la taifa na Huduma za Jumla** Serikali iridhie mkakati bora wa matumizi ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama, mkakati wa kuongeza mikopo yenye masharti nafuu na utaratibu madhubuti wa ufuatiliaji juu ya shughuli za kigeni nchini. Mikakati hii ikiunganishwa pamoja na Juhudi za uhamasishaji wa biashara ya nje kutaimarisha Shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu zenye nguvu. Hivyo, Kupunguza hasara ya kubadilisha fedha za kigeni inayochangia kuongeza deni la taifa	Serikali imepunguza mafunzo yasiyo ya lazima na safari za nje ya nchi, sherehe za Sikukuu, kuendesha semina katika mahoteli yenye gharama kubwa nk Serikali imeendela kuboresha makusanyo ya mapato yatakayorahisisha kuwa na fedha za kutosha kugharamia michango yote ya kisheria	**Imetekelezwa**

Kiambatisho 3.6: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya nyuma ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali juu ya Ripoti ya Jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Na	Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali	Majibu ya Serikali	Maoni ya Ukaguzi
	2011/2012 hadi 2013		
	Kutotekelezwa kwa mapendekezo matano ya nyuma yaliyotolewa Januauri 2015 na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali		
1	**Mamlaka ya Mapato Tanzania kukamilisha kushughulikia madai ya Kodi** Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ilielekeza Serikali ihakikishe Mamlaka ya Mapato wanashughulikia kikamilifu madai mbalimbali ya kesi za kodi kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali.	Mamlaka ya Mapato kupitia Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Mapato na Mahakama ya Rufaa imeshughulikia kwa ufanisi kesi za kodi. Ndani ya mwezi Aprili, Bodi ya Rufaa za kodi ilikuwa na kesi 117 zenye thamani ya shilingi bilioni 116 na kesi 63 zenye thamani ya shilingi bilioni 66 ziliamuliwa. Mamlaka ya Mapato ilishinda kesi 50 zenye thamani ya shilingi bilioni 58 . Mamlaka ya Mapato ilishindwa kesi 13 zenye thamani ya shillingi 8 (12.5%) . Kwahiyo, bado kuna kesi 54 zinazosubiri maamuzi ya Mahakama.	**Utekelezaji haujakamilika** Ufuatiliajiwa rufaa ambazo hazijahitimishwa utafanyika katika ukaguzi ujao
1.2	**Serikali kulipa madeni ya PSPF** Serikali ilielekezwa kulipa mara moja deni la PSPF ili kuondoa mzigo wa fedha wa kuhudumia wastaafu katika siku za usoni.	Serikali ilimuelekeza Mkaguzi Mkuu wa ndani kuhakiki madeni yote inayodaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama PSPF, LAPF, NSSF na GEPF mchakato wa uhakiki uko hatua za mwisho. Madeni yote yaliyohakikiwa yatajumuishwa ili kutambua madeni yote. Serikali iko kwenye maandalizi ya kutoa Amana kwa Mifuko yote ndani ya mwaka huu wa fedha.	**Ukekelezaji haujakamilika** Tumekubali majibu ya Uongozi. Tutafanya tathimini ya utekelezaji katika ukaguzi ujao.

Na	Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali	Majibu ya Serikali	Maoni ya Ukaguzi
1.3	**Usimamizi wa Misamaha ya Kodi** Serikali ilielekezwa kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi na kuwajibisha kampuni zilizotumia vibaya misamaha ya kodi kama ilivyotajwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	Mamlaka ya Mapato imeweka udhibiti wa usimamizi wa misamaha ya kodi kwa kuongeza wafanyakazi zaidi na vitendea kazi vya kutosha. Mameneja wote wa Mikoa wameweka vipaumbele vya udhibiti wa Misamaha ya kodi katika shughuli zao za kila siku. Na kwa nyongeza, Utungaji wa sheria ya ongezeko la thamani (VAT) ya 2014 umepunguza mianya ya misamaha isiyokuwa na tija. Jitihada zimefanyika kama alivyopendekeza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ifuatavyo Ukaguzi wa mapato ulifanyika kwenye Makampuni ya Madini yakiwemo Geita na Resolute kwa misamaha ya kodi kwenye mafuta na kiasi cha shilingi milioni 16.7 kilikusanywa. Ukaguzi wa Kodi ulifanyika kwa kampuni za Kiliwarrior Expedition na Hoteli ya Kilimakyaro ambazo zilitumia vibaya misamaha ya kodi wakati wa kuingiza na kusajili magari, hivyo, kiasi cha shilingi 519,744,470 kilikusanywa.	**Utekelezaji hujakamilika .**
1.4	**Uchunguzi juu ya tuhuma za ujenzi wa jengo la Watu Mashuhuri katika Uwanja wa ndaege wa Kimataifa wa Julius Nyerere** Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali iliiagiza Serikali kupitia vyombo vyake kama TAKUKURU	Serikali ya Tanzania ililipa Shilingi 1,042,286 ,911.00 tu katika mradi mzima na kwa mtazamo huo Serikali haikupata hasara ya bilioni 9.0 kama ilivyooneshwa na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali	**Utekelezaji haujakamilika** Uchunguzi wa kijinai haujahitimishwa kama

Na	Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali	Majibu ya Serikali	Maoni ya Ukaguzi
	kufanya uchunguzi wa jinai kwa Watuhumiwa waliohusika kuisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 9.0 na kuchukua hatua za kisheria		ilivyoelekezwa na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali.
1.5	**Kupunguza gharama za matangazo ya bajeti kwenye Magazeti** Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ilielekeza Serikali kupunguza gharama za matangazo ya bajeti kwenye Magazeti	Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Mkutano Uliofanyika Januari 2015 Mkoani Mtwara ulizielekeza Wizara, Idara na Wakala wa Serikali juu ya mikakati ya kupunguza gharama. Maelekezo hayo yametoa majibu mazuri	**Imetekelezwa**
2 2	**Kutotolewa fedha za kutosha kwa Wakala wa umeme vijijini (REA)** Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015 imependekeza kuwa serikali inapaswa kutoa fedha kwa Wakala wa umeme vijijini (REA) kutoka vyanzo vyake yenyewe ili kuwezesha upelekwaji wa umeme vijijini	Katika mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya Shilingi 200,000,000,000 zimetengwa kwa ajili ya REA ambapo jumla ya Shilingi 172,099,000,000 zilipelekwa REA Mei,2015	**Utekelezaji haujakamilika** Hata hivyo, naishauri Serikali kutoa fedha kama zilivyoidhinishwa
